**30 APRILI, 2024**

# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA KUMI NA TANO

**Kikao cha Kumi na Sita – Tarehe 30 Aprili, 2024**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Katibu.

**NDG. YONA KIRUMBI - KATIBU MEZANI:**

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na: -

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:**

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Kilimo kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

**NAIBU WAZIRI WA MADINI:**

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Madini kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

**MHE. MAIMUNA A. PATHAN K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA NISHATI NA MADINI:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Madini kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

**SPIKA:** Ahsante sana, Katibu.

**NDG. YONA KIRUMBI - KATIBU MEZANI:**

## MASWALI NA MAJIBU

**SPIKA:** Maswali, tunaanza na Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa John Marko Sallu, Mbunge wa Handeni Vijijini, sasa aulize swali lake.

Na. 202

### Hitaji la Kituo cha Afya Tarafa ya Kwamsisi - Handeni

**MHE. JOHN M. SALLU** aliuliza:-

Je, lini Serikali itaanza ujenzi wa Kituo cha Afya Tarafa ya Kwamsisi – Handeni?

**SPIKA:** Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Dkt. Dugange, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua mahitaji ya vituo vya afya kwenye Kata za kimkakati kote nchini. Katika mwaka wa fedha 2025/2026, Serikali kupitia mapato ya ndani ya Halmashauri ya Wilaya ya Handeni itatenga shilingili milioni 50 kwa ajili ya kuanza ujenzi. Aidha, Serikali itaendelea kutenga bajeti kwa awamu kwa ajili ya kuendeleza ujenzi wa Kituo cha Afya cha Kwamsisi – Handeni, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa John Sallu, swali la nyongeza.

**MHE. JOHN M. SALLU:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi. Naomba niulize maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza; lini Serikali itajenga vituo vya afya kwenye Tarafa ya Magamba na Tarafa ya Mkumbulu hususan kwenye Kata ya Segera ambapo pana ahadi nyingi za Viongozi Wakuu wa nchi?

Mheshimiwa Spika, swali la pili; Kituo cha Afya Kabuku ni cha zamani, lakini hakina wodi. Je, lini Serikali itajenga wodi kwenye Kituo cha Afya cha Kabuku? Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, tunatambua kwamba kuna uhitaji wa vituo vya afya kwenye Tarafa hiyo ya Magamba na Kata ya Segera ambayo ameitaja Mheshimiwa Mbunge. Nimhakikishie tu kwamba tunaendelea kwa awamu kujenga vituo vya afya katika Kata zote za kimkakati na tutakwenda pia kuweka kipaumbele kwenye Kata hizo ambazo Mheshimiwa Mbunge amezitaja ikiwa zitakidhi vigezo vya kuwa na vituo vya afya.

Mheshimiwa Spika, pili, kuhusiana na Kituo cha Afya cha Kabuku, ni kweli kituo hiki ni cha siku nyingi na kinatoa huduma kwa wananchi wengi, lakini kina upungufu wa baadhi ya majengo hususan wodi. Naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tumeweka mkakati wa kukamilisha ukarabati na upanuzi wa hospitali kongwe za Halmashauri na baada ya hapo tutakwenda kuanza ukarabati na upanuzi wa vituo vya afya kikiwemo Kituo cha Afya cha Kabuku, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, maswali yawe mafupi. Mheshimiwa Ally Kassinge, swali la nyongeza.

**MHE. ALLY M. KASSINGE:** Mheshimiwa Spika, lini Serikali itapeleka fedha katika Halmashauri ya Wilaya ya Kilwa kwa ajili ya ujenzi wa Kituo cha Afya katika Kata ya Likawage?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Kassinge alishaleta mahitaji ya kituo cha afya katika Kata hiyo ya Likawage. Nimhakikishie kwamba Serikali imeshaweka mkakati wa kupeleka fedha kwa ajili ya ujenzi wa kituo hicho, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mohamed Monni, swali la nyongeza.

**MHE. MOHAMED L. MONNI:** Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu alifanya ziara Wilaya ya Chemba na kuahidi vituo viwili vya afya Kata ya Paranga na Kata ya Jangalo. Nataka kujua ni lini ahadi hizo zitatekelezwa? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba ahadi za viongozi wetu wa kitaifa ni kipaumbele namba moja katika utekelezaji wa shughuli zote za Ofisi ya Rais, TAMISEMI ikiwemo ujenzi wa vituo vya afya.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba tu nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge na wananchi wa Chemba kwamba wawe na uhakika kuwa yale ni maelekezo ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, hivyo, Ofisi ya Rais, TAMISEMI ilishaweka mkakati na tutakwenda kujenga vituo hivyo, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Abubakari Damian Assenga Mbunge wa Kilombero, sasa aulize swali lake.

Na. 203

**Ushuru wa Mazao Chini ya Tani Moja**

**MHE. ABUBAKARI D. ASENGA** aliuliza: -

Je, kwa nini wananchi wa Wilaya ya Kilombero wanatozwa Ushuru wa Mazao chini ya tani moja kinyume na maelekezo ya Serikali?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. FESTO J. DUGANGE)** alijibu: -

**SPIKA:** Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Kilombero ina Halmashauri mbili ambazo ni Halmashauri ya Mji wa Ifakara na Halmashauri ya Wilaya ya Mlimba. Ushuru wa Mazao katika Halmashauri hizo hutozwa kwa mujibu wa Kifungu cha 16 (1)(a) na (b) *(cash crops and food crops)* cha Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa, Sura 290. Sheria hiyo imeweka kiwango kisichozidi asilimia tatu ambacho hutozwa kwa mazao yasiyozidi tani moja yanayosafirishwa kwenda nje ya Halmashauri.

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na changamoto kwa baadhi ya wafanyabiashara wanaosafirisha mazao nje ya Halmashauri kukwepa kulipa ushuru huo kwa kusafirisha mazao hayo kidogo kidogo kwa hutumia maguta, pikipiki na bajaji ili yasifikie ujazo wa tani moja ambao unapaswa kulipiwa ushuru. Wafanyabiashara hao wanapobainika hutozwa ushuru wa mazao kulingana na wingi wa mazao waliyoyasafirisha.

Mheshimiwa Spika, aidha, Serikali inazielekeza Mamlaka za Wilaya ya Kilombero na Halmashauri nyingine kote nchini kuzingatia sheria na kuacha kuwatoza ushuru wakulima wanaosafirisha mazao kihalali ndani ya halmashauri yenye uzito wa chini ya tani moja, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Abubakari Damian Assenga swali la nyongeza.

**MHE. ABUBAKARI D. ASSENGA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru na kwa kweli nashukuru sana kwa majibu haya ya Serikali na wananchi wanaona kabisa Serikali ya Awamu ya Sita inaendelea kuwapenda.

Mheshimiwa Spika, wananchi wanatuambia katika geti la Idete, Kivukoni na Kidatu bado wanatozwa chini ya tani moja. Je, Serikali inatuelekezaje tukikamata ushahidi kwamba chini ya tani moja wananchi wanaendelea kutozwa?

Mheshimiwa Spika, swali la pili; kutokana na wananchi wetu wa ukanda wa Morogoro Chini kwa maana ya Ulanga, Malinyi, Mlimba na Halmashauri ya Mji wa Ifakara mwaka huu kukumbwa na mvua nyingi sana na mafuriko makubwa yatakayopunguza mazao: Je, Serikali haioni umuhimu wa kusamehe kabisa tozo ndogo ndogo zinazotokana na mambo ya kilimo ili kutoa afueni kwa wananchi wetu ambao wameathirika kwa kiasi kikubwa sana na mvua hizo? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Abubakari Assenga, amelifuatilia suala hili la kuhakikisha kwamba wananchi wa Halmashauri ya Mji wa Ifakara hawatozwi ushuru wa mazao wanaposafirisha ndani ya Halmashauri na uzito ambao hauzidi tani moja.

Mheshimiwa Spika, nitoe kauli ya Serikali kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, kwamba ni kosa na ni uvunjivu wa sheria kama kuna wataalam katika mageti ambayo Mheshimiwa Mbunge ameyataja, wanatoza ushuru kwa wakulima wa ndani ya Halmashauri wanaosafirisha mazao chini ya tani moja ndani ya Halmashauri. Ni kosa na tutachukua hatua za kinidhamu ikithibitika na tukiwathibitisha hao ambao wanafanya hivyo. Kwa hiyo, waache mara moja, wafuate sheria ambazo zimewekwa ili wananchi waendelee kufanya shughuli zao za kiuchumi kwa ufanisi zaidi.

Mheshimiwa Spika, pili, niwape pole wananchi wa Halmashauri ya Mji wa Ifakara kwa ajili ya mafuriko. Mheshimiwa Mbunge pia ulikuwa huko, ninakuhakikishia tu kwamba Serikali itaendelea kuona namna nzuri ya kuboresha huduma hizo ili wananchi hawa waweze kurudi kwenye hali yao ya kawaida, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Selemani Zedi, swali la nyongeza.

**MHE. SELEMANI J. ZEDI:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa watoza ushuru ndani ya Jimbo la Bukene bado wanatoza ushuru wa mazao kwa wakulima wa kawaida kabisa ambao siyo wafanyabiashara, je, Serikali iko tayari kutoa katazo kwa hao wataalamu watoza ushuru kwamba waache kuwatoza ushuru wakulima wa kawaida ambao siyo wafanyabiashara na ambao hawasafirishi mazao nje ya Halmashauri ya Bukene? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Zedi, hebu uliza swali lako nilielewe vizuri.

**MHE. SELEMANI J. ZEDI:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa watoza ushuru...

**SPIKA:** Hayo maelezo nimeshayasikia. Swali lako kwa Mheshimiwa ili nilielewe vizuri.

**MHE. SELEMANI J. ZEDI:** Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri yuko tayari kutoa kauli kwa watoza ushuru hao waache kuwatoza wakulima ambao siyo wafanyabiashara?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, Sheria ya Ushuru wa Mazao, Kifungu cha 16 (1) (a) na (b) kinaeleza wazi kwamba ni marufuku na haitakiwi kutoza ushuru kwa wakulima wa kawaida ambao wanalima ndani ya Halmashauri.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nitumie nafasi hii kumsisitiza Mkurugenzi wa Halmashauri ya Nzega Vijijini na katika Jimbo la Bukene kuhakikisha wanafuata sheria hii na kuacha kuwatoza wakulima ushuru wa mazao ambayo hawayasafirishi nje ya Halmashauri na wala hayajazidi tani moja, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Sina uhakika kama nimeelewa sana. Mkulima wa kawaida anatozwaje? Sijaelewa swali lile, hebu wewe uliyeelewa

naona umemjibu. Mkulima wa kawaida, yaani ana mazao yake nyumbani, anafuatwa kwenda kutozwa ushuru, ama!

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, nilivyomwelewa Mheshimiwa Mbunge ni kwamba, kuna wakulima ambao wanalima ndani ya Halmashauri, lakini haendi kupeleka mnadani wala hatoi nje ya Halmashauri, na anasafirisha kwenda nyumbani kutoka shambani.

**MHE. SELEMANI J. ZEDI:** Mheshimiwa Spika, ni sahihi kabisa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Zedi naona umesimama, yuko sahihi Mheshimiwa Naibu Waziri?

**MHE. SELEMANI J. ZEDI:** Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Naibu Waziri, yuko sahihi kabisa.

**SPIKA:** Kama ndivyo, Mheshimiwa Naibu Waziri basi hilo katazo lisielekee Bukene peke yake, lielekee kila mahali, kwa sababu kama watu wanatozwa kwa mazao shambani, lielekee kila mahali. Tusaidie kutoa hilo katazo ili usiendelee kuulizwa na Wabunge wengine. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, naomba kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, nirejee na kusisitiza kwamba utozaji wa ushuru wa mazao ni kwa mujibu wa Sheria ya Ushuru wa Mazao, Kifungu cha 16 (1) (a) na (b) ambapo naomba sasa Halmashauri zote kote nchini zizingatie sheria hiyo, kwa kutowatoza wakulima wa ndani ya Halmashauri wanaotoa mazao yao shambani kupeleka majumbani, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Deus Clement Sangu, Mbunge wa Kwela, sasa aulize swali lake.

Na. 204

**Ahadi ya Ujenzi wa Barabara ya Chombe hadi Kaoze - Jimbo la Kwela**

**MHE. DEUS C. SANGU** aliuliza:-

Je, lini ahadi ya ujenzi wa barabara ya Chombe hadi Kaoze – Kwela itatekelezwa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua umuhimu wa ujenzi wa Barabara ya Chombe hadi Kaoze – Kwela yenye urefu wa kilometa 15. Barabara hii inaunganisha Vijiji vya Kaoze, Kiandaigonda na Chombe na ipo sambamba na milima ya Lyambalyamfipa ambayo imeathiriwa na maji ya mvua.

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Wakala ya Barabara za Vijijini na Mijini *(TARURA)* imekamilisha usanifu wa madaraja na barabara na kubaini gharama ya shilingi bilioni 2.3. Hata hivyo, katika mwaka wa fedha 2024/2025, Serikali imetenga shilingi milioni 500 kupitia fedha za tozo ya mafuta kwa ajili ya kujenga kipande cha barabara kati ya kijiji cha Kaoze na Kiandaigonda.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kutenga fedha kwa ajili ya barabara hii ili kukamilisha ujenzi wa kipande cha kutoka Kijiji cha Kiandaigonda hadi Chombe.

**SPIKA:** Mheshimiwa Deus Sangu, swali la nyongeza.

**MHE. DEUS C. SANGU:** Mheshimiwa Spika, barabara ya Chombe Kiandaigonda - Kaoze ni barabara ambayo imeandikiwa maandiko ya kuomba maombi maalum kwa miaka miwili mfululizo kwa maana ya fedha shilingi bilioni 2.4. Nataka kujua je, Serikali mna mpango gani wa kupitia hayo maombi na kuweza kutekeleza kwa kuleta fedha hizi kutengeneza barabara hii?

Mheshimiwa Spika, swali la pili. Daraja linalounganisha Kijiji cha Ilembo na Makao Makuu ya Kata ya Mkuyi imeharibiwa sana na tumeleta maombi maalum ya shilingi bilioni 1.35. Je, Serikali mna mpango gani wa kuleta fedha hizi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Spika, naomba nijibu maswali ya Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kuhusu swali lake la kwanza, Serikali inatambua uhitaji huo na maombi hayo ya dharura na Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ofisi ya Rais, TAMISEMI aliyepita, tayari alikuja kufanya ziara katika eneo hilo, pia Mtendaji Mkuu wa *TARURA* alifika kuona eneo hilo. Kwa hiyo, tayari Serikali inatambua umuhimu na iko kwenye mchakato. Tumelipokea ombi hili na tunaendelea kulifanyia kazi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu swali la pili kuhusiana na barabara aliyoitaja, tumepokea maombi na tunaendelea kuyafanyia kazi. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. John Pallangyo, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. JOHN D. PALLANGYO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa nafasi hii.

Je, ni lini ahadi aliyoitoa Hayati Dkt. John Pombe Magufuli ya kujenga Barabara ya King'ori kuanzia Malula hadi Ngarenanyuki kwa kiwango cha lami itatekelezwa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, tayari tumeshakutana na Mheshimiwa Mbunge, tumezungumza kuhusu maombi yake ya barabara hiyo na ahadi za Viongozi Wakuu wa nchi ni kipaumbele namba moja. Kwa hiyo, nikuhakikishie Mheshimiwa Mbunge Serikali imepokea na tunafanyia kazi. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Issa Mtemvu, swali la nyongeza.

**MHE. ISSA J. MTEMVU:** Mheshimiwa Spika, barabara ya Malambamawili – King'azi karibu kilometa nne imeharibika sana, sasa hivi hakuna mawasiliano, je, Serikali mko tayari kupeleka fedha maalum kwa ajili ya utatuzi wa barabara hiyo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua changamoto za miundombinu katika maeneo mengi ya nchi ikiwemo barabara aliyoitaja Mheshimiwa Mbunge. Tunatambua kutokana na hali ya mabadiliko ya tabianchi na mvua nyingi zinazoendelea sehemu nyingi za nchi, barabara zinaharibika. Kwa hiyo, Serikali tayari imetenga fedha ya dharura.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mama Samia Suluhu Hassan amesikia kilio cha Watanzania na ameongeza bajeti ya dharura ya *TARURA* kutoka shilingi bilioni 21 mpaka shilingi bilioni 131. Pia ameongeza fedha maalum shilingi bilioni 350 kwa ajili ya kuweza kusaidia ukarabati wa barabara hizi. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba maombi yake ya barabara hii tayari yameifikia Serikali na Serikali italifanyia kazi. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Christine Ishengoma, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA:** Mheshimiwa Spika, je, ni lini ahadi ya viongozi ya ujenzi wa barabara kuanzia Mzumbe hadi Mgeta itatekelezwa kwa kiwango cha lami? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Spika, kama nilivyotangulia kusema, ahadi za viongozi Wakuu wa nchi, kwetu sisi ni kipaumbele namba moja. Kwa hiyo, kwa sababu maombi hayo yameshafika Serikalini, basi nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tumeyapokea, tutayachakata na kuyafanyia kazi. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Cosato David Chumi, swali la nyongeza.

**MHE. COSATO D. CHUMI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi. Barabara ya kuanzia Changarawe inayopita katika Vijiji vya Mtula – Bumilayinga - Matanana mpaka Kisada ni ya muhimu kwa sababu ya uzalishaji wa zao la parachichi...

**SPIKA:** Swali.

**MHE. COSATO D. CHUMI:** Mheshimiwa Spika, je, Serikali iko tayari kutuongezea fedha ili kujenga barabara hiyo kwa uimara na ubora?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua umuhimu mkubwa sana wa barabara zetu hizi na hasa katika kuwawezesha wananchi kiuchumi. Kwa hiyo, kama maombi haya tayari yamefika katika meza ya Serikali, nikuhakikishie Mheshimiwa

Mbunge, Mheshimiwa Rais anatoa fedha nyingi kuhakikisha barabara hizi zinajengwa. Kwa hiyo, Serikali italifanyia kazi jambo hili ili barabara hii iweze kujengwa. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Jacqueline Kainja Andrea, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 205

**Uhitaji wa Nyumba za Walimu Nchini**

**MHE. JACQUELINE K. ANDREA** aliuliza: -

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga nyumba za Walimu nchini?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua uwepo wa changamoto ya upungufu wa nyumba za walimu wa shule za msingi na sekondari nchini ambayo inatakiwa kutatuliwa.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2022/2023 na 2023/2024, Serikali kupitia fedha za programu za kuimarisha Elimu ya Awali na Msingi *(BOOST)* na Sekondari *(SEQUIP)* pamoja na fedha za Serikali Kuu, imejenga nyumba 860 za walimu wa shule za msingi na sekondari zitakazochukua familia 2,018.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2024/2025, Serikali itajenga jumla ya nyumba za walimu 562 zitakazochukua familia 1,124. Serikali itaendelea kutenga fedha kupitia programu za miradi mbalimbali na Serikali Kuu kwa ajili ya ujenzi wa nyumba za walimu ili Walimu wetu wapate mahali bora pa kuishi.

**SPIKA:** Mheshimiwa Jacqueline Kainja Andrea, swali la nyongeza.

**MHE. JACQUELINE K. ANDREA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa nafasi nami niweze kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ambayo Serikali imejibu, je, Serikali ina mpango gani madhubuti kuhakikisha ujenzi huu wa nyumba za Walimu unaenda kwa kasi? Kwa mfano, kwa Mkoa wangu wa Tabora, Wilaya ya Urambo nyumba tulizonazo ni nane, lakini jumla ya shule zote za sekondari pamoja na *primary* ni 107. Je, kuna jitihada gani za makusudi za kuhakikisha changamoto hii inapungua? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili. Pamoja na ujenzi wa nyumba 860 ambazo Serikali imejenga, je, Serikali haioni kuna haja ya kuangalia kipaumbele sana kwenye maeneo ambayo jiografia yake ni chechefu? Kwa mfano, kwa Wilaya ya Urambo tuna Shule ya Msumbiji walimu wanaishi kilometa 15 kutoka shuleni na mazingira ni ya mbuga na maji ni mengi, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mbunge amefanya kazi kubwa sana kuwatetea wananchi wake na Serikali inatambua mahitaji makubwa ya miundombinu hii ya nyumba za walimu. Kwa kutambua uhitaji huo, Serikali imekuwa ikiwashirikisha wananchi kupitia halmashauri kujenga nyumba za walimu.

Mheshimiwa Spika, mpaka sasa Serikali tayari imepokea maboma 2,470 ya nyumba za walimu na Serikali inaendelea kutafuta fedha ili kuweza kuunga mkono jitihada za wananchi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu swali la pili la Mheshimiwa Mbunge, nachukua nafasi hii kuendelea kuwasisitiza wakurugenzi wote wa halmashauri kuweza kufanya tathmini sahihi ya uhitaji wa nyumba hizi za walimu kwa kuzingatia mazingira halisi ya maeneo husika ili wananchi waweze kushirikiana na Serikali katika kutatua

kero hii, kwa maana ya ujenzi wa nyumba hizo za walimu, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Leah Komanya, swali la nyongeza.

**MHE. LEAH J. KOMANYA:** Mheshimiwa Spika, je, Serikali haioni haja ya kukamilisha maboma 18 ya nyumba za walimu katika Jimbo la Meatu? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua umuhimu mkubwa sana wa kuunga mkono jitihada za wananchi pale wanapokuwa wamejenga maboma. Mpaka muda huu, tayari Serikali imefanya tathmini kubaini maboma katika sekta ya elimu yapo kiasi gani na Serikali imebaini kwamba inahitajika shilingi bilioni 300 kwa ajili ya ukamilishaji wa maboma hayo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali kwa kadri ya upatikanaji wa fedha itahakikisha inaunga mkono jitihada za wananchi kwa kukamilisha maboma hayo, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Shamsia Mtamba, swali la nyongeza.

**MHE. SHAMSIA A. MTAMBA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa fursa hii, je, ni upi mkakati wa Serikali wa kuhakikisha wanajenga nyumba za walimu katika Shule ya Msingi Kivava?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kama nilivyotangulia kusema, Serikali inatambua umuhimu mkubwa sana na uhitaji wa nyumba hizi za walimu. Kupitia miradi yake tofauti, Mradi wa *BOOST* na mradi wa *SEQUIP,* tayari Serikali inatenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa nyumba hizi za walimu. Pia Serikali itaendelea kuwashirikisha wananchi kupitia halmashauri kuona kwamba kunakuwa na jitihada za pamoja katika kujenga miundombinu hiyo ya nyumba za Walimu. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba suala lako tumelipokea na litafanyiwa kazi na Serikali. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, Mheshimiwa Saashisha Elinikyo Mafuwe, Mbunge wa Hai, sasa aulize swali lake.

Na. 206

**Kuteketeza Miti ya Mikaratusi Nchini**

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE** aliuliza: -

Je, Serikali inatoa tamko gani kuhusu kuteketeza miti ya mikaratusi nchini baada ya tafiti kuonesha inaharibu mazingira?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, Mheshimiwa Hamza, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kuna zaidi ya *species* 500 za miti ya mikaratusi duniani. Sisi Tanzania kupitia *TAFORI* imeruhusu aina 25 za miti ya mikaratusi ili kupata fursa mbalimbali zitokanazo na aina hii ya miti ya mikaratusi hasa kwenye viwanda vya mazao yaliyosindikwa.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, Serikali kupitia Taasisi ya Utafiti wa Misitu Nchini *(TAFORI)* inaendelea na utafiti wa kina wa miti hii

ili kujua taarifa za kitaalamu pamoja na ushauri kuhusu athari za kimazingira. Mara baada ya tafiti kukamilika, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira pamoja na Wizara ya Maliasili na Utalii zitatoa elimu kwa wananchi kuhusu miti ya mikaratusi, nakushukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Saashisha Mafuwe, swali la nyongeza.

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE:** *Mheshimiwa Spika, ahsante, kwa kweli sijafurahishwa na majibu ya swali hili kwa Serikali lakini naomba niulize maswali mawili ya nyongeza.* **[Maneno Haya Siyo Sehemu ya Taarifa Rasmi za Bunge]**

**SPIKA:** Ngoja, ngoja, hujafurahishwa kwamba siyo majibu ya swali lako, ama sicho ulichouliza?

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE:** *Mheshimiwa Spika, ni majibu ya swali langu lakini hayajanitosheleza pale ambapo nilikuwa natamani kufika.* **[Maneno Haya Siyo Sehemu ya Taarifa Rasmi za Bunge]**

**SPIKA:** Kama hayajajitosheleza Kanuni zetu zinataka Serikali ijibu swali kwa ukamilifu. Ukishaanza na haya maneno ya mwanzo, uwe na uhakika wa kinachafuata. Hayajajitosheleza kwa wewe uonavyo.

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE:** Mheshimiwa Spika, naomba niulize maswali mawili ya nyongeza.

**SPIKA:** Tunaenda vizuri. Mimi nataka Mbunge ujibiwe swali lako kwa kadiri unavyowawakilisha wananchi wako. Umeanza na maelezo ya halijajitosheleza, ndiyo nataka hapo tupamalize kwanza halafu tuanze huku kwingine. Umeridhika na majibu, lakini una maswali ya nyongeza. Kama hujaridhika na majibu maana yake, niiambie Serikali ikajibu upya.

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE:** Mheshimiwa Spika, kwa kiwango alichojibu nimeridhika, naomba niendelee na maswali ya nyongeza.

**SPIKA:** Ahsante sana. Kwa hiyo, yale maneno ya mwanzo tunayafuta. Serikali imejibu sawa sawa na wewe sasa una maswali ya nyongeza Mheshimiwa Mbunge.

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa taarifa za kitaalamu zinaonyesha miti hii ya mikaratusi inatumia lita 15 mpaka 20 kwa siku kwa mti mmoja na tafiti zipo na zinapatikana, je, Serikali iko tayari sasa kuhudumia miti hii kwa kutengeneza skimu maalum za kumwagilia miti hii wakati wakiendelea na mchakato wa kufanya utafiti?

Mheshimiwa Spika, swali la pili; kwa kuwa bado Serikali haina taarifa za utafiti wa athari za miti hii. Je, Serikali iko tayari kupokea tafiti za watu binafsi ambazo ziko nyingi, zimefanyika kuhusiana na madhara na athari za miti hii ili ziweze kuzitumia kama tafiti rasmi za Serikali?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mafuwe, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, ni kweli hata sisi Wizara ya Maji, Wizara ya Maliasili na Mazingira tumegundua kwamba ipo baadhi ya miti ambayo inatumia na inakunywa maji mengi mpaka kufikia hatua ya athari ya kupunguza vyanzo vyetu vya maji na hatimaye kupotea kabisa kutokana na miti hiyo ilivyo.

Mheshimiwa Spika, tumegundua miti hii ipo katika *species* tofauti, maana yake *species* zipo nyingi na aina za miti zipo nyingi. Kwa mfano, hata ukiangalia mikoko kama mikoko, watu wengi wanafahamu mikoko ni ile ya baharini tu, lakini ipo mikoko zaidi ya *species* 20 na hii nayo yote inatumia hayo maji.

Mheshimiwa Spika, nimwambie tu kwamba mpango na ushauri ambao Mheshimiwa ametushauri wa kuandaa skimu maalumu, hili jambo lipo katika mipango yetu ya Wizara na tayari tulishalifikiria. Nimwambie tu Mheshimiwa kwamba asiwe na wasiwasi, tunakwenda kuondoa ama kupunguza changamoto hii

ingawa Serikali tunahimiza watu wapande miti ya aina tofauti ili kunusuru mazingira yetu.

Mheshimiwa Spika, kingine, Serikali ipo tayari kupokea tafiti kutoka Taasisi za Serikali na Taasisi za watu binafsi tukiwa na lengo la kuondoa changamoto hii. Kwa muda mrefu Wizara nyingi tumekuwa tukipoea tafiti hizo. Kitu cha msingi tunachokitaka, tafiti zifuate utaratibu na mwisho zitoe mapendekezo nini tufanye kama Wizara ili kuweza kuondoa changamoto hiyo. Kama Wizara, tupo tayari kupokea hizo tafiti, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Madini, Mheshimiwa Asia Abdukarimu Halamga, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 207

**Kuwawezesha Wananchi wa Hanang Vifaa vya Kuchimbia Madini Chumvi**

**MHE. ASIA A. HALAMGA** auliza: -

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwawezesha vifaa vya kuchimbia madini ya chumvi wananchi wa Kata ya Gendabi - Hanang?

**SPIKA:** Naibu Waziri wa Madini, Mheshimiwa Dkt. Kiruswa, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MADINI** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kutokana na umuhimu wa sekta ya uzalishaji chumvi nchini, Serikali kupitia Wizara ya Madini imeendelea kuchukua hatua mbalimbali ikiwemo kuondoa kodi na tozo mbalimbali ambazo zilikuwa zinafikia 17 zilizokwaza ukuaji wa sekta ndogo ya chumvi.

Mheshimiwa Spika, Shirika la Madini la Taifa *(STAMICO)* ambalo ndilo mlezi wa wachimbaji wadogo limeendelea kutoa mafunzo kwa wazalishaji wa chumvi nchini katika masuala mbalimbali yahusuyo mikopo, vifaa na uzalishaji wa chumvi bora kwa kuzingatia mahitaji ya soko.

Mheshimiwa Spika, *STAMICO* itafika katika Kata ya Gendabi, Wilaya ya Hanang kutoa mafunzo kuhusu upatikanaji wa vifaa, mikopo na masoko kwa wazalishaji wa chumvi wa eneo hilo, ahsante sana.

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Mbunge naona ameridhika na majibu, umekaa. Mheshimiwa Asia Halamga, swali la nyongeza.

**MHE. ASIA A. HALAMGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, swali langu la kwanza, kwa kuwa Gendabi sasa hivi inazalisha kwa mwaka mmoja zaidi ya tani 80,000 ya chumvi, je, Serikali haioni haja sasa ya kuleta vifaa vya kisasa ili kuweza kuwasaidia wananchi kuleta tija ya uzalishaji mkubwa zaidi kwa sababu kwa sasa hivi kwa kutumia tu uchimbaji wa kawaida wa kienyeji tunazalisha zaidi ya chumvi tani 80,000? Ni lini Serikali sasa italeta vifaa vya kisasa ili kuweka tija ya kuzalisha zaidi na pia kuongeza soko la ndani pamoja na soko la nje? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naishukuru Serikali kwa kuja kutuletea semina kwa wachimbaji wetu wadogo ili kuweza kujua fursa za mikopo na mambo mengine. Je, ni lini sasa Serikali itakuja kuwapa elimu watu wetu wa Gendabi, Wilaya ya Hanang?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MADINI:** Mheshimiwa Spika, kuhusu kupeleka vifaa kuwasaidia wachimbaji wa Gendabi na Hanang kufanya uchimbaji wenye tija, napenda kumjulisha Mheshimiwa Mbunge huyu makini wa vijana ambaye ni msemaji mzuri wa

kundi analoliwakilisha Bungeni ambalo ni wananchi wa Mkoa wa Manyara kwamba, sasa hivi Wizara ya Madini kupitia Shirika lake la *STAMICO* lina programu maalum ya kujenga vituo vya mfano vya uchakataji madini kwa wachimbaji wadogo ikiweko chumvi.

Mheshimiwa Spika, mradi wa kwanza wa aina hiyo unakwenda kujengwa katika eneo la Nangurukuru, Lindi. Baada ya hapo nitumie nafasi hii kuwaagiza pia wafike kule Hanang waangalie wingi wa chumvi inayozalishwa hapo ili mtambo kama huo pia uweze kuwekezwa kule. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa swali lake la pili kwamba ni lini watakuja, nimhakikishie kwamba *STAMICO* wana *program* ya kuzunguka nchi nzima kutoa mafunzo. Niwaelekeze kwamba wawapatie kipaumbele wananchi wa Hanang ambao pia ni wachimbaji wazuri wa chumvi na tunahitaji wazalishe kwa tija, ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Kilimo, Mheshimiwa Japhet Ngailonga Hasunga, Mbunge wa Vwawa, sasa aulize swali lake.

Na. 208

**Mkakati wa Kutafuta Masoko ya Zao la Kahawa**

**MHE. JAPHET N. HASUNGA** aliuliza: -

Je, upi mkakati mahsusi wa Serikali wa kutafuta masoko ya zao la kahawa?

**SPIKA:** Naibu Waziri wa Kilimo, Mheshimiwa Silinde, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, tasnia ya kahawa inatekeleza Mkakati wa Miaka Mitano kwa Maendeleo ya Tasnia ya Kahawa (2021 – 2025). Malengo ya mkakati huo ni kuongeza wigo wa masoko,

kuongeza mauzo ya kahawa katika soko la ndani kutoka asilimia saba hadi asilimia 15 ya kahawa yote inayozalishwa nchini. Ili kutimiza lengo hili Serikali inafanya yafuatayo: -

(a) Kuweka mazingira mazuri ya biashara ili kuvutia uwekezaji kwenye viwanda vya kuongeza thamani yaliyopelekea ongezeko la viwanda kutoka 21 hadi kufikia viwanda 37 vilivyopo sasa;

(b) Kuongeza kodi kwa bidhaa za kahawa zinazotoka nje ya nchi kutoka 25% mpaka 35% ya thamani ya kahawa;

(c) Kubuni na kutengeneza migahawa inayotembea kwa kutumia pikipiki za miguu mitatu zitakazotumika katika uuzaji wa kahawa katika maeneo mbalimbali ya Umma na kwenye mikusanyiko ya watu; na

(d) Kuondoa kodi kwenye vifungashio vya kahawa ambavyo kwa kiasi kikubwa vinapatikana nje ya nchi.

**SPIKA:** Mheshimiwa Japhet Hasunga, swali la nyongeza.

**MHE. JAPHET N. HASUNGA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali. Upi mkakati wa Serikali wa kuvisaidia viwanda angalau vitatu katika hivyo 37 ili viweze kusindika kahawa, yaani kupata *instant coffee* ambayo inaweza ikakidhi mahitaji ya soko la ndani na nje ya nchi?

Mheshimiwa Spika, swali la pili; kwa kuwa sasa hivi dunia imebadilika, watu wanaingia mikataba ya baadaye, upi mkakati wa Serikali wa kuingia mikataba ya baadaye *(future and forward contract)* kupitia Bodi ya Kahawa na *TMX* ili kuwahakikishia wakulima kwamba bei zinajulikana miaka hata mitatu, minne ijayo? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge wa Jimbo la Vwawa kwamba moja ya mikakati ya Wizara ni kuongeza viwanda vitakavyopata ile *instant*

*coffee,* ile kahawa ambayo imeboreshwa zaidi ili iweze kutumika hapa nchini. Kwa hiyo, jambo hilo tunalo na ndiyo maana tuliitisha kwenye vikao vya wadau ili kuweza kujadili.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, sasa hivi tunachokifanya ni kutafuta namna bora ambayo tunaweza tukawafikia ikiwemo kutafuta fedha pamoja na mitambo ambapo angalau viwanda vitatu mpaka vitano tutaweza kuvisaidia ili kuzalisha kahawa yetu nchini.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili linalohusu mikataba ya baadaye ni jambo jema, nasi tumeliona ndiyo njia pekee ambayo tunaweza tukasaidia wakulima wetu na mauzo ya kahawa nje ya nchi. Kwa hiyo, jambo hili Mheshimiwa Hasunga sisi tumelipokea na tunalifanyia kazi. Tukishamaliza tathmini zetu, maana yake tutalileta kwenu wadau wa kahawa ili lianze kutekelezeka, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Sophia Mwakagenda, swali la nyongeza.

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA**: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kupata nafasi ya swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, zao la kahawa katika dunia ni zao ambalo linanunuliwa namba mbili, yaani baada ya petroli ni kahawa. Hamwoni sasa Serikali ina haja ya kuwekeza zaidi na kwa haraka zao hili ili liweze kupata viwanda, kama swali la msingi lilivyouliza katika Taifa letu la Tanzania hususani Nyanda za Juu Kusini?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, ni kweli tunatambua kwamba kahawa ni moja ya yale mazao yetu makubwa matano ambayo yanaingizia Serikali fedha za kigeni na ni moja ya zao ambalo sisi tumeliwekea msisitizo mkubwa. Katika kikao cha wadau wa kahawa, Mheshimiwa Sophia na Wabunge wengi tuliwaalika mwone namna bora ambavyo sisi Wizara tumejipanga kuhakikisha kwamba tunasogea mbele. Kwa hiyo,

tuna mkakati madhubuti kuhakikisha tunasaidia ikiwemo wananchi wa Nyanda za Juu Kusini, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Anatropia Theonest, swali la nyongeza.

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Mheshimiwa Spika, wakulima wa kahawa hupatwa na changamoto ya kupata fedha huku wakisubiri msimu kufika mwisho na kusababisha kukopa au kula kitu kinaitwa butura. Sasa nini mkakati wa Serikali kuwasaidia kuweza kupata fedha kabla ya msimu ili waweze kuandaa mashamba yao na pale wanapouza waweze kulipa tofauti na ilivyo leo ambavyo inatumika *system* ya butura? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, ndiyo maana sasa hivi minada ya kahawa inafanyika *online*. Moja ya masharti ambayo tumeyaweka ni kuhakikisha kwamba wanunuzi wa kahawa wanalipa ndani ya muda mfupi ili wakulima wetu na wafanyabiashara wa kahawa fedha zao zisiweze kuchukua muda mrefu au kukopwa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, jambo hilo lipo, lakini tutaongeza kasi zaidi ili wakulima wetu waweze kulipwa kwa wakati na kupata fedha, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea na Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Mheshimiwa Cecilia Daniel Paresso, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 209

**Kufikisha Mawasiliano ya Simu Vijiji Visivyo na Mawasiliano – Karatu**

**MHE. CECILIA D. PARESSO** aliuliza: -

Je, lini Serikali itafikisha mawasiliano ya simu katika vijiji visivyo na mawasiliano – Karatu?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Cecilia Daniel Paresso, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote *(UCSAF)* imejenga minara tisa ya mawasiliano ya simu katika Wilaya ya Karatu. Minara hiyo ilijengwa na *Vodacom* pamoja na *Halotel* katika Kata za Baray, Buger, Daa, Endabash, Endamarariek, Mang'ola, Mbulumbulu, Rhotia na Endamaghang. Miradi hiyo ilitekelezwa katika awamu kati ya Machi, 2013 na Desemba, 2018.

Mheshimiwa Spika, aidha, Serikali kupitia *UCSAF* iliingia makubaliano na Kampuni ya Simu ya *Vodacom* kufikisha huduma za mawasiliano katika Kijiji cha Endamaghang kilichopo katika Kata ya Endamaghang, ambapo mkataba ulisainiwa tarehe 13 Mei, 2023 kwa utekelezaji wa miezi 24.

Mheshimiwa Spika, kwa upande mwingine Serikali imeshafanya tathmini ya changamoto ya upatikanaji wa huduma ya mawasiliano katika maeneo ya Endesh, Karatu, Matala, Ziwa Manyara eneo la Endela, Ziwa Manyara eneo la Endabash, Tloma, Oldeani, Lositete, Kilimatembo na Masamburai. Miradi hii ya kufikisha huduma za mawasiliano inatekelezwa kwa kadiri ya upatikanaji wa fedha.

**SPIKA:** Mheshimiwa Cecilia Daniel Paresso, swali la nyongeza.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza.

(a) Mheshimiwa Spika, je, ni lini wananchi hawa katika maeneo haya ambayo tathmini imefanyika wategemee kwa uharaka kupata huduma hiyo ya mawasiliano?

(b) Mheshimiwa Spika, swali la pili, katika maeneo ambayo tayari minara imeshafungwa, bado kuna baadhi ya maeneo kuna uhafifu wa upatikanaji wa mawasiliano. Je, Serikali kwa kushirikiana na wadau, iko tayari kutathmini yale maeneo ambayo tayari yameshafungwa lakini kuna uhafifu wa mawasiliano?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Cecilia, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kuhusu lini waweze kutegemea kupata mawasiliano, tayari wataalamu wetu wanaendelea na michakato kadiri ya taratibu za kiserikali, na kabla ya mwakani maeneo mengi yatakuwa yamefikiwa na huduma ya mawasiliano.

Mheshimiwa Spika, maeneo ambayo minara ipo lakini kuna huduma hafifu, tayari wataalamu wetu wamefika huko na wameweza kufanya tathmini kwa nini maeneo yale yamekuwa na uhafifu wa mawasiliano. Katika baadhi ya maeneo imeonekana kuwa kuna jiografia ya miinuko, hivyo tunaangalia namna ya kuweka *buster stations* za kuwezesha mawasiliano hayo kufika hata kwenye maeneo ya mabonde na kwenye miinuko.

**SPIKA:** Mheshimiwa Fatma Toufiq, swali la nyongeza.

**MHE. FATMA H. TOUFIQ:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa ya kuuliza swali la nyongeza. Je, Serikali ina kauli gani kuhusu usimikaji wa minara katika Vijiji vya Sankwaleto na Gonga katika Wilaya ya Chemba? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Fatma Toufiq, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kauli ambayo Serikali tunaweza tukasema kwa maeneo haya aliyotaja Mheshimiwa Mbunge ni kwamba tutaendelea kuhakikisha tunakuja kusimika minara. Kwa pale ambapo minara imekwishasimikwa tutahakikisha kwamba inamaliziwa ili huduma ya mawasiliano iweze kuwa bora kwa wananchi wote.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo, Mheshimiwa Mwanakhamis Kassim Said, Mbunge wa Magomeni, sasa aulize swali lake.

Na. 210

**Kuhamasisha Timu ya Taifa ya Mpira wa Miguu**

**MHE. MWANAKHAMIS KASSIM SAID** aliuliza: -

Je, kuna mikakati gani ya kuhamasisha timu ya Taifa ili ifanye vizuri katika *AFCON* 2027 kama inavyofanyika kwa vilabu vya Yanga na Simba?

**SPIKA:** Naibu Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, Mheshimiwa Mwinjuma, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, nakushukuru, kwa niaba ya Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mwanakhamis Kassim Said, Mbunge wa Magomeni, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama unavyofahamu, nchi yetu kwa kushirikiana na nchi za Kenya na Uganda itakuwa mwenyeji wa mashindano ya *AFCON* 2027. Ili kuhakikisha timu ya Taifa inafanya vizuri katika mashindano hayo, Serikali imeweka mikakati

mbalimbali ikiwemo ujenzi wa viwanja vya mpira katika majiji ya Dodoma na Arusha, ukarabati wa viwanja vya Benjamin Mkapa na Uhuru, kuwatafuta na kuwaleta nchini wachezaji wenye asili ya Tanzania wanaoishi na kucheza nje ya nchi ili kuchezea timu ya Taifa, kuhakikisha timu ya Taifa inashiriki mechi za kirafiki na mataifa mbalimbali na kufanya kambi katika mazingira mazuri ili kuwa na maandalizi bora.

Mheshimiwa Spika, mikakati mingine ni kuwashirikisha wadau mbalimbali wa michezo kuchangia timu za Taifa kwa lengo la kuhakikisha upatikanaji wa rasilimali fedha za kugharamia timu za Taifa zinazoshiriki mashindano ya kimataifa, kuwa mwenyeji wa mashindano ya *CHAN* mwaka 2024 ambayo ni maandalizi kwa timu ya Taifa kuelekea *AFCON* 2027, kuajiri kocha na benchi la ufundi lenye sifa na uzoefu katika mpira wa miguu duniani na kuhudumia timu zote za Taifa zinazoshiriki mashindano ya kimataifa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mwanakhamis Kassim Said, swali la nyongeza.

**MHE. MWANAKHAMIS KASSIM SAID:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri. Ili mashindano haya yafane lazima nchi yetu iwe na timu itakayoshiriki. Naomba kuuliza:-

(a) Je, Serikali ina maandalizi gani ya kuisimamia timu yetu ya Taifa?

(b) Je, kuna juhudi gani zilizopo za kuwashirikisha wasanii ili kupata ushereheshaji? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru...

**SPIKA:** Nimeona umetikisa kichwa kidogo, swali la pili hujamsikia?

**NAIBU WAZIRI WA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Spika, la pili sijalipata vizuri.

**SPIKA:** Anasema kwamba wasanii mtawashirikishaje kwenye kusherehesha?

**NAIBU WAZIRI WA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Spika, kwanza Serikali inafahamu ulazima na umuhimu wa kuwahamasisha Watanzania ili kuwa na mashindano ya *AFCON* yatakayofana. Hakuna hamasa kubwa kama kuwa na timu bora ambayo inakwenda kushiriki mashindano haya, siyo kama washiriki, bali washindani.

Mheshimiwa Spika, kwa kufahamu hilo, Serikali kwa sasa inaandaa mkakati maalum kwa ajili ya kutengeneza timu yetu, siyo tu kwa ajili ya mashindano ya *AFCON* 2027 bali pia kwa mashindano yote mengine yatakayofuata ambayo Tanzania itakuwa inashiriki.

Mheshimiwa Spika, mkakati uliopo sasa hivi ni kutengeneza timu tatu za Taifa ambazo zitakuwa zinapishanishwa na umri. Ya kwanza itakuwa chini ya miaka 17 ambayo itapatikana kutokana na wachezaji watakaokuwa wanafanya vizuri kwenye UMISETA kila mwaka. Mpango wa Serikali ni kuwachagua wachezaji hao kama timu na kuwaweka kwenye shule moja ambazo tumeshaanza kuzibainisha ili wapate usimamizi wa Walimu magwiji katika mchezo wa mpira wa miguu na Serikali itakuwa inagharamia kwa 100% matunzo ya timu hii. Timu hii pia itapata mechi kadhaa za mazoezi na mafunzo ndani na nje ya nchi ili kuiimarisha.

Mheshimiwa Spika, pia katika umri huu tutakuwa tuna mpango wa kuwapeleka wachezaji kadhaa kila mwaka kuwatafutia vituo vya michezo kwenye nchi zilizoendelea kwenye mpira wa miguu na *academies* ambazo zimefanikiwa sana duniani ili kuhakikisha wanajifunza zaidi, wanaendeleza vipaji vyao na wanalelewa katika misingi ya mpira wa miguu tayari kuja kulitumikia Taifa muda utakapofika.

**SPIKA:** Ahsante sana, au bado la pili?

**NAIBU WAZIRI WA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Spika, hata la kwanza sijamaliza.

**SPIKA:** Haya malizia.

**NAIBU WAZIRI WA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Spika, timu ya pili itakuwa ni chini ya umri wa miaka 23 ambayo itakuwa ikipatikana kutokana na wachezaji wanaocheza ligi kuu, ligi daraja la kwanza pamoja madaraja mengine ya chini; vilevile na mashindano yasiyo rasmi kama *Ndondo Cup* na wachezaji wenye asili ya Kitanzania wanaocheza mpira nje ya nchi. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, timu hii kwa sababu itakuwa inashirikisha wachezaji wengi ambao wanashiriki katika ligi rasmi itakuwa ikikutana kila wakati kunapokuwa na mapumziko ya ligi hizo. Timu hii nayo itakuwa ikigharamiwa na kusimamiwa kwa 100% na Serikali.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ameshaelewa majibu.

**MHE. NAIBU WAZIRI WA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Spika, kuhusiana na swali lake la pili, kwa sasa tunachofanya ni kuandaa mpango maalum wa kuwashindanisha wasanii kutengeza nyimbo maalum kwa ajili ya *AFCON*. Msanii atakayeshinda wimbo wake, utakuwa wimbo maalum kwa *AFCON*. Huu ni mpango wa kwanza, lakini kuna maeneo mengi ambayo tunataka kuwashirikisha wasanii kwa ajili ya kufanya *AFCON* 2027 kufana, ahsante.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge wawili mliosimama, ulizeni maswali kwa kifupi. Mheshimiwa Angelina Malembeka.

**MHE. ANGELINA ADAM MALEMBEKA:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa timu ya *Bunge Sports* huwa inashiriki mashindano mbalimbali ndani na nje ya nchi na hutuletea ushindi mkubwa, kwa maana ya makombe na medali mbalimbali, je, ni lini Wizara itatambua mchango wa *Bunge Sports* kwa timu nzima na watu mmoja mmoja waliotuletea ushindi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa swali hili la nyongeza. Ukweli ni kwamba, Wizara na Serikali inatambua mchango mkubwa unaoletwa na timu za Waheshimiwa Wabunge kwa kushinda mashindano mbalimbali ambayo Bunge hili linashiriki. Kwa kulifahamu hilo, tumepanga kwamba mwaka huu tutashirikiana na ofisi yako ili kuhakikisha kwamba maandalizi ya *Bunge Sports Club* yanafanyika kwa umakini zaidi ili kuweza kushinda zaidi.

**SPIKA:** Mheshimiwa Yahaya Massare, swali kwa ufupi.

**MHE. YAHAYA O. MASSARE:** Mheshimiwa Spika, historia inatuonesha kwamba mashindano ya Taifa ndiyo huleta na kufanya timu ya Taifa ya Tanzania hasa mwaka 1980 kule nyuma wakati tunashiriki kwa mara ya kwanza *Taifa CUP,* ndiyo ilikuwa inatoa wachezaji wa timu Taifa...

**SPIKA:** Mheshimiwa swali lako.

**MHE. YAHAYA O. MASSARE:** Mheshimiwa Spika, je, Serikali iko tayari sasa kuanzisha mashindano ya *Taifa CUP under 17, under 23* na mashindano ya watu wakubwa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri nadhani majibu yako ya swali la nyongeza la kwanza la muuliza swali yanajibu swali la Mheshimiwa Mbunge. Kwa hiyo, tutamtafutia *Hansard,* tutampatia Mheshimiwa Mbunge.

**NAIBU WAZIRI WA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

**SPIKA:** Ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Mheshimiwa Atupele Fredy Mwakibete, Mbunge wa Busokelo, swali lake litaulizwa kwa niaba yake na Mheshimiwa Masache Njelu Kasaka. *(Makofi)*

Na. 211

**Kukuza Vipaji kwa Watanzania Waliogundua Teknolojia Mbalimbali**

**MHE. MASACHE N. KASAKA K.n.y. MHE. ATUPELE F. MWAKIBETE** aliuliza: -

Je, Serikali imejipangaje kukuza vipaji kwa Watanzania waliogundua teknolojia mbalimbali hapa nchini?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Mheshimiwa Kipanga, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua umuhimu wa elimu, ujuzi na ubunifu katika kumwezesha mtu kumudu mazingira yake ikiwemo kupata mahitaji ya kijamii na kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, kwa kutambua umuhimu wa kukuza ubunifu na ugunduzi katika kuongeza kasi ya maendeleo nchini, Serikali imeandaa Mwongozo wa Kitaifa wa Kutambua na Kuendeleza Ugunduzi, Ubunifu na Maarifa Asilia wa Mwaka 2018 ambao unasaidia Serikali na taasisi husika kutoa huduma bora kwa wananchi wanaojishughulisha na mambo ya teknolojia na ubunifu wakiwemo wagunduzi wa teknolojia mbalimbali. Hii ni pamoja na kupata maelekezo na miongozo sahihi ya sehemu za kupata huduma zinazohusiana na sayansi, teknolojia na ubunifu.

Mheshimiwa Spika, aidha, Serikali imeanzisha Mashindano ya Kitaifa ya Sayansi, Teknolojia na Ubunifu yajulikanayo kama MAKISATU kwa lengo la kuibua na kuendeleza bunifu na teknolojia zinazozalishwa nchini. Mathalan, bunifu na teknolojia 283 zilizoibuliwa kupitia MAKISATU zinaendelezwa na Serikali kupitia Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia *(COSTECH)* ambapo bunifu 42 kati ya hizo zimefikia hatua ya kuingia sokoni.

**SPIKA:** Mheshimiwa Masache Njelu Kasaka, swali la nyongeza.

**MHE. MASACHE N. KASAKA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali. Nina maswali madogo mawili ya nyongeza. Kuendeleza ubunifu kunahitaji uwekezaji wa kutosha: -

(a) Je, Serikali imejipangaje juu ya uwekezaji kwenye bunifu hizi?

(b) Je, Serikali haioni haja ya kuweka mitaala ya wabunifu wakati huu ambapo Serikali inaboresha mitaala, ili kuwaendeleza wabunifu wetu?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Kasaka, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kwenye eneo la kwanza, kuhusiana na Serikali kufanya uwekezaji, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tayari Serikali imefanya uwekezaji mkubwa sana kwenye upande huu wa ubunifu. Kwanza naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tumeanzisha mfuko maalum ambao tutahakikisha kwamba tunakusanya fedha kwa ajili ya kuhakikisha kwamba bunifu hizi zinaweza kufadhiliwa.

Mheshimiwa Spika, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge na Bunge lako Tukufu kwamba mpaka kufikia mwaka wa fedha 2022/2023 jumla ya fedha za Kitanzania shilingi bilioni 64.9 zimeelekezwa au kugawanywa kwenye bunifu mbalimbali kwa ajili ya kuziendeleza.

Mheshimiwa Spika, eneo la pili ambalo linakwenda sambamba na mikakati yetu kama Serikali ni kuanzisha vituo atamizi katika vyuo vyetu vikuu vyote nchini; ambapo tutahakikisha kwamba zile bunifu tukishazipata tunazipeleka huko kwa ajili ya kuendelea kufanyiwa utafiti na kuendelezwa.

Mheshimiwa Spika, kwenye halmashauri zetu katika shule zetu za msingi, sekondari na vyuo vyetu vya kati tumeweza kuanzisha madawati mbalimbali kama mkakati wa kuhakikisha

kwamba tunaibua bunifu hizi huko ziliko na kuzileta huku juu kwa ajili ya kuziendeleza.

Mheshimiwa Spika, eneo la pili ni kuhusiana na mitaala yetu. Mwaka 2023 tulipitisha mitaala pamoja na Sera yetu ya Elimu ambayo inatambua fani na kada mbalimbali ikiwemo na hii ya ubunifu. Kwa hiyo, kwenye mtaala wetu tumezingatia. Kwa vile sasa hivi ndiyo tunaanza kutekeleza matokeo ya mtaala huu, yatakuja kuonekana baada ya kukamilisha mzunguko wenyewe kamili.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Tunaendelea na Wizara ya Maji, Mheshimiwa Kasalali Emmanuel Mageni, Mbunge wa Sumve, sasa aulize swali lake.

Na. 212

**Usambazaji wa Maji kutoka Ziwa Victoria – Sumve**

**MHE. KASALALI E. MAGENI** aliuliza: -

Je, lini Serikali itaanza kusambaza maji ya bomba kutoka Ziwa Victoria katika vijiji vyote vya Jimbo la Sumve?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Kasalali Emmanuel Mageni, Mbunge wa Jimbo la Sumve, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Jimbo la Sumve lina vijiji 59 ambapo kati ya hivyo vijiji 13 vinapata huduma ya majisafi na salama kupitia mtandao wa bomba, vijiji 39 vinapata huduma kupitia pampu za mkono, na vijiji saba vikiwa havina huduma.

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea na utekelezaji wa mradi wa kutoa maji Ziwa Victoria kwenda Miji ya Usagara,

Ukiliguru, Sumve hadi Kolomije, na vijiji 24 vya Wilaya za Misungwi na Kwimba, ikiwa ni jitihada za kuboresha huduma ya maji katika Wilaya hizo, ikiwemo Jimbo la Sumve. Mradi huo unahusisha ujenzi wa chanzo cha maji, matanki sita yenye jumla ya ujazo wa lita milioni 5.63, mtambo wa kusafisha na kutibu maji, vituo 80 vya kuchotea maji, jengo la pampu, nyumba moja ya watumishi na ofisi mbili za *CBWSO*, ununuzi na ufungaji wa pampu na ulazaji wa mabomba ya usambazaji maji umbali wa kilometa 261.1.

Mheshimiwa Spika, hadi sasa utekelezaji wa mradi huo umefikia wastani wa asilimia 30 ambapo unatarajiwa kukamilika mwezi Machi, 2025. Mradi huu utakapokamilika utanufaisha wakazi takribani 162,377 wakiwemo wananchi 47,122 wa Jimbo la Sumve.

**SPIKA:** Mheshimiwa Kasalali Mageni, swali la nyongeza.

**MHE. KASALALI E. MAGENI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru.

(a) Je, ni lini Serikali itatimiza ahadi yake ya kuchimba visima na kusambaza maji katika Vijiji vya Ngogo, Mwabuchuma, Shilanona, Nanyambu, Busule, Nkungulu na Mwaswengele vinavyopatikana katika Jimbo la Sumve?

(b) Je, ni lini Serikali itakamilisha miradi ya kusambaza maji katika vijiji vya Lyoma na Sumaha ambavyo mpaka sasa miradi haijakamilika kwa sababu tunasikia pampu hazijafika *site*?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa visima vitano katika Vijiji vya Ngogo, Busule, Nkungulu, Shilanona na Nanyambu unatarajiwa kuanza mwezi Mei. Mradi huo utahusisha uchimbaji na kujenga miundombinu kama tanki, kulaza mabomba pamoja na vituo vya kuchotea maji.

Mheshimiwa Spika, mradi huu unaendelea katika maeneo mbalimbali nchini yakiwepo hata maeneo ya Wilaya ya Rungwe ikiwepo katika Kata ya Kisondela katika Kijiji cha Mpuga na Isuba. Mradi huu unatarajiwa kukamilika katika mwaka wa fedha unaokuja.

Mheshimiwa Spika, kipengele cha pili kwa upande wa *pump* katika Vijiji vya Uwala, Sumaha pamoja na Dioma, nitumie fursa hii kumwelekeza *RM* wa Mwanza kuhakikisha anamwelekeza mkandarasi wetu ahakikishe kwamba anakamilisha ufungaji wa *pump* kabla ya mwezi wa Saba kwa sababu mkandarasi huyu alishalipwa pesa.

Mheshimiwa Spika, pia nitumie fursa hii kuwaomba wakandarasi wengine wote ambao tayari wameshalipwa fedha lakini wamekuwa wakijificha kwenye kivuli cha kwamba wakandarasi hatujalipwa; wakandarasi wengi tumewalipa na naomba wakae *site*. Wasipokuwepo, tukianza kwenda huko *site,* kwa kweli patachimbika kwa sababu tunataka Watanzania wapate maji.

**SPIKA:** Haya, ahsante sana. Mheshimiwa Agnes Elias Hokororo, Mbunge wa Viti Maalum, swali lake litaulizwa na Mheshimiwa Yahya Mhata.

Na. 213

**Ujenzi wa Bwawa la Lukuledi na Mtambaswala Mtwara**

**MHE. YAHYA A. MHATA K.n.y. MHE. AGNES E. HOKORORO** aliuliza: -

Je, lini Mabwawa ya Lukuledi na Mtambaswala yatajengwa – Mtwara?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, Bwawa la Lukuledi lililopo Wilaya ya Masasi Mkoani Mtwara ni moja ya bwawa lililo katika mpango wa kufanyiwa usanifu wa kina na Serikali katika mwaka wa fedha 2024/2025. Aidha, taratibu za ujenzi wa bwawa hilo zitaanza mara baada ya kukamilika kwa usanifu.

Mheshimiwa Spika, vilevile kwa upande wa Mtambaswala, Serikali imepanga kufanya tathmini ya kitaalamu katika mwaka wa fedha 2024/2025 kuona kama katika eneo hilo kuna uwezekano wa kujenga bwawa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Yahya Mhata, swali la nyongeza.

**MHE. YAHYA A. MHATA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Serikali, naomba kuuliza swali moja tu la nyongeza. Kwa kuwa katika bajeti ya mwaka 2023/2024 mabwawa haya yalipangiwa bajeti yake, sasa majibu ya Mheshimiwa Waziri kwamba usanifu huu utafanyika katika mwaka ujao wa fedha, je, haoni kwamba bajeti ile ambayo ilipangiwa mabwawa haya haikutumika vizuri?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa miradi ya maji una *study* mbili; kuna *feasibility study*, ambayo inahitaji kutengewa fedha, inafuatiwa na usanifu wa kina, napo tunatenga fedha. Baada ya hapo, maana yake mradi uko tayari sasa kwa ajili ya kutafutiwa fedha ili uweze kutekelezwa.

Mheshimiwa Spika, namwomba Mheshimiwa Mbunge tutakapotoka hapa tuweze kuwasiliana na kuona ni namna gani Serikali itaenda kuangalia njia mbadala kuhakikisha tunaharakisha utekelezaji wa mradi huu ili Watanzania na wananchi wa Mkoa wa Mtwara wapate maji safi na salama na waweze kuwa wanafanya shughuli zao za kila siku.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Tecla Mohamedi Ungele, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake. *(Makofi)*

Na. 214

**Ujenzi wa Vituo vya Polisi Njinjo na Kibutuka – Lindi**

**MHE. TECLA. M. UNGELE** aliuliza: -

Je, lini Serikali itajenga Vituo vya Polisi Njinjo – Kilwa na Kibutuka – Liwale?

**SPIKA:** Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Sillo, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, Serikali imetenga eneo kwenye Kata ya Njinjo lenye ukubwa wa meta za mraba 3,034.5 na Kata ya Kibutuka lenye ukubwa wa meta za mraba 2,023.5 kwa ajili ya ujenzi wa vituo vya polisi vya kata. Ujenzi wa vituo hivyo umeshaingizwa kwenye mpango wa ujenzi wa vituo vya polisi vya kata vitakavyojengwa nchi nzima na Ofisi ya Rais, TAMISEMI kuanzia mwaka wa fedha 2024/2025.

**SPIKA:** Mheshimiwa Tecla Ungele, swali la nyongeza.

**MHE. TECLA M. UNGELE:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa majibu ya Serikali. Umbali wa kutoka Kilwa Masoko kwenda Liwale ni kilometa 261 na ndiyo maana nimeomba kujengwa Kituo cha Polisi hapo Njinjo. Umbali wa kutoka Nachingwea kwenda Liwale ni kilometa 131, je, Serikali ipo tayari kuambatana nami kwenda kuangalia na kushuhudia adha wanayopata kule kwa ajili ya usalama wa wananchi katika maeneo hayo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia kama majibu yalivyotolewa, tunaomba kipaumbele kiwekwe kwa vituo hivyo kujengwa haraka iwezekanavyo. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Tecla, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza la kuongozana kwenda kwenye maeneo tajwa, namhakikishia kwamba baada ya Bunge la bajeti niko tayari kuongozana na Mheshimiwa Mbunge ili kuona uhalisia wa umbali wa maeneo aliyoyataja na kuona ujenzi wa vituo hivyo unaenda mara moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili kuhusu *commitment* ya Serikali, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kama nilivyosema kwenye jibu la msingi, katika mwaka huu wa fedha 2024/2025 vituo vya polisi alivyotaja, vinaanza kujengwa kwenye Kata ya Njinjo pamoja na Kata ya Kibutuka, kama ambavyo nimejibu kwenye jibu la msingi.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea na Wizara ya Afya, Mheshimiwa Amour Khamis Mbarouk, Mbunge wa Tumbe, sasa aulize swali lake.

Na. 215

**Sheria ya Kuzuia Uvutaji wa Sigara Hadharani**

**MHE. AMOUR KHAMIS MBAROUK** aliuliza: -

Je, lini Serikali italeta Sheria ya Kuzuia Uvutaji wa Sigara na mazao mengine ya Tumbaku hadharani?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Amour Khamis Mbarouk, Mbunge wa Tumbe, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, tayari Serikali ilishapitisha Sheria ya Udhibiti wa Tumbaku ijulikanayo kama *"The Tobacco Products Regulation Act, 2003"* ambayo imetoa katazo la uvutaji wa sigara hadharani. Pia sheria hiyo imezuia matangazo ya tumbaku na bidhaa zitokanazo na tumbaku kwenye maeneo ya umma ikiwemo vyombo vya habari, *billboards* na kwenye matamasha mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**SPIKA:** Kabla sijampa mwenye swali nafasi ya kuuliza swali la nyongeza, Mheshimiwa Naibu Waziri, jibu lako linasema tayari Serikali ilishapitisha sheria. Serikali inapitishaje sheria Mheshimiwa Waziri? Hebu fanya hayo marekebisho hapo halafu nimpe nafasi ya kuuliza maswali ya nyongeza mhusika.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, tayari Bunge limeshapitisha Sheria ya Udhibiti wa Tumbaku ijulikanayo kama "*The Tobacco Products Regulation Act, 2003.*"

Mheshimiwa Spika, niishie hapo?

**SPIKA:** Ishia hapo hapo, umeshaeleweka, lakini ni Bunge limeshatunga sheria. Bunge limeshatunga sheria, Bunge halipitishi sheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Amour, swali la nyongeza.

**MHE. AMOUR KHAMIS MBAROUK:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri. Mimi nauliza maswali mawili. Sheria hiyo itaanza kutumika lini? Kwa sasa ni ipi kauli ya Serikali kwa wale wanaotoa huduma wakati huo huo wanaendelea kuvuta sigara? Anauza *chips* na sigara mdomoni.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nampongeza Mheshimiwa Mbunge kwa kuling'amua hili eneo muhimu sana ambalo linachangia kwa kiasi kikubwa sana kwenye magonjwa yasiyoambukiza. Likiguswa vizuri, tutapunguza matatizo makubwa sana na tutapunguza gharama kubwa ambazo Serikali inaingia sasa hivi katika kutibu magonjwa mbalimbali yasiyoambukizwa ambayo yanachangiwa na eneo hili.

Mheshimiwa Spika, nikijibu maswali yake mawili; moja, sheria hiyo imeanza kutumika, siyo kwamba haitumiki, lakini suala ni kwamba tuiongezee nguvu na sasa tuanze kutumia nguvu zaidi na kuwa makini katika kufuatilia mambo haya.

Mheshimiwa Spika, pili, tamko letu ni nini? Tamko letu ni moja, wote tunajua madhara na wote wakati wote tumekuwa tukielezwa madhara yanayotokana na tumbaku. Kwa hiyo, wote tuwe mabalozi wa kuhakikisha tunahamasisha jamii kulikataa hilo.

Mheshimiwa Spika, kuna mikoa ambayo tukianzisha mjadala wa kusema sasa tunaacha tumbaku, Wabunge humu ndani tunaweza tukagawanyika makundi mengi sana. Kwa hiyo, hapo kuna changamoto pia. Kwa hiyo, tuendelee kuhamasishana wakati kwa pamoja tunatafuta njia mbadala kwa maeneo yanayolima tumbaku wapate mazao gani mbadala ya kibiashara.

Mheshimiwa Spika, pia, ni tatizo la kidunia kwa sababu duniani kote wanatumia zaidi ya dola trilioni 1.4 kutatua tatizo hili na kila mahali wanapambana. Sisi Tanzania tunaathirika kama dunia inavyoathirika, kwa hiyo, wote pamoja tupambane nalo na tuelewe namna ya kufanya.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea na Wizara ya Ujenzi, Mheshimiwa Zaytun Seif Swai, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 216

**Ujenzi wa Daraja la Mto Athumani – Ngorongoro**

**MHE. ZAYTUN S. SWAI** aliuliza: -

Je, Serikali haioni haja ya kujenga Daraja la Mto Athumani - Ngorongoro ili kunusuru maisha ya wananchi nyakati za mvua?

**SPIKA:** Naibu Waziri wa Ujenzi, Mheshimiwa *Engineer* Msongwe, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, daraja la Mto Athumani liko katika barabara ya mkoa ya Mto wa Mbu – Selela – Engaruka – Ngaresero – Sale – Wasso hadi Loliondo yenye urefu wa kilometa 217 katikati ya Kijiji cha Selela na Engaruka mkoani Arusha. Maandalizi ya Ujenzi kwa kiwango cha lami, sehemu ya barabara ya kutoka Selela hadi Engaruka yenye urefu wa kilometa 27, ikiwemo ujenzi wa daraja la Mto Athumani yanaendelea. Kazi za ujenzi zimepangwa kuanza katika mwaka wa fedha 2024/2025.

**SPIKA:** Mheshimiwa Zaytun Swai, swali la nyongeza.

**MHE. ZAYTUN S. SWAI:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu ya Serikali, wananchi wa Wilaya za Monduli na Ngorongoro wanataka kusikia ni lini daraja katika Mto Athuman litajengwa. Je, ni upi mkakati wa muda mfupi wa Serikali kujenga daraja la muda ili barabara hii iweze kupitika?

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili; ni upi mkakati wa Serikali kutumia rasilimali zilizopo kama mawe katika ujenzi wa madaraja kama haya ili kuokoa gharama za ujenzi kwa Serikali?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, naomba kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge na Wananchi husika wa maeneo hayo kwamba daraja la Mto Athuman limepewa kipaumbele sana na Serikali hasa ikizingatiwa kwamba ndiyo daraja ambalo linakwenda kwenye kiwanda ambacho kinajengwa cha magadi.

Mheshimiwa Spika, tunavyoongea, tayari Wizara imeshapeleka maombi ya fedha isiyopungua shilingi bilioni 6.6 kwa ajili ya kuanza ujenzi wa haraka wa daraja hilo pamoja na madaraja mengine madogo ambayo yatakuwa 13. Kwa hiyo, tunalichukua kwa umuhimu mkubwa kuhakikisha kwamba tunalijenga.

Mheshimiwa Spika, kuhusu rasilimali mawe, nataka kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba teknolojia hiyo ipo inafahamika na inatumika. Hata hivyo, ninachotaka kukuhakikishia Mheshimiwa Mbunge ni kwamba mawe yana ubora wake, siyo kila mawe yaliyopo mahali popote pale unaweza ukajenga. Ndiyo maana unaweza ukaona barabara inajengwa, natoa mfano, Mkoa wa Lindi, lakini kokoto tukachukua Goba kwa sababu ya ubora wake.

Mheshimiwa Spika, daraja linahitaji mawe ambayo ni bora sana. Pale ambapo mawe yanafaa, na daraja ni la kawaida, tunatumia teknolojia hiyo na tumeendelea kufanya hivyo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Spika, hoja ya dharura.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa kipindi cha Maswali kutoka kwenu na Majibu kutoka upande wa Serikali. Kabla sijaleta tangazo la wageni nililonalo hapa mbele, mambo ya msingi kuhusu maswali ambayo tulishayazungumza mara kadhaa na tunaendelea kukumbushana, Mheshimiwa *Chief Whip*, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge na Uratibu tafadhali tufikishie ujumbe huu kwa wanaojibu maswali hapa mbele.

Kwanza, ile ya "kwa niaba ya Waziri," anapokuja kujibu swali hapa, tayari tunajua yeye ni kwa niaba. Kwa hiyo, asitusomee kwa sababu muda ni ule ule na Wabunge wengi wanahitaji kuuliza maswali inatupotezea muda. Kwa niaba, waanze pale Serikali inaanza, majibu yasomwe kama majibu. Yale ya "kwa niaba" yabaki kwenye karatasi.

Pili, tusaidie wanapojibu, kwa sababu mimi nikishamtambua Mbunge nimeshamtambua huyo Mbunge, Waziri atumie muda mfupi badala ya kuanza tena, naomba kujibu swali la Mheshimiwa fulani, ambaye mimi nimeshamtaja. Kwa sababu yeye hawezi kumtaja kama mimi sikumtaja. Kwa kuwa nakuwa nimeshamtaja, basi tupunguze ule muda wa kuanza tena kumtambua Mbunge mara kumi kumi wakati ameshatajwa na anayekuwa amekaa hapa mbele.

Kwa hiyo, haya nilishayasema huko nyuma, narejea tena kwamba Wabunge ni wengi kama sisi wote tunavyowaona kwamba huwa wanasimama kuhitaji maswali na muda wetu hautoshi kwa sababu ni saa moja. Kwa hiyo, tunajaribu kupunguza wingi wa maneno ili tumpe nafasi Mbunge anayetaka kuwakilisha wananchi wake kwa kupitia maswali.

Waheshimiwa Wabunge, jambo lingine ni shukrani zenu. Anayekuwa amekuja kukaa hapa mbele, tayari anawashukuru. Kwa hiyo, ninyi mpunguze zile "nakushukuru Mheshimiwa Spika kwa muda. Zile sekunde zinaweza zikatumika na Mheshimiwa Mbunge mwingine zikikusanywa kwenye kuuliza swali.

Kwa hiyo na shukrani zile zote zinakuwa zimeshapokelewa. Hivyo usiwe na wasiwasi, ukishatajwa, nenda moja kwa moja kwenye swali, itatusaidia Waheshimiwa Wabunge wengi kupata nafasi ya kuuliza. Kama leo Waheshimiwa Wabunge wengi wamesimama, lakini hawajapata nafasi ya kuuliza kwa sababu ya muda tulionao. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, nina tangazo la wageni hapa na tangazo lingine linatoka kwa Katibu wa Bunge. Kwanza, tangazo la wageni, tutaanza na wageni waliokaa jukwaa la Spika, ambao ni wageni wa Mheshimiwa Antony Peter Mavunde, Waziri wa

Madini. Tutaanza na Bwana Kheri Mahimbali ambaye ni Katibu Mkuu, karibu sana. *(Makofi)*

Vilevile yupo pia Bwana Msafiri Mbibo ambaye ni Naibu Katibu Mkuu, yupo Meja Jenerali Mstaafu Michael Isamuhyo ambaye ni Mwenyekiti wa Bodi *STAMICO*, yupo Profesa Justian Ikingula ambaye ni Mwenyekiti wa Bodi *GST*, yupo Bwana Augustine Ollal ambaye ni Mkurugenzi wa Sera na Mipango, karibuni sana. *(Makofi)*

Pia yupo Bi. Monyshoze Mazanda ambaye ni Mjumbe wa Baraza Kuu, UVCCM Taifa, karibuni sana. *(Makofi)*

Wengine ni Bwana Charles Saimon Mamba ambaye ni Mwenyekiti wa CCM Wilaya ya Dodoma, yupo pia Bi. Sofia Abdallah Kibaba ambaye ni Katibu wa CCM Wilaya ya Dodoma na pia yupo Bwana Aman Hamza Mulagizi, Katibu Mwenezi wa CCM, Wilaya ya Dodoma, karibuni sana. *(Makofi)*

Tuna wageni mbalimbali wa kwenu Waheshimiwa Wabunge, tutaanza na mgeni wa Mheshimiwa Ramadhani Ighondo ambaye ni mdogo wake kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma. *(Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa Francis Ndulane ambaye ni mdau wa maendeleo Wilaya ya Kilwa, Mkoani Lindi. *(Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa Abdallah Chaurembo mpiga kura wake kutoka Mbagala. *(Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa Ng'wasi Kamani ni Mkufunzi wa Chuo cha Mipango Dodoma. *(Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa Florent Kyombo, mpiga kura wake kutoka Nkenge, Mkoa wa Kagera. *(Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa Dkt. Ritta Kabati ambaye ni mdogo wake kutoka Arusha. *(Makofi)*

Wapo wageni wanne wa Mheshimiwa Saashisha Mafuwe ambao ni wanafunzi wenzake wa Shahada ya Uzamili kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma. *(Makofi)*

Wageni 21 wa Mheshimiwa Hussein Nassor Amar ambao ni wanafunzi wa Vyuo Vikuu na Kati vya hapa Jijini Dodoma kutoka Nyang'hwale, Mkoa wa Geita, karibuni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Hussein Nassor Amar anao wageni wengine ambao ni wanafunzi 100 na walimu nane kutoka Shule ya Sekondari ya Jamhuri ya Jijini Dodoma, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni wawili wa Mheshimiwa Zuberi Kuchauka ambao ni wanafunzi wa Chuo Kikuu Mzumbe, wanaotoka Morogoro. *(Makofi)*

Tunao wageni watatu wa Mheshimiwa Dkt. Florence Samizi ambao ni Askofu na Wachungaji kutoka Muhambwe, Mkoa wa Kigoma, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni kumi wa Mheshimiwa Mwantatu Mbaraka Khamis ambao ni viongozi wa Chama cha Mazingira na Ufugaji Tija, Tanzania kutoka Zanzibar. *(Makofi)*

Wapo wageni 16 wa Mheshimiwa Mohamed Monni ambao ni wanafunzi wa Chuo cha Elimu ya Biashara *(CBE)* kutoka Wilaya ya Chemba, Mkoani Dodoma. *(Makofi)*

Wengine ni wageni 110 wa Mheshimiwa Husna Sekiboko ambao ni viongozi wa Umoja wa Wanawake Tanzania kutoka Wilaya ya Lushoto, Mkoa wa Tanga, ahsante sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tangazo lingine linatoka kwa Katibu wa Bunge, mnatangaziwa kwamba leo tarehe 30 Aprili, 2024 kutakuwa na semina kuhusu Tathmini ya Maendeleo ya Sekta ya Kilimo nchini itakayotolewa na Wizara ya Kilimo. Semina hii itafanyika saa 7.00 mchana ukumbi wa Pius Msekwa. Waheshimiwa Wabunge, wote mnakaribishwa kuhudhuria semina hii muhimu kwa ajili ya kupata uelewa wa mpango wa mageuzi ya kilimo na kilimo cha umwagiliaji nchini. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya matangazo hayo, tunaendelea na ratiba yetu.

**MHE. BAHATI K. NDINGO:** Mheshimiwa Spika, hoja ya dharura.

**SPIKA:** Hoja ya dharura, Mheshimiwa Bahati Ndingo.

## HOJA YA DHARURA

**MHE. BAHATI K. NDINGO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipatia fursa. Tunayo dharura kubwa ambayo imeendelea kudumu kwa muda mrefu, lakini sasa hali imezidi kuwa mbaya. Ndani ya Wilaya ya Mbarali, Kata ya Igava, katika vijiji vinne, hali ya kuzagaa kwa tembo imekuwa ni ngumu kwetu. Jambo hili nimeliripoti takribani miezi mitatu. Nimeshaliripoti kwa Mheshimiwa Waziri, lakini bado hatua stahiki hazijachukuliwa.

Mheshimiwa Spika, mbaya zaidi, usiku wa kuamkia jana na leo, wananchi wa Kata ya Igava wameshindwa kurudi majumbani mwao wakiongozwa na Mheshimiwa Diwani kutokana na tembo kuzagaa, lakini mbaya zaidi, tembo hao wamekuwa wakizagaa mpaka kwenye maeneo ya shule. Watoto waliopo kwenye Kata ya Igava hawaendi shuleni sasa hivi. Ndani ya vijiji hivi vinne, Kijiji cha Igunda, Kijiji cha Ikanutwa, Kijiji cha Igava na Kijiji cha Iwalanje, mazao yote ya mahindi yameshaliwa na tembo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wananchi hawana chakula na kuanzia mwishoni mwa wiki iliyopita wameanza kuhamia kula mpunga ambao umekauka. Hali ya wasiwasi kwa wananchi ni kubwa na hawafanyi shughuli yoyote zaidi ya kujilinda na kulinda familia zao dhidi ya tembo. Kwa hali ilipofikia, tunahitaji kuona Serikali inalichukua jambo hili kwa dharura. Wananchi wa Igava na maeneo mengine mengi wana changamoto kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa udharura wa jambo hili, naomba Waheshimiwa Wabunge wenzangu waniunge mkono tuweze kulijadili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa tuketi.

Waheshimiwa Wabunge, amesimama Mheshimiwa Bahati Keneth Ndingo kuhusu Hoja ya Dharura, Kanuni inayohusika…

Waheshimiwa Wabunge, mnaozungumza tusikilizane, ahsanteni sana.

Kanuni ya 54 inaeleza kuhusu Kuahirisha Shughuli za Bunge, ili kujadili jambo la dharura na kanuni hiyo inataka nikishamsikiliza Mheshimiwa Mbunge nifanye tathmini ya hilo jambo kama ni dharura au hapana. Nikishajiridhisha kama ni dharura, ndiyo Mheshimiwa Mbunge anapewa nafasi ya kutoa hoja yake ili Waheshimiwa Wabunge wamuunge mkono.

Kwa hiyo, ni lazima niwe nimempa nafasi ya kutoa hiyo hoja, japo niliwaona mmesimama, ndiyo maana nikasema tuketi, lakini Kanuni ya 55 inaweka masharti ya jumla kuhusu jambo la dharura na mazingira ambayo jambo linaweza kuhesabika kuwa la dharura.

Pia inaeleza ni jambo la aina gani linaweza kuwa jambo la dharura. Sasa Mheshimiwa Mbunge hapo ameeleza madhara ambayo wananchi wa Mbarali wanayapata, lakini katika kueleza kwake kwa sehemu, akasema pia athari hizo ziko sehemu mbalimbali. Nimetazama, baadhi ya Waheshimiwa Wabunge, waliokuwa wamesimama ni wale ambao wanapata hizo changamoto za kuzagaa kwa tembo ama ndovu katika maeneo yao.

Waheshimiwa Wabunge, tutakumbuka miezi kadhaa ya hapo nyuma, Serikali ilichukua hatua mbalimbali ilipopata taarifa juu ya kuzagaa kwa tembo katika maeneo yetu ya uwakilishi na maeneo mengine, ilibidi zitumwe ndege. Kwingine walitumwa wale wataalamu ili kwenda kuwasogeza hao ndovu ama tembo kwenye maeneo yao.

Sasa nilikuwa najaribu kutazama upande wa Serikali, simwoni Mheshimiwa Naibu Waziri. Ama yupo mimi ndio simwoni! Hata Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii, wote hawapo!

Kwa kutokuwepo kwao, hoja hii hata nikiitoa tuijadili, kidogo hatua zile za kuchukua inaweza kuwa hatuna hakika na Serikali inafanya nini kwenye hayo maeneo kwa sasa. Kwa hiyo, wangekuwepo ningewasikiliza tuone Serikali inafanya nini kwa sasa. Ila kwa sababu tuko hapa Bungeni bado, naamini Mheshimiwa Waziri wa Nchi atafanya mawasiliano nao ili nipate maelezo ya kwa sasa ni hatua gani Serikali inachukua katika hayo maeneo ambayo tembo wamezagaa? Halafu baada ya hapo sasa, Mheshimiwa Bahati, nitafanya maamuzi kama hili jambo limeshaanza kufanyiwa kazi kwa mujibu wa Kanuni yetu ya 55, kwa maana ya kwamba, Serikali imeshachukua ule utaratibu wa kawaida ama ikiwa la, basi Waheshimiwa Wabunge mtanisikia. *(Makofi)*

Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Uratibu na Bunge, *Chief Whip*, tafadhali wasiliana na Wizara nipate majibu hapa mbele kuhusu hilo jambo, wanachukua hatua gani kwenye maeneo ambayo tembo wameenda kwenye maeneo ya wananchi ili Bunge liweze kufanya maamuzi.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea wakati nikisubiri taarifa hiyo.

Katibu.

**NDG. YONA KIRUMBI – KATIBU MEZANI:**

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Madini kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, namwita sasa Mheshimiwa Waziri wa Madini, Mheshimiwa Antony Peter Mavunde, aje awasilishe Hoja ya Wizara ya Madini. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MADINI:** Mheshimiwa Spika, baada ya kupokea taarifa iliyowasilishwa Bungeni na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini iliyochambua Bajeti ya Wizara ya Madini, naomba kutoa hoja kwamba, Bunge lako Tukufu sasa likubali kupokea, kujadili na kupitisha Taarifa ya Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Madini kwa mwaka wa fedha 2023/2024, pamoja na Madakirio ya Mapato na Matumizi ya Kawaida na ya Maendeleo ya Wizara ya Madini na Taasisi zake kwa mwaka wa fedha 2024/2025. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba hotuba yangu yenye kurasa 120 iingizwe kwenye Kumbukumbu Rasmi za Bunge kama ilivyowasilishwa kwenye Ofisi za Bunge.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote, namshukuru Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema, kwa kuniwezesha kuwasilisha Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Madini kwa mwaka wa fedha 2024/2025 mbele ya Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, natumia fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa utendaji wake makini, miongozo, maagizo na maelekezo mbalimbali anayotupatia kwa ajili ya kuiendeleza Sekta.

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya kipekee, natumia fursa hii adhimu kutoa shukrani zangu za dhati kwa Mheshimiwa Rais kwa kuniamini na kunipa dhamana ya kusimamia Sekta ya Madini. Ni ahadi yangu kwa Mheshimiwa Rais na Bunge lako Tukufu pamoja na Watanzania kwamba nitaitumikia nafasi hii kwa uadilifu, uaminifu na kwa uwezo wangu wote ili kuendeleza sekta hii muhimu.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Uongozi wa Serikali ya Awamu ya Sita, Mheshimiwa Rais ametuonesha kwa vitendo namna anavyoithamini sekta ya madini. Katika kipindi hicho tumeshuhudia kuendelea kuongezeka kwa mchango wa sekta ya madini kwenye pato la Taifa kutoka asilimia sita nukta saba mwaka 2020 hadi kufikia asilimia tisa nukta moja mwaka 2022. Ongezeko la ukusanyaji wa maduhuli ya Serikali kutoka shilingi

bilioni 588.05 mwaka 2020/2021 hadi shilingi bilioni 678.04 mwaka 2022/2023.

Mheshimiwa Spika, mafanikio mengine ni pamoja na hatua za uendelezaji wa madini muhimu na madini mkakati ambapo Serikali imetoa leseni ya uchimbaji mkubwa wa madini tembo *(Heavy Mineral Sands)* kwa mradi wa tajiri uliopo Wilaya ya Pangani, Mkoa wa Tanga, pamoja na leseni ya ujenzi wa kiwanda cha kusafisha madini ya metali, Wilaya ya Kahama, Mkoa wa Shinyanga.

Mheshimiwa Spika, namshukuru kwa dhati Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa miongozo mbalimbali anayoitoa kwenye Sekta ya Madini. Aidha, napenda kumshukuru Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Mbunge na Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa uongozi madhubuti na maelekezo anayoyatoa ili kufanikisha utendaji kazi Serikalini.

Mheshimiwa Spika, pia, napenda kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Doto Mashaka Biteko, Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, kwa kuaminiwa na kuteuliwa na Mheshimiwa Rais kushika nyadhifa hizo.

Mheshimiwa Spika, naomba kutumia fursa hii kukupongeza wewe binafsi…

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, subiri kidogo. Waheshimiwa Wabunge, kelele ni nyingi sana. Tafadhali ongeeni kwa sauti ya chini kwa sababu najua mnaongea mambo ya muhimu sana. Ongeeni kwa sauti ya chini ili tumsikilize Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MADINI:** Mheshimiwa Spika, naomba kutumia fursa hii kukupongeza wewe binafsi kwa kuendelea kuliongoza Bunge kwa ustadi, umahiri, hekima, busara na ubunifu mkubwa. Aidha, nampongeza Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu, Mbunge, Naibu Spika na Wenyeviti wote wa Bunge kwa kuendelea kushirikiana nawe katika kuliongoza Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa weledi mkubwa.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwapongeza Mheshimiwa Dkt. David Mathayo David, Mbunge na pia ni Mwenyekiti; na Mheshimiwa Kilumbe Shabani Ng'enda, Mbunge na pia ni Makamu Mwenyekiti kwa kuchaguliwa kuiongoza Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini.

Mheshimiwa Spika, aidha, nawapongeza Wajumbe wa Kamati kwa kuteuliwa kuwa Wajumbe wa Kamati ambayo imeendelea kuisimamia sekta kwa ufanisi mkubwa. Pia nalipongeza Bunge lako Tukufu kwa kazi nzuri ambazo linalofanya katika kuisimamia na kuishauri Serikali ikiwemo Wizara ya Madini.

Mheshimiwa Spika, kipekee kabisa, natumia fursa hii kuwashukuru sana wananchi wa Jimbo la Dodoma Mjini kwa kuendelea kunipa ushirikiano kama Mbunge wao na kunivumilia ninapokuwa nikitekeleza majukumu mengine ya kitaifa kama Waziri wa Madini.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwashukuru kwa dhati kabisa Dkt. Steven Lemomo Kiruswa, Mbunge na Naibu Waziri wa Madini, Bwana Kheri Abdul Mahimbali, Katibu Mkuu, Bwana Msafiri Lameck Mbibo, Naibu Katibu Mkuu na Dkt. Abdulrahman Shabani Mwanga, Kamishna wa Madini, kwa ushirikiano wanaonipatia katika kutekeleza majukumu ya Wizara.

Mheshimiwa Spika, pia naishukuru Menejimenti ya Wizara, Wenyeviti wa Bodi, Wakuu wa Taasisi za chini ya Wizara, wafanyakazi na wadau wote kwa ushirikiano wao katika kufanikisha majukumu ya sekta.

Mheshimiwa Spika, naishukuru sana familia yangu, mke wangu mpendwa Jacquelyne Moses Lupasa na watoto wangu Atarah na Allan Mavunde, kwa upendo, uvumilivu, ushirikiano na maombi yao wakati wote ninapotekeleza majukumu yangu.

Mheshimiwa Spika, kwa masikitiko makubwa naungana na wenzangu kutoa pole kwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, familia na Watanzania wote kwa ujumla kwa kuondokewa na viongozi wetu mashuhuri na shupavu ambao ni Hayati Ali Hassan Mwinyi, Rais Mstaafu wa Awamu ya

Pili wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Hayati Edward Ngoyai Lowassa, Waziri Mkuu Mstaafu.

Mheshimiwa Spika, vilevile natoa pole kwa wananchi wa Jimbo la Mbarali na Jimbo la Kwahani kwa kuondokewa na Wabunge wao Mheshimiwa Francis Mtega na Mheshimiwa Ahmed Yahya Abdulwakil. Tunawaombea kwa Mwenyezi Mungu, awapumzishe kwa amani.

Mheshimiwa Spika, sasa naomba kujielekeza katika maeneo mahsusi ya hotuba yangu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa kipindi cha kuanzia Julai, 2023 hadi Machi, 2024, bei ya madini ya dhahabu kwa wakia ilipanda hadi kufikia wastani wa Dola za Marekani 2,138 ikilinganishwa na bei ya wastani wa Dola za Marekani 1,854 katika kipindi cha Julai, 2022 hadi Machi, 2023. Aidha, mwenendo wa biashara ya madini ya Almasi duniani, haujaimarika kutokana na mdororo wa uchumi.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2023/2024, Wizara ilipangiwa kukusanya shilingi trilioni 1.006. Hadi kufikia Machi, 2024, Wizara imekusanya shilingi 589,000,000,000, kati ya fedha hizo shilingi bilioni 548,000,000,000 zimekusanywa na kuwasilishwa Hazina na shilingi bilioni 41.18 zilikusanywa na kutumika na taasisi zilizo chini ya Wizara.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2023/2024, Wizara iliidhinishiwa bajeti ya shilingi bilioni 89.36. Baada ya marejeo yaliyofanyika kwa kuongeza fedha za maendeleo shilingi 74,000,000,000.00 ilifanya bajeti ya Wizara kufikia shilingi 163,000,000,000.00.

Mheshimiwa Spika, katika bajeti hiyo, shilingi 45,000,000,000.00 ni fedha za matumizi mengineyo, shilingi 20,000,000,000.00 ni mishahara ya watumishi na shilingi 96,000,000,000.00 ni fedha za miradi ya maendeleo. Hadi kufikia Machi, 2024 Wizara imepokea shilingi bilioni 135.69 ambapo kati ya fedha hizo shilingi bilioni 35.11 ni matumizi mengineyo na shilingi bilioni 16 ni mishahara na shilingi bilioni 84 ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, katika kuimarisha ukusanyaji wa maduhuli, Wizara imeendelea kupambana na kudhibiti vitendo vya utoroshaji wa madini nchini ambapo katika kipindi cha Julai, 2023 hadi Machi 2024 Wizara kwa kushirikiana na mamlaka nyingine za Serikali imefanikiwa kukamata madini ya aina mbalimbali yenye thamani ya shilingi bilioni 3.971.

Mheshimiwa Spika, aidha, madini yaliyokamatwa yalitaifishwa na wahusika 157 walifikishwa kwenye vyombo vya sheria. Pia mchango wa sekta ya madini katika pato la Taifa uliongezeka na kufikia asilimia 9.1 kwa mwaka 2022 ikilinganishwa na mchango wa asilimia 7.3 kwa mwaka 2021.

Mheshimiwa Spika, katika kuendeleza madini muhimu na madini mkakati, Leseni ya Uchimbaji Mkubwa wa Madini *(Heavy Mineral Sands)* imetolewa kwa Kampuni ya *Nyati Mineral Sands Limited* na Leseni ya Usafishaji Madini imetolewa kwa Kampuni ya *Tembo Nickel Refining Company Limited*. Aidha, Wizara imepokea ombi la leseni ya uchimbaji wa madini Kinywe la Kampuni ya *Duma Tanz-Graphite Limited.*

Mheshimiwa Spika, ili kuongeza manufaa yatokanayo na Madini Muhimu na Madini Mkakati, kwa mara ya kwanza kitajengwa kiwanda kikubwa na cha kisasa cha usafishaji na uongezaji thamani madini cha *Multi Metals Processing Facility* katika eneo maalumu la Ukanda wa Kiuchumi la *Buzwagi Special Economic Zone* lililopo Wilaya ya Kahama.

Mheshimiwa Spika, kwa kutambua mchango wa wachimbaji wadogo katika kukuza uchumi wa mtu mmoja mmoja na Taifa kwa ujumla, Wizara imeliwezesha Shirika la Madini la Tanzania *(STAMICO)* kununua mitambo mitano ya uchorongaji kwa ajili ya wachimbaji wadogo.

Mheshimiwa Spika, mitambo hiyo tayari imeanza kazi rasmi ya uchorongaji kuanzia tarehe 4 Desemba, 2023 katika maeneo ya leseni za wachimbaji wadogo ya Nyamongo - Tarime, Itumbi - Chunya, Rwamgasa - Geita, Katente - Bukombe, Buhemba - Butiama na Nholi - Dodoma.

Mheshimiwa Spika, Wizara na taasisi zake imetoa mafunzo kwa wachimbaji wadogo 10,213 kuhusu usalama migodini, afya na utunzaji wa mazingira, biashara ya madini, ulipaji wa kodi na tozo mbalimbali za Serikali. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na Shirikisho la Vyama vya Wachimbaji Wadogo Tanzania *(FEMATA)* imeratibu ziara ya mafunzo kwa wachimbaji na wafanyabiashara zaidi ya 100 nchini China.

Mheshimiwa Spika, Wizara kupitia taasisi zake imeendelea kuwahamasisha wachimbaji wadogo kutunza kumbukumbu za uzalishaji na biashara za madini ikiwa ni pamoja na vigezo vitakavyowawezesha kupata mikopo kwenye taasisi za fedha. Hadi kufikia Machi, 2024 jumla ya shilingi bilioni 187 zilikopeshwa kwa wachimbaji ikilinganishwa na shilingi bilioni 145 zilikopeshwa kwa mwaka 2022.

Mheshimiwa Spika, natumia fursa hii kuzishukuru Benki za *CRDB, NMB,* AZANIA na *KCB* kwa kukubali kuwakopesha wachimbaji. Natoa wito kwa taasisi nyingine za fedha zione umuhimu wa kuwakopesha wachimbaji kwa lengo la kuwawezesha kufanya tafiti zao kwa tija.

Mheshimiwa Spika, Wizara kupitia Tume ya Madini imetoa leseni ya kusafisha madini ya *Nickel, Cobalt* na Shaba kwa kampuni ya *Tembo Refining Company Limited.* Aidha, ili kuvutia shughuli za uongezaji thamani madini nchini, Serikali imepunguza malipo ya mrabaha kutoka asilimia sita hadi asilimia nne na kufuta ada ya ukaguzi ya asilimia moja kwa madini yatakayouzwa kwenye viwanda vya usafishaji dhahabu vilivyopo hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, ili kuvutia uwekezaji nchini, Wizara ilitangaza fursa za uwekezaji na kutoa elimu kwa umma kupitia ziara mbalimbali za viongozi kwenye vyombo vya habari, mikutano ya kitaifa, kikanda na kimataifa.

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia Machi 2024, kiasi cha karati 4,115 za madini ya almasi, karati 19,728 na tani 35 za madini ya *Tanzanite* na kiasi cha karati 86,920 na tani 45,875 za madini mengine ya vito yaliuzwa katika masoko ya madini. Mauzo ya

madini hayo yamechangia makusanyo, mrabaha na ada ya ukaguzi kiasi cha shilingi bilioni 133.

Mheshimiwa Spika, Wizara imeiwezesha Tume ya Madini katika kuendeleza ujenzi wa jengo la Ofisi ya Makao Makuu ambapo ujenzi huo umefikia 77%. *STAMICO* imewezeshwa kununua mitambo miliwi ya uzalishaji wa mkaa mbadala *(coal briquettes)* ambayo imesimikwa eneo la Kisarawe – Pwani na Kiwira – Mbeya. *GST* imewezeshwa kununua vitendea kazi kwa ajili ya shughuli za utafutaji madini na Kituo cha *TGC* kimewezeshwa kuboresha miundombinu ya kufundishia kwa lengo la kukuza shughuli za uongezaji thamani madini nchini.

Mheshimiwa Spika, Wizara imetoa vibali 252 vya kuingiza, kupitisha, kutengeneza na kuuza baruti nchini pamoja na vibali vya kusafirisha baruti nje ya nchi. Fedha zilizopatikana kupitia utoaji wa vibali hivyo ni jumla ya Dola za Marekani 126,600. Vilevile Wizara ilitoa vibali nane kwa ajili ya utengenezaji wa baruti aina ya *emulsion* ambayo kwa kutumia gari la *Mobile Manufacturing Unit (MMU)*.

Mheshimiwa Spika, kati ya vibali hivyo, saba vilitolewa kwa Kampuni ya *Orica Tanzania Limited* na kibali kimoja kwa Kampuni ya *Dangote Cement Limited* ambavyo vitatumika kwa muda wa miaka miwili. Kupitia vibali hivyo, jumla ya Dola za Marekani 9,600 zimekusanywa.

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia mwaka 2024 Wizara kupitia Tume ya Madini ilipokea na kupitia jumla ya mipango 801 ya ushirikishwaji wa Tanzania katika shughuli za madini ambapo mipango 797 iliidhinishwa na mipango minne haikukidhi vigezo. Hivyo, wahusika walitakiwa kufanya marekebisho stahiki.

Mheshimiwa Spika, ajira 19,356 zilizalishwa kupitia sekta ya madini ambapo ajira 18,853 sawa na 97% zilizotolewa kwa Watanzania na ajira 505 sawa na asilimia tatu zilitolewa kwa wageni. Aidha, kwa upande wa wajibu wa uwajibikaji kwa wawekezaji kwenye sekta ya madini husussan, kwa jamii zinazozunguka miradi ya wawekezaji, shilingi bilioni 17 zimetumika kwa ajili ya miradi mbalimbali ya *CSR*, kwa halmashauri na miji

inayozunguka migodi ya *Tembo Nickel*, *Geita Gold*, *Bulyanhulu Gold Mine Limited*, *North Mara Gold Mine Limited*, *Williamson Diamond Limited*, *Shanta Mining Company Limited, Dangote Cement Limited*, *Uranex Tanzania Limited*, *Ruvuma Coal Limited* na *Buckreef Gold Company Limited*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sambamba na usimamizi wa utekelezaji wa *CSR* katika kipindi husika, Wizara na Taasisi zake imetoa mafunzo kuhusu Kanuni za *CSR* kwa wadau mbalimbali wa Sekta ya Madini, wakiwemo: Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini; Kampuni ya *Geita Gold Mining Limited, Tancoal Energy Limited, North* Mara na Bulyanhulu; Chama cha Wanawake Wachimbaji Madini *(TAWOMA)*; Viongozi wa Mikoa ya Geita na Ruvuma; na Viongozi wa Halmashauri za Wilaya ya Nyang'hwale, Simanjiro, Songwe, Ikungi na Msalala. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Wizara iliandaa mapendekezo ya marekebisho ya Sheria ya Madini Sura 123 ambayo yaliwasilishwa na kusomwa kwa mara ya kwanza katika Mkutano wa Kumi na Nne wa Bunge kupitia Muswada wa Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Na. 4 ya mwaka 2024.

Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha kuwa mchango wa sekta ya madini katika kuliingizia Taifa fedha za kigeni unaongezeka. Wizara itaendelea kusimamia utekelezaji wa matakwa ya kifungu cha 10 cha Sheria ya Mamlaka ya Nchi kuhusu Umiliki na Utajiri Asilia na Maliasili za Nchi, Sura ya 449 kinachoweka sharti la mapato yatokanayo na uvunaji wa rasilimali hii ya nchi, ikiwemo madini kuwa katika taasisi za fedha zilizopo nchini.

Mheshimiwa Spika, aidha, Wizara inaendelea kushirikiana na mamlaka nyingine za Serikali ikiwemo *BoT* kuhakikisha kuwa malipo ya mauzo ya madini yaliyofanyika nje ya nchi yanarejeshwa nchini. Lengo ni kuhakiki kama malipo haya yamefanyika na kuhifadhiwa kwa kuzingatia masharti ya Kanuni za Fedha za Kigeni za Mwaka 2022. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Tume ya Madini imetekeleza shughuli zifuatazo: -

(i) Usimamiaji na usimamizi wa Leseni za Madini;

(ii) Usimamizi na ukaguzi wa biashara ya madini; na

(iii) Shughuli za ukaguzi wa migodi, mazingira na usimamizi wa baruti.

Mheshimiwa Spika, *STAMICO* imetekeleza miradi mitano ya maendeleo ikiwemo: Mradi wa Makaa ya Mawe wa Kabulo – Kiwira; Mradi wa Uchorongaji, Mradi wa Mkaa Mbadala *(coal briquettes);* Mradi wa Kokoto Chigongwe na Mradi wa Vituo vya Mfano vya Wachimbaji Wadogo. *STAMICO* pia imetekeleza Miradi ya Ubia Kiwanda cha Kusafisha Dhahabu Mwanza na Mgodi wa Dhahabu wa *Backreef* pamoja na Kampuni Tanzu ya Mradi wa *STAMIGOLD* Biharamulo.

Mheshimiwa Spika, *GST* imetekeleza shughuli zifuatazo: -

(i) Kufanya utafiti wa Jiosayansi na kuboresha kanzidata ya rasilimali madini ya Taifa;

(ii) Utoaji wa huduma za maabara; na

(iii) Ufuatiliaji wa majanga ya asili ya jiolojia na kutoa elimu kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, Kituo cha *TGC* kimeendelea na utekelezaji wa majumuku yake mbalimbali ikiwemo:-

(i) Udahili wa wanafunzi na utoaji wa mafunzo; na

(ii) Uzalishaji wa bidhaa na utoaji wa huduma kwa wadau muhimu wa madini.

Mheshimiwa Spika, *TEITI* imendelea na utekelezaji wa majukumu yake ikiwemo, ukamilishaji wa Ripoti ya 14 ya *TEITI* ya mwaka 2021/2022; kushiriki katika Mikutano ya Kimataifa ya Uwazi na Uwajibikaji; na kufanya Tathmini ya utekelezaji wa vigezo vya *EITI* nchini.

Mheshimiwa Spika, katika kuandaa Mpango na Bajeti ya Mwaka 2024/2025 Wizara imezingatia miongozo ifuatayo:-

(i) Mwongozo wa Kitaifa wa Maandalizi wa Mpango na Bajeti ya Mwaka 2024/2025;

(ii) Ilani ya CCM kwa ajili ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020;

(iii) Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano;

(iv) Sera ya Madini ya 2009;

(v) Dira ya Taifa ya Maendeleo ya Mwaka 2025; na

(vi) Maelekezo ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na viongozi wengine wa kitaifa pamoja na maelekezo ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini yaliyotolewa kwa nyakati tofauti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, eneo la kwanza ni kuimarisha ukusanyaji wa maduhuli na kuongeza mchango wa sekta ya sekta madini kwenye pato la Taifa. Katika eneo hili Wizara imepanga kutekeleza mipango mbalimbali ikiwemo kuhamasisha na kuanza kwa uzalishaji wa kampuni zilizopewa leseni za uchimbaji; usafishaji na biashara ya madini na kuimarisha usimamizi wa migodi na uchimbaji madini.

Mheshimiwa Spika, hatua nyingine ni kuimarisha ukaguzi na usimamizi wa shughuli za uchimbaji wa madini kwa manunuzi ya vitendea kazi kama magari na pikipiki katika mikoa yote ili iweze kunufaisha nchi na wawekezaji; na kuimarisha, kusimamia masoko na vituo vya madini nchini.

Mheshimiwa Spika, eneo la pili ni kuendeleza madini muhimu na madini mkakati. Wizara imepanga kutekeleza yafuatayo ili kunufaika na fursa zilizopo:-

(i) Kufanya tafiti kwa lengo la kubaini maeneo yenye madini mkakati na muhimu kwa ajili ya kuhamasisha wawekezaji.

(ii) Kuvutia wawekezaji kwa utafutaji wa uchimbaji madini mkakati na madini muhimu kwa kuandaa mazingira rafiki; na

(iii) Kukamilisha uandaaji wa mpango mkakati wa uendelezaji na uvunaji wa madini mkakati na madini muhimu nchini.

Mheshimiwa Spika, kuanzia sasa hatutatoa leseni ya kati na leseni kubwa ya uchimbaji wa madini yote yakiwemo madini mkakati na madini muhimu kwa mwekezaji yeyote kama hatakuwa na mpango mzuri wa kuongeza thamani ya madini hapa nchini. Lengo ni kuifanya nchi yetu ya Tanzania kunufaika na rasilimali madini ambayo Mwenyezi Mungu ametujalia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali imetenga eneo maalumu la Ukanda wa Kiuchumi la Buzwagi *Special Economic Zone* lililopo Wilaya ya Kahama. Eneo hilo lina ukubwa wa ekari 1,333, litatumika kwa ajili ya Ujenzi wa Kiwanda cha Usafishaji na Uongezaji Thamani *(Multi Metals Processing Facility), Steel Balls Manufacture, Mine Conveyor Belts, Solar Farms and Portable Water Plant*.

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa viwanda hivyo utaongeza fursa za ajira, ujuzi kwa Watanzania, kuchochea upatikanaji wa mapato na upatikanaji wa bidhaa za migodini ambazo awali zilikuwa zikiagizwa nje ya nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la tatu, kuhamasisha uwekezaji, uongezaji thamani madini na uanzishwaji wa minada na maonesho ya madini vito. Serikali itaendelea kutangaza fursa mbalimbali zinazopatikana kwenye mnyororo wa thamani wa madini nchini kupitia makongamano, maonesho, tovuti na vyombo habari.

Mheshimiwa Spika, pia Wizara itaendelea kutoa ushirikiano kwa wamiliki wa viwanda vya usafishaji wa madini ya dhahabu nchini ili kupata ithibati ya *LDMA*. Vilevile Serikali itaendelea na jitahada za kuanzisha minada na maonesho ya kimataifa ya madini ya vito kwa lengo la kupata masoko, bei shindani, kuvutia uwekezaji na kutangaza fursa za madini ya vito zilizopo nchini.

Mheshimisimiwa Spika, eneo la nne ni kuendelea kufanya utafiti wa kina wa Jiofizikia *(High-resolution Airborne Geophysical Survey)*. Wizara itafanya yafuatayo katika utekelezaji wa shughuli hii: Kufanya tafiti za kina za jiofizikia *(High-resolution Airborne Geophysical Survey)* ili kuainisha tabia za miamba na kujenga mfumo wa kutunza na kusambaza taarifa za *Jiosayansi.*

Mheshimiwa Spika, la tano, kuwaendeleza wachimbaji wadogo na kuwasogezea huduma za ugani. Wizara itaendelea na juhudi za kuwaendeleza wachimbaji wadogo kwa kutoa mafunzo ya mara kwa mara kuhusu masuala muhimu ya kuzingatia katika uendeshaji wa shughuli za madini.

Mheshimiwa Spika, lingine ni kufanya utafiti na kutenga maeneo kwa ajili ya wachimbaji wadogo; kuimarisha miundombinu na utendaji wa vituo vya mfano ili kutoa huduma kwa wachimbaji wadogo; kuwaunganisha wachimbaji wadogo wa taasisi za fedha ili wapate mikopo kwa ajili ya uendeshaji wa shughuli zao na kuwezesha upatikanaji wa vitendea kazi kwa wachimbaji wadogo ikiwemo mitambo ya uchorongaji.

Mheshimiwa Spika, la sita, kuzijengea uwezo taasisi chini ya Wizara ili ziweze kutekeleza majukumu yake. Wizara itafanya yafuatayo: -

(i) Itaiwezesha Tume ya Madini kupata rasilimali fedha na vifaa kwa ajili ya kutekeleza majumu yake kwa ufanisi;

(ii) Itaendelea kuimarisha *STAMICO* ili ishiriki kikamilifu kwenye shughuli za madini;

(iii) Kuimarisha *GST* ili iweze kufanya tafiti za Jiosayansi kubaini maeneo mapya yenye mashapu ya madini; na

(iv) Itaendelea kuimarisha Kituo cha *TGC* kwa lengo la kuendelea kutoa mafunzo na kuhamasisha shughuli za uongezaji thamani madini; na

(v) Kuiwezesha *TEITI* kupata rasilimali mbalimbali ili iweze kutekeleza majukumu yake ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, maeneo mengine yatakayotekelezwa na Wizara, eneo la kwanza ni *Vision* 2030, "Madini ni maisha na utajiri." Wizara kupitia *GST* itaendelea kufanya utafiti wa kina wa jiofizikia kwa kutumia teknolojia ya kisasa ili kutambua tabia za miamba na kurahisisha tafiti nyingine za jiosayansi ili kuwezesha na kubaini aina mbalimbali za madini yapatikanayo nchini.

Mheshimiwa Spika, hadi sasa utafiti wa kina wa jiofizikia umefanyika kwa 16% ya eneo lote la nchi yetu ya Tanzania. Aidha, *GST* inatarajiwa kufanya utafiti wa kina wa jiofizikia katika *blocks* mbili kubwa zenye jumla ya kilometa za mraba 165,574. Baadhi ya maeneo yatakayopitiwa yapo kwenye Mikoa ya Rukwa, Katavi, Mbeya, Songwe na Kigoma. Malengo ya Wizara ni kufanya utafiti wa kina wa jiofizikia kufikia angalau 50% ifikapo mwaka 2030. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, dhana hii ya *Vision* 2030 inakusudia kuiendeleza Sekta ya Madini kwa kufanya yafuatayo: -

(i) Kufanya utafiti wa kina wa jiofizikia;

(ii) Kujenga maabara ya kisasa kwa ajili ya kufanya uchunguzi wa miamba, udongo, maji na madini;

(iii) Kuanzisha makumbusho maalumu ya madini;

(iv) Kuwawezesha wachimbaji wadogo kupitia *STAMICO* kwa kuwapatia mashine 15 za uchorongaji na kuyafanya madini mkakati na madini muhimu yawe na nguvu ya soko kuongeza thamani hapa nchini;

(v) Kuwaendeleza wawekezaji wazawa ili kuongeza wigo wa uwekezaji unaotokana na Watanzania;

(vi) Kuongeza ushiriki wa Watanzania *(local content)* katika kusambaza bidhaa na kutoa huduma migodini; na

(vii) Kuandaa mazingira rafiki ili kuvutia uwekezaji mkubwa kutoka nje ya nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ufanisi wa malengo haya mahsusi ya mkakati wa sekta kwenye *Vision* 2030 utategemea ushiriki wa wadau mbalimbali ikiwemo taasisi za Serikali, sekta binafsi, asasi za kiraia na Jumuiya ya Kimataifa pamoja na mabadiliko chanya ya kiuchumi na kisiasa.

Mheshimiwa Spika, napenda kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa madini ni maisha na utajiri. Inamanisha, huwezi kutenganisha maisha ya Mtanzania na sekta ya madini, kwa kuwa kufanikiwa kwa tafiti za kina na kupatikana kwa taarifa sahihi kutachochea sekta nyingine kukua ili ikiwemo sekta ya maji, kilimo, utalii, ujenzi na mawasiliano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, eneo la pili, ni Programu *ya Mining for a Brighter Tomorrow (MBT)*. Programu ya *Mining for Brighter Tomorrow (MBT)* ni mahususi kwa ajili ya kuwainua wachimbaji wanawake na vijana ambayo italenga maeneo yafuatayo: Utoaji wa leseni katika maeneo ya wachimbaji na wachimbaji kunufaika na vitendea kazi ikiwemo magari, vifaa na mitambo ya uchimbaji. Aidha, kupitia programu hii itasaidia kuchochea ukuaji wa sekta ya madini na uchumi wa Taifa na kuongeza ajira kwa Watanzania.

Mheshimiwa Spika, eneo la tatu ni utoaji wa vifaa vya uongezaji thamani ya madini kwa wahitimu wa *TGC*. Wizara imedhamiria kuhamasisha kwa vitendo shughuli za kuongeza thamani ya madini nchini kwa kuwapatia vifaa wahitimu wa kozi mbalimbali za uongezaji thamani madini ili waweze kuendeleza ujuzi na kujiajiri ikiwa ni njia mojawapo ya kukuza na kusambaza tasnia hii kwa faida ya sasa na vizazi vijavyo.

Mheshimiwa Spika, usimamizi wa sheria. Sheria, kanuni na miongozo na taratibu ni muhimu katika kusimamia maendeleo na

ustawi wa sekta ya madini. Katika hili, Wizara ya Madini itaendelea kusimamia mfumo wa kisheria na usimamizi wa sekta ya madini ikiwa ni pamoja na kuchukua hatua stahiki kwa watakaobainika kukiuka sheria na kanuni zinazosimamia sekta hii.

Mheshimiwa Spika, Wizara kwa kushirikiana na wadau, tutaendelea kufanya marekebisho ya mfumo wa kisheria na usimamizi wa sekta ya madini pale itakapoonekana kuna umuhimu ili kuendelea kuweka mazingira bora ya uwekezaji katika sekta hii muhimu kwa uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, ili kuleta ufanisi katika uingiaji wa mikataba ya wamiliki wa leseni na mtoa msaada kiufundi *(technical support),* Wizara imejipanga kutengeneza kanuni ambazo wadau wote watashirikishwa ili kuwa na nyenzo imara ya kusimamia masuala haya kwa manufaa ya pande zote zinazohusika kwenye leseni. Lengo ni kuhakikisha kuwa hakuna mchimbaji anayepoteza haki yake kwa sababu tu ya mmiliki wa leseni kupata mshirika.

Mheshimiwa Spika, kwa wamiliki wa leseni *(PML)* ambao watataka kunufaika na msaada wa kiufundi wanashauriwa wasiingize wachimbaji wadogo ndani ya leseni zao, bali wachimbe wenyewe ili wakipata msaada wa kiufundi iwe rahisi kwao kufanya makubaliano nao.

Mheshimiwa Spika, tutaweka utaratibu wa kumtaka kila mmiliki wa leseni ya uchimbaji mdogo *(PML) a*mbaye ndani ya eneo lake la leseni kuna wachimbaji wadogo wengine. Akitaka kuuza leseni yake au kuingia makubaliano na mwekezaji suala linaloweza kuwaondoa wachimbaji wadogo ndani ya leseni yake au kuathiri kwa aina yoyote ya uwekezaji wa wachimbaji hao hasa maduara hayo atatakiwa kufanya mambo yafuatayo: -

(i) Kuwapa kwanza nafasi ya upendeleo *(the right of first refusal),* wachimbaji wadogo waliopo ndani ya leseni yake haki ya kununua au kuingia mkataba wa uwekezaji kabla ya kwenda kwa mtu mwingine; na

(ii) Uwepo wa Mikataba iliyosajiliwa na Tume ya Madini kati ya mmiliki wa leseni *(PML)* na wachimbaji waliopo ndani ya leseni zao ili watambulike rasmi na Tume ya Madini kwa lengo la kusimamia maslahi yao pindi inapotokea changamoto juu ya maslahi yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa leseni zote zinazotolewa na Serikali kwa ajili ya vikundi vya wachimbaji wadogo litawekwa sharti la lazima la kukitaka kikundi chenye lengo la kutaka kupata msaada wa kiufundi au kuuza leseni yake kwa mwekezaji kupata kwanza kibali cha Katibu Mtendaji wa Tume baada ya kujiridhisha juu ya msaada wa kiufundi unaotaka kutolewa na pia kujiridhisha namna ambavyo pande zote zitanufaika ili kuepusha migogoro isiyo la lazima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, eneo la tano ni ushiriki wa Watanzania katika shughuli za madini na uwajibikaji wa kampuni kwa jamii. Kufuatia marekebisho ya Sheria ya Madini ya Mwaka 2017, kulitungwa Kanuni za Ushirikishwaji wa Watanzania za Mwaka 2018 ili kutoa tafsiri na kuweka usimamizi thabiti katika utekelezaji wa masuala ya ushirikishwaji wa Watanzania katika sekta ya madini nchini *(local content)*, uwajibikaji wa kampuni kwa jamii *(Corporate Social Responsibilities)*.

Mheshimiwa Spika, Kanuni kuhusu ushirikishwaji wa Watanzania katika sekta ya madini zinazitaka kampuni za uchimbaji madini kununua vifaa vinavyozalishwa nchini, kuajiri Watanzania na kutumia huduma za bidhaa zinazozalishwa ndani ya nchi.

Mheshimiwa Spika, Wizara itaendelea kusimamia utekelezaji wa Kifungu cha 105 cha Sheria ya Madini pamoja na Kanuni za Wajibu wa Wamiliki wa Leseni za Madini za Mwaka 2023. Sheria na Kanuni hizo zinawataka wamiliki wa leseni za madini nchini kushirikiana na Mamlaka za Serikali za Mitaa kuandaa mpango mahsusi kwa wajibu wa kampuni kwa jamii kwa kuzingatia vipaumbele vya jamii zinazozunguka maeneo yenye leseni. Wamiliki wote wa leseni za madini nchini wana wajibu wa kuwasilisha nakala ya mipango iliyoidhinishwa ili Tume ya Madini iweze kufuatilia utekelezaji wa mipango hiyo.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa utekelezaji wa Kanuni za *CSR* za Mwaka 2023 unaonekana kuwa na changamoto, napenda kulijulisha Bunge lako kwamba, Wizara itaandaa kikao cha wadau wote wanaoguswa kwa aina moja au nyingine na kanuni hizi ili kujadiliana kwa pamoja kuja na mwarobaini wa suala hili kwa manufaa ya wawekezaji, jamii inayozunguka migodi na Taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, kazi zitakazotekelezwa na taasisi zilizo chini ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2024/2025, eneo la kwanza ni Tume ya Madini.

(a) Eneo lake la kwanza itakuwa ni kuimarisha usimamizi wa shughuli za madini na ukusanyaji wa maduhuli ya Serikali. Tume ya Madini itatekeleza yafuatayo: -

(i) Kuimarisha mfumo wa usimamizi wa leseni ili kuongeza kasi ya utoaji wa leseni;

(ii) Kuendelea kufuatilia leseni ili kubaini leseni zenye makosa mbalimbali ikiwemo zisizoendelezwa na kuzifuta kwa kuzingatia sheria;

(iii) Kuimarisha usimamizi wa uzalishaji na biashara ya madini ya ujenzi na viwandani; na

(iv) Kuboresha mfumo wa masoko ya madini na kuongeza vitendea kazi.

Mheshimiwa Spika, aidha, Tume ya Madini inatarajia kununua vifaa mbalimbali vya maabara ili kuiongezea uwezo maabara yake ya uchunguzi wa sampuli za madini.

(b) Kuimarisha ukaguzi wa usalama, afya na utunzaji mazingira.

Mheshimiwa Spika, Tume ya Madini itaendelea kuimarisha usimamizi na ukaguzi wa migodi kwenye masuala ya usalama, afya na utunzaji wa mazingira. Aidha, Tume ya Madini itaendelea kusimamia utunzaji na matumizi sahihi ya baruti, kufanya ukaguzi

wa mitambo ya uchenjuaji madini, pamoja na kukagua na kuidhinisha mipango ya uendelezaji na ufungaji wa migodi.

Mheshimiwa Spika, pia Tume ya Madini itaendelea kutoa elimu na miongozo kwa wamiliki wa miradi ya uchimbaji na uchenjuaji wa madini ili waweke mipango mizuri ya kusimamia usalama, afya na utunzaji wa mazingira.

(c) Kuendelea kusimamia mazingira ya kuwawezesha wananchi kunufaika na rasilimali madini.

Mheshimiwa Spika, ili kuhakikisha Watanzania wananufaika na shughuli za madini, Tume ya Madini itaendelea kusimamia ushiriki wa Watanzania kwenye shughuli za madini. Aidha, Tume itaendelea kuhakikisha wamiliki wa leseni za madini wanatekeleza wajibu wao kwa jamii inayozunguka eneo la mradi kwa kuzingatia sheria.

(d) Kuelimisha umma na kuboresha mawasiliano kati ya Tume na wadau mbalimbali kuhusu masuala ya madini.

Mheshimiwa Spika, katika kujenga uelewa na kuboresha mawasiliano ya tume na wadau wa madini, Tume ya Madini itaendelea kutoa elimu kwa umma kuhusu masuala mbalimbali yanayohusu sekta ya madini, ikiwa ni pamoja na namna ya kupata leseni za madini, utekelezaji wa sheria zinazosimamia shughuli za madini, utunzaji wa mazingira na ulipaji wa ada, kodi na tozo mbalimbali za Serikali. Aidha, Tume ya Madini itaendelea kutoa elimu na kuhamasisha wananchi kushiriki katika fursa zilizopo katika sekta ya madini.

(e) Kuendeleza rasilimali watu na kuboresha mazingira ya kufanyia kazi.

Mheshimiwa Spika, Tume ya Madini itaendelea kuimarisha na kuboresha utendaji kazi wa watumishi kwa kuwaongezea ujuzi na weledi kupitia mafunzo ya muda mfupi na mrefu. Aidha, Tume ya Madini itaendelea kuboresha mazingira ya utendaji kazi kwa kujenga ofisi za Maafisa Madini Wakazi, katika Mikoa ya Kimadini ya Rukwa, Songwe na Mahenge.

Mheshimiwa Spika, eneo la pili ni Taasisi ya Jiolojia na Utafiti wa Madini Tanzania *(GST),* ambao wao katika sehemu yao ya kwanza:-

(a) Kufanya tafiti za jiosayansi na kuboresha kanzidata ya rasilimali madini ya Taifa.

Mheshimiwa Spika, *GST* inakusudia kufanya ugani wa jiolojia na jiokemia katika *QDS* 2 mpya, *QDS* 221 na 222 zilizopo Mkoa wa Pwani na kuchora ramani zake katika *scale* ya 1:100,000, kuhuisha ramani katika *scale* ya 1:100,000, na kubainisha madini kwenye ramani mbili zenye upungufu wa taarifa mpya za uwepo wa madini *(mineral occurrence mapping)* katika *QDS* 2 (*QDS* 275 na 276) zilizopo Mkoa wa Ruvuma na Njombe.

Mheshimiwa Spika, aidha, *GST* itafanya tafiti nne maalum za jiosayansi na utafiti wa kina kwenye maeneo yenye madini ya viwandani, madini ya dhahabu na madini mkakati. Pia *GST* imepanga kufanya ununuzi wa *Helicopter Jet Ranger* kwa ajili ya kuongeza nguvu katika shughuli za utafiti wa kina wa madini hapa nchini.

(b) Kuwaendeleza wachimbaji wadogo kwa kufanya tafiti za jiosayansi.

Mheshimiwa Spika, katika kuwaendeleza wachimbaji wadogo na wa kati, *GST* inalenga kufanya utafutaji wa madini kwa lengo la kubainisha ulalo, mwelekeo na tabia za mbale katika maeneo mawili ya wachimbaji wadogo yaliyopo mikoa ya Kigoma na Katavi.

(c) Kuboresha Huduma za Maabara.

Mheshimiwa Spika, *GST* imepanga kuendelea kufanya chunguzi kwa kuzingatia vigezo vya ithibati *(accreditation)*. Aidha, *GST* imepanga kupata ithibati za madini mengine zaidi ya dhahabu na makaa ya mawe ili kuongeza wigo wa utoaji huduma kwa wateja.

Mheshimiwa Spika, *GST* imepanga kujenga maabara mpya ya kisasa *(State-of-Art Laboratory)* katika eneo la Kizota Dodoma. Maabara hiyo itafanya uchunguzi wa madini, ikiwemo yale yanayohitajika kwenye nishati safi kama vile *Nickel, Cobalt* na *Lithium.* Vilevile *GST* itaendelea na ujenzi wa maabara nyingine katika maeneo ya Chunya na Geita kwa lengo la kusogeza huduma karibu na wananchi wanaojihusisha na shughuli za madini.

(d) Kuboresha ufuatiliaji wa mienendo ya majanga ya asili ya jiolojia na kuelimisha wananchi namna bora ya kupunguza athari za majanga.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza jukumu hilo, *GST* itakusanya takwimu kutoka vituo vitano vya kudumu vya kunakili mienendo ya mitetemo vilivyopo Arusha, Dodoma, Geita, Mtwara na Mbeya. Kuendelea kuunganisha vituo viwili vya kupima mitetemo vilivyopo Dodoma na Arusha, katika mfumo mubashara, ili kuwezesha upatikanaji wa taarifa kwa wakati mara tetemeko linapotokea pamoja na kusimika mtambo mmoja mpya kwa ajili ya Ukanda wa Bonde la Ufa, Mkondo wa Magharibi Mkoa wa Kigoma.

Mheshimiwa Spika, ili kuhakikisha mapato ya Shirika la Madini la Taifa *(STAMICO),* yanakua na kuimarika, Shirika limepanga kuongeza usimamizi kwenye uwekezaji uliopo katika miradi yake kama ifuatavyo: -

(a) Kuendelea na uzalishaji wa makaa ya mawe na mkaa mbadala *(Rafiki Briquettes)*.

Mheshimiwa Spika, Shirika litaendelea na uzalishaji mkubwa wa makaa ya mawe katika eneo la Kabulo-Kiwira ambapo jumla ya tani 600,000 zimepangwa kuchimbwa. Aidha, Shirika linatarajia kuongeza uzalishaji wa mkaa mbadala *(Rafiki briquettes)* kwa kununua mitambo minne. Pia Shirika limepanga kununua vifaa kwa ajili ya kuongeza ufanisi katika mradi huo na kujenga ghala kwa ajili ya kuhifadhi mkaa.

(b) Kuimarisha shughuli za uchorongaji.

Mheshimiwa Spika, Shirika litaendelea kuimarisha shughuli za uchorongaji kwa kutangaza na kutafuta kandarasi katika migodi mikubwa na ya kati. Aidha, Shirika limepanga kununua mitambo miwili ya uchorongaji ili kukidhi ongezeko la huduma za uchorongaji.

(c) Kuanza Uzalishaji wa Kokoto – Chigongwe.

Mheshimiwa Spika, Shirika limepanga kuanza uzalishaji wa kokoto katika leseni zake za Chigongwe Dodoma, ambapo uzalishaji unatarajiwa kuwa tani 178,000.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ni kuwezesha shughuli za uchimbaji mdogo na kuimarisha vituo vya mfano. *STAMICO* itaendelea kuwezesha wachimbaji wadogo kwa kununua mitambo mitano ya uchorongaji, kutekeleza mpango wa mafunzo kwa wachimbaji wadogo katika maeneo mbalimbali nchini na kuviongezea uwezo vituo vya mfano vya Lwamgasa, Katente na Itumbi pamoja na kuimarisha miundombinu iliyopo.

Mheshimiwa Spika, aidha, *STAMICO* itaendelea na taratibu za ujenzi wa vituo viwili vipya vya mfano vya kuchakata madini ya chumvi na chokaa katika Mkoa wa Lindi na Tanga mtawalia. Hadi sasa eneo la ujenzi wa kituo cha mfano cha chumvi limepatikana huko Nangurukuru - Lindi na taratibu za kumpata mzabuni kwa ajili ya ujenzi zinaendelea. Aidha, Shirika litaendelea na taratibu za kupata eneo la kujenga kiwanda cha chokaa Kona Z, Mkoani Tanga.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kuendeleza Leseni za Shirika, *STAMICO* itaendelea na utafutaji wa madini katika leseni zake, ikiwemo leseni ya uchimbaji wa dhahabu katika eneo la Pida lililopo Mkoa wa Mara pamoja na leseni ya madini mkakati na muhimu ya *Cobalt* na *Nickel* pale Kagera, Shaba - Kilimanjaro, *Lithium* - Dodoma, Kinywe - Lindi na *Rare Earth Elements* - Songwe.

Mheshimiwa Spika, kuhusu utekelezaji wa miradi ya ubia na kampuni tanzu, Shirika litaimarisha ufuatiliaji wa miradi ya ubia

ambayo ni mgodi wa *Buckreef* na Kiwanda cha Kusafisha Dhahabu Mwanza pamoja na kampuni tanzu ya *STAMIGOLD* ili kuongeza ufanisi na kuwezesha ukusanyaji wa mapato kutoka kwenye miradi hiyo. Aidha, Shirika litaendelea kuiwezesha *STAMIGOLD* kufanya utafiti zaidi wa maeneo ya leseni zake ili kubaini mashapo mapya na kuongeza uhai wa mgodi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Kituo cha Jemolojia Tanzania *(TGC)*:-

(a) Ujenzi wa Jengo la Kituo.

Mheshimiwa Spika, *TGC* imepanga kuimarisha miundombinu ya kutolea mafunzo kwa kuanza ujenzi wa jengo la ghorofa nane, ambalo litakuwa na miundombinu mbalimbali ikiwemo madarasa, karakana za uongezaji thamani madini, maabara za madini ya vito na bidhaa za usonara, *mineral gallery,* ofisi, hosteli kwa ajili ya wanafunzi, *canteen* na maduka.

(b) Utoaji wa mafunzo na huduma nyingine.

Mheshimiwa Spika, kituo kitafanya udahili wa wanafunzi 101 utakaojumuisha wanafunzi 60 wa kozi za muda mrefu na wanafunzi 41 wa kozi za muda mfupi. Kozi hizo zitahusisha fani za teknolojia ya madini ya vito na usonara, utambuzi wa madini ya vito, ukataji na ung'arishaji wa madini ya vito. Vilevile, kituo kitatoa huduma za maabara kwa madini ya vito na bidhaa za usonara.

(c) Uzalishaji wa Bidhaa.

Mheshimiwa Spika, kituo kinatarajia kununua mashine 27 za kukata na kung'arisha vito na kutengeneza bidhaa za usonara. Kupatikana kwa mashine hizo kutaongeza uwezo wa *TGC* kuzalisha bidhaa mbalimbali zikiwemo vinyago, mikufu, hereni na bidhaa nyinginezo za urembo na mapambo.

Mheshimiwa Spika, Taasisi ya Uhamasishaji Uwazi na Uwajibikaji katika Rasilimali Madini, Mafuta na Gesi Asilia *(TEITI)* itaandaa na kuweka wazi ripoti ya 15 ya *TEITI* inayoonesha

ulinganishi wa malipo ya kampuni za madini, mafuta na gesi asilia na mapato ya Serikali kwa mwaka 2022/2023.

Mheshimiwa Spika, *TEITI* itaweka wazi mikataba ambayo Serikali imeingia na kampuni za madini, mafuta na gesi asilia. *TEITI* itaweka wazi orodha ya wamiliki wa hisa katika kampuni za madini, mafuta na gesi asilia. *TEITI* itaendelea kuhamasisha na kutoa elimu kwa umma kuhusu matumizi ya takwimu za ripoti ya *TEITI* ili kutambua mchango wa sekta ya uziduaji katika uchumi wa nchi yetu ya Tanzania.

Mheshimiwa Spika, shukrani. Natambua wazi kuwa Serikali ya Awamu ya Sita imeendelea na juhudi kubwa za kuhakikisha kuwa uchumi wa nchi yetu unaimarika. Kasi, juhudi na ubunifu mkubwa wa utendaji kazi anaoendelea nao Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania vinadhihirisha wazi kuwa nchi yetu inaendelea kukua kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, aidha, kipekee nitumie fursa hii kumshukuru kwa dhati Mheshimiwa Rais kwa miongozo na maelekezo yake anayotupatia katika sekta ya madini ambayo yanaifanya sekta hii kuendelea kukua na kuvutia wawekezaji kwa manufaa ya Taifa.

Mheshimiwa Spika, nichukue fursa hii kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Philip Isdory Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa maelekezo na miongozo mbalimbali katika sekta ya madini ambayo amekuwa akiitoa, kusimamia utendaji wa shughuli mbalimbali kwa manufaa ya Taifa.

Mheshimiwa Spika, naomba pia nimshukuru Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Mbunge na Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa hotuba yake ambayo imetoa mwelekeo wa shughuli za Serikali kwa mwaka wa fedha 2024/2025.

Mheshimiwa Spika, kipekee namshukuru Mheshimiwa Dkt. Doto Mashaka Biteko, Mbunge na Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, ambaye amekuwa na msaada mkubwa kwenye sekta ya

madini kwa kutoa ushauri, maelekezo na miongozo mbalimbali ili kuhakikisha sekta hii inakuwa na mchango endelevu kwenye ukuaji wa uchumi wa nchi yetu ya Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ili Wizara iweze kutekeleza majukumu na malengo yaliyopangwa, yakiwemo ukusanyaji wa maduhuli ya shilingi 1,164,850,027,000.00, naomba Bunge lako Tukufu liridhie na kupitisha makadirio ya shilingi 231,983,614,000.00 kwa ajili ya matumizi ya Wizara na taasisi zake kwa mwaka wa fedha 2024/2025 kwa mchanganuo ufuatao: -

(i) Shilingi 140,661,200,000.00 sawa na 60% ya bajeti yote ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

(ii) Shilingi 91,322,414,000.00 sawa na 39.37% ya bajeti yote ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Kati ya fedha hizo, shilingi 24,872,875,000.00 ni kwa ajili ya mishahara ya watumishi na shilingi 66,449,539,000 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo ya Wizara na Taasisi zilizo chini yake.

Mheshimiwa Spika, kwa mara nyingine naomba nitoe shukrani zangu za dhati kwa Waheshimiwa Wabunge wote kwa kunisikiliza. Majedwali na vielelezo mbalimbali kwa ajili ya kutoa ufafanuzi wa masuala na takwimu muhimu kuhusu sekta ya madini vimeambatanishwa pamoja na hotuba hii.

Mheshimiwa Spika, hotuba hii pia inapatikana katika tovuti ya Wizara ya Madini kwa kikoa cha *https://www.madini.go.tz.*

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

## HOTUBA YA MHESHIMIWA ANTHONY PETER MAVUNDE (MB.), WAZIRI WA MADINI AKIWASILISHA BUNGENI MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025 - KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI

### A. UTANGULIZI

**1.** ***Mheshimiwa Spika,*** baada ya kupokea taarifa iliyowasilishwa Bungeni na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya

Nishati na Madini iliyochambua bajeti ya Wizara ya Madini, naomba kutoa hoja kwamba, Bunge lako Tukufu sasa likubali kupokea, kujadili na kupitisha Taarifa ya Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Madini kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 pamoja na Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Kawaida na ya Maendeleo ya Wizara ya Madini na Taasisi zake kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

**2.** ***Mheshimiwa Spika,*** awali ya yote, ninamshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema, kwa fadhila zake na kuijalia nchi yetu amani na utulivu na kutuwezesha kushiriki katika mkutano huu wa 15 wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwa unyenyekevu mkubwa, ninamuomba Mwenyezi Mungu atuongoze vyema na kutupa busara na hekima katika kujadili Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Madini kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 kwa nia njema ya kuendeleza nchi yetu na kuboresha ustawi na maendeleo ya watanzania.

**3.** ***Mheshimiwa Spika,*** nitumie fursa hii kumpongeza na kumshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa utendaji wake wenye maono, maridhiano, weledi, uwajibikaji na ujasiri kwa manufaa mapana ya Taifa. Aidha, Mheshimiwa Rais amekuwa na mchango mkubwa sana katika maendeleo ya Sekta ya Madini kwa kutoa miongozo, maagizo na maelekezo mbalimbali kwa ajili ya kuvutia uwekezaji na kuikuza sekta.

**4.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa namna ya kipekee nitumie fursa hii adhimu kutoa shukrani zangu za dhati kwa Mheshimiwa Rais kwa kuniamini na kunipa dhamana ya kusimamia Sekta ya Madini. ***Ni ahadi yangu kwa Mheshimiwa Rais, na Bunge lako Tukufu pamoja na Watanzania kwamba nitaitumikia nafasi hii kwa uadilifu, uaminifu na kwa uwezo wangu wote ili kuendeleza sekta hii muhimu***.

**5.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Uongozi wa Serikali ya Awamu ya Sita, Mheshimiwa Rais ametuonesha kwa vitendo namna anavyoithamini Sekta ya Madini kwa kushiriki yeye mwenyewe katika shughuli za madini ikiwemo kufanya uhamasishaji mkubwa kwenye uwekezaji. Pia, ameshiriki kwenye

hafla za utiaji saini mikataba ya uchimbaji wa madini, ununuzi na uzinduzi wa mitambo maalum ya uchorongaji kwa ajili ya kuwawezesha wachimbaji wadogo kuongeza tija na uwezeshaji katika ujenzi wa miundombinu mbalimbali ya shughuli za madini.

**6.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Awamu ya Sita tumeshuhudia mafanikio mbalimbali katika Sekta ya Madini ikiwemo: kuendelea kuongezeka kwa Mchango wa Sekta ya Madini kwenye Pato la Taifa kutoka asilimia 6.7 mwaka 2020, asilimia 7.3 mwaka 2021 hadi kufikia asilimia 9.1 mwaka 2022; ukusanyaji wa maduhuli ya Serikali uliongezeka kutoka shilingi 588,047,051,190.03 mwaka 2020/2021, shilingi 623,237,296,973.40 mwaka 2021/2022 hadi shilingi 678,042,598,813.92 mwaka 2022/2023.

**7.** ***Mheshimiwa Spika,*** mafanikio mengine ni pamoja na kuongezeka kwa masoko na vituo vya ununuzi wa madini kutoka 41 na 61 mwaka 2020/2021 hadi kufikia 42 na 100 mwaka 2023/2024 ambapo kulifanyika biashara ya madini yenye thamani ya shilingi 2,095,960,697,019.40 na shilingi 1,926,415,580,991.11 mtawalia. Aidha, Serikali imenunua mitambo mitano (5) ya uchorongaji kwa ajili ya wachimbaji wadogo na kuigawanya kwenye maeneo mbalimbali ya uchimbaji mdogo wa madini nchini.

**8.** ***Mheshimiwa Spika,*** ili kuendeleza Madini Muhimu na Madini Mkakati, Serikali imetoa leseni ya uchimbaji mkubwa wa madini Tembo (Heavy Mineral Sands) kwa mradi wa Tajiri uliopo Wilaya ya Pangani, Mkoa wa Tanga pamoja na Leseni ya Ujenzi wa Kiwanda cha Kusafisha Madini ya Metali Wilaya ya Kahama, Mkoa wa Shinyanga.

**9.** ***Mheshimiwa Spika***, namshukuru kwa dhati Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa miongozo yake mbalimbali anayoitoa yenye lengo la kuhakikisha kuwa Sekta ya Madini inakuwa na mchango endelevu na kuwanufaisha watanzania na Taifa kwa ujumla.

**10.** ***Mheshimiwa Spika***, napenda kumshukuru Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb.), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya

Muungano wa Tanzania kwa uongozi madhubuti na maelekezo anayoyatoa ili kufanikisha utendaji kazi Serikalini. Nimshukuru zaidi kwa hotuba yake iliyojaa maono mazuri aliyoiwasilisha hapa bungeni ambayo inatoa mwelekeo wa utekelezaji wa kazi za Serikali. Hotuba hiyo kwa kiasi kikubwa imeonesha mapitio ya uendeshaji wa shughuli za Serikali katika kipindi cha Mwaka wa Fedha 2023/2024 na Mpango wa Bajeti ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 pamoja na utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 2020.

**11.** ***Mheshimiwa Spika,*** napenda kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Doto Mashaka Biteko (Mb.), Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati kwa kuaminiwa na kuteuliwa na Mheshimiwa Rais kushika nyadhifa hizo. Aidha, nimshukuru kwa kazi kubwa aliyoifanya ya kuisimamia na kuijenga Sekta ya Madini kwa ubunifu na uadilifu mkubwa alipokuwa Waziri wa Madini.

**12.** ***Mheshimiwa Spika***, Viongozi hawa wote wamekuwa tayari kushirikiana nasi muda wote, kutusikiliza na kutupa maelekezo na miongozo mbalimbali ambayo yametusaidia sana katika kutekeleza majukumu ya Wizara kwa ufanisi zaidi.

**13.** ***Mheshimiwa Spika,*** naomba nitumie fursa hii kukupongeza wewe binafsi kwa kuendelea kuliongoza Bunge kwa ustadi, umahiri, hekima, busara na ubunifu mkubwa. Aidha, niwapongeze Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu (Mb.), Naibu Spika na Wenyeviti wa Bunge kwa kuendelea kushirikiana nawe katika kuliongoza Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa weledi mkubwa. Ni dhahiri kuwa mmeonesha ukomavu mkubwa wa kisiasa wakati wote wa kuendesha vikao vya Bunge. Tuna imani kuwa mtaendelea kuliongoza Bunge kufanya maamuzi sahihi na yenye tija kwa maslahi mapana ya Taifa na kulifanya Bunge letu liendelee kuheshimika ndani na nje ya nchi yetu.

**14.** ***Mheshimiwa Spika,*** naomba niwapongeze Mheshimiwa Dkt. David Mathayo David (Mb.), Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini na Mheshimiwa Kilumbe Shabani Ng'enda (Mb.), Makamu Mwenyekiti wa Kamati kwa kuchaguliwa kuiongoza Kamati hii. Aidha, nawapongeza wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini

kwa kuteuliwa kuwa wajumbe wa Kamati hiyo. Tunaipongeza Kamati kwa kazi nzuri wanayoifanya ya kutoa ushauri na maelekezo mbalimbali ambayo yanasaidia kuongeza ufanisi na umakini wa utendaji kazi wa Wizara. Vilevile, ninaishukuru Kamati kwa kujadili kwa kina Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fungu 100, kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 na kuyapitisha kwa kauli moja.

***Napenda kuliahidi Bunge lako Tukufu kuwa nitaendelea kuipa Kamati ushirikiano wa dhati katika kuhakikisha kuwa Sekta ya Madini inaendelea kuimarika na kuwanufaisha watanzania.***

**15.** ***Mheshimiwa Spika,*** napenda kutoa shukrani na pongezi kwa Bunge lako Tukufu kwa kazi nzuri ambazo limekuwa likifanya katika kuisimamia na kuishauri Serikali, ikiwemo Wizara ya Madini. Kupitia kwako, naliomba Bunge liendelee kutupatia ushirikiano ili kuiendeleza sekta hii muhimu katika kujenga uchumi shindani kwa maendeleo ya Taifa. Aidha, napenda kuwapongeza Waheshimiwa Mawaziri na Naibu Mawaziri wote kwa kuaminiwa na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuongoza Wizara mbalimbali. Pia, ninawashukuru wote kwa ushirikiano wanaonipa katika kutekeleza majukumu ya kusimamia Sekta ya Madini.

**16.** ***Mheshimiwa Spika***, kipekee kabisa, nitumie fursa hii kuwashukuru wananchi wa Jimbo la Dodoma Mjini kwa kuendelea kunipa ushirikiano kama Mbunge wao na kunivumilia ninapokuwa nikitekeleza majukumu mengine ya kitaifa kama Waziri wa Madini.

**17.** ***Mheshimiwa Spika,*** napenda nimshukuru kwa dhati kabisa Dkt. Steven Lemomo Kiruswa (Mb.), Naibu Waziri wa Madini, kwa ushirikiano anaonipa katika kutekeleza majukumu ya Wizara. Aidha, napenda kumshukuru Bw. Kheri Abdul Mahimbali, Katibu Mkuu, Bw. Msafiri Lameck Mbibo, Naibu Katibu Mkuu na Dkt. AbdulRahman Shabani Mwanga, Kamishna wa Madini kwa uchapakazi wao mahiri na ushirikiano wanaonipatia katika kutekeleza majukumu ya Wizara. Pia, niishukuru Menejimenti ya Wizara pamoja na Wenyeviti wa Bodi, Wakuu wa Taasisi zilizo chini

ya Wizara ya Madini pamoja na wafanyakazi wote kwa ushirikiano na utendaji kazi mzuri katika kutekeleza majukumu yao.

**18.** ***Mheshimiwa Spika,*** naishukuru sana familia yangu mke wangu Jacquelyne Moses Lupasa na watoto wangu Atarah na Allan kwa upendo, uvumilivu, ushirikiano na maombi yao wakati wote ninapotekeleza majukumu yangu. Wamekuwa wavumilivu na wenye ushirikiano mkubwa kwa kipindi chote ninapokuwa ninatekeleza majukumu ya ubunge na uwaziri na wamekubali kubeba baadhi ya majukumu ya familia.

**19.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa masikitiko makubwa naungana na wenzangu kutoa pole kwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, familia na watanzania wote kwa ujumla kwa kuondokewa na Viongozi wetu mashuhuri, shupavu, walioipenda na kuitumikia nchi hii ambao ni Hayati Ali Hassan Mwinyi, Rais Mstaafu wa Awamu ya Pili wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Hayati Edward Ngoyai Lowassa, Waziri Mkuu Mstaafu na Dkt. Ibrahim Msabaha aliyewahi kuwa Waziri wa Nishati na Madini. Tunawaombea kwa Mwenyezi Mungu awapumzishe kwa amani.

**20.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa masikitiko makubwa niungane na watanzania wengine kutoa pole kwa wananchi wa Jimbo la Mbarali kwa kuondokewa na aliyekuwa Mbunge wao Mheshimiwa Francis Mtega na wananchi wa Jimbo la Kwahani kwa kuondokewa na aliyekuwa Mbunge wao Mheshimiwa Ahmed Yahya Abdulwakil. Mwenyezi Mungu awarehemu.

**21.** ***Mheshimiwa Spika,*** kufuatia majanga mbalimbali yaliyosababishwa na mvua zinazoendelea kunyesha na ajali za barabarani naomba kutoa pole kwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na watanzania wote kwa ujumla kutokana na vifo, majeraha, upotevu na uharibifu wa mali na miundombinu. Majanga hayo ni pamoja na maporomoko ya udongo yaliyotokea huko Hanang na mafuriko ya Rufiji.

**22.** ***Mheshimiwa Spika,*** baada ya kutoa salamu za shukrani na pole, naomba sasa nijielekeze katika maeneo mahsusi ya hotuba hii ambayo ni: Mwenendo wa Biashara ya Madini Duniani; Mapitio

ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024; na Mpango na Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2024/2025.

## B. MWENENDO WA BIASHARA YA MADINI DUNIANI

**23.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa kipindi cha kuanzia Julai, 2023 hadi Machi, 2024, bei ya madini ya dhahabu kwa wakia ilipanda hadi kufikia wastani wa Dola za Marekani 2,138.01 ikilinganishwa na bei ya wastani wa Dola za Marekani 1,854.54 katika kipindi cha Julai 2022 hadi Machi 2023. Kuongezeka kwa bei ya dhahabu kunatokana na sababu mbalimbali ikiwemo mahitaji makubwa ya madini hayo duniani.

**24.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa upande wa madini ya almasi, katika kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024, mwenendo wa biashara ya madini hayo duniani umeendelea kusuasua kutokana na mdororo wa uchumi uliosababishwa na madhara ya vita kati ya Urusi na Ukraine. Madini hayo yameshuka bei duniani kwa asilimia 19 kwa mwezi Machi, 2024. Aidha, wastani wa mauzo ya madini ya almasi katika kipindi husika ni karati 201.71 yenye thamani ya dola za Marekani 43,231,183.71 ikilinganishwa na karati 271.74 yenye thamani ya dola za Marekani 50,824,739.77 katika kipindi cha Julai 2022 hadi Machi, 2023. Hatua zilizoanza kuchukuliwa na wazalishaji mbalimbali wa almasi duniani ni kupunguza uzalishaji wa almasi ili kuimarisha bei ya madini hayo.

**25.** ***Mheshimiwa Spika***, napenda kulifahamisha Bunge lako Tukufu kwamba nchi yetu ni miongoni mwa nchi zilizobarikiwa kuwa na madini mkakati ambayo uhitaji wake ni mkubwa kwenye nishati safi na salama na teknolojia nyingine za kisasa duniani. Aidha, uhitaji huu unatokana na utekelezaji wa azimio la pamoja la dunia la kupunguza hewa ya ukaa ifikapo 2050 (*Net Zero Emission*). Miongoni mwa madini mkakati yanayopatikana nchini ni pamoja na lithium, cobalt, nikeli, shaba, aluminium, zinki, kinywe na *rare earth elements* (REE).

**26.** ***Mheshimiwa Spika***, ili nchi yetu iweze kunufaika na madini hayo, Wizara imeandaa mkakati wa uendelezaji wa madini muhimu na madini mkakati hapa nchini. Mkakati huo unalenga kuhakikisha kwamba madini hayo yanaongezwa thamani hapa

nchini ikiwemo kuzalisha bidhaa zinazohitajika katika soko kama vile betri za magari ya umeme na hivyo kuongeza manufaa kwa nchi ikiwemo kuongeza mapato ya Serikali na ajira kwa Watanzania.



***Picha Na. 1:*** *Ujenzi wa kiwanda cha GodMwanga Gems Ltd cha kuchakata madini ya kinywe kilichopo Wilaya ya Handeni-Tanga.*

**27. Mheshimiwa Spika,** ili kuongeza manufaa yatokanayo na madini muhimu na madini mkakati, kwa mara ya kwanza kitajengwa kiwanda kikubwa na cha kisasa cha usafishaji na uongezaji thamani madini cha Multi Metals Processing Facility katika eneo maalumu la ukanda wa kiuchumi la Buzwagi Special Economic Zone lililopo Wilaya ya Kahama.

## C. MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024

### I. Mapato

**28.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha 2023/2024, Bunge lako Tukufu liliidhinisha bajeti ya jumla ya shilingi 89,357,491,000.00 kwa Wizara ya Madini. Baada ya marejeo yaliyofanyika kwa kuongeza fedha za maendeleo shilingi 74,823,300,000.00 ilifanya bajeti ya Wizara kufikia shilingi 163,008,241,000.00. Kati ya bajeti hiyo, shilingi 45,877,443,000.00 ni fedha za matumizi mengineyo, shilingi 20,307,498,000.00 mishahara ya watumishi wa Wizara na taasisi zake na shilingi 96,823,300,000.00 ni kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

**29.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa upande wa ukusanyaji wa maduhuli ya Serikali, katika mwaka 2023/2024, Wizara ilipangiwa kukusanya jumla ya shilingi 1,006,705,169,300.00. Kati ya fedha hizo, shilingi 882,128,205,000.00 zilipangwa kukusanywa na kuwasilishwa Hazina na shilingi 124,576,964,300.00 zilipangwa kukusanywa na kutumiwa na taasisi zilizo chini ya Wizara.

**30.** ***Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024, Wizara imepokea jumla ya shilingi 135,695,115,605.50 sawa na asilimia 83.24. Kati ya fedha hizo shilingi 35,109,940,171.76 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo, shilingi 16,322,908,519.34 ni kwa ajili ya mishahara na shilingi 84,262,266,914.40 ni matumizi ya maendeleo. Aidha, shilingi 924,951,402.63 zimepokelewa kupitia akaunti ya amana kwa ajili ya awamu ya pili ya ujenzi wa jengo la Wizara ya Madini Makao Makuu pamoja na Jengo la Ofisi ya Makao Makuu ya Tume ya Madini. Majengo yote yanajengwa hapa Jijini Dodoma.

**II. Miradi ya Maendeleo**

**31.** ***Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024, Wizara ilipokea na kutumia fedha za maendeleo shilingi 75,907,393,763.15 kwa ajili ya kukamilisha usanifu wa jengo la Kituo cha Jemolojia Tanzania (TGC); ununuzi wa magari; kugharamia mihadi ya kisheria (Deed of Settlement) kati ya Serikali na Kampuni ya *Winshear Gold Corporation*; na kuwajengea uwezo watumishi wa TGC na watendaji wa Wizara katika shughuli za uongezaji thamani madini.

**III. Utekelezaji wa Shughuli Mahsusi**

**32.** ***Mheshimiwa Spika,*** ili kuhakikisha Sekta ya Madini inaendelea kukua na kuwanufaisha watanzania ikiwa ni pamoja na kuongeza mchango wake kwenye Pato la Taifa, mwaka 2023/2024 Wizara ilijielekeza katika utekelezaji wa shughuli zifuatazo: kuimarisha ukusanyaji wa maduhuli na kuongeza mchango wa Sekta ya Madini kwenye Pato la Taifa; kuendeleza madini muhimu na madini mkakati; kuwaendeleza na kusogeza huduma za ugani kwa wachimbaji wadogo; kuhamasisha shughuli za uongezaji thamani madini; kuhamasisha uwekezaji na biashara katika Sekta

ya Madini na uanzishwaji wa minada na maonesho ya madini ya vito; na kuzijengea uwezo taasisi zilizo chini ya Wizara ya Madini ili ziweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.

**(a) Kuimarisha Ukusanyaji wa Maduhuli na Kuongeza Mchango wa Sekta ya Madini kwenye Pato la Taifa**

**33.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha 2023/2024, Wizara ilipangiwa kukusanya maduhuli ya shilingi 1,006,705,169,300.00 kutoka katika vyanzo mbalimbali. Kati ya fedha hizo, shilingi 882,128,205,000.00 zilipangwa kukusanywa na kuwasilishwa Hazina ambapo hadi Machi, 2024 shilingi 548,297,119,748.13 zimekusanywa na kuwasilishwa Hazina. Makusanyo hayo ni sawa na asilimia 62.1 ya lengo la makusanyo kwa mwaka.

**34.** ***Mheshimiwa Spika,*** Taasisi zilizo chini ya Wizara zilipangiwa kukusanya na kutumia shilingi 124,576,964,300.00 ambapo hadi kufikia Machi, 2024 shilingi 41,184,565,856.15 zilikusanywa sawa na asilimia 33 ya lengo la makusanyo kwa mwaka. Aidha, malengo ya makusanyo hayo hayakufikiwa kutokana na mvua kubwa zilizonyesha mwaka huu. Mvua hizo ziliathiri kwa kiasi kikubwa miradi ya STAMICO ikiwemo shughuli za uchorongaji, uzalishaji na usafirishaji wa makaa ya mawe na usimikaji wa mitambo miwili (2) ya kuzalisha mkaa mbadala unaotokana na makaa ya mawe (coal briquette).

**35.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kupambana na kudhibiti vitendo vya utoroshaji wa madini nchini unaofanywa na wachimbaji na wafanyabiashara wa madini wasio waaminifu. Katika kipindi cha kuanzia Julai 2023 hadi Machi 2024 Wizara kwa kushirikiana na mamlaka nyingine za Serikali imefanikiwa kukamata madini ya aina mbalimbali yenye thamani ya jumla ya shilingi 3,971,436,761.29 katika Mikoa ya kimadini ya Geita, Songwe, Chunya, Kahama, Mbeya na Kilimanjaro. Aidha, madini hayo yaliyokamatwa yalitaifishwa na wahusika 157 walifikishwa kwenye vyombo vya Sheria. ***Napenda kuwahimiza wachimbaji na wafanyabiashara kuzingatia Sheria, Kanuni na Taratibu zinazosimamia Sekta ya Madini.***

**36.** ***Mheshimiwa Spika***, kutokana na jitihada zilizofanyika kumekuwa na ongezeko la ukusanyaji wa maduhuli ambapo katika kipindi cha Julai, 2023 hadi Machi, 2024 jumla ya shilingi 548,297,119,748.13 zimekusanywa na kuwasilishwa katika Mfuko Mkuu wa Serikali ikilinganishwa na shilingi 509,389,265,413.90 zilizokusanywa katika kipindi kama hicho Mwaka wa Fedha 2022/2023 sawa na ongezeko la asilimia 7.4. Aidha, ili kuongeza maduhuli ya Serikali, Wizara imeimarisha usimamizi na ukaguzi kwenye maeneo ya uchimbaji, masoko ya madini, vituo vya ununuzi wa madini na mipaka ya nchi.

**37.** ***Mheshimiwa Spika***, kasi ya ukuaji wa Sekta ya Madini na mchango wake kwenye Pato la Taifa imeendelea kuimarika. Mathalani, mwaka 2022 Sekta ya Madini ilikua kwa asilimia 10.9 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 9.4 mwaka 2021. Aidha, mchango wa Sekta ya Madini katika Pato la Taifa uliongezeka na kufikia asilimia 9.1 kwa mwaka 2022, ikilinganishwa na mchango wa asilimia 7.3 mwaka 2021. Pia, mchango wa Sekta ya Madini katika Pato la Taifa kwa robo ya tatu (Januari hadi Septemba, 2023) ulifikia asilimia 10.9 ikilinganishwa na asilimia 9.5 kwa kipindi kama hicho mwaka 2022.

**38.** ***Mheshimiwa Spika,*** mwenendo wa mapato ya fedha za kigeni kupitia Sekta ya Madini umekuwa ukiimarika mwaka hadi mwaka. Mwaka 2023 madini yenye thamani ya dola za Marekani milioni 3,551.4 yaliuzwa nje ya nchi sawa na asilimia 56.2 ya mauzo ya bidhaa zisizo za asili (non traditional goods) ikilinganishwa na mauzo ya dola za Marekani milioni 3,395.3 sawa na asilimia 56.0 mwaka 2022. Hivyo, mauzo ya madini ya mwaka 2023 yaliongezeka kwa dola za Marekani milioni 156.1 ambayo ni asilimia 4.6 kutoka mauzo ya mwaka 2022.

**39.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka 2023, jumla ya vibali 11,258 vya kuuza madini nje ya nchi vilitolewa ikilinganishwa na vibali 10,318 vilivyotolewa Mwaka 2022. Ongezeko la vibali hivyo kwa kiasi kikubwa limetokana na kuongezeka kwa uhitaji wa madini ya vito na makaa ya mawe nje ya nchi. Aidha, katika kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024, jumla ya vibali 115 vya uingizaji madini nchini vilitolewa ikiwa ni hatua mojawapo ya kusimamia na kudhibiti biashara ya madini nchini.

**40.** ***Mheshimiwa Spika,*** mwenendo wa mapato ya kodi yatokanayo na Sekta ya Madini umekuwa ukiongezeka mwaka hadi mwaka. Mwaka 2022/2023 mapato ya kodi yatokanayo na Sekta ya Madini yalifikia shilingi 3,143,212,216,996.76 sawa na asilimia 13.9 ya mapato yote ya kodi yaliyokusanywa na TRA. Aidha, mapato haya yameongezeka kwa asilimia 50.3 kutoka shilingi 2,091,256,445,986.27 mwaka 2021/2022.

### *(b)* Kuendeleza Madini Muhimu na Madini Mkakati

**41.** ***Mheshimiwa Spika***, jitihada mbalimbali zimeendelea kufanyika kuhakikisha madini muhimu na madini mkakati yananufaisha Taifa. Jitihada hizo ni pamoja na kufanya tafiti na kutangaza fursa za uwepo wa madini nchini kupitia maono ya ***Vision 2030: Madini ni Maisha na Utajiri***. Aidha, suala la madini muhimu na madini mkakati ni miongoni mwa maboresho yaliyopendekezwa kufanyika katika Sheria ya Madini, Sura 123 kupitia muswada wa marekebisho ya Sheria mbalimbali namba 4 wa Mwaka 2024 ambao ulisomwa kwa mara ya kwanza katika mkutano wa 14 wa Bunge. Lengo la maboresho hayo ni kuweka usimamizi thabiti wa madini mkakati na madini muhimu ili kupata manufaa mapana kupitia mnyororo wa thamani wa madini hayo.

**42.** ***Mheshimiwa Spika***, kwa kipindi cha kuanzia Julai 2023 hadi Machi 2024, leseni ya Uchimbaji Mkubwa wa Madini ya *Heavy Mineral Sands* imetolewa kwa Kampuni ya Nyati Mineral Sands Limited (NYSL) katika mradi wa Tajiri uliopo Wilaya ya Pangani mkoani Tanga na leseni ya usafishaji madini imetolewa kwa kampuni ya Tembo Nickel Refining Company Limited uliopo Wilaya ya Kahama mkoani Shinyanga.

**43.** ***Mheshimiwa Spika,*** thamani ya uwekezaji katika miradi hii inatarajiwa kuwa jumla ya dola za Marekani milioni 760.23 sawa na shilingi trilioni 1.78. Uwekezaji huu utaongeza ajira, kodi, tozo mbalimbali, manufaa yatokanayo na uwajibikaji wa kampuni za madini kwa jamii (CSR) na ushirikishwaji wa watanzania katika uuzaji wa bidhaa na utoaji huduma katika shughuli za madini na uhawilishaji wa teknolojia kwa watalaam wa kitanzania.

**44. *Mheshimiwa Spika,*** Serikali inaendelea kuhamasisha uwekezaji katika madini muhimu na mkakati ili madini hayo yaweze kunufaisha Taifa kutokana na uhitaji wake kwa ajili ya teknolojia mbalimbali pamoja na kupunguza hewa ya ukaa duniani. Kutokana na uhamasishaji huo Wizara imeendelea kupokea maombi mbalimbali ya uwekezaji kwenye madini hayo ikiwemo ombi la leseni ya uchimbaji wa madini ya kinywe la Kampuni ya Duma Tanzgraphite Limited (DTL) katika eneo la Epanko, Wilaya ya Ulanga.

***Kwa kuwa kuna uhitaji mkubwa wa madini hayo duniani kwa sasa, nachukua fursa hii kuwakaribisha wawekezaji kuendelea kuwekeza nchini kwenye utafutaji, uchimbaji, uchenjuaji na uongezaji thamani pamoja na biashara ya madini nchini hususani kwenye madini muhimu na mkakati.***




***Picha Na. 2:*** *Waziri wa Madini Mhe. Anthony P. Mavunde (Mb.) akiwa kwenye hafla ya kukabidhi leseni za uchimbaji mkubwa wa madini mkakati.*

### (c) Kuwaendeleza Wachimbaji Wadogo na Kusogeza Huduma za Ugani kwa Wachimbaji Wadogo

**45. *Mheshimiwa Spika,*** kwa kutambua mchango wa wachimbaji wadogo katika kukuza uchumi wa mtu mmoja mmoja na Taifa kwa ujumla, Wizara imeliwezesha Shirika la Madini la Taifa (STAMICO) kununua mitambo mitano (5) ya uchorongaji kwa ajili ya wachimbaji wadogo. Mitambo hiyo tayari imeanza kazi ya

uchorongaji kuanzia tarehe 4 Desemba, 2023 katika maeneo ya leseni za wachimbaji wadogo ya Nyamongo-Tarime, Itumbi-Chunya, LwamgasaGeita, Katente-Bukombe, Buhemba-Butiama na NholiDodoma.




***Picha Na. 3:*** *Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania akiwa na Mhe. Anthony P. Mavunde (Mb.), Waziri wa Madini wakati wa uzinduzi wa Mitambo ya uchorongajii inayomilikiwa na STAMICO kwa ajili ya kuwahudumia wachimbaji wadogo.*

**46.** ***Mheshimiwa Spika,*** STAMICO inakusudia kufanya ujenzi wa vituo vipya viwili vya mfano vya kuchakata madini ya chokaa na chumvi. Kituo kwa ajili ya kuchakata madini ya chokaa kitajengwa katika eneo la Kona Z Mkoa wa Tanga na kituo kwa ajili ya kuchakata chumvi kitajengwa katika eneo la Nangurukuru-Kilwa. Aidha, STAMICO imeanza utekelezaji wa hatua za mwanzo za kuainisha mahitaji ya ujenzi wa vituo hivyo.

**47.** ***Mheshimiwa Spika***, kupitia vituo vya mfano vilivyopo Katente, Lwamgasa na Itumbi, STAMICO imeendelea kutoa huduma ya uchenjuaji wa dhahabu na kwa gharama nafuu kwa wachimbaji wadogo na kukusanya jumla ya shilingi milioni 794.13 katika kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024. Aidha, STAMICO imekifanyia maboresho Kituo cha Mfano cha Lwamgasa ili kuongeza uwezo wa kituo kuchenjua mbale ya madini ya dhahabu kutoka tani 9 hadi tani 30 kwa siku.

**48.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuwaendeleza wachimbaji wadogo ili kuwawezesha kushiriki kikamilifu katika shughuli za madini. Wizara na taasisi zake ilitoa mafunzo kwa wachimbaji wadogo 10,213 kuhusu masuala ya usalama migodini, afya na utunzaji wa mazingira. Aidha, wachimbaji hao walipatiwa

mafunzo kuhusu biashara ya madini pamoja na ulipaji kodi na mirabaha ya Serikali.

**49.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kwa kushirikiana na Shirikisho la Vyama vya Wachimbaji Wadogo Tanzania (FEMATA) iliratibu ziara ya mafunzo kwa wachimbaji na wafanyabiashara zaidi ya 100 nchini China. Katika ziara hiyo wachimbaji wadogo walipata fursa ya kutembelea viwanda vinavyotengeneza mitambo na vifaa vya uchimbaji na uchenjuaji wa madini pamoja na kukutana na wafanya biashara wa madini wa China. Ziara hiyo iliwawezesha wachimbaji hao kupata ujuzi, uzoefu na kujifunza kuhusu teknolojia mpya na kutafuta masoko ya madini.

**50.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia taasisi zake imeendelea kuwahamasisha wachimbaji wadogo kutunza kumbukumbu za uzalishaji na biashara za madini ikiwa ni moja ya vigezo vitakavyowawezesha kupata mikopo kwenye taasisi za fedha. Katika kipindi cha Julai 2023 hadi Machi, 2024 jumla ya shilingi bilioni 187 zilikopeshwa kwa wachimbaji ikilinganishwa na shilingi bilioni 145 zilikopeshwa kwa mwaka 2022.

***Nitumie fursa hii kushukuru benki za CRDB, NMB, AZANIA* na *KCB kwa kukubali kuwakopesha wachimbaji. Nitoe wito kwa taasisi nyingine za fedha zione umuhimu wa kuwakopesha wachimbaji kwa lengo la kuwawezesha kufanya shughuli zao kwa tija.***

**(c) Kuhamasisha Shughuli za Uongezaji Thamani Madini**

**51.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Tume ya Madini imeendelea kusimamia Kanuni za Madini (Uongezaji Thamani Madini) za Mwaka 2020 ambazo zinasimamia na kuratibu shughuli za uongezaji thamani madini kwa kila aina ya madini yapatikanayo hapa nchini. Aidha, katika kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024, Wizara kupitia Tume ya Madini imetoa leseni ya kusafisha madini ya nickel, cobalt na shaba kwa Tembo Nickel Refining Company Limited.

**52.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeanzisha majadiliano na wachimbaji wakubwa wa madini ya dhahabu nchini kwa ajili ya kutenga sehemu ya uzalishaji wao ili kusafisha madini ya dhahabu

katika viwanda vilivyopo nchini. Kwa upande mwingine, Wizara kupitia Kituo cha Jemolojia (TGC) kilichopo Jijini Arusha imeendelea kusimamia utolewaji wa mafunzo ya uongezaji thamani madini ya vito na baadhi ya madini ya metali.



***Picha Na. 4:*** *Wanafunzi wakiwa katika mafunzo ya uongezaji thamani madini ya vito katika Kituo cha TGC*

**53.** ***Mheshimiwa Spika*****,** Wizara imeendelea kuvutia na kuhamasisha shughuli za uongezaji thamani madini nchini kwa kupunguza malipo ya mrabaha kutoka asilimia 6 hadi 4 na kufuta ada ya ukaguzi ya asilimia 1 kwa madini yatakayouzwa kwenye viwanda vya usafishaji dhahabu vilivyopo nchini.

**54.** ***Mheshimiwa Spika*****,** katika kuhakikisha tunakuwa na wataalamu wa uongezaji thamani madini ya vito nchini, Wizara kupitia Kituo cha TGC imeendelea na maandalizi ya ujenzi wa jengo la ghorofa nane (8) litakalokuwa na madarasa, vyumba vya kulala wanafunzi, karakana za uongezaji thamani madini, maabara za madini ya vito, bidhaa za usonara na ofisi za watumishi. Hadi kufikia Machi, 2024 Mshauri Elekezi alikuwa amekamilisha kazi ya usanifu wa jengo na taratibu za kumpata mkandarasi wa ujenzi zinaendelea.

**(e) Kuhamasisha Uwekezaji, Biashara na Uanzishwaji wa Minada na Maonesho ya Madini ya Vito**

**55.** ***Mheshimiwa Spika*****,** katika kuhamasisha uwekezaji nchini, Wizara ilitangaza fursa za uwekezaji na kutoa elimu kwa Umma

kupitia ziara mbalimbali za viongozi, kwenye vyombo vya habari, mikutano ya kitaifa, kikanda na kimataifa.

**56. *Mheshimiwa Spika,*** Wizara ilishiriki kwenye mikutano, makongamano na maonesho ya Kitaifa, Kikanda na Kimataifa kwa lengo la kutangaza fursa za uwekezaji zilizopo nchini na kuvutia wawekezaji. Fursa hizo zilitangazwa kupitia Mkutano wa Future Minerals Forum– Saudi Arabia, Mining Indaba–Afrika Kusini, Prospectors and Developers Association of Canada (PDAC)– Canada, Africa Down Under–Australia na African Diamond Producers Association (ADPA)– Zimbabwe.




***Picha Na. 5:*** *Katibu Mkuu wa Wizara ya Madini Bw. Kheri Abdul Mahimbali akishiriki mkutano wa Mining Indaba–Afrika Kusini*

**57. *Mheshimiwa Spika,*** Wizara iliandaa na kushiriki mikutano ya ndani ikiwemo Mkutano wa Kimataifa wa Madini uliofanyika JNICC–Dar es Salaam, Mkutano wa Sita wa Wakandarasi wa Utafutaji Madini kwenye Sakafu ya Bahari Kuu ulioandaliwa na *International Seabed Authority (ISA)* uliofanyika Oktoba, 2023 Dar es Salaam.



***Picha Na. 6:*** *Baadhi ya washiriki wa mkutano wa sita (6) wa kimataifa wa wakandarasi wanaojihusisha na uchimbaji madini yanayopatikana chini ya sakafu ya bahari kuu uliofanyika Jijini Dar es Salaam*

**58.** ***Mheshimiwa Spika,*** kupitia mikutano hiyo kampuni mbalimbali zilionesha nia ya kuwekeza nchini na washiriki walipata nafasi ya kujifunza na kuongeza ujuzi kuhusu matumizi ya teknolojia za kisasa katika shughuli za madini, kufahamu hatua zilizofikiwa kuhusu utafutaji wa madini chini ya sakafu ya bahari kuu, kujenga na kukuza diplomasia ya uchumi ambayo ni msingi wa ustawi wa biashara na uwekezaji baina ya nchi yetu na nchi nyingine.

**59.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara ilishiriki maonesho mbalimbali ikiwemo Maonesho ya Sita ya Teknolojia na Uwekezaji katika Sekta ya Madini yaliyofanyika mjini Geita, Maonesho ya Kwanza ya Teknolojia na Uwekezaji katika Sekta ya Madini yaliyofanyika Lindi-Ruangwa na Maonesho ya 47 ya Kimataifa ya Sabasaba yaliyofanyika mwaka 2023. Washiriki waliotembelea mabanda ya Wizara na taasisi zake walipata elimu kuhusu masuala ya Sera, Sheria na Miongozo mbalimbali inayosimamia Sekta ya Madini pamoja na kufahamu fursa za uwekezaji zilizopo.

**60.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea na juhudi za kuanzisha minada na maonesho ya madini ya vito ya kitaifa na kimataifa. Katika kujenga uwezo wa uendeshaji wa minada na

maonesho hayo, Wizara ilishiriki katika Maonesho ya 68 na 69 ya Kimataifa ya Vito na Bidhaa za Usonara jijini Bangkok Thailand pamoja na kushiriki katika shughuli nyingine kujifunza masuala ya uongezaji thamani madini na minada ya madini ya vito. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na Soko la Bidhaa Tanzania imeendelea kuandaa mfumo wa usimamizi na uendeshaji wa minada ya ndani ya madini ya vito.




***Picha Na. 7:*** *Naibu Katibu Mkuu Bw. Msafiri Mbibo akiwa na washiriki wa Maonesho ya Kimataifa ya 68 ya Madini ya vito Bangkok, Thailand*

**61.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024, kiasi cha karati 4,115.22 za madini ya almasi, karati 19,728.45 na tani 35.43 za madini ya tanzanite na kiasi cha karati 86,920.09 na tani 45,875.42 za madini mengine ya vito yaliuzwa katika masoko ya madini. Mauzo ya madini hayo yamechangia makusanyo (mrabaha na ada ya ukaguzi) kiasi cha shilingi bilioni 133.79.

**62.** ***Mheshimiwa Spika,*** watanzania na wadau wameendelea kuelimishwa na kufahamishwa kuhusu uwepo wa fursa za uwekezaji katika Sekta ya Madini nchini ikiwemo sheria, kanuni na miongozo inayosimamia sekta. Aidha, elimu ilitolewa kupitia njia mbalimbali za mawasiliano kupitia jarida maalumu na program maalumu za urushwaji wa vipindi mubashara vilivyoelezea masuala mbalimbali yanayohusu Sekta ya Madini.

**(f) Kuzijengea Uwezo Taasisi Zilizo Chini ya Wizara ili Ziweze Kutekeleza Majukumu Yake**

***63. Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kuhakikisha kuwa taasisi zilizo chini yake zinatekeleza majukumu yake kwa ufanisi kwa kuzipatia vitendea kazi na rasilimaliwatu. Tume ya Madini imewezeshwa kuendelea na ujenzi wa jengo la ofisi makao makuu ambapo ujenzi umefikia asilimia 77; STAMICO imewezeshwa kununua mitambo 2 ya uzalishaji wa mkaa mbadala (*coal briquette*) ambayo imesimikwa Kisarawe-Pwani na Kiwira-Mbeya; GST imewezeshwa kununua vitendea kazi kwa ajili ya shughuli za utafiti wa madini; na Kituo cha TGC kimewezeshwa kuboresha miundombinu ya kufundishia kwa lengo la kukuza shughuli za uongezaji thamani madini nchini.

**IV. Utekelezaji wa Maeneo Mengine**

***64. Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024, Wizara imefanya utekelezaji kwenye maeneo mengine kama ifuatavyo:

**a) Shughuli za Baruti**

***65. Mheshimiwa Spika,*** mahitaji na matumizi ya baruti kwa sasa yameongezeka kutokana na kuimarika kwa shughuli za uchimbaji wa madini na ujenzi wa miundombinu mbalimbali. Katika kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024, vibali 252 vya kuingiza, kupitisha, kutengeneza na kuuza baruti nchini pamoja na vibali vya kusafirisha baruti nje ya nchi vimetolewa. Fedha zilizopatikana kupitia utolewaji wa vibali hivyo ni jumla ya dola za Marekani 126,600.

***66. Mheshimiwa Spika,*** Wizara ilitoa vibali nane (8) kwa ajili ya utengenezaji wa baruti aina ya *emulsion* kwa kutumia gari za *Mobile Manufacturing Unit* (MMU). Kati ya vibali hivyo, saba (7) vilitolewa kwa Kampuni ya Orica Tanzania Limited na kibali kimoja (1) kwa Kampuni ya Dangote Cement Limited ambavyo vitatumika kwa muda wa miaka miwili. Kupitia vibali hivyo jumla ya dola za Marekani 9,600 zimekusanywa.

**67.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara ilifanya ukaguzi kwenye maeneo yaliyoombewa kujengwa maghala ya kuhifadhi baruti. Maeneo yaliyofanyiwa ukaguzi ni Saleni – Pwani, Manyoni na Itigi – Singida, Kahama na Bushimangila–Shinyanga na Eneo Tengefu la Mirerani – Manyara. Ukaguzi huo ulibaini kuwa maeneo hayo yalikidhi matakwa ya Sheria ya Baruti, Sura ya 45 na hivyo kupewa vibali vya ujenzi wa maghala ya kuhifadhi baruti.

**68.** ***Mheshimiwa Spika,*** maghala nane (8) mapya ya kuhifadhi baruti yaliyojengwa na Kampuni za Siontinto, Solar Nitro Chemicals Ltd, ESAP Mining Services na Shanta Gold Mine yalikaguliwa na leseni zilitolewa. Aidha, Wizara ilifanya ukaguzi wa maghala 30 ya kuhifadhi baruti ili kuhakikisha shughuli za baruti zinafanyika kwa mujibu Sheria ya Baruti, Sura ya 45.

### b) Ushirikishwaji wa Watanzania Katika Shughuli za Madini (Local Content) na Wajibu wa Kampuni kwa Jamii (CSR)

**69.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024, Wizara kupitia Tume ya Madini ilipokea na kupitia jumla ya mipango 801 ya ushirikishwaji wa Watanzania katika shughuli za Madini ambapo mipango 797 iliidhinishwa na mipango minne (4) haikukidhi vigezo hivyo wahusika walitakiwa kufanya marekebisho stahiki. Aidha, Wizara kupitia Tume ya Madini ilipokea na kuchambua maombi ya vibali vya ununuzi 154 kutoka katika migodi ya Geita Gold Mining Limited, Bulyanhulu Gold Mine Limited, North Mara Gold Mine Limited, Shanta Mining Company Limited, Lindi Jumbo Limited, Buckreef Gold Company Limited, Mamba Corporation Limited, Tembo Nickel, Mantra Tanzania Limited, Zeus Resources na AUMS Tanzania Limited. Pia, maombi 447 ya ununuzi wa bidhaa na huduma (local content) yalipokelewa yaliidhinishwa na kupata kibali cha ununuzi.

**70.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2023 kampuni za kitanzania ziliuza migodini bidhaa na huduma zenye thamani ya dola za Marekani bilioni 1.48 ambayo ni sawa na asilimia 90 ya mauzo yote yaliyofanyika migodini yenye thamani ya dola za Marekeni bilioni 1.65. Mauzo hayo yaliyofanywa na kampuni za kitanzania kwa mwaka 2023 yalikuwa ni zaidi ya mauzo yaliyofanywa mwaka 2022 ambayo yalikuwa na thamani ya dola

za Marekani milioni 713 sawa na asilimia 82 ya mauzo yote ya dola za Marekani milioni 874 kwa mwaka huo.

**71.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuimarisha utoaji wa huduma migodini, kampuni tatu (3) za kitanzania zimejenga viwanda vya kutengeneza vifaa vinavyotumika migodini katika eneo la Buzwagi Special Economic Zone. Kampuni hizo ni Max Steel Limited iliyopo Dar es Salaam ambayo inatarajia kuzalisha vifaa (wire mesh and rock bolts) vinavyotumika kushikiza na kuzuia kudondoka kwa miamba kwenye migodi ya chini ya ardhi ambapo ujenzi wake umefikia asilimia 90. Aidha, kampuni ya Rock Solutions Limited inajenga kiwanda cha kuzalisha *core trays* jijini Mwanza na ujenzi wake umefikia asilimia 90. Pia, kampuni ya East African Conveyors Supplies Limited imejenga kiwanda cha kuzalisha *conveyor belts* Manispaa ya Kahama ambapo ujenzi wake umekamilika na wameshaanza usambazaji wa bidhaa hizo katika migodi ya ndani na nje ya nchi.

***Napenda kutumia fursa hii kupitia Bunge lako Tukufu kuwahamasisha watanzania kuchangamkia fursa ya kuanzisha viwanda vya kuzalisha vifaa pamoja na bidhaa mbalimbali zinazotumika migodini.***

**72.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kuhakikisha kuwa watanzania wanapatiwa kipaumbele kwenye ajira zinazozalishwa katika migodi mikubwa na ya kati ya uchimbaji madini hapa nchini. Hadi kufikia Machi 2024 jumla ya ajira 19,356 zilizalishwa, ambapo ajira 18,853 sawa na asilimia 97 zilitolewa kwa watanzania na ajira 505 sawa na asilimia 3 zilitolewa kwa wageni. Ajira kwa watanzania kwenye migodi zitaendelea kuongezeka ikiwa ni utekelezaji wa Sheria ya Madini, Sura 123 na Kanuni za Madini (Ushirikishwaji wa Watanzania) za mwaka 2018.

**73.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kuhakikisha kwamba wawekezaji kwenye Sekta ya Madini wanawajibika kwa jamii zinazozunguka miradi ya wawekezaji hao (CSR). Katika kipindi cha Julai, 2023 hadi Machi, 2024 kiasi cha shilingi 17,084,055,359.58 kimetumika kwa ajili ya miradi mbalimbali ya CSR kwa Halmashauri na miji inayozunguka migodi ya Tembo Nickel, Geita Gold, Bulyanhulu Gold Mine Limited, North Mara Gold Mine

Limited, Williamson Diamond Limited, Shanta Mining Company Limited, Dangote Cement Limited, Uranex Tanzania Limited, Ruvuma Coal Limited na Buckreef Gold Company Limited.

***Nitoe rai kwa wamiliki wa leseni za Madini na Halmashauri husika kufuata Sheria ya Madini na Kanuni zinazosimamia utekelezaji wa shughuli za CSR.***

**74.** ***Mheshimiwa Spika,*** sambamba na usimamizi wa utekelezaji wa CSR, katika kipindi cha Julai, 2023 hadi Machi, 2024 Wizara na Taasisi zake imetoa mafunzo kuhusu Kanuni za CSR kwa wadau mbalimbali wa Sekta ya Madini. Wadau hao ni pamoja na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini; Kampuni za Geita Gold Mining Limited, Tancoal Energy Limited, North Mara na Bulyanhulu; Chama cha Wanawake Wachimbaji Madini (TAWOMA); Viongozi wa Mikoa ya Geita na Ruvuma; na Viongozi wa Halmashauri za Wilaya ya Nyang'hwale, Simanjiro, Songwe, Ikungi na Msalala. Mafunzo hayo yalisaidia kuongeza uelewa wa kanuni za CSR na wajibu wa kila mdau katika utekelezaji wake.

### c) Marekebisho ya Sheria na Uandaaji wa Kanuni

**75.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kuhakikisha kunakuwa na mazingira bora ya uwekezaji kwa wadau wa Sekta ya Madini. Lengo ni kuwezesha wadau hao kufanya shughuli zao katika mazingira rafiki na yatakayoleta tija.

**76.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara iliandaa mapendekezo ya marekebisho ya Sheria ya Madini Sura ya 123 ambayo yaliwasilishwa na kusomwa kwa mara ya kwanza katika mkutano wa 14 wa Bunge kupitia Muswada wa Marekebisho ya Sheria mbalimbali Na. 4 ya Mwaka 2024.

### d) Upatikanaji wa Fedha za Kigeni

**77.** ***Mheshimiwa Spika***, katika kuhakikisha kuwa mchango wa Sekta ya Madini katika kuliingizia taifa fedha za kigeni unaongezeka, Wizara itaendelea kusimamia utekelezaji wa matakwa ya kifungu cha 10 cha Sheria ya Mamlaka ya Nchi Kuhusu Umiliki wa Utajiri Asilia na Maliasilia za Nchi, Sura ya 449

kinachoweka sharti la mapato yatokanayo na uvunaji wa maliasilia za nchi ikiwemo madini kuwekwa katika taasisi za fedha zilizopo nchini. Aidha, Wizara inaendelea kushirikiana na mamlaka nyingine za Serikali ikiwemo BoT katika kuhakikisha kuwa malipo ya mauzo ya madini yaliyofanyika nje ya nchi yanarejeshwa nchini. Lengo ni kuhakiki kama malipo hayo yamefanyika na kuhifadhiwa kwa kuzingatia masharti ya Kanuni za Fedha za Kigeni za Mwaka 2022.

> ***Nitoe wito kwa wachimbaji na wafanyabiashara ya madini kuzingatia sheria na kanuni zinazoelekeza kufungua akaunti katika taasisi za kifedha zilizopo nchini na kurejesha fedha za mauzo ya madini yaliyofanyika nje ya nchi katika akaunti hizo.***

**78.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara pia inaendelea kusimamia kwa karibu kuhakikisha miradi mipya ya uchimbaji wa madini inaanza uzalishaji. Miradi hiyo ni pamoja na mradi wa Heavy Mineral Sands–Kigamboni chini ya Kampuni ya Nyati; mradi wa madini ya kinywe uliopo Mahenge chini ya Kampuni ya Faru Graphite; mradi wa madini ya nikeli uliopo Kabanga chini ya Kampuni ya Tembo Nickel; mradi wa madini ya dhahabu uliopo wilayani Sengerema chini ya Kampuni ya Uchimbaji ya Sotta; mradi wa madini adimu (Rare Earth Elements) uliopo Ngualla, Songwe chini ya Kampuni ya Mamba. Kuanza kutekelezwa kwa miradi hiyo kutaongeza wigo wa faida za kiuchumi na kijamii kwa nchi yetu ikiwemo upatikanaji wa fedha za kigeni.

### e) Kuendeleza Rasilimaliwatu na Kuboresha Mazingira ya Kufanyia Kazi

**79.** ***Mheshimiwa Spika,*** Rasilimaliwatu ni nyenzo muhimu katika kuhakikisha utendaji kazi unaimarika na malengo ya Wizara yanafikiwa. Hivyo Wizara imeendelea kusimamia utendaji kazi na maslahi ya watumishi wake pamoja na kujaza nafasi zilizo wazi. Katika kipindi cha kuanzia Julai, 2023 hadi Machi, 2024 Wizara imejaza nafasi wazi 56 za watumishi. Nafasi 30 zimejazwa kwa ajira mpya na 26 kwa utaratibu wa uhamisho. Aidha, watumishi 239 wamepatiwa mafunzo ya muda mfupi na mrefu ndani na nje ya

nchi. Pia, Wizara imeendelea kusimamia na kuhakikisha maslahi na stahiki za watumishi zinapatikana kwa wakati.

**80.** ***Mheshimiwa Spika,*** pamoja na kuwa na Rasilimaliwatu, suala la mazingira bora ya kufanyia kazi ni muhimu. Hivyo, Wizara imeendelea kuhakikisha watumishi wake wanapatiwa vitendea kazi. Aidha, ujenzi wa jengo la makao makuu ya Wizara umefikia asilimia 80 na ujenzi wa makao makuu ya Tume umefikia asilimia 90. Kukamilika kwa majengo hayo kutawezesha watumishi kuwa na mazingira bora ya kufanyia kazi.

### f) Masuala Mtambuka

**81.** ***Mheshimiwa Spika,*** suala la afya ya watumishi ni jambo muhimu ili kuwezesha watumishi kutoa huduma nzuri na inayofaa. Hivyo, Wizara imeendelea kutoa mafunzo yanayohusu udhibiti wa Magonjwa Sugu Yasiyoambukiza (MSY). Aidha, Wizara imeendelea kuziwezesha timu za michezo ambapo watumishi wamehamasishwa kushiriki mazoezi na bonanza zinazoandaliwa na timu hizo kwa ajili ya kuimarisha afya zao. Pia, Wizara imeendelea kuwahudumia watumishi wanaoishi na Virusi vya UKIMWI waliojitokeza kwa hiari yao. Huduma hizo ni pamoja na kuwapatia fedha kwa ajili ya huduma ya lishe bora. Vilevile, Wizara imeendelea kushawishi watumishi kupima afya kwa hiari na kuwapatia vifaa kinga ili kupambana na maambukizi ya Virusi vya UKIMWI.

**82.** ***Mheshimiwa Spika,*** pamoja na suala la afya, maadili ya watumishi ni muhimu katika utekelezaji wa majukumu yao. Hivyo, Wizara imeendelea kutoa mafunzo juu ya uadilifu na kutekeleza Mpango Mkakati dhidi ya rushwa kwa kuelimisha watumishi kuhusu madhara yake na hatua za kisheria zinazoweza kuchukuliwa kwa mtumishi atakayebainika kujihusisha na vitendo hivyo.

## V. Utekelezaji wa Shughuli za Taasisi Zilizo Chini ya Wizara

**83.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kuzisimamia na kuziwezesha taasisi zake tano (5) ili ziendelee kutekeleza majukumu kwa ufanisi na kuzingatia Sera, Sheria na Miongozo

inayosimamia Sekta ya Madini. Taasisi hizo ni Tume ya Madini; Taasisi ya Jiolojia na Utafiti wa Madini Tanzania (GST); Shirika la Madini la Taifa (STAMICO); Kituo cha Jemolojia Tanzania (TGC); na Taasisi ya Uhamasishaji Uwazi na Uwajibikaji katika Rasilimali Madini, Mafuta na Gesi Asilia (TEITI). Taarifa ya utekelezaji wa taasisi ni kama ifuatavyo:

**(a) Tume ya Madini**

**(i) Utoaji na Usimamizi wa Leseni za Madini**

**84.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024, Tume ya Madini ilitoa leseni 10,067 ikilinganishwa na lengo la kutoa leseni 6,921. Leseni zilizotolewa ni kama ifuatavyo: Leseni ya Uchimbaji Mkubwa wa Madini (SML)- 01; Leseni za Uchimbaji wa Kati wa Madini (MLs)- 30; Leseni za Utafutaji wa Madini (PLs) - 333; Leseni za Uchimbaji Mdogo (PMLs) – 6,934; leseni kubwa za biashara (DLs) – 1,117; Leseni Ndogo za Biashara (BLs) – 1,616; Leseni za Uchenjuaji wa Madini (PCLs) – 35; na Leseni ya Usafishaji wa Madini (RFL) - 01. Ongezeko hilo la leseni ni matokeo ya uhamasishaji wa uwekezaji uliofanywa katika Sekta ya Madini.

**85.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024, leseni 96 za utafutaji wa madini, leseni 11 za uchimbaji wa kati wa madini na leseni 02 za uyeyushaji wa madini zilipewa hati za makosa kutokana na kutozingatia masharti ya leseni ikiwa ni pamoja na kutolipa ada za mwaka na kutoendeleza maeneo ya leseni. Aidha, leseni 09 za utafutaji madini na leseni 02 za uchimbaji wa kati zilifutwa baada ya wamiliki wake kushindwa kurekebisha makosa.

**(ii) Usimamizi, Ukaguzi na Biashara ya Madini**

**86.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024, vituo saba (7) vipya vya ununuzi wa madini vilianzishwa. Vituo hivyo ni Mundarara-Longido, Chalinze-Pwani, Matabe-Geita, Buhemba-Butiama, SugutiMusoma (V), Itilima-Kishapu na Mbangala-Songwe na kufanya idadi ya vituo vya ununuzi wa madini kufikia 100.

**87.** ***Mheshimiwa Spika,*** Tume ya Madini kwa kushirikiana na Mamlaka mbalimbali za Serikali ziliendelea kusimamia uendeshaji wa masoko na vituo vya ununuzi wa madini. Kupitia usimamizi huo, kwa kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024 mauzo ya shilingi 1,926,415,580,991.11 yalifanyika katika masoko ikilinganishwa na mauzo ya shilingi 1,676,948,980,375.31 yaliyofanyika katika kipindi cha Julai 2022 hadi Machi 2023. Kutokana na mauzo hayo, Serikali imekusanya kiasi cha shilingi 133,794,780,812.84 ikiwa ni tozo ya mrabaha na ada ya ukaguzi ikilinganishwa na shilingi 117,616,806,020.64 zilizokusanywa katika kipindi kama hicho mwaka 2022/2023.

### (iii) Utambuzi na Uthaminishaji wa Madini

**88.** ***Mheshimiwa Spika,*** Tume ya Madini iliendelea kusimamia shughuli za uchambuzi na uthaminishaji wa madini yote yaliyozalishwa na kutoa vyeti vya uthaminishaji wa madini pamoja na vibali vya usafirishaji (export permits na kimberley process certificates) na uingizaji madini (import permits). Katika kipindi cha kuanzia Julai 2023 hadi Machi 2024, jumla ya vibali 8,758 vya usafirishaji madini nje ya nchi vilitolewa ikilinganishwa na vibali 4,835 vilivyotolewa katika kipindi kama hicho mwaka 2022/2023. Thamani ya madini kwa vibali hivyo ni dola za Marekani 2,649,204,639.48 Aidha, jumla ya vibali 119 vya uingizaji madini nchini (*Import permits*) vilitolewa ambapo madini yenye thamani ya dola za Marekani 13,745,895.00 yaliruhusiwa kuingia nchini.

### (iv) Ukaguzi wa Hesabu za Fedha na Kodi

**88.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024, Tume ya Madini imefanya ukaguzi kwa kampuni 19. Kati ya kampuni hizo, tatu (3) ni za madini ya viwandani, tisa (9) ni za madini ujenzi, tano (5) ni za biashara ya dhahabu katika soko la dhahabu Geita na mbili (2) ni za madini ya shaba na dhahabu. Kaguzi hizo zimewezesha kubainisha kutolipwa kwa malipo kiasi cha shilingi 1,339,905,656.30. Kati ya fedha hizo shilingi 256,381,076.28 zimelipwa baada ya ukaguzi. Kampuni tano (5) zinazodaiwa shilingi 616,571,373.00 zimeahidi kulipa deni kwa awamu. Sambamba na hilo, Tume imeendelea kuchukua hatua mbalimbali za kuhakikisha deni lote linalipwa kupitia vikao vya

maridhiano na pale itakapobidi kampuni hizo zitachukuliwa hatua za kisheria.

### (v) Shughuli za Ukaguzi wa Migodi, Mazingira na Usimamizi wa Baruti

**90.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024, shughuli za ukaguzi migodi na mazingira zilihusisha ukaguzi uliolenga usalama, afya, mazingira na matumizi salama ya baruti katika shughuli za uchimbaji wa madini kama ifuatavyo**:**

- **Ukaguzi katika Migodi ya Wachimbaji Wakubwa**

**91.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024, migodi mikubwa nane (8) ilikaguliwa. Migodi hiyo ni Williamson Diamond Limited (WDL), Buckreef Gold Company, North Mara Gold Mine, Geita Gold Mine, Bulyanhulu Gold Mine, Stamigold Biharamulo Mine, El Hillal Minerals na Tembo Nickel Corporation Limited.

**92.** ***Mheshimiwa Spika,*** kufuatia ukaguzi huo mapungufu mbalimbali yalibainika ikiwemo maghala ya kuhifadhi baruti kuwa mbali na shughuli za uzalishaji chini ya ardhi, kutofanyika kwa kaguzi za mara kwa mara katika bomba linalosafirisha maji kutoka kwenye mabwawa ya Kuhifadhia Topetaka (TSF) kuelekea katika mitambo ya kutibu maji machafu (*waste water treatment plant*), kutokuwepo kwa eneo maalum lililotengwa kwa ajili ya kuhifadhia miambataka (waste rock dump) na kutokuwepo kwa maghala ya baruti hivyo kutumia mkandarasi kwa ajili ya shughuli za usambazaji na ulipuaji. Migodi ilielekezwa kurekebisha mapungufu hayo na tayari wamerekebisha.

- **Ukaguzi katika Migodi ya Wachimbaji wa Kati**

**93.** ***Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024, jumla ya migodi 56 ya uchimbaji wa kati ilikaguliwa katika sehemu mbalimbali nchini. Katika kaguzi hizo mapungufu mbalimbali yalibainika ikiwemo utunzaji usiofaa wa taka ngumu na kutozingatia matumizi ya vifaa kinga. Aidha, wahusika walielekezwa kurekebisha mapungufu yaliyojitokeza kwa

kuzingatia Sheria ya Madini, Sura ya 123 na Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, Sura ya 191 ambapo migodi husika imerekebisha mapungufu yaliyobainika.

- **Ukaguzi katika Migodi ya Wachimbaji Wadogo**

**94.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024, ukaguzi ulifanyika kwenye migodi ya wachimbaji wadogo 22,431 katika mikoa 30 ya kimadini nchini. Katika kaguzi hizo baadhi ya mapungufu yaliyobainika ni pamoja na kutofukiwa kwa mashimo ya uchimbaji, kutotumika kwa vifaa kinga, matumizi yasiyo sahihi ya vifaa kinga, na uhifadhi usio salama wa baruti na vilipuzi. Wahusika walielekezwa kufanyia kazi mapungufu yaliyobainika ili kuwa na uchimbaji salama na wenye tija.

- **Ukaguzi wa Maghala, Stoo na Masanduku ya Kuhifadhia Baruti**

**95.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024, jumla ya maghala ya kuhifadhia baruti 93, stoo za kuhifadhia baruti 269 na masanduku ya kuhifadhia baruti 268 yalikaguliwa. Kaguzi hizo zilifanyika katika mikoa ya kimadini ya Dar es Salaam, Mara, Kahama, Njombe, Shinyanga, Geita, Rukwa, Lindi, Ruvuma, Tanga, Mirerani, Manyara, Mwanza, Kigoma, Dodoma, Mbeya, Chunya, Mahenge, Songwe, Katavi, Kilimanjaro na Tabora. Kaguzi hizo zilibaini uwepo wa mpangilio hatarishi wa vilipuzi na baadhi ya miundombinu ya utunzaji wa baruti kutokuwa na vipima joto na mitungi ya kuzimia moto. Aidha, wahusika walirekebisha mapungufu hayo kama walivyoelekezwa.

- **Ukaguzi wa Mitambo ya Kuchenjua Dhahabu (Vat Leaching, CIP na Elution)**

**96.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024, Tume ya Madini ilifanya ukaguzi wa mitambo ya *Vat leaching* 852 kati ya 1,949, CIP 49 kati ya 52 na *elution plants* 204 zilizopo nchini. Mitambo hiyo ilikaguliwa katika mikoa ya kimadini ya Geita, Mbogwe, Mwanza, Chunya, Shinyanga, Songwe, Kahama, Tabora, Singida, Dodoma, Simiyu na Mara. Kaguzi hizo

zilibaini kutokuwepo kwa mifereji kwenye maeneo yenye udongo wa mabaki ya dhahabu (tailings) na baadhi ya *elution plants* kutokuwa na mfumo wa kuchuja hewa wakati wa uoshaji. Aidha, wahusika walirekebisha mapungufu hayo kama walivyoelekezwa

- **Ukaguzi wa Mabwawa ya Topetaka (TSF)**

**97.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024, jumla ya mabwawa ya topetaka 20 yalikaguliwa kwa lengo la kutoa vibali vya ujenzi au kutumia mabwawa hayo. Katika ukaguzi huo miradi 10 ya uchimbaji madini ilikidhi vigezo vya kupewa vibali vya ujenzi wa TSF. Aidha, wamiliki wa miradi 7 kati ya 10 waliopewa vibali vya ujenzi.

**98.** ***Mheshimiwa Spika,*** kaguzi maalum kwenye mabwawa 63 ya kuhifadhia topetaka yaliyopo katika mikoa mbalimbali ya kimadini hapa nchini zilifanyika kwa lengo la kujiridhisha kuhusu usalama wake kufuatia taarifa ya uwepo wa mvua za El-nino. Ukaguzi huo ulibaini kuwa mabwawa hayo yapo katika hali inayostahimili matumizi kwa kuzingatia miongozo ya uendeshaji wake.

- **Kupitia Taarifa za Mipango ya Ufungaji Migodi (MCP)**

**99.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024, Mipango ya Ufungaji Migodi 15 ilijadiliwa na Kamati ya Kitaifa ya Ufungaji Migodi (NMCC). Kati ya Mipango hiyo, Mipango ya migodi mitano (5) ilikidhi vigezo na kuidhinishwa. Migodi hiyo ni Sunshine Mining Co. Ltd, Minjingu Mines and Fertilizers Ltd, Maweni Limestone Limited, Kerai Construction Limited na Even Company Limited. Mipango ya migodi 10 haikuidhinishwa kutokana na mapungufu yaliyobainika na wahusika walielekezwa kurekebisha mapungufu hayo.

**(b) Shirika la Madini la Taifa (STAMICO)**

**100.** ***Mheshimiwa Spika,*** STAMICO imepewa dhamana ya kuwekeza katika miradi ya kimkakati kwa niaba ya Serikali na kuwezesha, kuhamasisha na kusaidia shughuli za wachimbaji wadogo ili ziwe zenye tija na zinazozingatia utunzaji wa mazingira.

Katika kipindi cha Julai, 2023 hadi Machi, 2024 STAMICO imetekeleza majukumu yake kama ifuatavyo:

**(i) Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo Inayomilikiwa na Kusimamiwa na STAMICO**

***101. Mheshimiwa Spika,*** STAMICO inamiliki na kusimamia miradi mitano (5) ambayo ni: mradi wa makaa ya mawe wa Kabulo-Kiwira; mradi wa mkaa mbadala (coal briquettes); mradi wa uchorongaji; mradi wa kuchimba kokoto, na mradi wa usimamizi wa vituo vya mfano vya wachimbaji wadogo wa madini.

- **Mradi wa Makaa ya Mawe wa Kabulo - Kiwira**

***102. Mheshimiwa Spika***, STAMICO imeendelea na shughuli za uchimbaji wa makaa ya mawe ambapo katika kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024, maboresho yafuatayo yamefanyika: kukamilisha ujenzi wa mizani (3); kukarabati na kununua vifaa vya maabara, wheel loader na mtambo wa kusaga makaa ya mawe (coal crusher) wenye uwezo wa kuchakata tani 200 hadi 250 kwa saa katika *size* nne (4) tofauti na kukamilisha usimikaji wake; kusimika kangavuke kwa ajili ya kuhakikisha uzalishaji hausimami umeme unapokatika; na kujenga kituo cha kujazia mafuta ili kuwezesha upatikanaji wa mafuta kwa wakati kwa mitambo. Uboreshaji huo umewezesha jumla ya tani 125,134 za makaa ya mawe kuzalishwa ambapo tani 124,220 ziliuzwa na kuingizia Shirika fedha kiasi cha shilingi 11,953,131,278.00 na shilingi 1,837,504,358.00 zimelipwa Serikalini kama mrabaha na tozo mbalimbali. Kiasi cha tani 914 kilichobaki kinasubiri kuuzwa.

- **Mradi wa Uchorongaji**

***103. Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024, STAMICO ilipata kandarasi tatu (3) mpya za uchorongaji kama ifuatavyo: Kampuni ya *Fluxing Resources* ya Chemba - Dodoma yenye thamani ya shilingi milioni 650; mgodi wa Shanta Gold Mine - Singida yenye thamani ya shilingi bilioni 2.75 na Buckreef yenye thamani ya shilingi bilioni 5.01. Aidha, STAMICO inaendelea na utekelezaji wa kandarasi katika mgodi wa GGML uliopo katika Mkoa wa Geita.

- **Mradi wa Mkaa Mbadala (Coal Briquettes)**

**104.** ***Mheshimiwa Spika***, STAMICO imeendelea na uzalishaji wa mkaa mbadala kutokana na makaa ya mawe unaotambulika kama Rafiki Briquettes. Aidha, STAMICO imeendelea na usimikaji wa mitambo miwili (2) yenye uwezo wa kuzalisha tani 20 kwa saa katika maeneo ya Kiwira na Kisarawe kwa ajili ya kuanza uzalishaji mkubwa. Vilevile, shirika linaendelea na jitihada za kuongeza uzalishaji katika mradi wa mkaa mbadala wa kupikia ambapo hadi kufikia Machi 2024 Shirika limenunua mitambo mingine miwili (2) ambayo tayari imewasili nchini yenye uwezo wa kuzalisha tani 20 kwa saa na kufanya idadi ya mitambo kuwa minne (4) hadi kufikia Machi, 2024.




***Picha Na. 8:*** *Mtambo wa kuzalisha mkaa mbadala wa kupikia (Rafiki Briquettes)*

- **Mradi wa Kokoto - Chigongwe**

**105.** ***Mheshimiwa Spika***, shirika linaendelea na usimikaji wa mtambo wa kusaga kokoto katika eneo la Chigongwe, Dodoma. Usimikaji wa mtambo huo wenye uwezo wa kuzalisha tani 150 hadi 200 kwa saa unaendelea ambapo hadi kufikia Machi, 2024 umefikia asilimia 95. Mtambo unatarajia kuanza uzalishaji katika mwaka wa fedha 2024/2025.

- **Mradi wa Vituo vya Mfano vya Wachimbaji Wadogo**

**106.** ***Mheshimiwa Spika***, moja ya majukumu ya STAMICO ni kuwezesha, kuhamasisha au kusaidia uendelezaji wa shughuli za uchimbaji mdogo nchini. Katika kutekeleza jukumu hilo, Shirika limeendelea kutoa huduma za uchenjuaji madini ya dhahabu

katika vituo vya mfano vya Lwamgasa, Katente na Itumbi. Aidha, ili kukidhi mahitaji yanayoongezeka, Shirika limekamilisha upanuzi wa kituo cha Lwamgasa kutoka kuzalisha tani 9 kwa siku hadi tani 30 kwa siku kwa kujenga *Carbon in Pulp (CIP)* na *Elution Plant*. Hadi kufikia Machi 2024 kazi ya kufanya majaribio ya mitambo hiyo na makabidhiano ilikuwa imeanza.

**(ii) Utekelezaji wa Miradi ya Ubia na Kampuni Tanzu**

**107.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024, STAMICO imeendelea kusimamia utekelezaji wa miradi ya ubia ambayo ni Kiwanda cha Kusafisha Dhahabu Mwanza na Mgodi wa Dhahabu wa Buckreef pamoja na Kampuni yake tanzu ya STAMIGOLD Biharamulo.

- **Mradi wa STAMIGOLD Biharamulo**

**108.** ***Mheshimiwa Spika***, *STAMIGOLD* ni mgodi unaomilikiwa na Serikali kupitia STAMICO inayomiliki hisa asilimia 99 na Ofisi ya Msajili wa Hazina inayomiliki hisa asilimia 1. Katika kipindi cha kuanzia Julai 2023 hadi Machi 2024 mgodi umezalisha dhahabu wakia 7,449.60 na kupata shilingi 36,579,416,773.00. Aidha, kiasi cha shilingi 1,463,176,670.93 kimelipwa Serikalini kama mrabaha na ushuru wa huduma na shilingi 914,485,419.33 ikiwa ni ada ya usimamizi. Pia, kwa sasa mgodi umeunganishwa kwenye Gridi ya Umeme ya Taifa ambapo imepunguza gharama za nishati kwa wastani wa kiasi cha shilingi 700,000,000.00 kwa mwezi. Vilevile, mgodi umenunua *wheel loader* ambayo imesaidia kuokoa takribani kiasi cha shilingi 35,000,000.00 kwa mwezi ambazo zilikuwa zinatumika kukodisha mtambo huo.

- **Kiwanda cha Kusafisha Dhahabu Mwanza**

**109.** ***Mheshimiwa Spika***, Kiwanda cha Kusafisha Dhahabu cha Mwanza kinamilikiwa kwa ubia kati ya STAMICO na kampuni za Rozzela ya Umoja wa Falme za Kiarabu (Dubai) na ACME Consultant Engineers PTE ya Singapore ambapo STAMICO inamiliki hisa asilimia 25 kwa niaba ya Serikali, na wabia wenza wanamiliki hisa asilimia 75. Katika kipindi cha kuanzia Julai, 2023 hadi Machi, 2024 kiwanda kimesafisha dhahabu gramu 802,518.19 yenye

thamani ya dola za Marekani 45,740,550.96 ambapo kiasi cha dola za Marekani 1,829,622.1 kimelipwa Serikalini kama mrabaha.

**110. *Mheshimiwa Spika*,** mnamo Agosti 2023, Kiwanda cha Kusafisha Dhahabu cha Mwanza kilipata vyeti vya ithibati (ISO) vitatu (3). Ithibati hizo ni ISO 9001:2015 Mifumo ya Usimamizi wa Ubora, ISO 14001:2015 - Mifumo ya Usimamizi wa Mazingira na ISO 45001:2018 - Usimamizi na Usalama wa Afya Kazini. Aidha, mikakati iliyopo kwa sasa imelenga kukidhi vigezo vya kupata ithibati za *London Bullion Market Association* (LBMA) pamoja na *Dubai Multi Commodities Center* (DMCC). Kukamilika kupatikana kwa Ithibati hizo kutawezesha dhahabu inayosafishwa katika Kiwanda hicho kutambuliwa kwenye masoko ya Kimataifa na kuweza kununuliwa kwa ajili ya kuhifadhiwa kama fedha.

- **Mgodi wa Dhahabu wa *Buckreef***

**111. *Mheshimiwa Spika*,** mgodi wa dhahabu wa Buckreef uliopo mkoani Geita unamilikiwa kwa ubia kati ya *STAMICO* yenye hisa asilimia 45 na *TANZAM2000* yenye hisa asilimia 55. Mgodi huu una mashapo yenye *metric* tani 38.57 zenye wastani wa ubora wa 1.77 gramu kwa tani. Kulingana na mashapo yaliyopo kwa sasa mgodi huu unatarajiwa kuwa na uhai wa miaka 15. Katika kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024, mgodi umezalisha wakia 13,577.43 za dhahabu na kuuza wakia 13,534.41 zenye thamani ya dola za Marekani 26,618,917. Aidha, mgodi umefanikiwa kulipa Serikalini dola za Marekani 1,943,180.94 kama mrabaha, ada ya ukaguzi na ushuru.

### (c) Taasisi ya Jiolojia na Utafiti wa Madini Tanzania (GST)

**111. *Mheshimiwa* Spika**, jukumu la Taasisi ya Jiolojia na Utafiti wa Madini Tanzania ni kufanya tafiti za jiosayansi na ugani wa jiolojia kwa lengo la kuvutia uwekezaji katika Sekta ya Madini. Kupitia tafiti hizi taarifa mbalimbali za jiosayansi za uwepo wa madini nchini huandaliwa ili kuhamasisha uwekezaji katika utafutaji wa madini wa kina (detailed exploration) kwa lengo la kuanzisha migodi mipya. Aidha, taarifa hizo za jiosayansi zinazozalishwa hutumika katika sekta nyingine za kiuchumi kama vile kilimo, maji, ujenzi na mipango miji. Pia, GST ina jukumu la kufanya uratibu wa

kujikinga na majanga ya asili ya jiolojia ikiwemo matetemeko ya ardhi, milipuko ya volkano na maporomoko ya ardhi. Katika kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024, GST imetekeleza majukumu yake kama ifuatavyo:

**(i) Kufanya Tafiti za Jiosayansi na Kuboresha Kanzidata ya Rasilimali Madini ya Taifa**

**113.** ***Mheshimiwa Spika,*** GST imetoa ushauri elekezi wa jiolojia, jiokemia na jiofizikia kwa wadau mbalimbali ikiwemo mgodi wa almasi wa Mwadui, wachimbaji wadogo na wa kati 19 na taasisi nne (4) za Serikali. Aidha, GST ilipokea taarifa 368 za jiosayansi kutoka kwa wamiliki 15 wa leseni za madini na kuzifanyia uchambuzi wa awali. Matokeo ya uchambuzi huo yalibaini kuwa baadhi ya taarifa hazikidhi matakwa ya sheria. Ili kuondoa mapungufu hayo, GST imeendelea kutoa elimu kwa wamiliki wa leseni kuhusu namna bora ya uandaaji na umuhimu wa uwasilishaji wa taarifa kwa mujibu wa sheria, kanuni, na miongozo.

**114.** ***Mheshimiwa Spika,*** ili kuboresha upatikanaji wa taarifa za jiolojia nchini, GST imeandaa ramani na taarifa 92 na kuziweka kwenye mfumo wa kidijitali. Aidha, ramani 30 zinaendelea kuandaliwa katika mfumo wa kidijitali na kazi hiyo imekamilika kwa asilimia 97.

**115.** ***Mheshimiwa Spika,*** GST ilifanya tafiti maalum katika maeneo matatu (3), utafiti wa kwanza ulifanyika kufuatia taarifa zilizosambaa kwamba, kulikuwa na madini ya thamani katika eneo la machimbo ya kifusi cha ujenzi wa mradi wa SGR lililopo Mkoa wa Shinyanga. Taarifa hizo zilisababisha kusimamishwa shughuli za uchimbaji wa kifusi katika eneo hilo kupisha uchunguzi. Matokeo ya utafiti huo yalionesha uwepo wa madini ya quartz (amethyst) ambayo hayakuwa na ubora na wingi unaokidhi viwango vya kuchimbwa kwa faida.

**116.** ***Mheshimiwa Spika,*** utafiti wa pili ulifanyika katika eneo la Vikonje Chamwino kutathmini hali ya jiolojia kwenye eneo lililotengwa kwa ajili ya ujenzi wa majengo ya Serikali. Utafiti huo ulikamilika na taarifa kuwasilishwa kwa mamlaka husika. Aidha, utafiti wa tatu ulifanywa kwa kushirikiana na STAMICO kwenye

leseni 14 za uchimbaji mdogo wa madini ya dhahabu wilayani Chunya. Matokeo ya awali ya utafiti yalionesha uwepo wa mwamba wenye dhahabu.

**117. *Mheshimiwa Spika,*** GST kwa kushirikiana na Wizara ya Maji, Nishati na Madini ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ) ilifanya ugani wa jiolojia katika visiwa vya Pemba na Unguja. Lengo la ugani huo ni kutengeneza ramani ya jiolojia ya visiwa hivyo. Ugani huu umekamilika na zoezi la uchoraji ramani na uandaaji wa taarifa unaendelea.

**(ii) Utoaji wa Huduma za Maabara**

**118. *Mheshimiwa Spika,*** GST imeendelea kufanya uchunguzi wa sampuli za miamba na udongo kutoka kwa wateja kupitia maabara yake ya jiosayansi kwa kuzingatia viwango vinavyokubalika kimataifa. Kwa kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024 jumla ya sampuli 10,307 za miamba na udongo zimefanyiwa uchunguzi kati ya sampuli 17,000 zilizokusudiwa katika mwaka mzima. Aidha, GST imezalisha vyungu vya uchunguzi wa maabara (Crucibles) 22,989 na *Cupels* 6,484 kwa ajili ya matumizi ya maabara yake.



***Picha Na. 9:*** *Vikombe Vya Kuyeyushia Sampuli za Miamba ya Madini ya Dhahabu Vinavyotengezwa Katika Maabara ya GST*

**119. *Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024 maabara ya GST ilifanyiwa ukaguzi wa nje na Shirika linalodhibiti ubora wa huduma za maabara katika nchi zilizopo Kusini mwa Bara la Afrika (SADCAS). Kutokana na ukaguzi huo,

Taasisi imekidhi vigezo vya kuendelea kuwa na Ithibati (Maintained Accreditation Status).

> ***Kupitia Bunge lako Tukufu napenda kutoa wito kwa wachimbaji wa madini kuendelea kuitumia maabara ya GST kwa kuwa ina ithibati na inakidhi viwango vilivyothibitishwa kimataifa.***

**(iii) Ufuatiliaji wa Majanga ya Asili ya Jiolojia na Kutoa Elimu kwa Wananchi**

**120.** ***Mheshimiwa Spika,*** GST imeendelea kufanya ufuatiliaji wa majanga ya asili ya jiolojia kama vile; matetemeko ya ardhi, milipuko ya volkano na maporomoko ya ardhi. Katika kutekeleza jukumu hili, GST ilikusanya na kuchakata taarifa za mitetemo kutoka katika vituo vinne (4) vilivyopo Dodoma, Mbeya, Geita na Arusha. Taarifa zinaonesha kuendelea kuwepo kwa matetemeko ya ardhi katika Mkoa wa Singida yenye ukubwa wa kati ya 4.1 na 5.3 katika kipimo cha *Richter.* Matetemeko hayo yalisababisha kujitokeza kwa nyufa kwenye baadhi ya nyumba na hivyo kuleta taharuki kwa jamii. GST ilitoa elimu kuhusu namna ya kujikinga na kuchukua tahadhari wakati majanga ya namna hii yanapotokea.

**121.** ***Mheshimiwa Spika,*** GST kwa kushirikiana na Taasisi nyingine za Serikali ilifanya uchunguzi ili kubaini chanzo cha tukio la kuporomoka kwa tope katika Mlima Hanang Mkoani Manyara lililotokea tarehe 3 Desemba, 2023. Tukio hilo lilisababisha vifo na majeraha kwa watu, upotevu wa mali, uharibifu wa miundombinu na mali. Uchunguzi ulibaini kwamba, maporomoko hayo yalichochewa na kunyesha kwa mvua kubwa juu ya Mlima Hanang ambako kulisababisha kutokea kwa maporomoko.

**122.** ***Mheshimiwa Spika,*** kufuatia tukio lililotokea Wilaya ya Hanang, Ofisi ya Waziri Mkuu kwa kushirikiana na Wizara ya Madini kupitia GST pamoja na taasisi nyingine zinatarajia kufanya utafiti wa kina wa jiosayansi katika eneo la Mlima Hanang ili kubaini endapo athari nyingine zitajitokeza.

### (d) Kituo cha Jemolojia Tanzania (TGC)

***123. Mheshimiwa Spika,*** Kituo cha Jemolojia Tanzania kinatoa mafunzo ya uongezaji thamani madini katika fani za utambuzi wa madini ya vito; uchongaji wa vinyago vya miamba na madini; ukataji na ung'arishaji wa madini ya vito na utengenezaji wa bidhaa za usonara. Aidha, TGC inatoa huduma za utambuzi wa madini ya vito kupitia maabara yake. Pia, TGC inatengeneza bidhaa zinazotokana madini ya vito na miamba. Katika kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024 TGC imetekeleza majukumu yafuatayo:




***Picha Na. 10:*** *Baadhi ya Bidhaa Zinazozalishwa na Kituo cha Jemolojia Tanzania -Arusha*

#### (i) Udahili wa Wanafunzi na Utoaji wa Mafunzo

**124.** ***Mheshimiwa Spika,*** Kituo cha TGC kilidahili wanafunzi 37 na kuendelea kutoa mafunzo kwa jumla ya wanafunzi 84 wa ngazi za astashahada (NTA Level 4 na 5) na stashahada (NTA Level 6) katika fani ya Teknolojia ya Vito na Usonara. Aidha, Kituo kilidahili wanafunzi 19 katika kozi za muda mfupi za kipindi cha miezi 3 na 6 kuhusu utambuzi na uthaminishaji wa madini ya vito (gemology), usanifu wa madini ya vito (lapidary) na usonara (jewellery).

**125.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024, TGC iliingia makubaliano ya ushirikiano na Taasisi ya Jemolojia ya nchini Thailand. Lengo la makubaliano hayo ni kuipatia TGC uzoefu na kuiimarisha ili kuongeza tija katika utoaji

wa mafunzo ya uongezaji thamani na utambuzi wa madini ya vito hivyo kuendana na viwango vya kimataifa.

**(ii) Uzalishaji wa Bidhaa na Utoaji wa Huduma kwa Wadau wa Madini**

**126.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024, Kituo cha TGC kiliendelea na utengenezaji wa bidhaa zitokanazo na madini ya vito na miamba ambapo jumla ya bidhaa 1,987 zikiwemo vinyago, hereni, pete, tuzo na nyinginezo zilizalishwa ikilinganishwa na jumla ya bidhaa 1,323 zilizozalishwa katika kipindi kama hicho mwaka 2022/2023. Aidha, Kituo kilitoa huduma za ukataji wa madini yenye uzito wa *carat* 107 na kufanya utambuzi wa sampuli 398 za madini ya vito kutoka kwa wadau mbalimbali.

**(e) Taasisi ya Uhamasishaji Uwazi na Uwajibikaji Katika Rasilimali Madini, Mafuta na Gesi Asilia (TEITI)**

**127.** ***Mheshimiwa Spika,*** *TEITI* ina jukumu la kuhamasisha uwazi na uwajibikaji katika usimamizi wa rasilimali madini, mafuta na gesi asilia ili kuongeza mapato na manufaa yatokanayo na Sekta ya Uziduaji. Katika kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024, TEITI imetekeleza majukumu yake kama ifuatavyo:

**(i) Ukamilishaji wa Ripoti ya 14 ya TEITI kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022**

**128.** ***Mheshimiwa Spika,*** Taasisi ya TEITI ipo kwenye hatua za kukamilisha ripoti ya ulinganishi wa malipo ya kampuni za madini, mafuta na gesi asilia na mapato ya Serikali kwa mwaka 2021/2022 ambapo kwa mara ya kwanza ripoti hii inaandaliwa na wataalamu wa ndani wa TEITI. Kampuni zilizochaguliwa kwa ajili ya zoezi la ulinganishi ni kampuni 56 zinazojihusisha na shughuli za madini, mafuta na gesi asilia pamoja na watoa huduma katika Sekta ya Uziduaji. Kigezo kilichotumika kuchagua kampuni hizo ni; kampuni zilizolipa Serikalini kiasi cha fedha kisichopungua shilingi bilioni 2 kwa mwaka wa fedha 2021/2022 ikijumuisha mrabaha na tozo nyinginezo.

**129.** ***Mheshimiwa Spika,*** Kwa mara ya kwanza, ripoti ya TEITI itahusisha takwimu za wachimbaji wadogo wa madini waliolipa Serikalini kiasi cha fedha cha kuanzia shilingi milioni 500 hadi bilioni 2 kwa mwaka 2021/2022. Ripoti hii inatarajiwa kuwekwa wazi kabla ya tarehe 30 Juni, 2024.

**(ii) Kushiriki katika Mikutano ya Kimataifa ya Uwazi na Uwajibikaji**

**130.** ***Mheshimiwa Spika,*** ili kuijengea uwezo TEITI katika kusimamia majukumu yake, TEITI imekuwa ikishiriki katika mikutano, warsha na makongamano mbalimbali ndani na nje ya nchi. Sambamba na hilo, hivi karibuni TEITI ilishiriki Mkutano wa Kimataifa wa Uwazi na Uwajibikaji (EITI Global Conference) uliofanyika jijini Dakar, nchini Senegal. Katika mkutano huo, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, alishiriki na kuhutubia kwa njia ya mtandao. Katika hotuba yake Mheshimiwa Rais alielezea hatua mbalimbali ambazo nchi yetu imechukua kwa vipindi tofauti ili kuboresha mifumo ya uwazi na uwajibikaji. Aidha, Mheshimiwa Rais alieleza dhamira na utayari wa nchi yetu kuhakikisha usimamizi bora wa rasilimali madini, mafuta na gesi asilia unaozingatia viwango vya kimataifa vya uwazi na uwajibikaji. Mkutano huo ulitoa fursa ya kubadilishana uzoefu kwa nchi wanachama wa Umoja wa EITI.

**(iii) Tathmini ya Utekelezaji wa Vigezo vya EITI Nchini**

**131.** ***Mheshimiwa Spika,*** Taasisi ya EITI ina jukumu la kufanya tathmini ya utekelezaji wa shughuli za uhamasishaji uwazi na uwajibikaji kwa nchi wanachama ikiwemo Tanzania. Novemba 2023 Bodi ya EITI iliwasilisha Ripoti ya mwisho ya Tathmini iliyofanyika Aprili 2023 kuhusu utekelezaji wa vigezo vya EITI kwa lengo la kupima kama nchi inaendelea kutimiza kikamilifu vigezo vya kuimarisha uwazi katika usimamizi wa rasilimali madini, mafuta na gesi asilia.



***Picha Na. 11:*** *Waziri wa Madini Mhe. Anthony P. Mavunde (Mb.), akikabidhiwa ripoti ya tathmini ya TEITI.*

**132.** ***Mheshimiwa Spika***, matokeo ya tathmini hiyo yanaonesha kuwa Tanzania imetekeleza vigezo vya EITI vya mwaka 2019 kwa kupata alama 77 kati ya 100. Bodi hiyo imepongeza juhudi za Serikali na wadau mbalimbali katika kufanikisha utekelezaji wa shughuli za uhamasishaji uwazi na uwajibikaji hapa nchini.

**(iv) Utoaji wa Elimu kwa Umma kuhusu Matumizi ya Takwimu zinazotolewa na Ripoti za TEITI**

**133.** ***Mheshimiwa Spika***, TEITI imeendelea kuelimisha Umma kuhusu matumizi ya ripoti zake kupitia runinga, redio, tovuti, mitandao ya kijamii na kwenye maonesho mbalimbali. Aidha, TEITI ilishiriki katika Jukwaa la uziduaji lililoandaliwa na kuratibiwa chini ya mwamvuli wa Asasi za Kiraia zinazojihusisha na shughuli za uziduaji. TEITI ilitumia jukwaa hilo kutoa elimu kwa umma kuhusu matumizi ya takwimu zilizopo kwenye ripoti zake.

## D. MPANGO NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025

**134.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuandaa Mpango na Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2024/2025, Wizara imezingatia miongozo ifuatayo: Mwongozo wa Kitaifa wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti wa Mwaka 2024/2025; Ilani ya CCM kwa ajili ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020; Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa

Miaka Mitano 2021/2022 – 2025/2026; Sera ya Madini ya Mwaka 2009; Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025; Maelekezo ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na viongozi wengine wa kitaifa pamoja na maelekezo ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini ambayo yaliyotolewa kwa nyakati tofauti.

**I. Maeneo ya Utekelezaji kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025**

**135. *Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2024/2025, Wizara ya Madini itatekeleza majukumu mbalimbali kama ifuatavyo: kuimarisha ukusanyaji wa maduhuli na kuongeza mchango wa Sekta ya Madini kwenye Pato la Taifa; kuendeleza madini muhimu na madini mkakati; kuhamasisha uwekezaji, uongezaji thamani madini, uanzishwaji wa minada na maonesho ya madini ya vito; kuendelea kufanya utafiti na ugani wa jiosayansi ikiwemo utafiti wa kina wa jiofizikia (*High-resolution Airborne Geophysical Survey*); kuwaendeleza wachimbaji wadogo na kuwasogezea huduma za ugani; na kuzijengea uwezo taasisi zilizo chini ya Wizara ya Madini ili ziweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi na tija zaidi.

**(i) Kuimarisha Ukusanyaji wa Maduhuli na Kuongeza Mchango wa Sekta ya Madini kwenye Pato la Taifa**

**136. *Mheshimiwa Spika,*** katika kuimarisha ukusanyaji wa maduhuli ya Serikali na kuongeza mchango wa Sekta ya Madini, Wizara imepanga kutekeleza mikakati ifuatayo: kuhamasisha kuanza kwa uzalishaji kwa kampuni zilizopewa leseni za uchimbaji, usafishaji na biashara ya madini na kuimarisha usimamizi wa migodi ya uchimbaji madini.

**137. *Mheshimiwa Spika,*** sambamba na hayo, Wizara itaendelea kuimarisha udhibiti wa vitendo vya utoroshaji wa madini kwenda nje ya nchi na biashara haramu ya madini nchini; kuimarisha ukaguzi na usimamizi wa shughuli za uchimbaji wa madini kwa kununua wa vitendea kazi kama magari na pikipiki kwa ajili ya mikoa yote ili kuongeza ufanisi wa kazi; kuimarisha na kusimamia masoko na vituo vya ununuzi wa madini nchini; na kuendeleza mikakati ya kuimarisha usimamizi wa madini ya ujenzi, soko la

Tanzanite na vito vingine hapa nchini ili kuongeza mapato yatokanayo na madini hayo.

**(ii) Kuendeleza Madini Muhimu na Madini Mkakati**

**138.** ***Mheshimiwa Spika,*** madini muhimu na madini mkakati ni madini ambayo yana mahitaji makubwa kwenye maendeleo ya uchumi na ulinzi wa Taifa. Madini hayo ni pamoja na lithium, kinywe, helium, nikeli, cobalt, titanium, shaba, aluminium, niobium na rare earth elements ambayo yanatumika kutengeneza vifaa vya kisayansi na kiteknolojia.

**139.** ***Mheshimiwa Spika,*** kutokana na umuhimu wa madini hayo, Wizara imepanga kutekeleza yafuatayo ili kunufaika na fursa zilizopo: kufanya tafiti kwa lengo la kubaini maeneo yenye madini mkakati na muhimu kwa ajili ya kuhamasisha uwekezaji; kufanya utafiti wa mahitaji ya madini mkakati na madini muhimu ili kuyafikia masoko mbalimbali duniani; kuvutia wawekezaji katika utafutaji na uchimbaji wa madini mkakati na madini muhimu kwa kuandaa mazingira rafiki; kutoa leseni za utafutaji, uchimbaji na biashara ya madini mkakati na madini muhimu; na kukamilisha uandaaji wa mpango mkakati wa uendelezaji na uvunaji wa madini mkakati na madini muhimu nchini.

> ***Kuanzia sasa hatutatoa Leseni ya Kati (ML) na Kubwa (SML) ya Uchimbaji wa madini yote yakiwemo madini mkakati na madini muhimu kwa Mwekezaji yoyote kama hatokuwa na mpango mzuri wa kuongeza thamani madini hapa nchini, lengo ni kuifanya nchi yetu ya Tanzania kunufaika na rasilimali madini ambayo Mwenyezi Mungu ametujaalia.***

**140.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali imedhamiria kutekeleza kwa dhati shughuli za uongezaji thamani madini muhimu na madini mkakati nchini kwa kutengeneza bidhaa zitokanazo na madini ghafi. Ili kufanikisha hilo, Serikali imetenga eneo maalumu la ukanda wa kiuchumi la Buzwagi Special Economic Zone lililopo Wilaya ya Kahama. Eneo hilo lenye ukubwa wa ekari 1,333 awali lilikuwa na shughuli za uchimbaji madini kupitia Kampuni ya Barrick.

**141.** ***Mheshimiwa Spika***, pamoja na masuala mengine, eneo hilo litatumika kwa ajili ya ujenzi wa viwanda vya kuongeza thamani madini na uzalishaji wa bidhaa za migodini. Ujenzi wa viwanda hivyo utaongeza fursa za ajira, ujuzi kwa watanzania, kupunguza gharama za uzalishaji na kuchochea upatikanaji wa mapato. Aidha, viwanda vitakavyojengwa kwa awamu ya kwanza ni kiwanda cha usafishaji na uongezaji thamani madini (Multi Metals Processing Facility), *Steel Balls Manufacture*, *Mine Conveyor Belts, Solar Farms* na *Portable Water Plant*. Hatua hii itasaidia upatikanaji wa bidhaa za migodini ambazo awali zilikuwa zikiagizwa kutoka nje ya nchi.

### (iii) Kuhamasisha Uwekezaji, Uongezaji Thamani Madini, Uanzishwaji wa Minada na Maonesho ya Madini ya Vito

**142.** ***Mheshimiwa Spika,*** ili kuhamasisha uwekezaji, Wizara itaendelea kutangaza fursa mbalimbali zinazopatikana kwenye mnyororo wa thamani wa madini nchini kupitia makongamano, maonesho, tovuti na vyombo vya habari; kuwaendeleza wachimbaji wadogo waweze kukua kutoka uchimbaji mdogo na kufikia uchimbaji wa kati na hatimaye uchimbaji mkubwa kwa kuwapa mafunzo kuhusu uchimbaji, uchenjuaji na biashara ya madini.

**143.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika eneo la uongezaji thamani, Wizara itaendelea kutoa ushirikiano kwa wamiliki wa viwanda vya usafishaji wa madini ya dhahabu nchini ili kupata ithibati ya LBMA. Kama ilivyoelezwa hapo awali, kupatikana kwa Ithibati hiyo kutawezesha dhahabu inayosafishwa katika viwanda hivyo kutambuliwa kwenye masoko ya Kimataifa na kuweza kununuliwa kwa ajili ya kuhifadhiwa kama fedha.

**144.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali itaendelea na jitihada za kuanzisha minada na maonesho ya kimataifa ya madini ya vito kwa lengo la kupata masoko, bei shindani, kuvutia uwekezaji na kutangaza fursa za madini ya vito zilizopo nchini.

**(iv) Kuendelea Kufanya Utafiti wa Kina wa Jiofizikia (High-resolution Airborne Geophysical Survey)**

**145.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika utekelezaji wa shughuli hii, Wizara itafanya yafuatayo: kufanya tafiti za kina za jiofizikia (high-resolution airborne geophysical survey) ili kuainisha tabia za miamba; na kujenga mfumo wa kutunza na kusambaza taarifa za jiosayansi.

**(v) Kuwaendeleza Wachimbaji Wadogo na Kuwasogezea Huduma za Ugani**

**146.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara itaendelea na juhudi za kuwaendeleza wachimbaji wadogo kwa kutoa mafunzo ya mara kwa mara kuhusu masuala muhimu ya kuzingatia katika uendeshaji wa shughuli za madini; kufanya utafiti na kutenga maeneo kwa ajili ya wachimbaji wadogo; na kuimarisha miundombinu na utendaji wa vituo vya mfano ili kutoa huduma kwa wachimbaji wadogo.

**147.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara itaendelea kufanya majadiliano na mamlaka zenye dhamana ili kuwezesha ujenzi wa miundombinu mbalimbali hususan ya barabara na umeme kwenye maeneo ya migodi ya uchimbaji mdogo; kuwaunganisha wachimbaji wadogo na taasisi za fedha ili wapate mikopo kwa ajili ya uendeshaji wa shughuli zao; kuwezesha upatikanaji wa vitendea kazi kwa wachimbaji wadogo ikiwemo mitambo ya uchorongaji; na kuhamasisha wachimbaji wadogo kushiriki katika maonesho mbalimbali ya madini ili kujengewa uelewa wa jinsi shughuli za madini zinavyofanyika.

**(vi) Kuzijengea Uwezo Taasisi Zilizo Chini ya Wizara ya Madini ili Ziweze Kutekeleza Majukumu yake kwa Ufanisi na Tija zaidi**

**148.** ***Mheshimiwa Spika,*** ili kuzijengea uwezo taasisi zake, Wizara itafanya yafuatayo: kuiwezesha Tume ya Madini kupata rasilimali fedha na vifaa kwa ajili ya kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi; kuendelea kuiimarisha STAMICO ili ishiriki kikamilifu kwenye

shughuli za madini ikiwemo kuwawezesha wachimbaji wadogo kwa kuwapatia mafunzo na upatikanaji wa mikopo na vifaa.

**149.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara itaendelea kuiimarisha *GST* ili iweze kufanya tafiti za jiosayansi kubaini maeneo mapya yenye mashapo ya madini; kuimarisha Kituo cha *TGC* kwa lengo la kuendelea kutoa mafunzo na kuhamasisha shughuli za uongezaji thamani madini; na kuiwezesha *TEITI* kupata rasilimali mbalimbali ikiwemo vifaa na vitendea kazi ili iweze kutekeleza majukumu yake ipasavyo.

### II. Maeneo Mengine Yatakayotekelezwa na Wizara

**150.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara itatekeleza maeneo mengine yatakayosaidia kuboresha zaidi ufanisi wa sekta. Utekelezaji huo umejikita zaidi katika kupata taarifa za jiolojia kwa kufanya tafiti za kina kupitia "**Vision 2030: Madini ni Maisha na Utajiri**"; kuandaa Programu ya ***Mining for a Brighter Tomorrow - MBT*** kwa ajili ya kuwainua wachimbaji wanawake na vijana; kuongeza tija kwenye shughuli za uongezaji thamani madini kupitia utoaji wa vifaa vya uongezaji thamani madini kwa wahitimu wa TGC; usimamizi wa sheria; na ushiriki wa watanzania katika shughuli za madini na uwajibikaji wa kampuni kwa jamii.

### (i) Vision 2030: Madini ni Maisha na Utajiri

**151.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia GST itaendelea kufanya utafiti wa kina wa jiofizikia kwa kutumia teknolojia ya kisasa ili kutambua tabia za miamba na kurahisisha tafiti nyingine za jiosayansi zenye kuwezesha kubaini aina mbalimbali za madini yapatikanayo nchini. Hadi sasa utafiti wa kina wa jiofizikia umefanyika kwa asilimia 16 ya eneo lote la nchi. Aidha, GST katika mwaka wa fedha 2024/2025 inatarajia kufanya utafiti wa kina wa jiofizikia katika *blocks* mbili (2) zenye jumla ya kilometa za mraba 165,574. Baadhi ya maeneo yatakayopitiwa yapo kwenye mikoa ya Rukwa, Katavi, Mbeya, Songwe na Kigoma. Malengo ya Wizara ni kufanya utafiti wa kina wa jiofizikia kufikia angalau asilimia 50 ifikapo mwaka 2030.

**152.** ***Mheshimiwa Spika,*** dhana hii ya "Vision 2030" inakusudia kuiendeleza Sekta ya Madini kwa kufanya yafuatayo: kufanya tafiti za kina za jiofizikia (high-resolution airborne geophysical survey); kujenga maabara ya kisasa kwa ajili ya kufanya uchunguzi wa miamba, udongo, maji na madini; kuanzisha makumbusho maalum ya madini; kuwawezesha wachimbaji wadogo kupitia STAMICO kwa kuwapatia mashine 15 za uchorongaji; kuyafanya madini mkakati na madini muhimu yawe na nguvu ya soko; kuongeza thamani madini hapa nchini; kuwaendeleza wawekezaji wazawa ili kuongeza wigo wa uwekezaji unaotokana na Watanzania; kuongeza ushiriki wa Watanzania (local content) katika kusambaza bidhaa na kutoa huduma migodini; na kuandaa mazingira rafiki na kuvutia uwekezaji mkubwa kutoka nje ya nchi.

**153.** ***Mheshimiwa Spika,*** ufanisi wa malengo haya mahsusi na mkakati wa sekta kwenye Vision 2030, utategemea ushiriki wa wadau mbalimbali ikiwemo taasisi za Serikali, sekta binafsi, asasi za kiraia na jumuiya ya kimataifa pamoja na mabadiliko chanya ya kiuchumi na kisiasa.

> ***Napenda kulitaarifu Bunge lako tukufu kuwa, Madini ni Maisha na Utajiri, ina maanisha hauwezi kutenganisha maisha ya mtanzania na Sekta ya Madini kwa kuwa kufanikiwa kwa tafiti za kina na kupatikana kwa taarifa sahihi kutachochea sekta nyingine kukua ikiwemo Sekta za Maji, Kilimo, Utalii, Ujenzi na Mawasiliano***.

**(ii)** ***Programu ya Mining for a Brighter Tomorrow – MBT***

**154.** ***Mheshimiwa Spika,*** *Programu ya Mining for a Brighter Tomorrow - MBT* ni mahsusi kwa ajili ya kuwainua wachimbaji wanawake na vijana ambayo itatoa kipaumbele kwa wanawake na vijana katika maeneo yafuatayo: utoaji wa leseni katika maeneo ya uchimbaji; na wachimbaji kunufaika na vitendea kazi ikiwemo magari, vifaa na mitambo ya uchimbaji. Aidha, programu hiyo itasaidia kuchochea ukuaji wa Sekta ya Madini, uchumi wa Taifa na kuongeza ajira kwa watanzania.

### (iii) Utoaji wa Vifaa vya Uongezaji Thamani Madini kwa Wahitimu wa TGC

**155. *Mheshimiwa Spika,*** Wizara imedhamiria kuhamasisha kwa vitendo shughuli za uongezaji thamani madini nchini kwa kuwapatia vifaa wahitimu wa kozi mbalimbali za uongezaji thamani madini ili waweze kuendeleza ujuzi na kujiajiri ikiwa ni njia mojawapo ya kukuza na kusambaza tasnia hii kwa faida ya sasa na vizazi vijavyo.

### (iv) Usimamizi wa Sheria

**156. *Mheshimiwa Spika***, Sheria, Kanuni, Miongozo na Taratibu ni muhimu katika kusimamia maendeleo na ustawi wa Sekta ya Madini. Katika hili, Wizara itaendelea kusimamia Mfumo wa Kisheria na Usimamizi wa Sekta ya Madini ikiwa ni pamoja na kuchukua hatua stahiki kwa watakaobainika kukiuka Sheria na Kanuni zinazosimamia Sekta hii. Wizara kwa kushirikiana na wadau itaendelea kufanya marekebisho ya Mfumo wa Kisheria na Usimamizi wa Sekta ya Madini pale itakapoonekana kuna umuhimu ili kuendelea kuweka mazingira bora ya uwekezaji katika Sekta hii muhimu kwa uchumi wa nchi.

**157. *Mheshimiwa Spika,*** ili kuleta ufanisi katika uingiaji wa mikataba kati ya mmiliki wa leseni na mtoa msaada wa kiufundi (*Technical Support*), Wizara imejipanga kutengeneza kanuni ambazo wadau wote watashirikishwa ili kuwa na nyenzo imara ya kusimamia masuala haya kwa manufaa ya pande zote zinazohusika kwenye leseni. Lengo ni kuhakikisha kuwa hakuna mchimbaji anayepoteza haki yake kwa sababu tu ya mmiliki wa leseni kupata mshirika.

**158. *Mheshimiwa Spika,*** kwa wamiliki wa leseni (PML) ambao watataka kunufaika na msaada wa kiufundi, wanashauriwa wasiingize wachimbaji wadogo ndani ya leseni zao bali wachimbe wenyewe ili wakipata msaada wa kiufundi iwe rahisi kwao kufanya makubaliano nao.

**159. *Mheshimiwa Spika***, tutaweka utaratibu wa kumtaka kila mmiliki wa leseni ya uchimbaji mdogo (PML) ambaye ndani ya

eneo la leseni yake kuna wachimbaji wadogo wengine, akitaka kuuza leseni yake au kuingia makubaliano na mwekezaji suala linaloweza kuwaondoa wachimbaji wadogo ndani ya leseni yake au kuathiri kwa aina yoyote uwekezaji wa wachimbaji hao hasa maduara yao, atatakiwa kufanya mambo yafuatayo: -

**(i)** Kuwapa kwanza nafasi ya upendeleo (the right of first refusal) wachimbaji wadogo waliopo ndani ya leseni yake haki ya kununua au kuingia mkataba wa uwekezaji kabla ya kwenda kwa mtu mwingine; na

**(ii)** Uwepo wa mikataba iliyosajiliwa na Tume ya Madini kati ya wamiliki wa leseni (PML) na wachimbaji waliopo ndani ya leseni zao ili watambulike rasmi na Tume ya Madini kwa lengo la kusimamia maslahi yao pindi inapotokea changamoto yoyote juu ya maslahi yao.

**160.** ***Mheshimiwa Spika,*** Kwa Leseni zote zinazotolewa na Serikali kwa ajili ya vikundi vya wachimbaji wadogo, litawekwa sharti la lazima la kukitaka kikundi chenye lengo la kutaka kupata msaada wa kiufundi au kuuza leseni yake kwa Mwekezaji kupata kwanza kibali cha Katibu Mtendaji wa Tume baada ya kujiridhisha juu ya msaada wa kiufundi unaotaka kutolewa na pia kujiridhisha namna ambavyo pande zote zitanufaika ili kuepusha migogoro isiyo ya lazima.

**(v) Ushiriki wa Watanzania Katika Shughuli za Madini na Uwajibikaji wa Kampuni kwa Jamii**

**161.** ***Mheshimiwa Spika,*** kufuatia marekebisho ya Sheria ya Madini ya Mwaka 2017, kulitungwa Kanuni za Ushirikishwaji wa Watanzania za Mwaka 2018 ili kutoa tafsiri na kuweka usimamizi thabiti katika utekelezaji wa masuala ya Ushirikishwaji wa Watanzania katika Sekta ya Madini nchini (Local Content) na Uwajibikaji wa Kampuni kwa Jamii (Corporate Social Responsibilities).

**162.** ***Mheshimiwa Spika,*** kanuni kuhusu Ushirikishwaji wa Watanzania katika Sekta ya Madini nchini (Local Content) zinazitaka kampuni za uchimbaji madini kununua vifaa

vinavyozalishwa nchini, kuajiri watanzania na kutumia huduma na bidhaa zinazozalishwa ndani ya nchi.

**163.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara itaendelea kusimamia utekelezaji wa Kifungu cha 105 cha Sheria ya Madini pamoja na Kanuni za Wajibu wa Wamiliki wa Leseni za Madini za Mwaka 2023. Sheria na kanuni hizo zinawataka wamiliki wa leseni za madini nchini kushirikiana na Mamlaka za Serikali za Mitaa, kuandaa Mpango Mahsusi wa Wajibu wa Kampuni kwa Jamii (CSR) kwa kuzingatia vipaumbele vya Jamii zinazozunguka maeneo yenye leseni. Wamiliki wote wa leseni za madini nchini wana wajibu wa kuwasilisha nakala ya mipango iliyoidhinishwa ili Tume ya Madini iweze kufuatilia utekelezaji wa mipango hiyo.

**164.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa kuwa utekelezaji wa Kanuni za CSR za Mwaka 2023 unaonekana kuwa na changamoto, napenda kulijulisha Bunge lako Tukufu kwamba, Wizara itaandaa kikao cha wadau wote wanaoguswa kwa aina moja au nyingine na kanuni hizi ili kujadiliana kwa pamoja na kuja na mwarobaini wa suala hili kwa manufaa ya wawekezaji, jamii inayozunguka migodi na Taifa kwa ujumla.

## III. Kazi Zitakazotekelezwa na Taasisi Zilizo Chini ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025

### (i) Tume ya Madini

**165.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Mwaka wa Fedha 2024/2025 Tume ya Madini inatarajia kutekeleza kazi zifuatazo:

#### a) Kuimarisha Usimamizi wa Shughuli za Madini na Ukusanyaji wa Maduhuli ya Serikali

**166.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2024/2025 Tume ya Madini itatekeleza yafuatayo: kuimarisha mfumo wa usimamizi wa leseni ili kuongeza kasi ya utoaji wa leseni; kuendelea kufuatilia leseni ili kubaini leseni zenye makosa mbalimbali ikiwemo zisizoendelezwa na kuzifuta kwa kuzingatia Sheria; kutatua migogoro katika maeneo yenye shughuli za uchimbaji madini ili kuruhusu shughuli za uzalishaji wa madini kuendelea; kuimarisha usimamizi wa

uzalishaji na biashara ya madini ya ujenzi na viwandani; kuboresha Mfumo wa Masoko ya Madini (MMMIS) na kuongeza vitendea kazi.

**167.** ***Mheshimiwa Spika,*** hatua nyingine ni kuhakikisha maeneo yote yenye shughuli za madini yanafikiwa kwa urahisi kwa kununua magari na pikipiki. Aidha, Tume ya Madini inatarajia kununua vifaa mbalimbali vya maabara ili kuiongezea uwezo maabara yake kufanya uchunguzi wa sampuli za madini. Kuimarika kwa maabara hiyo kutarahisisha usuluhishi wa malipo ya mrabaha yatakayofanywa na migodi mikubwa na ya kati.

**168.** ***Mheshimiwa Spika,*** Tume ya Madini kwa kushirikiana na Mamlaka nyingine za Serikali itaendelea kufanya kaguzi kwa lengo la kudhibiti utoroshaji na biashara isiyo rasmi ya madini nchini. Utekelezaji wa kazi hizo utawezesha kuziba mianya ya utoroshaji na hivyo kuongeza ukusanyaji wa maduhuli.

**b) Kuimarisha Ukaguzi wa Usalama, Afya na Utunzaji Mazingira**

**169.** ***Mheshimiwa Spika***, katika kuimarisha uchimbaji wa madini ulio salama na unaozingatia utunzaji wa mazingira, Tume ya Madini itaendelea kuimarisha usimamizi na ukaguzi wa migodi kwenye masuala ya usalama, afya na utunzaji wa mazingira. Aidha, Tume ya Madini itaendelea kusimamia utunzaji na matumizi sahihi ya baruti, kufanya ukaguzi wa mitambo ya uchenjuaji madini pamoja na kukagua na kuidhinisha mipango ya uendelezaji na ufungaji migodi. Pia, Tume ya Madini itaendelea kutoa elimu na miongozo kwa wamiliki wa miradi ya uchimbaji na uchenjuaji wa madini ili waweke mipango mizuri ya kusimamia usalama, afya na utunzaji wa mazingira.

**c)Kuendelea Kuboresha Mazingira ya kuwawezesha Wananchi Kufaidika na Rasilimali Madini**

**170.** ***Mheshimiwa Spika***, ili kuhakikisha watanzania wananufaika na shughuli za madini, Tume ya Madini itaendelea kusimamia ushiriki wa watanzania (Local Content) kwenye shughuli za madini. Aidha, Tume itaendelea kuhakikisha wamiliki wa leseni za

madini wanatekeleza wajibu wao kwa jamii inayozunguka eneo la mradi (CSR) kwa kuzingatia Sheria.

**d)Kuelimisha Umma na Kuboresha Mawasiliano Kati ya Tume na Wadau Mbalimbali Kuhusu Masuala ya Madini**

**171.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kujenga uelewa na kuboresha mawasiliano ya Tume na wadau wa madini, Tume ya Madini itaendelea kutoa elimu kwa umma kuhusu masuala mbalimbali yanayohusu Sekta ya Madini ikiwa ni pamoja na namna ya kupata leseni za madini, utekelezaji wa sheria zinazosimamia shughuli za madini, utunzaji wa mazingira na ulipaji wa ada, kodi na tozo mbalimbali za Serikali. Aidha, Tume ya Madini itaendelea kutoa elimu na kuhamasisha wananchi kushiriki katika fursa zilizopo katika Sekta ya Madini.

**e)Kuendeleza Rasilimaliwatu na Kuboresha Mazingira ya Kufanyia Kazi**

**172.** ***Mheshimiwa Spika****,* Tume ya Madini itaendelea kuimarisha na kuboresha utendaji kazi wa watumishi kwa kuwaongezea ujuzi na weledi kupitia mafunzo ya muda mfupi na mrefu. Aidha, Tume ya Madini itaendelea kuboresha mazingira ya utendaji kazi kwa kujenga Ofisi za Maafisa Madini Wakazi katika Mikoa ya Kimadini ya Rukwa, Songwe na Mahenge.

**(ii)Taasisi ya Jiolojia na Utafiti wa Madini Tanzania (GST)**

**173.** ***Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha Mwaka wa Fedha 2024/2025 Taasisi ya Jiolojia na Utafiti wa Madini (GST) inatarajia kutekeleza kazi zifuatazo:

**a)Kufanya Tafiti za Jiosayansi na Kuboresha Kanzidata ya Rasilimali Madini ya Taifa**

**174.** ***Mheshimiwa Spika,*** ili kuboresha Kanzidata ya Rasilimali Madini ya Taifa, GST inakusudia kufanya ugani wa jiolojia na jiokemia katika QDS mbili (2) mpya (QDS 221 na 222) zilizopo Mkoa wa Pwani na kuchora ramani zake katika skeli ya 1:100,000; kuhuisha ramani katika skeli ya 1:100,000 na kubainisha madini

kwenye ramani mbili zenye upungufu wa taarifa mpya za uwepo wa madini (mineral occurance mapping) katika QDS mbili (2) (QDS 275 na 276) zilizopo Mkoa wa Ruvuma na Njombe.

**175.** ***Mheshimiwa Spika,*** GST itafanya tafiti nne (4) maalum za jiosayansi na utafiti wa kina kwenye maeneo yenye madini ya viwandani, madini ya dhahabu na madini mkakati. Aidha, GST itafanya utafiti kwa lengo la kuwapatia wadau taarifa sahihi na kutoa ushauri elekezi kwenye nyanja za jiolojia, jiokemia, jiofizikia na uchenjuaji madini.

**176.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuboresha Kanzidata ya Rasilimali Madini ya Taifa, GST inakusudia kuchora ramani 24 (digitalization), kudurufu ramani 30 na kuchakata picha za satelaiti; kuingiza taarifa/machapisho 500 katika mfumo wa dijitali; kukusanya, kuhakiki na kutathmini uhalisia wa taarifa na takwimu za jiosayansi kutoka katika leseni 40 za utafutaji na uchimbaji madini nchini; kuhuisha Kanzidata ya Rasilimali Madini ya Taifa; kukusanya miamba choronge mita 1,000 na kuchakata taarifa zake; na ununuzi wa *Helicopter Jet Ranger* kwa ajili ya kuongeza nguvu katika shughuli za utafiti wa kina wa madini.

**b) Kuwaendeleza Wachimbaji Wadogo kwa Kufanya Tafiti za Jiosayansi**

**177.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuwaendeleza wachimbaji wadogo na wa kati, GST inalenga kufanya utafutaji wa madini kwa lengo la kubainisha ulalo, mwelekeo na tabia za mbale katika maeneo mawili (2) ya wachimbaji wadogo yaliyopo Mikoa ya Kigoma na Katavi.

**b)Kuboresha Huduma za Maabara**

**178.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuboresha huduma za maabara, GST imepanga kuendelea kufanya chunguzi kwa kuzingatia vigezo vya ithibati (accreditation). Aidha, GST imepanga kupata ithibati za madini mengine zaidi ya dhahabu na makaa ya mawe ili kuongeza wigo wa utoaji huduma kwa wateja.

**179.** ***Mheshimiwa Spika,*** GST imepanga kujenga maabara mpya ya kisasa (State-of-Art Laboratory) katika eneo la Kizota Dodoma. Maabara hiyo itafanya uchunguzi wa madini ikiwemo yale yanayohitajika kwenye nishati safi kama vile *nickel, cobalt* na *lithium*. Aidha, GST itaendelea na ujenzi wa maabara nyingine katika maeneo ya Chunya na Geita kwa lengo la kusogeza huduma karibu na wananchi wanaojihusisha na shughuli za madini.

**180.** ***Mheshimiwa Spika,*** GST itafanya utafiti wa malighafi na kutengeneza vyungu (crucibles) 300,000 na vyungu vidogo (cupels) 75,000 kwa ajili ya kuyeyusha sampuli za dhahabu; uchunguzi wa sampuli 25,000 za udongo, miamba au madini; na uandaaji wa sampuli rejea (certified reference materials) za dhahabu, shaba, fedha, zinki, chuma na *cobalt*.

**c)Kuboresha Ufuatiliaji wa Mienendo ya Majanga ya Asili ya Jiolojia na Kuelimisha Wananchi Namna Bora ya Kupunguza Athari za Majanga**

**181.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kutekeleza jukumu hilo, GST itakusanya takwimu kutoka vituo vitano (5) vya kudumu vya kunakili mienendo ya mitetemo vilivyoko Arusha, Dodoma, Geita, Mtwara na Mbeya; kuchakata takwimu zilizokusanywa kutoka katika vituo vyote vitano (5) na kuhuisha ramani inayoonesha vitovu vya matetemeko ya ardhi nchini; kufanya matengenezo ya vifaa vya kunakili mitetemo; kuendelea kuunganisha vituo viwili (2) vya kupima mitetemo vilivyopo Dodoma na Arusha katika mfumo mubashara (real time) ili kuwezesha upatikanaji wa taarifa kwa wakati mara tetemeko linapotokea pamoja na kusimika mtambo mmoja mpya kwa ajili ya ukanda wa Bonde la ufa mkondo wa magharibi Mkoa wa Kigoma.

**182.** ***Mheshimiwa Spika,*** GST itaendelea kutoa elimu kwa umma juu ya namna bora ya kujikinga au kupunguza athari za majanga ya asili ya jiolojia. Elimu itatolewa kwa njia ya machapisho, semina na vyombo vya Habari.

**e) Kuimarisha Utekelezaji wa Majukumu ya Taasisi**

**183.** ***Mheshimiwa Spika,*** ili kuimarisha uwezo wa Taasisi katika kutekeleza majukumu yake, *GST* itaboresha mifumo ya ndani ya uchakataji, uhifadhi, usambazaji wa taarifa na takwimu za jiosayansi, taarifa za uwepo wa madini pamoja na kujenga uwezo watumishi 35 kwa kuwapatia mafunzo ya muda mfupi na mrefu.

**184.** ***Mheshimiwa Spika,*** ili kuboresha mazingira ya utendaji kazi, *GST* imepanga kununua vitendea kazi ikiwemo *Helicopter Jet Ranger* ya utafiti, kukarabati majengo, kufanya ujenzi wa maabara ya kisasa, kuboresha maslahi ya watumishi, kuboresha mifumo ya ukusanyaji mapato na kuboresha mifumo ya usimamizi wa rasilimali watu na fedha.

**(iii) Shirika la Madini la Taifa (STAMICO)**

**185.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Mwaka 2024/2025, STAMICO inatarajia kutekeleza shughuli zifuatazo:

**i. Kuimarisha Ukusanyaji wa Mapato**

***186. Mheshimiwa Spika*****,** ili kuhakikisha mapato ya Shirika yanakua na kuimarika, Shirika limepanga kuongeza usimamizi kwenye uwekezaji uliopo katika miradi yake kama ifuatavyo:

**a) Kuendelea na Uzalishaji wa Makaa ya Mawe na Mkaa Mbadala (Rafiki Briquettes)**

**187.** ***Mheshimiwa Spika*****,** Shirika litaendelea na uzalishaji mkubwa wa makaa ya mawe katika eneo la Kabulo-Kiwira ambapo katika mwaka 2024/2025 jumla ya tani 600,000 zimepangwa kuchimbwa. Ili kuimarisha na kuongeza uzalishaji huo, Shirika limepanga kununua mitambo na vifaa mbalimbali vikiwemo *dump trucks (7)*, *bull dozer D8 (1)*, *wheel loader (2)*, *longwall coal shearer (2),* na *excavator (1)*.

**188.** ***Mheshimiwa Spika*****,** Shirika linatarajia kuongeza uzalishaji wa mkaa mbadala (Rafiki briquettes) kwa kununua mitambo minne (4) ambapo kila mmoja utakuwa na uwezo wa kuzalisha tani 20

kwa saa. Pia, Shirika limepanga kununua vifaa kwa ajili ya kuongeza ufanisi katika mradi huo ambavyo ni *hauling trucks (4), drier (2), overhead crane (1), wheel loader (1), weight bridge (1), carbonizing vessel (1), carbonizing tray (1)* na kujenga ghala kwa ajili ya kuhifadhi mkaa.

**189. *Mheshimiwa Spika*,** Shirika limefanikiwa kupata mwekezaji Kampuni ya Adan Group kutoka nchini India ambayo tayari wamesaini Mkataba wa awali wa kuzalisha umeme megawati 2,000 kutokana na makaa ya mawe. Kwa mwaka 2024/2025 Shirika litahuisha taarifa ya upembuzi yakinifu ya mwaka 2006 ili kubaini kiasi halisi cha mashapo pamoja na gharama za uwekezaji.

**b) Kuimarisha Shughuli za Uchorongaji**

**190. *Mheshimiwa Spika*,** Shirika litaendelea kuimarisha shughuli za uchorongaji kwa kutangaza na kutafuta kandarasi katika migodi mikubwa na ya kati. Aidha, Shirika limepanga kununua mitambo miwili (2) ya uchorongaji ili kukidhi ongezeko la huduma za uchorongaji.

**c) Kuanza Uzalishaji wa Kokoto – Chigongwe**

**190. *Mheshimiwa Spika*,** Shirika limepanga kuanza uzalishaji wa kokoto katika leseni zake za Chigongwe Dodoma katika mwaka wa fedha 2024/25 ambapo uzalishaji unatarajiwa kuwa tani 178,000. Ili kuhakikisha uzalishaji unafanyika kwa ufanisi shirika limepanga kununua vifaa ambavyo ni *wheel loader (1), dump truck (3), excavator (1), lighting plant (2), light vehicle (1)* na *weight bridge (1)*. Aidha, ili kuhakikishia uwepo wa masoko uzalishaji wa kokoto utakapoanza, Shirika limeanza kufanya mazungumzo ya kuuza kokoto kwa kampuni kubwa za ujenzi katika miradi ya Serikali ikiwemo majengo, barabara, reli, viwanja vya mpira na viwanja vya ndege.

**ii. Kuwezesha Shughuli za Uchimbaji Mdogo na Kuimarisha Vituo vya Mfano**

**192. *Mheshimiwa Spika,*** STAMICO itaendelea kuwezesha wachimbaji wadogo kwa kununua mitambo mitano (5) ya uchorongaji; kutekeleza mpango wa mafunzo kwa wachimbaji wadogo katika maeneo mbalimbali nchini; kuviongezea uwezo vituo vya mfano vya Lwamgasa, Katente na Itumbi pamoja na kuimarisha miundombinu iliyopo. Aidha, STAMICO itaendelea kuwaunganisha wachimbaji wadogo na taasisi za fedha kwa lengo la kupata mikopo na vifaa kwa ajili ya kuendeleza shughuli za uchimbaji.

**193. *Mheshimiwa Spika*,** STAMICO itaendelea na taratibu za ujenzi wa vituo viwili vipya vya mfano vya kuchakata madini ya chumvi na chokaa katika Mkoa wa Lindi na Tanga mtawalia. Hadi sasa eneo la ujenzi wa kituo cha mfano cha chumvi limepatikana huko Nangurukuru – Lindi na taratibu za kumpata mzabuni kwa ajili ya ujenzi zinaendelea. Aidha, Shirika litaendelea na taratibu za kupata eneo la kujenga kiwanda cha chokaa Kona Z Tanga.

**iii. Kuendeleza Leseni za Shirika**

**194. *Mheshimiwa Spika*,** STAMICO itaendelea na utafutaji wa madini katika leseni zake ikiwemo leseni ya uchimbaji wa dhahabu katika eneo la Pida lililopo Mkoa wa Mara pamoja na leseni za madini mkakati na muhimu ya *cobalt* na nikeli - Kagera, shaba - Kilimanjaro, *lithium* - Dodoma, kinywe - Lindi na *rare earth elements* - Songwe.

**iv. Utekelezaji wa Miradi ya Ubia na Kampuni Tanzu**

***195. Mheshimiwa Spika,*** Shirika litaimarisha ufuatiliaji wa miradi ya ubia ambayo ni Mgodi wa *Buckreef* na Kiwanda cha Kusafisha Dhahabu Mwanza pamoja na Kampuni tanzu ya *STAMIGOLD* ili kuongeza ufanisi na kuwezesha ukusanyaji wa mapato kutoka kwenye miradi hiyo. Aidha, Shirika litaendelea kuiwezesha *STAMIGOLD* kufanya utafiti zaidi wa maeneo ya leseni zake ili kubaini mashapo mapya na kuongeza uhai wa mgodi.

**(iv) Kituo cha Jemolojia Tanzania (TGC)**

***196. Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha 2024/2025, Kituo cha Jemolojia Tanzania kinatarajia kutekeleza majukumu yafuatayo:

**a) Ujenzi wa Jengo la Kituo**

***197. Mheshimiwa Spika***, TGC imepanga kuimarisha miundombinu ya kutolea mafunzo kwa kuanza ujenzi wa jengo la ghorofa nane (8) ambalo litakuwa na miundombinu mbalimbali ikiwemo madarasa, karakana za uongezaji thamani madini, maabara za madini ya vito na bidhaa za usonara, *mineral gallery,* ofisi, hosteli kwa ajili ya wanafunzi, kantini na maduka.

**b) Utoaji wa Mafunzo na Huduma Zingine**

**198.** ***Mheshimiwa Spika,*** Kituo kitafanya udahili wa wanafunzi 101 utakaojumuisha wanafunzi 60 wa kozi za muda mrefu na wanafunzi 41 wa kozi za muda mfupi. Kozi hizo zitahusisha fani za teknolojia ya madini ya vito na usonara, (gem and jewellery technology), Utambuzi wa Madini ya Vito (gemology) na Ukataji na Ung'arishaji wa Madini ya Vito (lapidary).

**199.** ***Mheshimiwa Spika,*** Kituo kitatoa huduma za maabara kwa madini ya vito na bidhaa za usonara; kutoa ushauri kwa wadau wa madini; kufanya tafiti za kuyaongezea thamani madini; na kuhamasisha shughuli za uongezaji thamani madini nchini. Aidha, ili kuhamasisha umuhimu wa huduma za maabara Kituo kitatoa huduma za ugani ili kuhakikisha wadau wanapata taarifa sahihi za madini ya vito.

**c) Uzalishaji wa Bidhaa**

**200.** ***Mheshimiwa Spika***, Kituo kinatarajia kununua mashine 27 za kukata na kung'arisha vito na kutengeneza bidhaa za usonara. Kupatikana kwa mashine hizo kutaongeza uwezo wa TGC kuzalisha bidhaa mbalimbali zikiwemo vinyago, mikufu, hereni na bidhaa nyingine za urembo na mapambo.

**(v) Taasisi ya Uhamasishaji Uwazi na Uwajibikaji katika Rasilimali Madini, Mafuta na Gesi Asilia (TEITI)**

**201.** ***Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha Mwaka wa Fedha 2024/2025 TEITI inatarajia kutekeleza kazi zifuatazo: kuandaa na kuweka wazi ripoti ya 15 ya TEITI inayoonesha ulinganishi wa malipo ya kampuni za madini, mafuta na gesi asilia na mapato ya Serikali kwa Mwaka 2022/2023; kuweka wazi mikataba ambayo Serikali imeingia na kampuni za madini, mafuta na gesi asilia; kuweka wazi orodha ya wamiliki wa hisa katika kampuni za madini, mafuta na gesi asilia.

**202.** ***Mheshimiwa Spika,*** TEITI imepanga kuanzisha mfumo wa kielektroniki utakaotumiwa na makampuni ya uziduaji pamoja na Taasisi za Serikali kuripoti malipo yanayofanywa na kampuni hizo kwa Serikali; na kuhusisha taarifa za malipo ya fidia ya uharibifu wa mazingira uliosababishwa na shughuli za uziduaji kwenye ripoti ya TEITI. Mfumo huu utasaidia kupatikana kwa taarifa kutoka kwenye kampuni na hivyo kuongeza kasi ya uandaaji wa taarifa za TEITI.

**203.** ***Mheshimiwa Spika,*** TEITI itaendelea kuhamasisha na kutoa elimu kwa umma kuhusu matumizi ya takwimu za ripoti ya TEITI ili kutambua mchango wa Sekta ya Uziduaji katika uchumi wa nchi.

**E. SHUKRANI**

**204.** ***Mheshimiwa Spika,*** natambua wazi kuwa Serikali ya Awamu ya Sita imeendelea na juhudi kubwa za kuhakikisha kuwa uchumi wa nchi yetu unaimarika. Kasi, juhudi, na ubunifu mkubwa wa utendaji kazi anaoendelea nao Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania vinadhihirisha wazi kuwa nchi yetu inaendelea kukua kiuchumi.

**205.** ***Mheshimiwa Spika,*** kipekee nitumie fursa hii kumshukuru kwa dhati Mheshimiwa Rais kwa miongozo na maelekezo anayotupatia katika Sekta ya Madini ambayo yanaifanya Sekta hii kuendelea kukua na kuvutia wawekezaji kwa manufaa ya Taifa.

**206.** ***Mheshimiwa Spika,*** nichukue nafasi hii pia kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa maelekezo na miongozo mbalimbali katika Sekta ya Madini ambayo amekuwa akiitoa katika kusimamia utendaji wa shughuli mbalimbali kwa manufaa ya Taifa.

**207.** ***Mheshimiwa Spika,*** napenda pia nimshukuru Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb.), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa hotuba yake ambayo imetoa mwelekeo wa shughuli za Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

**208.** ***Mheshimiwa Spika,*** kipekee nimshukuru Mheshimiwa Dkt. Doto Mashaka Biteko (Mb.), Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, ambaye amekuwa na msaada mkubwa kwenye Sekta ya Madini kwa kutoa ushauri, maelekezo na miongozo mbalimbali ili kuhakikisha sekta hii inakuwa na mchango endelevu kwenye ukuaji wa uchumi wa nchi yetu.

**209.** ***Mheshimiwa Spika,*** napenda kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Steven Lemomo Kiruswa (Mb.), Naibu Waziri wa Madini kwa jinsi anavyoendelea kunipa ushirikiano katika kusimamia Sekta ya Madini. Amekuwa ni msaada mkubwa kwangu katika kuhakikisha Sekta ya Madini inatimiza malengo yake.

**210.** ***Mheshimiwa Spika,*** niwashukuru Bw. Kheri Abdul Mahimbali, Katibu Mkuu, na Bw. Msafiri Lameck Mbibo, Naibu Katibu Mkuu kwa namna wanavyosimamia vyema utekelezaji wa majukumu ya Wizara. Aidha, niwashukuru Dkt. AbdulRahman Shabani Mwanga, Kamishna wa Madini, Profesa Idris Suleiman Kikula, Mwenyekiti wa Tume ya Madini, Profesa Justinian Rwezaula Ikingura, Mwenyekiti wa Bodi ya *GST*, Meja Jenerali (Mstaafu) Michael Wambura Isamuhyo, Mwenyekiti wa Bodi ya *STAMICO*, Dkt. George Patrick Mofulu, Mwenyekiti wa Bodi ya *TGC,* CPA. Ludovick Silemwa Utouh, Mwenyekiti wa Kamati ya *TEITI*, Makamishna wa Tume ya Madini na wajumbe wa Bodi zote kwa kusimamia kwa umakini na weledi uendeshaji wa Taasisi za Wizara ya Madini.

**211.** ***Mheshimiwa Spika,*** niwashukuru Wakuu wa Idara na Vitengo, Wakuu wa Taasisi, pamoja na wafanyakazi wote wa Wizara na Taasisi zake kwa ushirikiano wanaonipa kwa kujituma bila kuchoka katika kutekeleza majukumu ya Wizara.

**212.** ***Mheshimiwa Spika,*** niwashukuru wadau wa Sekta ya Madini wakiwemo watafutaji, wachimbaji, wamiliki wa mitambo ya uchenjuaji pamoja na wafanyabiashara wa madini kwa kuendelea kutekeleza shughuli zao kwa kuzingatia Sheria, Kanuni na Taratibu za nchi. Hii imerahisisha usimamizi wa Sekta ya Madini. Aidha, nizishukuru taasisi za fedha hususan mabenki kwa kuendelea kuwapa mikopo wadau wa Sekta ya Madini wakiwemo wachimbaji wadogo. Aidha, nivishukuru vyombo vya ulinzi na usalama kwa kutuhakikishia usalama na kushirikiana nasi katika kudhibiti vitendo vya utoroshaji wa madini kwenye maeneo yenye shughuli za madini bila kusahau vyombo vya habari kwa ushirikiano wanaotupatia katika kuitangaza Sekta ya Madini.

**213.** ***Mheshimiwa Spika,*** naomba kutoa shukrani zangu za dhati kwa wananchi wa jimbo la Dodoma Mjini ambao kwa muda wote wameendelea kuniamini na kunipa ushirikiano katika kutekeleza majukumu yangu ya jimbo na Taifa. Nawaahidi na kuwahakikishia kuwa nitaendelea kuwatumikia kwa nguvu zangu zote na kwa kipaji nilichojaliwa na Mwenyezi Mungu katika kuleta maendeleo ya jimbo na Taifa kwa ujumla.

**214.** ***Mheshimiwa Spika,*** kipekee kabisa naomba nichukue fursa hii kuishukuru familia yangu kwa kunivumilia, kuniunga mkono, na kuniombea kwa Mwenyezi Mungu uzima na afya katika utekelezaji wa majukumu ya ubunge na uwaziri katika kujenga na kutetea maslahi ya Taifa.

## F. HITIMISHO

**215.** ***Mheshimiwa Spika,*** ili Wizara iweze kutekeleza majukumu na malengo yaliyopangwa ikiwemo ukusanyaji wa maduhuli ya shilingi 1,164,850,027,000.00, naomba Bunge lako Tukufu liridhie na kupitisha makadirio ya shilingi 231,983,614,000.00 kwa ajili ya matumizi ya Wizara na Taasisi zake kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 kwa mchanganuo ufuatao:

(i) shilingi 140,661,200,000.00 sawa na asilimia 60.63 ya bajeti yote ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo;

(ii) shilingi 91,322,414,000.00 sawa na asilimia 39.37 ya bajeti yote ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Kati ya fedha hizo, shilingi 24,872,875,000.00 ni kwa ajili ya mishahara ya watumishi (PE) na shilingi 66,449,539,000.00 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo (OC) ya Wizara na Taasisi zilizo chini yake.

**216.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa mara nyingine naomba nitoe shukrani zangu za dhati kwa Waheshimiwa Wabunge wote kwa kunisikiliza. Majedwali na vielelezo mbalimbali kwa ajili ya kutoa ufafanuzi wa masuala na takwimu muhimu kuhusu Sekta ya Madini vimeambatishwa pamoja na hotuba hii. Hotuba hii inapatikana katika tovuti ya Wizara ya Madini kwa kikoa cha *https://www.madini.go.tz.*

**217.** ***Mheshimiwa Spika,*** naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja imetolewa iamuliwe)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono, ahsante sana. Sasa tutamsikiliza Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini, namuona kwa niaba yake anakuja Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Nishati na Madini, Mheshimiwa Kilumbe Shabani Ng'enda aje awasiishe maoni ya Kamati. *(Makofi)*

**MHE. KILUMBE S. NG'ENDA – MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini, naomba uniruhusu kuwasilisha taarifa na pia unikubalie taarifa yote iingie kwenye Kumbukumbu Rasmi za Bunge *(Hansard)*.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema kwa kuturuzuku uhai na

afya njema na kutuwezesha Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini kuendelea kutekeleza majukumu yetu kwa maslahi ya nchi kwa kutoa ushauri unaostahili kwa Wizara ya Madini na Serikali kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 118 (9) cha Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023, naomba kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini, kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Madini - Fungu 100, kwa mwaka wa fedha 2023/2024 pamoja na Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii, kwa mwaka wa fedha 2024/2025.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Utekelezaji wa Bajeti wa 2023/2024 na Maoni ya Kamati kuhusu Bajeti ya 2024/2025 ni kutokana na majukumu ya msingi iliyopewa Kamati kwa mujibu wa Kanuni ya 117(2) ikisomwa kwa pamoja na Kifungu cha 7(1)(a) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Spika, ili kukidhi matakwa yaliyokusudiwa na Kanuni ya 118 (9) ya Kanuni za Bunge, taarifa hii imegawanyika katika sehemu zifuatazo: -

(a) Utangulizi unaoeleza msingi na muundo wa taarifa;

(b) Uchambuzi wa Utekelezaji wa Bajeti pamoja na Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024;

(c) Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025;

(d) Maoni, ushauri na Mapendekezo ya Kamati kwa Wizara na Serikali kwa ujumla; na

(e) Hitimisho ikijumuisha shukrani.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Kamati kuhusu Utekelezaji wa Bajeti na Majukumu ya Wizara - Fungu 100 kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 ulijikita katika maeneo makuu matano kama ifuatavyo: -

(a) Ukaguzi kuhusu miradi iliyotengewa fedha katika mwaka wa fedha 2023/2024;

(b) Uchambuzi kuhusu utekelezaji wa vipaumbele vya Wizara kwa mwaka wa fedha 2023/2024;

(c) Uchambuzi kuhusu ukusanyaji wa maduhuli kwa mwaka wa fedha 2023/2024;

(d) Uchambuzi kuhusu upatikanaji wa fedha hadi kufikia Mwezi Februari, 2024; na

(e) Uchambuzi kuhusu utekelezaji wa maoni, ushauri na mapendekezo ya Kamati.

Mheshimiwa Spika, ili kuzingatia masharti ya Kanuni ya 117 (1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023, Kamati ilifanya ziara tarehe 13 hadi tarehe 19 Machi, 2024 katika Mkoa wa Arusha na Dodoma ili kukagua miradi ifuatayo: -

(i) Ujenzi wa jengo la Kituo cha Jemolojia-*TGC* Arusha; na

(ii) Ujenzi wa jengo la Tume ya Madini Dodoma.

Mheshimiwa Spika, kuhusu matokeo ya ukaguzi na miradi iliyotengewa fedha, ujenzi wa jengo la Kituo cha Jemolojia Arusha, utekelezaji wa mradi huu unalenga kuimarisha utoaji wa mafunzo ya kuongeza thamani katika madini na kuanzisha karakana za uchakataji madini kwa gharama ya shilingi bilioni 35.5.

Mheshimiwa Spika, mradi huu utahusisha jengo la ghorofa nane litakalokuwa na miundombinu mbalimbali ikiwemo madarasa, karakana, viwanda vya kuongeza thamani kwenye

madini, maabara za madini na madini ya vito na bidhaa za usonara.

Mheshimiwa Spika, aidha, kutakuwa na eneo la makumbusho kwa ajili ya madini ya vito, eneo la maonesho ya minada, samani, eneo la kuegesha magari na maeneo maalaum kwa ajili ya mafunzo kwa watumishi kwa lengo la kuwaongezea uwezo *(capacity building)* pamoja na ununuzi wa vitendea kazi.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipotembelea na kukagua mradi huu, kiasi cha shilingi milioni 298.64 kilikuwa kimelipwa kwa Mshauri Elekezi kwa ajili ya usanifu wa jengo. Kiasi hicho cha fedha ni sehemu ya shilingi milioni 592.8 ambazo ni makubaliano baina ya *TGC* na kampuni hiyo. Sehemu ya malipo iliyosalia itahusisha maandalizi ya michoro ya mwisho ya usanifu pamoja na makadirio ya gharama za ujenzi.

Mheshimiwa Spika, miongoni mwa faida zinazotarajiwa kutokana na utekelezaji wa mradi huu ni pamoja na kuimarisha uwezo wa kituo kwa kutoa mafunzo kufikia kiwango cha kimataifa. Pamoja na faida hizo, uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa, utekelezaji wa mradi huo unakabiliwa na changamoto mbalimbali kama ifuatavyo: -

(a) Taratibu za manunuzi ya Umma kuchukua muda mrefu na hivyo kuathiri utekelezaji wa majukumu ya taasisi;

(b) Upungufu wa watumishi hasa wenye ujuzi katika tasnia ya madini ya vito; na

(c) Ufinyu wa eneo kwa ajili ya ujenzi wa jengo la kisasa pamoja na maegesho ya magari.

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa jengo la Tume ya Madini Dodoma. Mradi huu unahusu ujenzi wa jengo la ghorofa tatu ulioanza Januari, 2021, chini ya Mkandarasi *MCB Limited* na Mshauri Elekezi akiwa Wakala wa Majengo Tanzania *(TBA)*. Awali ilikadiriwa kuwa mradi ungegharimu kiasi cha shilingi bilioni 4.2. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 4.1 ni kwa ajili ya ujenzi na shilingi milioni 141.15 ni kwa ajili ya Mshauri Elekezi *(consultant)*.

Mheshimiwa Spika, kutokana na mwenendo usioridhisha wa mkandarasi *MCB Company Limited*, Tume ya Madini ilivunja mkataba na tarehe 8 Februari, 2023, ilisaini mkataba mpya na mkandarasi aliyeshinda zabuni, yaani Kampuni ya *Mohamed Builders Limited*, wenye thamani ya shilingi bilioni 6.5 kwa ajili ya kumalizia ujenzi.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilielezwa kuwa sababu ya ongezeko la gharama ni mkataba wa awali kutohusisha baadhi ya mahitaji muhimu kwenye jengo linalojengwa. Mabadiliko hayo yaliongeza gharama ya mradi kutoka shilingi bilioni 4.5 hadi kufikia shilingi bilioni 7.7.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilitembelea na kukagua mradi huo mwezi Machi, 2024 na utekelezaji wake ulikuwa 87.5%, huku ukitarajiwa kukamilika mwishoni mwa mwezi Aprili, 2024. Aidha, fedha ambazo zilikuwa zimelipwa kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huo ni shilingi bilioni 3.7. Maelezo zaidi kuhusu utekelezaji wa mradi huo ni kama inavyoonekana kwenye ukurasa wa tatu hadi wa 10 wa Taarifa ya Kamati.

Mheshimiwa Spika, katika uchambuzi wa utekelezaji wa vipaumbele vya Wizara kwa mwaka 2023/2024, Wizara ya Madini ilipanga kutekeleza vipaumbele sita ambavyo ni: -

(a) Kuimarisha ukusanyaji wa maduhuli na kuongeza mchango wa Sekta ya Madini kwenye pato la Taifa;

(b) Kuendeleza madini muhimu na madini mkakati;

(c) Kuendeleza na kusogeza huduma za ugani kwa wachimbaji wadogo;

(d) Kuhamasisha shughuli za uongezaji thamani madini;

(e) Kuhamasisha uwekezaji wa biashara katika Sekta ya Madini na Uanzishwaji wa minada na maonyesho ya madini ya vito; na

(f) Kuzijengea uwezo taasisi zilizo chini ya Wizara ili ziweze kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilifanya uchambuzi na kubaini kuwa utekelezaji wa vipaumbele unaridhisha jambo ambalo limeifanya Sekta ya Madini kuendelea kuongeza mchango wake katika pato la Taifa.

Mheshimiwa Spika, aidha, utekelezaji wa vipaumbele uliiwezesha Serikali kuendelea kudhibiti utoroshaji wa madini ambapo madini ya thamani ya shilingi bilioni 2.42 yalikamatwa katika kipindi cha Julai, 2023, hadi Februari, 2024. Maelezo zaidi kuhusu utekelezaji wa vipaumbele yanapatikana kwenye ukurasa wa 10 hadi wa 13 wa Taarifa ya Kamati.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa utekelezaji wa Mpango wa Bajeti wa Mwaka 2023/2024 kuhusu ukusanyaji wa maduhuli. Katika mwaka wa fedha wa 2023/2024, Wizara ya Madini Fungu 100 ilipangiwa kukusanya maduhuli yenye thamani ya shilingi trilioni 1.01 kutoka vyanzo vyake mbalimbali. Kati ya kiasi hicho cha fedha, shilingi bilioni 882.13 zilipangwa kukusanywa na kuwasilishwa Hazina na shilingi bilioni 124.58 zilipangwa kukusanywa na kutumiwa na taasisi zilizo chini ya Wizara.

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia mwezi Februari, 2024, fedha zilizokusanywa na kuwasilishwa Hazina zilikuwa ni shilingi bilioni 476.21, sawa na 54% ambayo ni chini ya wastani kama inavyoonekana kwenye kielelezo Na. 1 cha taarifa hii.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa makusanyo ya shilingi bilioni 124.58 ambayo yalipangwa kukusanywa na kutumiwa na taasisi, hadi mwezi Februari, 2024 ni kiasi cha shilingi bilioni 34.9 tu ndicho kilikuwa kimekusanywa sawa na 28.12% ya lengo kama inavyoonekana katika Kielelezo Na. 2 kwenye Taarifa ya Kamati.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilihoji sababu za makusanyo hayo ya taasisi kuwa chini ya lengo na ilielezwa kwamba ni kutokana na lengo kubwa lililowekwa na Serikali baada ya hoja zilizoibuliwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali *(CAG)* kwamba ni kwa nini Wizara inakusanya na kuvuka malengo kila

wakati? Maelezo zaidi kuhusu mwenendo wa ukusanyaji wa maduhuli ni kama inavyoonekana kwenye ukurasa wa 13 hadi wa 16 wa taarifa hii.

Mheshimiwa Spika, kuhusu uchambuzi kuhusu upatikanaji wa fedha, hadi kufikia Februari, 2024: Katika mwaka wa fedha 2023/2024, Wizara ya Madini Fungu 100 iliidhinishiwa jumla ya shilingi bilioni 163.01. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 45.88 sawa na 28.14%, ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo *(OC)*, shilingi bilioni 20.31 sawa na 12.46% ni kwa ajili ya mishahara na shilingi bilioni 96.82 sawa na 59.43% ni kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia Februari, 2024, Wizara ilikuwa imepokea jumla ya shilingi bilioni 125.24 sawa na 76.83% ya bajeti yote iliyoidhinishwa. Uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa kati ya fedha hizo zilizopokelewa, matumizi mengineyo ni shilingi 34.88 sawa na 76.02%, mishahara ni shilingi bilioni 14.46 sawa na 71.19% na miradi ya maendeleo ni shilingi bilioni 75.91 sawa na 78.48% ya bajeti iliyoidhinishwa.

Mheshimiwa Spika, Kamati imebaini kuwa, kwa ujumla fedha zilipatikana kwa kiasi cha kuridhisha, kwani ilikuwa ni juu ya wastani uliotarajiwa wakati huo.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa utekelezaji wa maoni, ushauri na mapendekezo ya Kamati kwa mwaka wa fedha 2023/2024. Taarifa ya Kamati kuhusu uchambuzi wa Bajeti ya Wizara hii kwa mwaka wa fedha 2023/2024, ilitoa jumla ya maoni 18 ili utekelezaji wake uchangie katika kuboresha utendaji kazi wa Wizara na Serikali kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa, kwa kiasi kikubwa Wizara imezingatia na kutekeleza maoni, ushauri na mapendekezo hayo na mengine utekelezaji wake unaendelea. Maelezo zaidi kuhusu utekelezaji wa maoni ni kama inavyoonekana kwenye ukurasa wa 18 hadi wa 19 wa Taarifa ya Kamati.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Wizara ya Madini Fungu 100 kwa Mwaka wa Fedha wa 2024/2025. Katika eneo hili, uchambuzi wa Kamati ulijielekeza katika maeneo yafuatayo: -

(a) Malengo ya Wizara kwa mwaka 2024/2025;

(b) Makadirio ya makusanyo ya maduhuli kwa mwaka wa fedha 2024/2025;

(c) Makadirio ya mapato mwaka wa fedha 2024/2025; na

(d) Mlinganisho wa bajeti ya Wizara dhidi ya Bajeti ya Taifa.

Mheshimiwa Spika, makadirio ya makusanyo ya maduhuli kwa mwaka wa fedha 2024/2025. Katika mwaka wa fedha 2024/2025, Wizara ya Madini Fungu 100 inakadiriwa kukusanya jumla ya shilingi trilioni 1.1. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 887.6 sawa na 84.34% zitakusanywa kupitia idara, vitengo vya Wizara na Tume ya Madini na zitawasilishwa Hazina. Aidha, shilingi bilioni 164.9 sawa na 15.66% zitakusanywa na kutumiwa na taasisi zilizo chini ya Wizara.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa, makadirio hayo yameongezeka kwa shilingi bilioni 45.78 sawa na 4.55% ikilinganishwa na makadirio ya mwaka wa fedha 2023/2024 ambayo yalikuwa shilingi trilioni 1.01 kama inavyoonekana kwenye Kielelezo Na. 5. Aidha, maelezo zaidi kuhusu makadirio ya makusanyo yanapatikana kwenye ukurasa wa 22 hadi 25 wa Taarifa ya Kamati.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2024/2025, Wizara ya Madini Fungu 100 inakadiriwa kutumia jumla ya shilingi bilioni 231.98. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 140.66 sawa na 60.64% ni kwa ajili ya maendeleo na shilingi bilioni 91.3 sawa na 39.37% ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida.

Mheshimiwa Spika, fedha za matumizi ya kawaida zinajumuisha shilingi bilioni 24.87 ambayo ni 10.72% kwa ajili ya mishahara na shilingi 66.45 sawa na 28.64% ni kwa ajili ya matumizi

mengineyo *(OC)* kwa Wizara na taasisi zake kama inavyoonekana kwenye Kielelezo Na. 6.

Mheshimiwa Spika, Kamati imefanya uchambuzi kwa kuzingatia Bajeti ya Wizara, kati ya mwaka 2023/2024 na 2024/2025 na imebaini kwamba, kwa ujumla bajeti imeongezeka kwa 41.7% kutoka shilingi bilioni 163.01 mwaka 2023/2024, hadi kufikia shilingi bilioni 231.98 mwaka 2024/2025. Ongezeko hilo la bajeti limegusa maeneo yote ya Wizara kwa maana ya mishahara, matumizi mengineyo na maendeleo. Kielelezo Na. 7 kinafafanua zaidi.

Mheshimiwa Spika, Kamati inapongeza hatua hiyo ya Serikali kuongeza Bajeti ya Wizara hii, kwani itakuwa ni chachu ya kuboresha utendaji na kuifanya Sekta ya Madini iendelee kufanya vizuri na kuongeza mchango kwenye pato la Taifa. Aidha, Wizara itumie nyongeza hiyo ya bajeti kuongeza ufanisi wa kiutendaji kwa watendaji wake. Maelezo zaidi kuhusu makadirio ya matumizi ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2024/2025 yanapatikana ukurasa wa 25 hadi 28 wa Taarifa ya Kamati.

Mheshimiwa Spika, baada ya uchambuzi na ufafanuzi wa yaliyobainika katika ukaguzi wa miradi iliyotengewa fedha pamoja na uchambuzi wa bajeti, Kamati inatoa maoni, ushauri na mapendekezo yafuatayo: -

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa miradi iliyotengewa fedha katika mwaka wa fedha 2023/2024, umekuwa ukisuasua kutokana na sababu mbalimbali ikiwemo mabadiliko ya usanifu na mabadiliko ya wakandarasi katika mradi wa jengo la *TGC* Arusha na ujenzi wa jengo la Tume ya Madini, Dodoma.

Mheshimiwa Spika, mabadiliko hayo yamesababisha kuongezeka kwa gharama na kuchelewa kukamilika kwa miradi katika muda uliopangwa. Ni vyema usanifu na tathmini ya kina vifanyike kwa kiwango cha kuridhisha kabla ya kuanza utekelezaji wa miradi hii ili kuepuka ongezeko la gharama na kuwezesha miradi kukamilika kwa wakati uliopangwa.

Mheshimiwa Spika, tozo katika halmashauri. Baadhi ya halmashauri nchini zimekuwa zikitunga sheria Ndogo *(By Laws)* za ukusanyaji wa tozo zinazokinzana na sheria mama, hivyo kusababisha usumbufu na kuongeza gharama kwa wachimbaji wa madini hasa madini ya ujenzi na madini ya viwandani. Ni vyema Serikali ikatatua changamoto hii kwa wakati kwa kuweka utaratibu utakaoondoa mgongano uliopo na kuwezesha wawekezaji kuendesha kazi zao bila usumbufu.

Mheshimiwa Spika, uhaba wa watumishi hasa wa kada muhimu kama vile ukaguzi na udhibiti wa madini unaozikumba Taasisi za *STAMICO, TGC* na *GST* unaathiri utendaji wa taasisi hizo. Kwa kuwa Wizara imepata vibali vya ajira mpya na ajira za uhamisho, ipunguze haraka uhaba uliopo kwa uhamisho wa watumishi kutoka taasisi nyingine za Umma, huku mchakato wa ajira mpya ukiendelea kwa mujibu wa taratibu.

Mheshimiwa Spika, utendaji wa taasisi chini ya Wizara ya Madini umeathiriwa na taratibu za ununuzi kuchukua muda mrefu na mabadiliko ya mifumo ya ununuzi kutoka *TANePS* kwenda mfumo wa *NeST*. Kamati inaunga mkono matumizi ya mifumo lakini ni vyema Serikali ihakikishe mifumo na taratibu za manunuzi zinaboreshwa na kurahisisha utendaji wa baadhi ya taasisi kulingana na upekee wake badala ya kuleta vikwazo.

Mheshimiwa Spika, maoni mahsusi kwa Shirika la Madini *(STAMICO)*. Kamati inapongeza hatua ya *STAMICO* kuondoa sharti la dhamana ya shilingi milioni 50 kwa Mawakala wa Mkaa *(coal briquettes)*. Hatua hiyo imewezesha mawakala 66 kuingia katika biashara ya nishati hiyo.

Mheshimiwa Spika, pia Kamati inapongeza hatua ya *STAMICO* kuendelea kulipa madeni ambayo *STAMIGOLD* inadaiwa na wazabuni ambapo deni lililobaki ni shilingi bilioni 18.5 kutoka deni la zamani ambalo lilikuwa shilingi bilioni 40.8 lililokuwepo hadi Juni, 2023. Aidha, juhudi za kulipa deni hilo ziendelee na ikiwezekana Serikali isaidie kulichukua ili wazabuni wasiendelee kuathirika.

Mheshimiwa Spika, pia, *STAMICO* ihakikishe mitambo mitano ya uchorongaji iliyowasilishwa nchini mwishoni mwa mwaka 2023 na kuanza kazi kwenye baadhi ya maeneo ikiwa ni pamoja na yenye leseni za wachimbaji wadogo Nyamongo – Tarime, Mkoani Mara, inalenga kuwasaidia na kuwanufaisha wachimbaji wadogo na siyo vinginevyo.

Mheshimiwa Spika, aidha, Wizara ihakikishe gharama wanayotozwa wachimbaji wadogo ni nafuu na inaenda sambamba na utoaji wa elimu ili kuwajengea ujuzi wa kutumia vifaa vya kisasa. Vilevile Serikali iendelee kuongeza mitambo na kuitawanya kwa usawa katika maeneo mengine ya wachimbaji wadogo nchini.

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na mchakato wa kuzalisha umeme wa *Megawatt* 200 katika Mgodi wa Makaa ya Mawe wa Kiwira kwa muda mrefu na utekelezaji wake umekwama. Kwa kuwa amepatikana mwekezaji *(Adan Group Company)* mwenye nia ya kuwekeza katika mradi huo na kuzalisha takribani *Megawatt* 2,000, Serikali isimamie mchakato huo kikamilifu na kuweka mazingira mazuri yatakayomwezesha mwekezaji huyo kutekeleza azma hiyo.

Mheshimiwa Spika, kutokana na umuhimu wa Tume ya Madini katika kuhakikisha kwamba mchango wa sekta ya madini kwenye pato la Taifa unaongezeka, ujenzi wa jengo la Ofisi ya Makao Makuu ya Tume ya Madini usimamiwe na kukamilika kwa wakati ili kuwawezesha watumishi wa taasisi hiyo kutekeleza majukumu yao katika mazingira bora na hivyo kuifanya sekta ya madini iendelee kuchangia katika pato la Taifa.

Mheshimiwa Spika, ulipaji wa fidia kwa wananchi wanaopisha maeneo yao ili kuruhusu uendelezaji wa shughuli za madini katika maeneo mbalimbali kwa njia ya uwekezaji unaendelea kuathiri wananchi kwa kupata fidia ndogo na inayochelewa. Kamati inaitaka Serikali isimamie kikamilifu suala hili ili kuboresha viwango vya fidia kuendana na thamani halisi ya maeneo ambayo wananchi wanayaachia, na kulipwa kwa wakati. Aidha, Serikali iwahamasishe na kuwaelimisha wananchi ili waone umuhimu wa kupewa hisa huru *(free carried interest)*.

Mheshimiwa Spika, Kamati inapongeza hatua ya Serikali ya kuanza kufuta leseni maeneo ambayo hayajaendelezwa kwa muda mrefu kinyume na matakwa ya sheria na kanuni, ambapo hadi Februari, 2024 leseni 2,648 zilifutwa. Kwa kuwa jambo hili lina manufaa makubwa kiuchumi, Kamati inashauri Serikali iendelee kuchukua hatua zaidi za kufuta leseni na kugawa maeneo husika kwa wawekezaji wengine ambao wana nia ya kuwekeza ndani ya muda uliotolewa kwenye leseni.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na Wakala wa Jiolojia Tanzania *(GST)* Kamati inashauri uimarishaji wa kanzidata ya miamba upewe kipaumbele ili kuwezesha nchi kuwa na taarifa sahihi kuhusu miamba, jambo ambalo litaisaidia nchi kutambua mapema na kuepuka majanga mbalimbali ya kiasili ikiwa ni pamoja na maporomoko ya udongo.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Serikali imedhamiria kuwa na taarifa sahihi za kijiofizikia, ikiwa ni pamoja na kuongeza kiwango cha utafiti wa maeneo yenye madini nchini kutoka asilimia 16 ya sasa, ni vyema mchakato wa kuongeza kiwango cha utafiti huo ukafanyika mapema ili wananchi waweze kunufaika na matokeo ya utafiti huo.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Kituo cha Jimuolojia Tanzania *(TGC)* Kamati inaipongeza Serikali kwa kutenga shilingi bilioni saba kwa ajili ya utekelezaji wa mradi wa majengo ya *TGC* ambao maandalizi yalianza muda mrefu lakini ujenzi haujakamilika.

Mheshimiwa Spika, mwisho, napenda kuchukua fursa hii kukushukuru sana wewe binafsi Dkt. Tulia Ackson, Mheshimiwa Naibu Spika, Wenyeviti, wa Bunge letu kwa kazi kubwa mnayoifanya na ushirikiano mkubwa mnaotupa. Kwa namna ya kipekee napenda kuwashukuru Wajumbe wote wa Kamati ya Nishati na Madini wakiongozwa na Mwenyekiti wetu Mheshimiwa Dkt. David Mathayo David kwa kazi kubwa wanayoifanya katika sekta hii ya madini.

Mheshimiwa Spika, napenda kumshukuru Waziri, mchapakazi na kijana, Mheshimiwa Antony Peter Mavunde, Naibu wake

Mheshimiwa Dkt. Steven Lemomo Kiruswa, Mbunge pamoja na watendaji wote wa Wizara hiyo wakiongozwa na Katibu Mkuu Ndugu Kheri Mahimbali; kijana mchapakazi huyu, pamoja na Naibu Katibu Mkuu, Ndugu Msafiri Mbibo kwa ushirikiano wao ambao umesaidia Kamati kuwezesha kufanikisha kazi zake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee napenda kuwashukuru watumishi wote wa Ofisi ya Bunge chini ya uongozi thabiti wa Katibu wa Bunge Ndugu Nenelwa Mwihambi, kwa ushirikiano ambao anaendelea kutupatia na kutuwezesha kukamilisha kazi zetu.

Mheshimiwa Spika, kabla sijawasilisha naomba uniruhusu pia niwashukuru wananchi wa Jimbo la Kigoma Mjini ambao wamenileta hapa Bungeni kwa imani waliyonionyesha ya kunipigia kura nyingi na kuniwezesha kuwa Mbunge wao na leo kuwa Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Madini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho, naomba sasa Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha Makadilio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Madini Fungu 100 kwa Mwaka wa Fedha wa 2024/2025 kama yalivyowasilishwa na mtoa hoja.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja na naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**30 APRILI, 2024**

# TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA NISHATI NA MADINI KUHUSU UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA WIZARA YA MADINI (FUNGU 100) KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024 PAMOJA NA MAONI YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025 – KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI

## SEHEMU YA KWANZA

### 1.0 UTANGULIZI

**Mheshimiwa Spika**, awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema kwa kuturuzuku uhai na afya njema na kutuwezesha Wajumbe wa Kamati kuendelea kutekeleza majukumu yetu kwa maslahi ya nchi kwa kutoa ushauri unaostahili kwa Wizara ya Madini na Serikali kwa ujumla.

Kwa mujibu wa **Kanuni ya 118 (9)** ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari 2023[1], naomba kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu, Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini, kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Madini **(Fungu 100)** kwa mwaka wa fedha 2023/2024 pamoja na maoni, ushauri na mapendekezo ya Kamati kuhusu makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara hii kwa mwaka wa fedha 2024/2025.

Uchambuzi wa utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2023/2024 na maoni ya kamati kuhusu bajeti ya mwaka 2024/2025 ni kutokana na majukumu ya msingi iliyopewa Kamati kwa mujibu wa kanuni ya 117(2) ikisomwa kwa pamoja na kifungu cha 7(1)(a) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari 2023[2].

**Mheshimiwa Spika**, ili kukidhi matakwa yaliyokusudiwa na Kanuni ya 118 (9) ya Kanuni za Bunge, taarifa hii imegawanyika katika sehemu zifuatazo: -

[1] Baada ya Waziri kuwasilisha Hotuba ya Bajeti kwa mujibu wa fasili (1), Mwenyekiti wa Kamati iliyopitia Makadirio husika na Msemaji wa Kambi Rasmi ya Walio Wachache Bungeni watatoa maoni yao kwa muda usiozidi dakika thelathini kila mmoja

[2] 7.-(1) Majukumu ya Kamati ya Kudumu ya Bunge za kisekta yatakuwa yafuatayo:- (a) kushughulikia bajeti ya Wizara inazozisimamia;

a) Sehemu ya Kwanza inahusu Utangulizi na inaeleza msingi na muundo wa taarifa;

b) Sehemu ya Pili inahusu uchambuzi wa utekelezaji wa bajeti pamoja na maoni, ushauri na mapendekezo ya Kamati kwa mwaka wa fedha 2023/2024;

c) Sehemu ya Tatu inahusu uchambuzi wa makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2024/2025;

d) Sehemu ya Nne inahusu maoni, ushauri na mapendekezo ya Kamati kwa Wizara na Serikali kwa ujumla; na

e) Sehemu ya Tano ni hitimisho ikijumuisha shukrani.

## SEHEMU YA PILI

## 2.0 UCHAMBUZI WA UTEKELEZAJI WA BAJETI PAMOJA NA MAONI, USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi wa Kamati kuhusu utekelezaji wa bajeti na majukumu ya Wizara ya Madini **(Fungu 100)** kwa mwaka wa fedha 2023/2024 ulijikita katika maeneo makuu matano (5) kama ifuatavyo: -

a) Ukaguzi kuhusu miradi iliyotengewa fedha katika mwaka wa fedha 2023/2024;

b) Uchambuzi kuhusu utekelezaji wa vipaumbele vya Wizara kwa mwaka wa fedha 2023/2024;

c) Uchambuzi kuhusu ukusanyaji wa maduhuli kwa mwaka wa fedha 2023/2024;

d) Uchambuzi kuhusu upatikanaji wa fedha hadi kufikia mwezi Februari, 2024; na

e) Uchambuzi kuhusu utekelezaji wa maoni, ushauri na mapendekezo ya Kamati.

## 2.1 Ukaguzi kuhusu miradi iliyotengewa fedha katika mwaka wa fedha 2023/2024

**Mheshimiwa Spika,** ili kuzingatia masharti ya Kanuni ya 117 (1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023[3], Kamati ilifanya ziara ya ukaguzi wa baadhi ya miradi inayotekelezwa na Wizara ya Madini. Ziara hiyo ilifanyika tarehe 13 na 19 Machi, 2024 katika mkoa wa Arusha na Dodoma mtawalia ambapo Kamati ilitembelea na kukagua miradi ifuatayo: -

a) Ujenzi wa jengo la Kituo cha Jemolojia-TGC (Mradi Na. 1120) Arusha; na

b) Ujenzi wa jengo la Tume ya Madini (Mradi Na. 6389), Dodoma.

### 2.1.1 Matokeo ya ukaguzi wa miradi iliyotengewa fedha

#### a) Ujenzi wa jengo la Kituo cha Jemolojia – TGC (Mradi Na. 1120), Arusha

**Mheshimiwa Spika,** utekelezaji wa mradi huu unalenga kuimarisha utoaji wa mafunzo ya kuongeza thamani katika madini na kuanzisha karakana za uchakataji madini. Aidha, gharama za mradi ni **shilingi 35, 506,452,970.** Kiasi hicho kimekusudia kujenga jengo la kisasa na litahusisha ujenzi wa jengo la ghorofa nane (8) litakalokuwa na miundombinu mbalimbali ikiwemo madarasa, karakana (viwanda) vya kuongeza thamani kwenye madini, maabara za madini ya vito na bidhaa za usonara, *mineral gallery*, ofisi, mabweni ya wanafunzi na maduka ya aina mbalimbali ikiwemo maduka ya usonara na vito. Vilevile, mradi utahusu ujenzi wa eneo la makumbusho kwa ajili ya madini ya vito, eneo la maonesho, minada, samani, eneo la kuegesha magari na maeneo maalum kwa ajili ya mafunzo kwa watumishi kwa lengo la kuwaongezea uwezo (capacity building) pamoja na ununuzi wa vitendea kazi.

**Mheshimiwa Spika,** kamati ilipotembelea na kukagua mradi huu kiasi cha **shilingi 298,637,533,** kilikuwa kimekwishalipwa kwa

[3] 117.-(1) Baada ya kuwasilishwa kwa mapendekezo ya mpango na kiwango cha ukomo wa Bajeti ya Serikali kwa mwaka wa fedha unaofuata kwa Wabunge, Kamati za Bunge za kisekta zitatembelea na kukagua utekelezaji wa miradi iliyotengewa fedha kwa mwaka wa fedha unaoisha, kwa siku zisizozidi saba.

mshauri elekezi kwa ajili ya usanifu wa jengo. Kiasi hicho cha fedha ni sehemu ya **shilingi 592,850,060** ambazo ni makubaliano baina ya TGC na kampuni hiyo. Sehemu ya malipo iliyosalia itahusisha maandalizi ya michoro ya mwisho ya usanifu pamoja na makadirio ya gharama za ujenzi.

Pamoja na hatua hizo, ukamilishaji wa taratibu za ununuzi na kupata mkandarasi zimechelewa kutokana na mabadiliko ya mfumo wa ununuzi wa umma katika mwaka wa fedha 2023/2024 kutoka mfumo wa awali wa TANePS, kwenda mfumo mpya wa NeST. Kwa mujibu wa taratibu, kabla ya kuanza kutumika kwa mfumo huo ililazimu watumishi kupatiwa mafunzo kuhusu mfumo na matumizi yake.

**Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa kuwajengea uwezo watumishi ndani na nje ya nchi, utaratibu ulianza katika mwaka wa fedha 2022/2023 ambapo tayari watumishi 9 wamepata mafunzo kwenye vyuo na taasisi zilizobobea kwenye masuala ya uongezaji thamani madini katika nchi za India, Thailand na China.

**Mheshimiwa Spika**, miongoni mwa faida zinazotarajiwa kutokana na utekelezaji wa mradi huu ni pamoja na kuimarisha uwezo wa kituo wa utoaji mafunzo kufikia kiwango cha kimataifa, kuweka mazingira bora na rafiki ya kutolea mafunzo, kituo kuweza kuchakata madini na kuzalisha bidhaa mbalimbali za vito na usonara na kuwa na miundombinu wezeshi kwa ajili ya minada na maonesho ya madini.

Pamoja na faida hizo zinazotarajiwa, uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa utekelezaji wa mradi huo unakabiliwa na changamoto mbalimbali kama ifuatavyo: -

i) Taratibu za ununuzi wa umma kuchukua muda mrefu na hivyo kuathiri utekelezaji wa majukumu ya Taasisi;

ii) Upungufu wa watumishi hasa wenye ujuzi katika tasnia ya madini ya vito; na

iii) Ufinyu wa eneo kwa ajili ya ujenzi wa jengo la kisasa pamoja na maegesho ya magari.

**Mheshimiwa Spika,** katika ukaguzi wa mradi huu Kamati ilibaini kwamba, jengo litajengwa katika eneo zuri na lenye watu wengi, na hivyo shughuli na huduma katika jengo hilo mara litakapokamilika zina uwezekano mkubwa wa kuwavutia watu wengi ikiwemo wafanyabiashara wakubwa wa madini ya vito kutoka ndani na nje ya nchi ikizingatiwa kuwa Arusha ni mji wa kitalii. Hata hivyo, Kamati ilibaini kuwa eneo lililotengwa kwa ajili ya maegesho ni dogo na hivyo lina uwezekano mkubwa wa kusababisha usumbufu kutokana na uhaba wa maegesho ya magari.

**b) Ujenzi wa jengo la Tume ya Madini (Mradi Na. 6389), Dodoma**

**Mheshimiwa Spika,** mradi huu unahusu ujenzi wa jengo la ghorofa tatu na ulianza Januari 2021 chini ya mkandarasi MCB Ltd ambayo ni kampuni inayomilikiwa na Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya (MUST) na mshauri elekezi akiwa Wakala wa Majengo Tanzania (TBA). Awali ilikadiriwa kuwa mradi ungegharimu **shilingi 4,211,002,617.00**, kati ya fedha hizo **shilingi 4,069,855,737.00** ni kwa ajili ya ujenzi na **shilingi 141,146,880.00** ni kwa ajili ya mshauri elekezi (consultancy). Hata hivyo, kutokana na mwenendo usioridhisha wa mkandarasi M/s MCB Company Ltd, Tume ya Madini ilivunja mkataba na kufanya mchakato wa ununuzi upya ili kumpata mkandarasi mwingine atakaetekeleza mradi na kuukamilisha kwa wakati.

**Mheshimiwa Spika,** tarehe 08 Februari, 2023 Tume ya Madini ilisaini mkataba na mkandarasi aliyeshinda zabuni, M/s Mohammed Builders Ltd wenye thamani ya **shilingi 6,505,035,057.97** kwa ajili ya kumalizia ujenzi**.** Kamati ilielezwa kuwa sababu ya ongezeko la gharama ni mkataba wa awali kutohusisha baadhi ya mahitaji muhimu kwenye jengo litakalojengwa kama vile, miundombinu ya kuzima moto, vipoza hewa (air conditions), mgahawa (canteen), ukuta wa jengo (fence), miundombinu ya kuzuia maji ya mvua, na kodi ya ongezeko la thamani (VAT).

**Mheshimiwa Spika,** kutokana na mabadiliko ya mkandarasi na kuongezeka kwa mahitaji muhimu kwenye jengo hilo, gharama halisi za mradi ziliongezeka kutoka **shilingi 4,211,002,617.00** hadi kufikia **shilingi 7,657,393, 617.03.**

Kamati ilipotembelea na kukagua mradi huu mwezi Machi 2024, utekelezaji wake ulikuwa umefikia **asilimia 87.5** huku ukitarajiwa kukamilika mwishoni mwa Aprili, 2024. Aidha, fedha ambazo zilikuwa zimelipwa kwa ajili ya utekelezaji huo ni **shilingi 3,703,763,638.31** kwa ajili ya kazi zilizotekelezwa na wakandarasi (MCB Company Ltd na M/s Mohammed Builders) na msimamizi mshauri (TBA).

**Mheshimiwa Spika,** mradi utakapokamilika unatarajiwa kuwawezesha watumishi wote wa tume ya madini makao makuu kuwa katika jengo moja na hivyo kuimarisha utoaji wa huduma kwa wananchi na wadau wengine.

### 2.1.2 Maoni ya jumla kuhusu utekelezaji wa miradi iliyotembelewa na Kamati

(a) Kwa kuwa ujenzi wa jengo la kituo cha Jemolojia ni muhimu ili kukisaidia kituo hicho kuimarisha uwezo wa kutoa mafunzo, kuchakata madini na kuzalisha bidhaa za vito na usonara, na kuwa na miundombinu wezeshi kwa ajili ya minada na maonesho ya madini, ni muhimu Wizara ihakikishe:-

(i) Mabadiliko ya mifumo ya ununuzi wa umma hayakwamishi utekelezaji wa mradi huu;

(ii) Inaendelea kutatua changamoto ya upungufu wa watumishi hasa wenye ujuzi wa madini ya vito ili mradi utakapokamilika kituo kiendelee na majukumu kwa kasi na ufanisi; na

(iii) Kituo kinapata eneo kubwa zaidi kwa ajili ya maegesho ya magari kwani lililopo ni finyu; na

(iv) Majengo ya zamani jirani na litakapojengwa jengo jipya yaboreshwe ili kukiwezesha kituo kuonekana ni cha kisasa.

(b) Ujenzi wa jengo la Tume ya Madini ni muhimu ili kuwezesha watumishi wa makao makuu kupata ofisi na mazingira mazuri ya kufanyia kazi. Kwa kuwa, mradi huo umechelewa kukamilika kutokana na mabadiliko ya wakandarasi pamoja na usanifu, Serikali ihakikishe:-

i. Kuna usimamizi wa karibu na madhubuti ili utekelezaji wa sehemu ya mradi iliyobaki ukamilike kwa wakati na kwa mujibu wa mkataba;

ii. Fedha zilizotengwa kwa ajili ya mradi huo zinatolewa kikamilifu na kwa wakati ili kutokwamisha utekelezaji wake; na

iii. Maandalizi ya ununuzi wa samani kwa ajili ya jengo yaanze mapema ili ujenzi utakapokamilika ofisi zianze kutumika.

**2.2 Uchambuzi wa Utekelezaji wa Vipaumbele vya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024**

**Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Madini ndiyo yenye dhamana ya kusimamia maendeleo ya Sekta ya Madini nchini kwa kuweka mifumo madhubuti kwa ajili ya kusimamia ufuatiliaji, uchimbaji, uongezaji thamani na biashara ya madini nchini ili kuongeza mchango wa Sekta ya Madini kwenye Pato la Taifa.

Katika mwaka wa fedha 2023/2024, Wizara ya Madini ilipanga kutekeleza vipaumbele sita (6) ambavyo ni: -

i) Kuimarisha ukusanyaji wa maduhuli na kuongeza mchango wa Sekta ya Madini kwenye Pato la Taifa;

ii) Kuendeleza madini muhimu na madini mkakati;

iii) Kuwaendeleza na kusogeza huduma za ugani kwa wachimbaji wadogo;

iv) Kuhamasisha shughuli za uongezaji thamani madini;

v) Kuhamasisha uwekezaji na biashara katika sekta ya madini na uanzishwaji wa minada na maonesho ya madini ya vito; na

vi) Kuzijengea uwezo taasisi zilizo chini ya Wizara ili ziweze kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imefanya uchambuzi wa utekelezaji wa vipaumbele hivi na kubaini kuwa, utekelezaji wake unaridhisha. Kutokana na juhudi za Serikali kuimarisha ukusanyaji wa maduhuli na kuongeza mchango wa sekta ya madini kwenye pato la Taifa; ukuaji wa sekta ya madini na mchango wake kwenye pato la Taifa umeendelea kuongezeka. Kwa mfano, ukuaji wa sekta ya madini ulifikia wastani wa **asilimia 10.2** katika robo ya tatu ya mwaka 2023 (Julai – Septemba, 2023), ikilinganishwa na ukuaji wa **asilimia 9.6** katika kipindi kama hicho mwaka 2022.

Aidha, mchango wa sekta ya madini kwenye pato la taifa katika kipindi hicho uliongezeka hadi **asilimia 10.9** ikilinganishwa na mchango wa **asilimia 9.5** kwa kipindi kama hicho mwaka 2022. Vilevile, udhibiti na ulinzi wa raslimali madini ambao umetekelezwa na Wizara kwa lengo la kukabili utoroshwaji wa madini uliwezesha kukamatwa kwa madini mbalimbali yenye thamani ya **shilingi 2,419,256,431.04** katika kipindi cha kuanzia Julai, 2023 hadi Februari, 2024. Maeneo ambayo madini hayo yalikamatwa ni Geita, Songwe, Chunya, Mbeya, Kahama na Kilimanjaro.

Kamati inashauri Wizara iendelee kuboresha mifumo ya ulinzi na udhibiti wa matukio ya utoroshaji madni ili nchi iendelee kunufaika na sekta hii. Aidha, mwenendo huu mzuri, unatoa taswira kwamba lengo la kuiwezesha sekta ya madini kuchangia asilimia 10 kwenye pato la taifa ifikapo 2025, linaweza kufikiwa au kuwa zaidi.

**Mheshimiwa Spika,** katika kipaumbele cha kuendeleza madini muhimu na madini mkakati, Wizara iliendeleza jitihada za kuhakikisha madini muhimu na madini mkakati yanalinufaisha Taifa. Juhudi hizo ni pamoja na kufanya tafiti na kutangaza fursa za uwekezaji katika utafiti na uchimbaji wa madini hayo, na kutoa leseni katika maeneo hayo.

**Mheshimiwa Spika,** katika kuwaendeleza na kusogeza huduma za ugani kwa wachimbaji wadogo; Serikali imeendelea kutoa elimu kwa wananchi kuhusu ushiriki wao katika shughuli za madini ikiwa ni sehemu ya kuendeleza shughuli za wachimbaji wadogo. Serikali imeliwezesha Shirika la Madini la Taifa (STAMICO) kununua mitambo mitano (5) ya uchorongaji (drilling rig) ili kuwasiaidia wachimbaji wadogo na kuigawa katika maeneo ya Itumbi (Chunya), Lwamgasa (Geita), Katente (Bukombe), Buhemba (Butiama), Nyamongo, Tarime na Dodoma. Mitambo hiyo ilianza uchorongaji Disemba, 2023 katika maeneo ya wachimbaji wadogo Nyamongo, Tarime mkoani Mara.

Aidha, STAMICO inaendelea kutekeleza mkakati wa kuwasaidia wachimbaji wadogo kwa kutoa mafunzo na kuanza ujenzi wa vituo vipya viwili vya mfano kwa madini ya chokaa katika mkoa wa Tanga na madini ya chumbi katika mkoa wa Lindi. **Kamati inashauri Serikali iendelee kuongeza kasi ya kusaidia wachimbaji wadogo, kwani maeneo ambayo yamefikiwa ni machache ikilinganishwa na maeneo ya wachimbaji wadogo nchini. Aidha, kuwawezesha wachimbaji wadogo kutaongeza mchango wa sekta ya madini kwenye uchumi na pato la Taifa.**

### 2.3 Uchambuzi wa Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti kwa Mwaka 2023/2024 kuhusu ukusanyaji wa Maduhuli

**Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2023/2024, Wizara ya Madini (Fungu 100) ilipangiwa kukusanya maduhuli yenye thamani ya Shilingi 1,006,705,169,300.00 kutoka vyanzo vyake mbalimbali. Kati ya kiasi hicho cha fedha, Shilingi 882,128,205,000.00 zilipangwa kukusanywa na kuwasilishwa Hazina na Shilingi 124,576,964,300.00 zilipangwa kukusanywa na kutumiwa na taasisi zilizo chini ya Wizara.

Hadi kufikia mwezi Februari, 2024 fedha zilizokusanywa na kuwasilishwa Hazina ni Shilingi 476,218,824,906.45, sawa na asilimia 54. ambayo ni chini ya wastani kama inavyoonekana kwenye Kielelezo Na. 1.

**Kielelezo Na.1: Ukusanyaji wa Maduhuli kufikia Februari, 2024**

| UKUSANYAJI WA MADUHULI KUFIKIA FEBRUARI, 2024 | | | |
|---|---|---|---|
| **CHANZO** | **MAKADIRIO** | **MAKUSANYO** | **ASILIMIA** |
| **Mapato mengineyo** | 2,000,000.00 | 0.00 | |
| **Marejesho ya fedha za Serikali** | 5,000,000.00 | 1,726,123.20 | **34.52** |
| **Ada ya Mwaka ya Leseni** | 40,000,000,000.00 | 33,095,227,192.19 | **82.74** |
| **Ada ya Ukaguzi** | 120,000,000,000.00 | 68,632,583,821.18 | **57.19** |
| **Ada za kijiolojia** | 18,950,000,000.00 | 8,631,387,743.31 | **45.58** |
| **Mrabaha** | 697,852,805,000.00 | 373,931,589,919.41 | **53.58** |
| **Adhabu na Faini za Malimbikizo ya Ada** | 4,618,400,000.00 | 1,635,160,659.71 | **35.41** |
| **Malipo ya huduma za Maabara** | 700,000,000.00 | 296,861,000.00 | **42.41** |
| **JUMLA** | **882,128,205,000.00** | **486,302,310,369.54** | **55.13** |

**Chanzo: Taarifa ya utekelezaji ya Wizara na usanifu wa KamatI**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilihoji sababu ya makusanyo kuwa madogo kiasi cha kusababisha Wizara ishindwe kufikia wastani wa makusanyo wa angalau asilimia 66.6 hadi mwezi Februari, 2024. Sababu kadhaa zilitolewa ikiwa ni pamoja na:-

a) Kushushwa kwa asilimia ya tozo za mrabaha kwa madini ya viwandani na nishati yanayouzwa nchini kutoka **asilimia 3 hadi asilimia 1;** na

b) Kusimama kwa uzalishaji katika baadhi ya migodi kutokana na sababu kadhaa ikiwa ni pamoja na uwepo wa maji mengi chini ya ardhi; changamoto ya umeme (Mgodi wa Sunshine)

migogoro ya umiliki wa ardhi (Edenville) na kuchelewa kuanza kwa uzalishaji wa miradi mipya.

**Mheshimiwa Spika**, **kwa upande wa makusanyo ya** Shilingi 124,576,964,300.00 **ambayo yalipangwa kukusanywa na kutumiwa na taasisi, hadi mwezi Februari, 2024 ni kiasi cha** Shilingi 34,886,713,089.31 **ndiyo kilikuwa kimekusasanywa. Makusanyo hayo ni sawa na** asilimia 28.12 **ya lengo kama inavyoonekana katika** Kielelezo Na.2.

**Kielelezo Na. 2: Ukusanyaji wa Maduhuli kufikia Februari, 2024**

| UKUSANYAJI WA MADUHULI YA TAASISI KUFIKIA FEBRUARI, 2024 | | | |
|---|---|---|---|
| **CHANZO** | **MAKADIRIO** | **MAKUSANYO** | **ASILIMIA** |
| **STAMICO** | 122,091,964,300.00 | 33,094,131,660.31 | **27** |
| **GST** | 2,235,000,000.00 | 1,659,411,324.00 | **74** |
| **TGC** | 250,000,000.00 | 133,170,105.00 | **53** |
| **Jumla** | 124,576,964,300.00 | 34,886,713,089.31 | **28** |

**Chanzo: Taarifa ya utekelezaji ya Wizara na usanifu wa KamatI**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilihoji sababu za makusanyo hayo ya Taasisi kutofikia lengo la angalau wastani wa asilimia 66 na ilielezwa kuwa ni kutokana na sababu zifuatazo:-

a) Lengo kubwa lililowekwa na Serikali baada ya hoja iliyoibuliwa na Mkaguzi Mkuu wa Serikali (CAG) kwamba, ni kwanini Wizara inafikia au kuvuka lengo la mapato;

b) STAMICO: Kuchelewa kukamilika kwa zoezi la kusimika mitambo miwili (2) ya kuzalisha mkaa mbadala wa makaa ya mawe ya kupikia (*coal briquettes*) iliyonunuliwa kutoka nchini China*; na*

c) TGC: Malipo ya ada za mafunzo na michango mingine hufanyika katika kipindi cha kuanzia Machi, 2024.

**Mheshimiwa Spika**, ni rai ya Kamati kwamba, Wizara ihakikishe lengo la makusanyo linafikiwa ifikapo tarehe 30 Juni, 2024 ili kutoathiri utekelezaji wa malengo yaliyowekwa na taasisi.

### 2.4 Uchambuzi kuhusu upatikanaji wa fedha hadi kufikia mwezi Februari, 2024

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imefanya uchambuzi wa Bajeti ya Wizara ya Madini **(Fungu 100)** ambayo katika mwaka wa fedha 2023/2024 iliidhinishiwa na Bunge lako Tukufu jumla ya **Shilingi 163,008,241,000.00**. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 45,877,443,000** sawa na **asilimia 28.14** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo (OC), **Shilingi 20,307,498,000.00** sawa na **asilimia 12.46** ni kwa ajili ya mishahara (PE), na **Shilingi 96,823,300,000.00** sawa na **asilimia 59.43** ni kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

**Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia Februari, 2024, Wizara ilikuwa imepokea jumla ya **Shilingi 125, 239,559,434.83** sawa na **asilimia 76.83** ya bajeti yote iliyoidhinishwa[4]. Uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa, kati ya fedha hizo zilizopokelewa, matumizi mengineyo ni **Shilingi 34,875,870,465.51** sawa na **asilimia 76.02**, mishahara ni **Shilingi 14,456,295,206.17** sawa na **asilimia 71.19** na miradi ya maendeleo **ni Shilingi 75,907,393,763.15** sawa na **asilimia 78.48** ya bajeti iliyoidhinishwa kama inavyoonekana kwenye **Kielelezo Na.3**

**Kielelezo Na. 3: Upatinakaji wa Fedha kufikia Februari, 2024**

| Eneo la Bajeti | Kiasi kilichoidhinishwa | Kiasi kilichopokelewa | Asilimia |
|---|---|---|---|
| Mishahara | 20,307,498,000 | 14,456,295,206.17 | 71.19 |
| Matumizi Mengineyo | 45,877,443,000 | 34,875,870,465.51 | 76.02 |
| Maendeleo | 96,823,300,000 | 75,907,393,763.15 | 78.48 |
| **Jumla** | **163,008,241,000** | **125,239,559,434.83** | **76.83** |

***Chanzo: Taarifa ya utekelezaji ya Wizara na Usanifu wa Kamati***

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imebaini kuwa kwa ujumla fedha zilipatikana kwa kiasi cha kuridhisha kwani ilikuwa ni juu ya wastani uliotarajiwa kwa wakati huo.

**Kamati inapongeza Wizara kwa hatua hiyo, na inatoa rai kwamba upatikanaji huo wa fedha uende sambamba na ufanisi katika**

[4] Taarifa ya utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Madini kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024: Fedha zilizopokelewa kufikia Februari, 2024 uk. 5&6

**utekelezaji wa vipaumbele vya wizara pamoja na miradi iliyokusudiwa kutekelezwa kwa manufaa ya maendeleo ya Sekta ya madini na uchumi wa Taifa kwa ujumla.**

## 2.5 Uchambuzi wa Utekelezaji wa Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati kwa mwaka wa fedha 2023/2024

**Mheshimiwa Spika**, taarifa ya Kamati kuhusu uchambuzi wa Bajeti ya Wizara hii kwa mwaka wa fedha 2023/2024, ilitoa jumla ya maoni 18 ili utekelezaji wake uchangie katika kuboresha utendaji kazi wa Wizara na Serikali kwa ujumla.

Kamati imepitia Taarifa ya utekelezaji wa Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati na kubaini kwa kiasi kikubwa Wizara imezingatia na kutekeleza Maoni, Ushauri na Mapendekezo hayo ya Kamati.

Hata hivyo, baadhi ya maoni utekelezaji wake ni endelevu na mengine bado hayajatekelezwa kikamilifu, hivyo Kamati inasisitiza Wizara kufanyia kazi ushauri uliotolewa na Kamati. Mfano wa maoni ambayo utekelezaji wake ni endelevu ni suala la wananchi wanaopisha miradi ya uchimbaji wa madini kupewa fidia kwa wakati zinazoendana na thamani halisi ya eneo, na ikiwezekana wapewe hisa huru (free carried interest) kama sehemu ya fidia ya maeneo yao wanayopisha. Kamati imebaini kuwa bado baadhi ya wananchi waliopisha miradi bado wanadai fidia na utaratibu bado unaendelea na kutokuanza kuwa kulipwa fidia kwa utaratibu wa kupewa hisa huru. **Ni rai ya Kamati kwamba, Serikali ifanyie kazi ushauri huu ili wananchi wanaopisha maeneo yao kwa ajili ya uendelezaji wa shughuli za madini wapewe hisa huru kama sehemu ya fidia ya maeno wanayoyatoa na hivyo kuendelea kunufaika na raslimali ya madini**.

**Mheshimiwa Spika,** miongoni mwa maoni ambayo utekelezaji wake haujafanyika ni suala linalohusu Serikali kuhakikisha STAMICO inashirikiana na TANESCO ili kutumia makaa ya mawe kuzalisha umeme ikiwa ni pamoja na umeme wa **MW 200** katika mgodi wa Kiwira, Mbeya. Kamati ilielezwa kwamba, STAMICO imeingia makubaliano ya awali na TANESCO kuhusu uchimbaji wa makaa ya mawe na uzalishaji wa umeme huo. Aidha, wataalamu

wa pande zote wameandaa TOR kwa aili ya mtaalam mshauri kuhuisha upembuzi yakinifu uliofanyika mwaka 2006 ili kujua gharama halisi za mtradi huo.

Uchambuzi wa Kamati umebaini kuna taarifa zinazokinzana kuhusu suala hili kwani mwezi Agosti, 2023 ilitolewa taarifa ilieleza kwamba, anatafutwa mwekezaji, lakini taarifa ya utekelezaji maoni iliyowasilishwa mwezi Februari, inaonesha kuwa zimeandaliwa hadidu za rejea ili kuhuisha upembuzi yakinifu wa mwaka 2006 kwa lengo la kujua gharama halisi za mradi.

Ni rai ya Kamati kwamba, iwapo kuna nia thabiti ya kutekeleza mradi huu basi Serikali ihakikishe inakuwa na usimamizi madhubuti kwa STAMICO na TANESCO ili kuhakikisha utekelezaji wa mradi huu unaanza mara moja, ili kuwezesha nchi kunufaika na raslimali hii na kuongeza uzalishaji wa umeme nchini.

## SEHEMU YA TATU

### 3.0 UCHAMBUZI WA MPANGO NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA WIZARA YA MADINI (FUNGU 100) KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025

**Mheshimiwa Spika**, ili kuzingatia matakwa ya Kanuni ya 117 (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari 2023, Kamati ilifanya uchambuzi wa makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Madini **(Fungu 100)** kwa mwaka wa fedha 2024/2025, na kufanya ulinganisho kuhusu makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara kwa mwaka wa fedha uliopita (2023/2024)[5]. Uchambuzi ulijielekeza katika maeneo yafuatayo: -

a) Malengo ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2024/2025;

b) Makadirio ya makusanyo ya maduhuli kwa mwaka wa fedha 2024/2025;

c) Makadirio ya matumizi mwaka wa fedha 2024/2025; na

[5] Baada ya kutembelea miradi, Kamati za Bunge za Kisekta, kwa kipindi kisichozidi isku tisa, zitafanya vikao vya kuchambua taarifa za utekelezaji wa bajeti za Wizara inazozisimamia kwa mwaka wa fedha unaoisha na kufanya ulinganisho kuhusu makadirio ya matumizi ya Serikali kwa mwaka wa fedha unaofuata.

d) Ulinganisho wa bajeti ya Wizara dhidi ya bajeti ya Taifa

### 3.1 Malengo ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi wa Kamati kuhusu bajeti ya Wizara ya Madini kwa mwaka wa fedha 2024/2025 umebaini kuwa, Wizara imezingatia miongozo mbalimbali kama vile Dira ya Taifa ya Maendeleo ya Mwaka 2025; Mpango wa Taifa wa Tatu wa Maendeleo wa Miaka Mitano 2021/22 - 2025/26, Ilani ya Uchaguzi Mkuu ya CCM ya Mwaka 2020 - 2025[6] na Sera ya Madini ya Mwaka 2009.

Ili kuhakikisha mipango hiyo inatekelezwa kikamilifu, Kamati imepitia vipaumbele vya Wizara na kubaini kuwa vipaumbele katika mwaka wa fedha 2024/2025 vitaendelea kuwa Sita (6) kama ilivyokuwa katika mwaka wa fedha 2023/2024 ingawa kuna utofauti wa maudhui ya vipaumbele katika mwaka ujao wa fedha ikilinganishwa na mwaka wa bajeti unaoisha.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilipohoji kuhusu mabadiliko hayo ilielezwa kwamba kutokana na umuhimu wake, kipaumbele Na. 4 kilichohusu "*kuhamasisha shughuli za uongezaji thamani madini*" kimeunganishwa na Kipaumbele Na. 5 kilichohusu "*kuhamasisha uwekezaji na biashara katika sekta ya madini na uanzishwaji wa minada na maonesho ya madini ya vito*" na kuwa kipaumbele kimoja katika mwaka ujao wa fedha.

Aidha, uchambuzi wa Kamati ulibaini kipaumbele kipya ambacho kimeongezwa katika mwaka ujao wa fedha, 2024/2025 ambacho kinahusu "*kuendelea kufanya utafiti wa kina wa jiofizikia kwa njia ya kurusha ndege (high- resolution airborne geophysical survey)*".

**Mheshimiwa Spika**, matumizi ya teknolojia ya kisasa ya ndege nyuki katika kukusanya taarifa zaidi na kuzingatia matokeo ya tafiti za awali, yatasaidia kuanisha uwepo na upatikanaji wa madini mbalimbali yakiwemo madini ya kimkakati, na kujenga mfumo wa kutunza na kusambaza taarifa za jiosayansi.

---
[6] Ilani ya Chama cha Mpainduzi kwa ajili ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020 (Uk. 108 -110).

Kamati inaipongeza Wizara kwa hatua hii muhimu ambayo itachangia kunusuru upotevu wa mitaji ya wawekezaji katika sekta ya madini, kwani watawekeza katika maeneo yenye uhakika wa madini, tofauti na ilivyo sasa ambapo wawekezaji hutumia fedha nyingi kufanya utafiti kabla ya kuanza uchimbaji na wakati mwingine kufanya uchimbaji katika maeneo ambayo hayana tafiti rasmi kuhusu uwepo wa madini katika maeneo husika**. Aidha, ni rai ya Kamati kuwa, utekelezaji wa kipaumbele hiki uendane sambamba na upatikanaji wa taarifa sahihi kuhusu maeneo na wingi wa madini ili kuvutia mitaji ya wawekezaji katika sekta ya madini.**

### 3.2 Makadirio ya Makusanyo ya Maduhuli mwaka wa fedha 2024/2025

**Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2024/2025, Wizara ya Madini **(Fungu 100)** inakadiria kukusanya jumla ya **Shilingi 1,052,480,027,000.00.** Kati ya fedha hizo, **Shilingi 887,630,000,000.00** sawa na **asilimia 84.34** zitakusanywa kupitia idara, vitengo vya Wizara na tume ya madini na zitawasilishwa Hazina**.** Aidha**, Shilingi 164,850,027,300.00** sawa na **asilimia 15.66** zitakusanywa na kutumiwa na taasisi zilizo chini ya Wizara kama inavyoonekana kwenye **Kielelezo Na. 4.**

**Kielelezo Na. 4: Makadirio ya Makusanyo ya Maduhuli kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025**

| | | |
|---|---|---|
| **Maduhuli yatakayokusanywa na kuwasilishwa Hazina** | | |
| **CHANZO** | **2024/2025** | **ASILIMIA** |
| **Wizara** | 3,001,000.00 | **0** |
| **Tume ya Madini** | 887,626,999,000.00 | **84.34** |
| **Jumla Ndogo** | **887,630,000,000.00** | **84.34** |
| **Maduhuli yatakayokusanywa na kutumiwa na Taasisi** | | |
| **CHANZO** | **2024/2025** | **ASILIMIA** |
| **STAMICO** | 161,509,027,000.00 | **15.35** |
| **GST** | 3,131,000,000.00 | **0.29** |
| **TGC** | 210,000,000.00 | **0.02** |
| **Jumla Ndogo** | **164,850,027,000.00** | **15.66** |
| **JUMLA KUU** | **1,052,480,027,000.00** | **100** |

**Chanzo: Randama ya Wizara na usanifu wa Kamati**

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa, makadirio hayo yameongezeka kutoka **Shilingi 1,006,705,169,300.00** mwaka 2023/2024 hadi kufikia **Shilingi 1,052,480,027,000.00** mwaka 2024/2025. Kiasi kilichoongezeka ni **shilingi 45,774,857,700.00** ambacho ni sawa na **asilimia 4.55**. ufafanuzi zaidi ni kama unavyoonekana kwenye **Kielelezo na. 5.**

Ongezeko zaidi linaonekana katika Taasisi ya Jiolojia na Utafiti wa Madini Tanzania (GST) kwa **asilimia 40.09** kutoka **Shilingi 2,235,000,000.00** hadi kufikia **Shilingi 3,131,000,000.00.** Kwa upande mwingine, makadirio ya maduhili yanayokusudiwa kukusanywa na Kituo cha Jimolojia Tanzania (TGC) yamepungua kwa **asilimia 16** kutoka **Shilingi 250,000000.00** hadi **Shilingi 210,000,000.00**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilihoji sababu ya ongezeko hilo la makadirio ya makusanyo kwa ujumla hasa ikizingatiwa kuwa kufikia Februari, 2024, wastani wa lengo la makusanyo kwa Makadirio ya Mwaka 2023/2024 lilikuwa halijafikiwa. Wizara ilieleza miongoni mwa sababu zilizofanya ongezeko la makadirio ya makusanyo ni pamoja na:-

a) Kuendelea na uzalishaji kwa mgodi wa Williamson Diamond Limited (WDL) na Mgodi wa Dhahabu Buhemba,
b) Kuongeza usimamizi wa madini ujenzi na Viwandani kwa kutumia mawakala na TAMISEMI;
c) **STAMICO**: Kufanya huduma ya uchorongaji na ushauri wa kijiolojia, uchimbaji na uchenjuaji, mradi wa wachimbaji wadogo, vituo vya mfano vya wachimbaji wadogo (Lwamgasa, katente na Itumbi), mradi wa *Coal Briquette na* mradi wa kusafisha dhahabu (gold refinery);
d) **GST:** Ada ya ushauri elekezi, tozo za huduma za maabara na tozo za ramani na machapisho ya jiosayansi.
e) **TGC:** Ada za wanafunzi Ngazi ya Cheti katika mafunzo ya ukataji na usanifu wa vito; na mauzo ya bidhaa na huduma.

**Kielelezo Na. 5: Ulinganisho wa Maduhulikati ya Mwaka wa Fedha 2023/2024 na 2024/2025**


| Maduhuli ya kuwasilishwa Hazina | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **CHANZO** | **2023/2024** | **2024/2025** | **ONGEZEKO (+)/ PUNGUZO (-)** | **ASILIMIA** |
| **WIZARA/TUME YA MADINI** | 882,128,205,000.00 | 887,630,000,000.00 | 5,501,795,000.00 | 0.62 |
| **Maduhuli ya kutumiwa na Taasisi** | | | | |
| **CHANZO** | **2023/2024** | **2024/2025** | **ONGEZEKO** | **ASILIMIA** |
| **STAMICO** | 122,091,964,300.00 | 161,509,027,000.00 | 39,417,062,700.00 | 32.28 |
| **GST** | 2,235,000,000.00 | 3,131,000,000.00 | 896,000,000.00 | 40.09 |
| **TGC** | 250,000,000.00 | 210,000,000.00 | **-40,000,000.00** | 16 |
| **Jumla Ndogo** | **124,576,964,300.00** | **164,850,027,000.00** | **40,273,062,700.00** | **32.33** |
| **JUMLA KUU** | **1,006,705,169,300/=** | **1,052,480,027,000.00** | **45,774,857,700.00** | **4.55** |

***Chanzo: Randama ya Wizara na usanifu wa Kamati***

### 3.3 Makadirio ya Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025

**Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2024/2025, Wizara ya Madini **(Fungu 100)** inakadiria kutumia jumla ya **Shilingi 231,983,614,000.00.** Kati ya fedha hizo **Shilingi 140,661,200,000.00** sawa na **asilimia 60.64** ni kwa ajili ya maendeleo na **Shilingi 91,322,414,000.00** sawa na **asilimia 39.37** ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Fedha za matumizi ya kawaida zinajumuisha **Shilingi 24,872,875,000.00 (asilimia 10.72)** kwa ajili ya mishahara na **Shilingi 66,449,539,000.00 (asilimia 28.64)** kwa ajili ya matumizi mengineyo (OC) kwa Wizara na Taasisi zake kama inavyoonekana kwenye **Kielelezo Na. 6.**

**Kielelezo Na. 6: Mchanganuo wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025**




**Chanzo: Randama ya Wizara na Usanifu wa Kamati**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imefanya uchambuzi kwa kulinganisha bajeti ya Wizara kati ya mwaka wa fedha 2023/2024 na 2024/2024 na imebaini kwamba, kwa ujumla bajeti imeongezeka kwa **asilimia 41.7** kutoka **Shilingi 163,008,241,000.00** mwaka 2023/2024 hadi kufikia **Shilingi 231,983,614,000.00** mwaka 2024/2025. Ongezeko hilo la bajeti limegusa maeneo yote ya Wizara kwa maana ya mishahara, matumizi mengineyo na maendeleo. Kielelezo Na. 7 kinafafanya zaidi.

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa ongezeko kuzwa zaidi liko katika fedha za miradi ya maendeleo ambazo zimeongezeka kutoka **Shilingi 96,823,300,000.00** mwaka 2023/2024 hadi kufikia **Shilingi 140,661,200,000.00** mwaka 2024/2025 sawa na ongezeko la **asilimia 45.28. Ni matumaini ya Kamati kwamba, ongezeko hilo litawezesha utekelezaji mzuri wa Mradi wa Usimamizi endelevu wa Rasilimali za Madini (SMMRP) ambao utatumia asilimia 95.7 ya fedha zote za maendeleo.**

Kupitia mradi huu Wizara imepanga kununua mitambo miwili (2) ya uzalishaji wa makaa ya mawe ya kupikia (*coal briqquette*) na ununuzi wa mtambo wa kuchakata madini ya chokaa (STAMICO); uimarishaji wa kanzidata ya miamba, utafiti wa kina wa kijiofizikia kwa kutumia ndege (high resolution airborne geophysical survey),

uimarishaji wa vituo vya kuratibu majanga ya asili, ununuzi wa helcopter jet ranger kwa ajili ya utafiti wa madini wa kina, ujenzi na ununuzi wa vifaa vya maabara ya jiosayansi (*geoscientific equipment and tools*) na kusogeza huduma za ugani kwa wadau (GST); kukamilisha ujenzi na ununuzi wa samani wa jengo la ofisi ya Makao Makuu ya Tume ya madini pamoja na ofisi tatu (3) za Afisa madini Mkazi (Tume ya Madini).

Aidha, fedha nyingine za maendeleo zimeelekezwa katika Mradi wa Kituo cha Jemolojia Tanzania (Tanzania Gemological Center-) ambao utatumia **asilimia 4.98** ya Bajeti yote ya Maendeleo. **Ni ushauri wa Kamati kwamba, miradi hii itekelezwa kikamlifu na kusimwamiwa vizuri ili kuleta tija na hivyo kuchangia ukuaji zaidi wa Sekta ya Madini na kuiwezesha kuchangia katika katika Pato la Taifa.**

**Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa mishahara, Kamati imebaini kuwa kuna ongezeko la **asilimia 22.48** kutoka **Shilingi 20,307,498,000.00** mwaka 2023/2024 hadi kufikia **Shilingi 24,872,875,000.00** sawa na **asilimia 22.48** mwaka 2024/2025. Vilevile, fedha za matumizi mengiyo zimeongezeka kwa **asilimia 44.84** kutoka **Shilingi 45,877,443,000.00** mwaka 2023/2024 hadi kufikia **shilingi 66,449,539,000.00** mwaka 2024/2025.

**Kamati inapongeza hatua hiyo ya Serikali kuongeza bajeti ya Wizara hii kwani itakuwa ni chachu ya kuboresha utendaji na kuifanya sekta ya madini iendelee kufanya vizuri na kuongeza mchango wake katika pato la taifa. Aidha, Wizara itumie nyongeza hiyo ya bajeti kuongeza ufanisi wa kiutendaji kwa watendaji wake.**

**Kielelezo Na. 7: Ulinganisho wa Bajeti ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 na 2024/2025**

| CHANZO | 2023/2024 | 2024/2025 | ONGEZEKO/ UPUNGUFU | ASILIMIA |
|---|---|---|---|---|
| Dev | 96,823,300,000 | 140,661,200,000 | 43,837,900,000 | 45 |
| OC | 45,877,443,000 | 66,449,539,000 | 20,572,096,000 | 44.84 |
| PE | 20,307,498,000 | 24,872,875,000 | 4,565,377,000 | 22.48 |
| Jumla Ndogo | **66,184,941,000** | **91,322,414,000** | 25,037,473,000 | 37.77 |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **JUMLA KUU** | **163,008,241,000** | **231,983,614,000** | **68,975,373,000** | **41.7** |

**Chanzo: Randama ya Wizara na Usanifu wa Kamati**

### 3.4 Uchambuzi wa Bajeti ya Wizara dhidi ya Bajeti ya Taifa

**Mheshimiwa Spika, s**ekta ya madini ni miongoni mwa sekta zinazochangia kwa kiasi kikubwa katika pato la Taifa kama ambavyo imeonekana kufikia 2023 mchango ni **asilimia 10.5**.

Kamati imefanya uchambuzi kwa kulinganisha asilimia ya Bajeti ya Wizara hii (Fungu 100) dhidi ya Bajeti ya Taifa kati ya mwaka 2023/2024 na 2024/2025 na kubaini kuwa Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2024/2025 imeongezeka kwa **asilimia 11.0** ikilinganishwa na mwaka 2023/2024, na kuifanya asilimia ya bajeti ya Wizara ya Madini (Fungu 100) dhidi ya bajeti ya Taifa kuongezeka kutoka **asilimia 0.37** mwaka 2023/2024 hadi **asilimia 0.47** mwaka 2024/2025 kama inavyoonekana kwenye Kielelezo Na. 8.

Aidha, Kamati imebaini kuwa OC imepungua kutoka **asilimia 0.82** hadi kufikia **asilimia 0.19**, Mishahara imeongezeka kutoka asilimia **0.19 hadi asilimia 1.16**. Ni raia ya **Kamati kwamba, kutokana na umuhimu wa sekta ya madini, Serikali iendelee kuoingezea Bajeti Wizara hii ili iendelee kuchangia kwenye Pato la Taifa.**

**Kielelezo Na. 8: Ulinganisho wa Bajeti ya Wizara dhidi ya Bajeti Kuu ya Taifa 2023/2024 na 2024/2025**

| **BAJETI YA WIZARA DHIDI YA BAJETI YA TAIFA 2023/2024** | | | |
|---|---|---|---|
| **AINA** | **BAJETI TAIFA** | **BAJETI MADINI** | **ASILIMIA** |
| **OC** | 5,578,433,000,000 | 45,877,443,000.00 | 0.82 |
| **MISHAHARA** | 10,882,126,000,000 | 20,307,498,000 | 0.19 |
| **MAENDELEO NDANI** | 11,873,900,000,000 | 22,000,000,000 | 0.19 |
| **MAENDELEO NJE** | 3,282,100,000,000 | 1,172,550,000 | 0.04 |
| **DENI LA SERIKALI** | 12,771,500,000,000 | 0 | - |
| **JUMLA** | **44,388,059,000,000.00** | **163,008,241,000.00** | **0.37** |
| | | | |
| **BAJETI YA WIZARA DHIDI YA BAJETI YA TAIFA 2024/2025** | | | |

| AINA | BAJETI TAIFA | BAJETI MADINI | ASILIMIA |
|---|---|---|---|
| OC | 33,556,600,000,000 | 66,449,539,000.00 | 0.19 |
| MISHAHARA | 11,997,800,000,000 | 24,872,875,000 | 0.21 |
| MAENDELEO NDANI | 12,148,300,000,000 | 140,661,200,000 | 1.16 |
| MAENDELEO NJE | 3,640,800,000,000 | 0 | - |
| DENI LA SERIKALI | 15,746,700,000,000 | 0 | - |
| **JUMLA** | **49,345,700,000,000.00** | **231,983,614,000.00** | **0.47** |

***Chanzo: Taarifa ya Mapendekezo ya Ukomo wa Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2024/2025, Randama ya Wizara ya Madini kwa mwaka 2024/2025 na Usanifu wa Kamati***

## SEHEMU YA NNE

## 4.0 MAONI, USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI

**Mheshimiwa Spika**, baada ya uchambuzi, ufafanuzi wa yaliyobainika katika ukaguzi wa miradi iliyotengewa fedha pamoja na uchambuzi wa Bajeti, Kamati inatoa maoni, ushauri na mapendekezo yafuatayo:-

### 4.1 MAONI YA JUMLA

#### (a) Kusuasua kwa utekelezaji kwa miradi iliyotengewa fedha

Utekelezaji wa miradi iliyotengewa fedha katika mwaka wa fedha 2023/2024 umekuwa wa kusuasua kutokana na sababu mbalimbali ikiwemo mabadiliko ya usanifu na mabadiliko ya wakandarasi katika Mradi wa Jengo la TGC-Arusha na Ujenzi wa Jengo la Ofisi ya Tume ya Madini-Dodoma mtawalia. Mabadiliko hayo yamesababisha kuongezeka kwa gharama na kuchelewesha kukamilika kwa miradi katika muda uliopangwa. Ni vyema usanifu na tathmini ya kina vikafanyika kwa kiwango cha kuridhisha kabla ya kuanza utekelezaji wa miradi hii ili kuepusha ongezeko la gharama na kuwezesha miradi kukamilika kwa wakati uliopangwa.

**(b) Tozo katika Halmashauri**

Baadhi ya Halmashauri nchini zimetunga sheria ndogo (by laws) za ukusanyaji wa tozo zinazokinzana na sheria mama, na hivyo kusababisha usumbufu na kuongeza gharama kwa wachimbaji wa madini hasa madini ujenzi na madini ya viwandani. Ni vyema Serikali ikatatua changamoto hii kwa wakati kwa kuweka utaratibu utakao ondoa mgongano uliopo na kuwezesha wawekezaji kuendesha kazi zao bila usumbufu.

**(c) Uhaba wa Watumishi**

Uhaba wa Watumishi hasa wa kada muhimu (core carders) kama vile ukaguzi na udhibiti wa madini unaozikabili Taasisi za STAMICO, TGC na GST unaathiri utendaji wa taasisi hizo. Kwa kuwa Wizara imepata vibali vya ajira mpya na ajira ya uhamisho, ipunguze haraka uhaba uliopo kwa uhamisho wa watumishi kutoka taasisi nyingine za Umma, huku mchakato wa ajira mpya ukiendelea kwa mujibu wa taratibu zilizopo. Aidha, nafasi chache za ajira ambazo zimepatikana zielekezwe kwenye kada muhimu ili kuwezesha taasisi hizo kujiendesha kwa ufanisi na hivyo kuchangia katika ukuaji wa sekta ya madini nchini.

**(d) Taratibu za ununuzi wa Umma kuchukua muda mrefu**

Utendaji wa taasisi chini ya Wizara ya Madini unaathiriwa na taratibu za ununuzi kuchukua muda mrefu, na pia mabadiliko ya mifumo ya ununuzi (kutoka TANePS kwenda mfumo mpya wa NeST). Kamati inaunga mkono matumizi ya mifumo, hata hivyo ni vyema Serikali ikahakikisha mifumo na taratibu za manunuzi zinaboresha na kurahisisha utendaji wa baadhi ya taasisi kulingana na upekee wake badala ya kuleta vikwazo.

## 4.2 MAONI MAHSUSI

### 4.2.1 SHIRIKA LA MADINI LA TAIFA (STAMICO)

(a) Kamati inapongeza hatua ya STAMICO kuondoa sharti la dhamana ya Shilingi Milioni 50 kwa mawakala wa mkaa wa *coal briquette*. Hatua

hiyo imewezesha mawakala 66 kuingia katika biashara ya nishati hiyo, na itavutia mawakala zaidi, na hivyo kuwezesha mkaa kuwafikia wananchi kwa urahisi na gharama nafuu. Ili kuendelea kupata manufaa katika matumizi ya mkaa huo, mawakala waruhusiwe kununua mkaa kwa thamani halisi ya mzigo na kuusambaza katika maeneo mengi.

(b) Kwa kuwa taasisi mbalimbali zimehamasika na kuanza kutumia mkaa wa *coal briquette* (hadi sasa kuna taasisi 10 ikiwemo shule ya Sekondari ya Baobab). Serikali iendelee kuhamasisha taasisi za umma na za binafsi zianze kutumia nishati hii.

(c) Taasisi zinazohusika na Mazingira, Madini na TAMISEMI ziungane na kuweka mkakati wa kuhamasisha matumizi ya mkaa wa *coal briquette* ili kufikia manufaa ya kiwango cha juu katika kunusuru uharibifu wa mazingira.

(d) Kamati inapongeza hatua ya STAMICO kuendelea kulipa madeni ambayo STAMIGOLD inadaiwa na wazabuni ambapo deni lililobaki ni Shilingi Bilioni 18.5. Aidha, juhudi za kulipa deni hilo ziendelee, na ikiwezekana Serikali isaidie kwa kulichukua ili wazabuni wasiendelee kuathirika.

(e) STAMICO ihakikishe mitambo mitano (5) ya uchorongaji iliyowasili nchini mwishoni mwa mwaka 2023 na kuanza kazi kwenye baadhi ya maeneo ikiwa ni pamoja na yenye leseni za wachimbaji wadogo Nyamongo (Tarime), mkoani Mara inalenga kuwasaidia na kuwanufaisha wachimbaji wadogo na si vinginevyo. Aidha, Wizara ihakikishe gharama wanayotozwa wachimbaji wadogo ni nafuu na inaenda sambamba na utoaji wa elimu ili kuwajengea ujuzi wa kutumia vifaa vya kisasa. Vilevile, Serikali iendelee kuongeza mitambo na kuitawanya kwa

usawa katika maeneo mengine ya wachimbaji wadogo nchini.

(f) Mchakato wa kuzalisha MW 200 katika mgodi wa Makaa ya Mawe Kiwira ni wa muda mrefu na utekelezaji wake umekwama. Kwa kuwa, amepatikana muwekezaji (Adan Group Company) mwenye nia ya kuwekeza katika mradi huo na kuzalisha takribani MW 2000, Serikali isimamie mchakato huo kikamilifu na kuweka mazingira mazuri yatakayomuwezesha muwekezaji huyo kutekeleza azima yake.

(g) STAMICO iendelee kutoa elimu kwa wachimbaji wadogo kwa kuongeza nakala za mwongozo kuhusu usimamizi wa mazingira, sheria za madini na kanuni hasa kwa kuzingatia kwamba, wananchi wanaoingia katika sekta ya madini wanaongezeka kila mara kutokana na kugunduliwa na kuanzishwa kwa maeneo mapya ya uchimbaji..

### 4.2.2 TUME YA MADINI

Kutokana na umuhimu wa Tume ya Madini katika kuhakikisha mchango wa Sekta ya Madini kwenye Pato la Taifa unaongezeka:-

(a) Ujenzi wa jengo la Ofisi ya Makao Makuu ya Tume ya Madini usimamiwe na kukamilika kwa wakati ili kuwawezesha watumishi wa taasisi hiyo kutekeleza majukumu yao katika mazingira bora na hivyo kuifanya sekta ya madini iendelee kuchangia katika pato la taifa;

(b) Ulipaji wa fidia kwa wananchi wanaopisha maeneo yao ili kuruhusu uendelezaji wa madini ya aina mbalimbali kwa njia ya uwekezaji, unaendelea kuwaathiri wananchi kutokana na fidia kuwa ndogo na kuchelewa. Serikali isimamie kikamilifu suala hili ili kuboresha viwango vya fidia kuendana na thamani

halisi ya maeneo ambayo wananchi wanayaachia na kulipwa kwa wakati. Aidha, Serikali ihamasishe na kuwaelemisha wananchi ili waone umuhimu wa kupewa hisa huru (free carried interest) kama fidia ya maeneo waliyopisha ili wanufaike na rasilimali madini iliyopo katika maeneo yao kwa muda mrefu;

(c) Wananchi katika baadhi ya maeneo yenye leseni za uwekezaji wa madini, wamekuwa na migogoro na baadhi ya wawekezaji hao, jambo linalosababisha athari kwa wananchi hao na mali zao. Ili kupunguza au kuondoa changamoto hizo, wananchi waelimishwe kuhusu umuhimu na manufaa ya uwekezaji katika maeneo waliyoachia. Aidha, wawekezaji wajenge mahusiano mazuri na wananchi wanaozunguka maeneo yao ya uwekezaji ikiwa ni pamoja na kutekeleza kikamilifu wajibu wao kwa jamii (CSR) ili kuleta maelewano baina ya wananchi na wawekezaji;

(d) Kamati inapongeza hatua ya Serikali ya kuanza kufuta leseni za maeneo ambayo hayajaendelezwa kwa muda mrefu kinyume na matakwa ya sheria na kanuni (ambapo hadi Februari, 2024 zilifutwa leseni 2,648). Kwa kuwa, jambo hili lina manufaa makubwa kiuchumi, Kamati inashauri Serikali kuendelea kuchukua hatua zaidi za kufuta leseni na kugawa maeneo husika kwa wawekezaji wengine ambao wana nia ya kuwekeza ndani ya muda uliotolewa kwenye leseni; na

(e) Kampuni ya Diamond Williamson inayomiliki asilimia 75 za mgodi wa almasi uliopo Mwadui, Shinyanga kwa asilimia kubwa imekamilisha kuwalipa fidia wananchi walioathirika na kubomoka kwa bwawa la tope la mgodi huo ili waweze kupisha maeneo yaliyoathirika na kuwa mali ya Mgodi. Hata hivyo, Kamati ilipofanya ziara mwezi Februari, 2024 iligundua baadhi ya wananchi waliokwishalipwa fidia wapo na wanaendelea kuyatumia maeneo

yaliyotwaliwa. Kwa kuwa, Serikali ni miongoni mwa walipa fidia kwa kuwa ina umiliki wa asilimia 25 katika mgodi huo, ni vyema Serikali ikahamisha wananchi hao ili kuondoa uwezekano wa kuibuka migogoro ya umiliki wa maeneo hayo katika miaka ijayo.

### 4.2.3 WAKALA WA JIOLOJIA NCHINI (GST)

(a) Uimarishwaji wa kanzi data ya miamba upewe kipaumbele ili kuwezesha nchi kuwa na taarifa sahihi kuhusu miamba, jambo ambalo litaisaidia nchi kutambua mapema na kuepuka majanga mbalimbali ya asili ikiwa ni pamoja na maporomoko ya udongo;

(b) Serikali iendelee kuimarisha vituo vya kuratibu majanga ya asili ili viweze kusaidia nchi kwa kutoa taarifa na kushauri namna ya kukabili majenga ya asili yanapotokea;

(c) Tathmini ya athari za kimazingira ifanyike kwa mabwawa yote ya tope kutoka katika migodi iliyopo nchini ili kubaini athari zinazoweza kutokea iwapo yataharibika au kupasuka. Aidha, Wizara ihakikishe inakamilisha mapitio ya kanuni za usalama, afya na utunzaji wa mazingira;

(d) Ujenzi na upanuzi wa Ofisi za Kanda za GST upewe kipaumbele ili kusogeza huduma karibu zaidi na jamii na kuwafikia wadau wengi zaidi;

(e) Ili kuendelea kuimarisha usalama na kuongeza imani kwa wateja wanafuta huduma za kimaabara, GST iimarishe mifumo ya ulinzi na usalama kwa kufunga mfumo wa CCTV katika maabara na maeneo yanayozunguka kituo;

(f) Kwa kuwa Serikali imedhamiria kuwa na taarifa sahihi za kijiofizikia ikiwa ni pamoja na kuongeza kiwango cha utafiti kutoka asilimia 16 ya sasa, ni

vyema mchakato wa kuongeza kiwango cha utafiti huo ukafanyika mapema ili wananchi waanze kunufaika na matokeo ya utafiti huo; na

(g) GST iendelee kujitangaza ili huduma zake zifahamike zaidi kwa wateja na wadau, hasa baada ya kuboresha huduma zake kwa kununua mitambo na vifaa vya kisasa.

### 4.2.4 KITUO CHA JEMOLOJIA TANZANIA (TGC)

(a) Kamati inaipongeza Serikali kwa kutenga Shilingi 7,000,000,000.00 kwa ajili ya utekelezaji wa mradi wa majengo ya TGC ambao maandalizi yalianza muda mrefu lakini ujenzi haujaanza kutokana na mabadiliko kadhaa ikiwa ni pamoja na usanifu kwa lengo la kuboresha zaidi. Serikali ihakikishe utekelezaji wa mradi huu unaanza na kukamilika kwa wakati ili kukiwezesha kituo kutoa huduma za kisasa;

(b) Kwa kuwa jengo litakalojengwa litakuwa na shughuli na huduma zitakazovutia watu mashuhuli na wafanyabiashara wa madini ya vito kutembelea kituo hicho, Serikali ihakikishe inatatua changamoto ya eneo la maegesho ili kuondoa usumbufu unaoweza kuwakumba wageni watakaotembelea kituo hicho; na

(c) Kwa kuwa katika mradi wa jengo la TGC Serikali imekusudia kuwa na kituo bora, makumbusho ya madini ya vito na minada ya madini, ni vyema upanuzi wa miundombinu ukahusu pia kubomoa majengo ya zamani yaliyopo na ambayo hayapo kwenye mpango wa sasa, ili kuongeza ukubwa wa eneo na kufanya maeneo yote yawe ya kisasa.

**SEHEMU YA TANO**

## 5.0 HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika**, napenda kuchukua fursa hii kukushukuru sana Spika wetu, Mhe. DKt. Tulia Ackson (Mb), Naibu Spika Mhe. Mussa Azzan Zungu (Mb) na Wenyeviti wote wa Bunge kwa kuendelea kuliongoza vyema Bunge letu.

### 5.1 Shukrani

Kwa namna ya kipekee napenda kuwashukuru Wajumbe wote wa Kamati ya Nishati na Madini kwa ushirikiano wao wakati wa kutekeleza majukumu ya Kamati na kushiriki vizuri katika uchambuzi wa Bajeti ya Wizara hii. Kwa heshima kubwa naomba majina yao yatambuliwe na kuingizwa kwenye Kumbukumbu za Taarifa Rasmi za Bunge (*hansard*) kama ifuatavyo: -

1. Mhe. Dkt. David Mathayo David, Mb - **Mwenyekiti**
2. Mhe. Kilumbe Shabani Ng'enda, Mb - **M/ Mwenyekiti**
3. Mhe. Aleksia Asia Kamguna, Mb - Mjumbe
4. Mhe. Tabasamu Hamisi Mwagao, Mb - Mjumbe
5. Mhe. Philipo Augustino Mulugo, Mb - Mjumbe
6. Mhe. Constantine John Kanyasu, Mb - Mjumbe
7. Mhe. Ussi Salum Pondeza, Mb - Mjumbe
8. Mhe. Sophia Hezron Mwakagenda, Mb - Mjumbe
9. Mhe. Tumaini Bryceson Magessa, Mb - Mjumbe
10. Mhe. Angeline Sylvester Lubala Mabula, Mb- Mjumbe
11. Mhe. Iddi Kassim Iddi, Mb - Mjumbe
12. Mhe. Jesca David Kishoa, Mb - Mjumbe
13. Mhe. John Marko Sallu, Mb - Mjumbe
14. Mhe. Juliana Didas Masaburi, Mb - Mjumbe
15. Mhe. Maimuna Ahmad Pathan, Mb - Mjumbe
16. Mhe. Masache Njelu Kasaka, Mb - Mjumbe
17. Mhe. Ndaisaba George Ruhoro, Mb - Mjumbe
18. Mhe. Nicodemas Henry Maganga, Mb - Mjumbe
19. Mhe. Joseph Kasheku Musukuma, Mb - Mjumbe
20. Mhe. Saada Mansour Hussein, Mb - Mjumbe
21. Mhe. Eng. Samwel Hhayuma Xaday, Mb - Mjumbe
22. Mhe. Martha Festo Mariki, Mb - Mjumbe
23. Mhe. Janeth Elias Mahawanga, Mb - Mjumbe

**Mheshimiwa Spika,** napenda kumshukuru Waziri wa Madini Mhe. Anthony Peter Mavunde (Mb), Naibu Waziri Mhe. Dkt. Stephen Lemomo Kiruswa (Mb) pamoja na watendaji wote wa Wizara hiyo wakiongozwa na Katibu Mkuu, Ndg. Kheri Mahimbali akisaidiwa na Ndg. Msafiri Mbibo, kwa ushirikiano wao ambao umeisaidia Kamati kutekeleza kwa ufanisi majukumu yake ya kikatiba. Aidha, Kamati itaendelea kutoa ushirikiano wa kutosha kwao kwa njia ya usimamizi na ushauri ili kuwezesha kufikiwa kwa utekelezaji wa malengo ya Wizara na nchi kwa ujumla.

**Mheshimiwa Spika,** kwa namna ya pekee napenda kuwashukuru watumishi wote wa Ofisi ya Bunge chini ya uongozi thabiti wa Katibu wa Bunge, Ndg. Nenelwa Joyce Mwihambi (*ndc*) kwa ushirikiano wao ambao umewezesha uratibu mzuri wa shughuli zote za Kamati na hatimaye kukamilisha Taarifa hii kwa wakati.

5.2 **Hoja**

**Mheshimiwa Spika**, naomba sasa Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Madini (Fungu 100)  kwa mwaka wa fedha 2024/2025 kama yalivyowasilishwa na mtoa hoja .

**Mheshimiwa Spika**, naunga mkono na naomba kuwasilisha.

Dkt. David Mathayo David, Mb
**MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU**
**YA BUNGE YA NISHATI NA MADINI**
30 Aprili, 2024

**SPIKA:** Makamu Mwenyekiti, ahsante sana kwa wasilisho hilo la maoni ya Kamati kuhusu hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Madini, tunakushukuru sana.

Waheshimiwa Wabunge, kama ilivyo ada, baada ya Mheshimiwa Waziri kuwasilisha hoja yake na Kamati yetu kuwasilisha maoni ya Kamati kwetu, sasa tunaanza uchangiaji. Tutaanza na Mheshimiwa Profesa Sospeter Mwijarubi Muhongo, atafuatiwa na Mheshimiwa Joseph Kasheku Musukuma, Mheshimiwa Profesa Shukrani Elisha Manya ajiandae.

**MHE. PROF. SOSPETER M. MUHONGO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana. Kwanza nianze kwa kusema kwamba, naomba niwashawishi Waheshimiwa Wabunge wengine kwamba yote aliyoyasema Mheshimiwa Waziri na aliyoyasema Makamu Mwenyekiti wa Kamati, ni sahihi kabisa. Nimewasikiliza kwa makini kweli kweli, sasa tunachopaswa sisi kufanya ni kuboresha.

Mheshimiwa Spika, cha kwanza kabisa, bajeti waliyoomba na hayo waliyotueleza mazuri, bajeti ni ndogo sana. Wao wanakusanya zaidi ya shilingi trilioni moja, lakini wanaomba bajeti ya shilingi bilioni 260 na kitu, fedha kidogo sana. Sasa nitatoa mchango wangu ndipo mtaona kwa nini fedha hizo ni kidogo mno.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri na Kamati wamesisitiza suala la kanzi data *(data base)* na niwaeleze Wizara ya Madini kwamba roho ya nchi kwenye sekta ya madini ni *geological survey.* Hata haya yote tunayoyafanya ni *geological survey*, na wawekezaji wote ni *geological survey*.

Mheshimiwa Spika, sasa angalia ramani wanazopaswa kuzitengeneza. Kwanza wanakwenda *field,* wanatengeneza *geological map,* wakiona kwamba kuna dalili nzuri wanatengeneza *geophysical map,* hizo walizokuwa wanasema Jiofizikia, kisha wakwenda kutengeneza *geochemical map*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, cha kwanza hao wataalamu hatunao wengi. Ninavyofahamu mimi, ma-*geologist* ambao wapo *GST* sasa hivi hawavuki 40. Sasa, kwa sababu hii taasisi ya *GST* ni ya utafiti, naomba nirudie tena, ni utafiti, hivyo hauwezi kufanywa vizuri na kijana aliyemaliza tu shahada ya kwanza, haiwezekani, haijawahi kutokea duniani. *Geological surveys* nyingi duniani, na ninashukuru nimefanya nazo kazi, hizi lazima zinataka watu waliobobea.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kutengeneza hizi ramani hata hizi za majanga, sasa hivi majanga yanayotupata Mheshimiwa Waziri pamoja na Kamati wamesema vizuri, lakini wale wataalamu pale *geological survey* wa *geohazards* hawapo. Kwa

hiyo, cha kwanza tusomeshe sana, na *Geological Surveys* tuwaongezee fedha. Ramani wanazozitengeneza Mwingereza alituachia *scale* ya 1:125,000, mwaka huu wameanza kutengeneza 1:100,000; lakini hizo scale ya laki moja ni chache mno. Kama tunatafuta madini kwa wingi, lazima twende kwenye scale ya 1:50,000, ambapo haipo ramani hata moja; na ramani za zamani lazima wazipitie.

Mheshimiwa Spika, hata mimi ramani yangu ipo hapo, niliwapa mwaka 2004, naviziavizia sijaona kama vijana wameipitia. Kwa hiyo, mahitaji ya hii Wizara ni wataalamu wengi, maabara za uhakika na nzuri halafu na fedha nyingi.

Mheshimiwa Spika, hawa *GST* kwa nini mimi nawaombea fedha? Ni kwa sababu ni lazima nao wawe na fedha ili watoe *grant*. *Grant* ni nini? *Doctor,* sema kwa Kiswahili.

*(Hapa Mhe. Prof. Sospeter M. Muhongo alimwuliza Mheshimiwa Mbunge aliyekuwa ameketi pembeni yake)*

**MHE. PROF. SOSPETER M. MUHONGO:** Mheshimiwa Spika, ni *grants*, *research grants,* sijui ndiyo fedha za kufanya utafiti!

Mheshimiwa Spika, hizi kazi wanazozifanya hawawezi kuzimaliza wenyewe, ni lazima wafanye na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na Chuo Kikuu cha Dodoma, lakini mwanafunzi anayefanya *Masters* au *Ph.D* anakwenda kudhaminiwa na *Geological Survey* kufanya utafiti na kumlipia kila kitu. Duniani kote wanafanya hivyo.

Mheshimiwa Spika, Hii kanzi data tunayoisema ni kweli kabisa kama Mheshimiwa Waziri na Kamati walivyosema kwamba ni lazima iwepo, na ni wao ndio watoe makadirio ya rasilimali madini tuliyonayo nchini. Kwa mfano, sasa hivi ukichunguza, wanasema dhahabu tuna tani milioni 45. Ripoti hii ni ya siku nyingi sana, na hata hivyo haijapitiwa, na dhahabu ipo takribani kila mahali.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kazi hii ni kubwa, inataka fedha nyingi, wataalamu, na maabara nzuri sana. Halafu hii kanzi data inabidi *geological survey* yake iwe mbele ya kampuni

zinazotafuta madini. Yaani yenyewe inakuwa imeshatengeneza ramani na imeshachoronga.

Mheshimiwa Spika, hii mitambo ya kuchoronga ambayo wameipeleka *STAMICO* miaka ya 1950, 1960, 1970 hata madini hapa *geological survey* ilikuwepo. Hiyo *helicopter* wanayotaka kununua miaka ya 1950, 1960 ilikuwepo. Sasa kama enzi ya ukoloni ilikuwepo jamani, turudi tuiwezeshe *Geological Survey*.

Mheshimiwa Spika, mchango wangu wa pili, kwa sababu mnasema kidogo dola zimekosekana, nimechukua mifano michache ya rasilimali madini tuliyonayo ya kutuongozea hizo dola; na mara nyingi sipendi kurudia. Niliwahi kuongelea kuhusu madini ya kimkakati, siyaongelei leo, nataka nichukue mifano miwili tu; nachukua aina ya gesi ya *helium.*

Mheshimiwa Spika, hii gesi haipo kule Nishati, inasimamiwa na Wizara ya Madini. Sasa *helium* matumizi yake ni makubwa kweli kweli hapa duniani. Yaani *nuclear reactors*, *rockets* zote mnazoziona, mkienda hospitali unapimwa na *MRI* zote hizo ndani yake zina gesi ya *helium*, *liquid helium,* matumizi yake ni makubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mtu kama *NASA* ya Marekani kwa mwaka inatumia *cubic feet* milioni 75 *(seventy five million cubic feet);* inatumiwa tu na *NASA;* ni kwa sababu ya mambo yao ya *rockets*. Sasa hivi matumizi ya *helium* duniani kipimo chake ni bilioni, *cubic feet* bilioni sita. Mzalishaji mkubwa ni Marekani kwa asilimia 40...

*(Hapa kengele ya kwanza ililia)*

**MHE. PROF. SOSPETER M. MUHONGO:** Loh, inabidi niende kasi sasa lakini Mheshimiwa Musukuma anipatie na za kwake. Kwa hiyo, ni kwamba Marekani imebaki na *8.5 billion cubic feet*. Sasa Tanzania tunayo.

Mheshimiwa Spika, kingine ambacho tumwombe Mheshimiwa Waziri na Serikali, tufanye maamuzi kwa haraka. Kule *Lake Rukwa* eneo moja tu lina *cubic feet* bilioni 138, ile *Block* ya

Rukwa *North*. Sasa kama matumizi ni ya bilioni sita duniani kwa mwaka, tunaweza tukawaambia wengine wote wasizalishe, sisi tukalisha dunia kwa miaka zaidi ya 20, na hapo ni *block* moja tu, bado ya *Lake Eyasi* na nyingine. Kwa hiyo, naomba twende kasi kwa hii *helium*.

Mheshimiwa Spika, halafu mnavyosikia watu wanakwenda mwezini na wameshaenda kule kufanya tathmini. Makisio ya awali yanaonesha kuna *helium* kiasi cha *cubic meter* milioni moja. Kwa hiyo, tukichelewa wanakwenda kuvuna mwezini. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, mfano wa pili ni *graphite*. Duniani sasa hivi walisema kwamba bado tuna kiasi cha *graphite* kama cha *800 million tones*, kinakwisha, lakini sisi tuna *graphite* nyingi sana. Mahenge tu kuna milioni 200, Lindi Jumbo kuna milioni 42 *tones*, Lindi kule Mbunyu kuna takribani milioni 180, ile ya Mererani hatujaipigia hesabu.

Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo naomba Serikali na kampuni na hiyo tume isimamie, kwa sababu matumizi ya *graphite* ni kutengeneza betri za gari. Hata hizi *break* zenu za gari zina *graphite*. Matumizi ni mengi sana. Matumizi yake wanasema yataongezeka mara 1,400 *percent; over one hundred four thousand percent*. Kwa hiyo, tukiipata hiyo *graphite* na tukiiuza, mambo ya kulia kwa sababu dola zimepungua hayatakuwepo.

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa ni kuhusu *gold reserve*. Nakushukuru kwani nilileta hapa wazo hilo likachukuliwa, lakini tunalifanya katika *refinery* mbili; moja, ipo Geita na moja ipo Mwanza. Sasa tutaliaje kwamba hatuna dola wakati tuna *refinery* mbili hizi ambazo kazi zake ni kuongeza thamani kutuletea dola zaidi na kuimarisha *gold reserve* yetu?

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa sisi tunaruhusu iende nje, nimalizie, *gold* tunayopeleka Dubai...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. PROF. SOSPETER M. MUHONGO:** Mheshimiwa Spika, dakika moja tu. *Gold* tunayopeleka Dubai, tumeifanya Serikali ya *United Arab Emirates reserve* yao kuwa takriban tani 74. Kwa hiyo, tukienda kuuza *gold* kule, tunawapatia wao *reserve*. Nyingine tunapeleka India. India kwenye *central bank* yao wana *reserve* ya tani 804, China wana tani zaidi ya 2,300, sisi sidhani kwamba tuna chochote. Sasa tujitahidi. Hapa mwisho nilitaka kuongeza lakini nashukuru, naomba hii bajeti ipite. Ni safari ndefu bado, lakini tuipitishe, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge kabla ya kuendelea, wapo wageni ambao wameingia baada ya sisi kuwa tumeshatangaza wageni. Kwa hiyo, nitawatangaza kwenu kabla hatujaendelea.

Tunao wageni wengine wa Mheshimiwa Waziri wa Madini, Mheshimiwa Antony Peter Mavunde, kwanza ni Bwana Ludovick Utouh ambaye ni Mwenyekiti wa Kamati ya *TEITI*. Haya amesimama, huku ndani nadhani ameshashuka.

Yupo Dkt. Venance Mwasse Mkurugenzi Mkuu *STAMICO,* yupo Mhandisi Ally Maganga, Mratibu Kituo cha *TGC*, yupo Bi. Mariam Mgaya - Kaimu Mtendaji *TEITI,* yupo Mhandisi Yahya Samamba - Katibu Mtendaji Tume ya Madini, yupo Dkt. Mussa Budeba - Mtendaji Mkuu *GST,* yupo Bwana Ally Said Ally - Mtendaji Mkuu *STAMIGOLD,* yupo *ACP* Paul Muzaga - Mwenyekiti wa Kikosi Kazi cha Kuzuia Utoroshaji Madini, yupo Ndugu John Bina - Rais wa Shirikisho la Wachimbaji Wadogo *(FEMATA),* yupo Mheshimiwa Jabir Shekimweri, Mkuu wa Wilaya ya Dodoma, yupo Bwana John Lipesi Kayombo - Mkurugenzi wa Jiji la Dodoma na mwingine ni Bwana Alhaj Adam Omar Kimbisa, Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Dodoma. Haya ahsanteni sana. *(Makofi)*

Yupo Mheshimiwa Profesa Davis Mwamfupe Meya wa Jiji la Dodoma, yupo Theobald Maingu Sabi - Mwenyekiti Umoja wa Benki Tanzania *(Tanzania Bankers Association),* yupo Abdulhabib Mwanyemba - Mwenyekiti Umoja wa Vijana CCM, Mkoa wa Dodoma, karibuni sana. *(Makofi)*

Wapo wageni wengine wa Mheshimiwa Antony Peter Mavunde ambao ni Wakurugenzi, Wakuu wa Idara, Wakuu wa Vitengo, Baraza la Madiwani Jiji la Dodoma, Umoja wa Vijana Mkoa wa Dodoma, Vyama vinavyojishughulisha na Uchimbaji wa Madini na Taasisi zote zilizo chini ya Wizara ya Madini, wote wasimame kwa pamoja, karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kati ya hawa wageni waliosimama, wapo wawekezaji wazawa kwenye hili eneo la madini na kwa niaba ya wenzao watatambuliwa hawa wachache ambao wamekuja kuwawakilisha. *(Makofi)*

Kwanza ni Ndugu God Mwanga, yupo Ndugu Baraka Ezekiel, huyu anatoka Busolwa, nadhani inaitwa *Busolwa Mine* au inaitwa? Mheshimiwa Musukuma, namuuliza Mheshimiwa Waziri, haya *Busolwa Mines, y*upo pia Onesmo Mbise huyu anatoka *Franone*, yupo bilionea Laizer, sijui yupo upande gani, lakini nimeambiwa yupo, karibuni sana. *(Makofi)*

Yupo pia Heneriko Yohana Maganga, naye sijui yupo upande gani, lakini huyu anajulikana kama Achimwene huyu anatoka Chunya, Mbeya, yupo mwekezaji mzawa mwingine anaitwa Sarah Masasi, ahsante sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, sasa mmeona wengi waliotajwa hapa siyo wengi, wote ni wanaume, huyu ndio ametajwa pekee yake mwanamke mwekezaji mzawa. Nimeambiwa huyu anawekeza kwenye *gold refinery* na *refinery* yake inaitwa *Geita Gold Refinery*, nimeambiwa hii ndio kubwa sijui ndio kubwa Afrika ama ni kubwa Afrika Mashariki ama ni kubwa Mwanza ama ni kubwa nchini? Naambiwa ni kubwa nchini, haya ahsante sana, hongera sana, Sarah Masasi kwa uwekezaji huo mkubwa. *(Makofi)*

Kuna wawekezaji wengine wazawa, kwa kweli tunawapongeza sana kwa kuingia kwenye shughuli hii ili tuweze kuwa tunaona tija, lakini tunafahamu mkiwezeshwa nyinyi basi mnawasaidia na Watanzania wenzenu. Basi tunawatakia kila la heri katika uwekezaji huu na kwa sababu mna nafasi leo ya kuwasikiliza Waheshimiwa Wabunge hapa mtakuwa mnasikiliza

na maeneo mengine Waheshimiwa Wabunge wanawakilisha ambayo bado hayajafikiwa na uwekezaji wenu, tunawatakia kila la heri katika hayo. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni wengine ambao wametembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo; hawa ni wanafunzi 116 na walimu watano wa Shule ya Msingi *Montfort* kutoka Mkoa wa Morogoro na hawa wameambatana na wanafunzi watano wenye ulemavu ambao ni viziwi, sina uhakika kama viziwi wanaitwa walemavu wa kusikia. Nadhani wanaitwa viziwi na wao hupenda kuitwa viziwi, ndio jina lao, haya wageni wetu, karibuni sana Bungeni na karibuni sana Dodoma. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, tunaendelea, Mheshimiwa Joseph Kasheku Musukuma, atafuatiwa na Mheshimiwa Profesa Shukrani Elisha Manya na Mheshimiwa Lucy John Sabu, ajiandae.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Kwanza, nianze kumpongeza sana Mheshimiwa Rais, kwa uteuzi wa Mheshimiwa Mavunde, kwenye Wizara ya Madini. Ni uteuzi mzuri na nampongeza sana Mheshimiwa Waziri kwa kuwa msikivu, tunamshauri vizuri, mimi ni Mjumbe wake kwenye Kamati yako, anasikiliza ushauri na ndio maana unaona Kamati yetu najua huko mbele haitakuwa na makolokolo mengi kwa kuwa Waheshimiwa Wabunge wenzetu wanaamini Kamati hii ina watu wabobevu kwenye Sekta hii ya Madini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kumshauri Mheshimiwa Waziri, mimi natoka kwenye Tasnia ya Uchimbaji, kuna kitu ningependa kwenye ushauri wangu akitilie maanani sana hasa kwenye wachimbaji hawa wa kati na wachimbaji wadogo, Sekta ya Uchimbaji Mdogo ni Sekta inayosimamiwa na Tume na ina Kamati zote, ina sekta zote zinazowasimamia wachimbaji wadogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa linapotokea tatizo hasa la ajali labda mgodi fulani umeanguka, usumbufu ni mkubwa sana hasa kwa *OSHA* na *NEMC,* wakati mchimbaji anafanya huo uchimbaji wake mdogo mdogo anasimamiwa kila siku na Tume na

anashauriwa na ripoti zote zipo. Ikitokea ajali badala ya kwenda kuchukua taarifa kwenye Tume, *OSHA* anakuja na yeye na makolokolo yake mengi na faini nyingi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu, juzi kasema isije ikaonekana kama *OSHA* na *NEMC* ni maadui wa wawekezaji. Ni vizuri kunapotokea majanga ichukuliwe kama ajali nyingine, siyo uvivu, hakuna mchimbaji anayetaka kuua watu. Inatokea ajali kama ajali za mabasi zinavyotokea au ajali nyingine, tuwachukulie na hawa ni wafanyabiashara na hii ni bahati mbaya, hakuna mtu anayetamani auwe watu kwenye kazi yake. Tunazingatia kweli suala la *safety,* lakini hii ni bahati mbaya, ikitokea isije kuwa mtu anaenda kupigwa faini hadi milioni 200, 300 mwisho wake anatelekeza mgodi anakimbia. Kwa hiyo, ushauri wangu kwa Mheshimiwa Waziri, wao kama Serikali wazungumze lugha moja na wawashauri wachimbaji wetu, badala ya kwenda kuwaletea tafrani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la pili, ni suala la *CSR,* kwanza, nimpongeze kwa kuja na wazo lake la kusema tunahitaji kupitia upya Kanuni mpya walizotoa juzi, hatuhitaji maneno. Nilishazungumza humu kwamba, sisi Geita ndio Wilaya pekee tumeanzisha *CSR* ya migodi. Sisi tuna miaka mitatu kwenye halmashauri yangu, tuna bajeti ya karibu bilioni 13, mpaka leo tumetumia 40% peke yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa ukileta Kanuni za kumpa ruhusa Mzungu afanye kila kitu mwenyewe, afanye *procurement* yeye, asimamie yeye, sisi ni watazamaji na hatuna uwezo wa kumhoji hata kuja kwenye halmashauri haji. Hizi siyo kanuni rafiki na kama kulitokea makosa, ni lazima Mheshimiwa Waziri akae na timu yake warekebishe kanuni. Tunahitaji kufuata taratibu kama tulizoenda kuzikuta Nyamongo, ambako *procure* zinafanywa na Serikali, halafu tunasimamia miradi, wao wanafanya kazi ya kukagua na kulipa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimwombe sana Mheshimiwa Waziri mimi na Waheshimiwa Wabunge wenzangu tunaotoka hasa kwenye migodi mikubwa wote tutakaposimama hapa kilio chetu ni

kimoja. Leo Geita hatujasaini *CSR* ya 2024/2025, ilikuwa tusaini mwezi Januari, lakini tumeomba bakaa tu, tueleze tumefanya nini kwenye bajeti tulizopitisha miaka mitatu. Tunaweza kuomba Serikalini tukapewa marejeo, lakini hatuwezi kuomba migodini kwa sababu ya kanuni mbovu walizozitengeneza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, namuunga mkono Mheshimiwa Waziri, halihitaji kuchukua muda na sisi watu wa Geita akikaa na sisi tutakaa, hatutasaini mkataba mpya. Kwa hiyo, mwaka huu hatutasaini mpaka apitishe kanuni ambazo zinatupa mamlaka ya kueleza watu tumepata shilingi bilioni 12 na zimetumika shilingi bilioni 12. Nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri, kwa wazo zuri na namwombea Mungu atimize ndogo yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala la pili, namuunga mkono sana kwenye utafiti na namuunga mkono sana Mheshimiwa Profesa Muhongo, utafiti ndio mkombozi hasa kwenye madini. Najiuliza mara mbili, watu waliosoma Maprofessa, Majiolojisti na Serikali watu waliosoma waliopo kwenye mamlaka, unawezaje kuendesha nchi kwa kutumia utafiti wa watu wa darasa la saba, halafu hawawatambui? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, anataka tukimuuliza mabilioni hayo anayokusanya yote, utafiti wote unafanywa na watu wa darasa la saba, halafu Serikali hawawatambui tunaita wawekezaji. Hapa ndio nataka Mheshimiwa Waziri anisikilize vizuri, tunahitaji kweli na Mheshimiwa Rais wetu anataka kweli tuwe na wawekezaji, hakuna mtu anakataa wawekezaji, lakini wawekezaji machokoraa hatuwataki kwenye nchi hii.

Mheshimiwa Spika, nimeanza kulalamika humu toka hii sekta inakusanya shilingi bilioni 81, wachimbaji wadogo leo tunaenda bilioni. Wameruhusu wachimbaji wadogo tuanzishe migodi na sisi kweli tuna njaa unaweza ukaanzisha mgodi, ukaa miaka miwili, miaka mitatu kama alivyozungumza kwenye ripoti yake. *Anatokea Mchina, China kule mwekezaji anapitiliza site, anakutana na mwenye leseni anatoa milioni 300, kwa kutumia technical support ya darasa la saba ananunua. Sasa hivi ukizunguka kila mahali Wachina wapo, sasa mwisho wake watakuja kuwa na wachimbaji wadogo wa China peke yake, hii*

*inaumiza sana. Leo hii hakuna mgodi ambao hakuna Mchina, ukiambiwa ameingia kwa milioni 200. Hivi tunahitaji kweli kuwa na wawekezaji wa milioni 200? Najua hili ni suala la diplomasia, lakini lazima tuelezane ukweli?...* **[Maneno Haya Siyo Sehemu ya Taarifa Rasmi za Bunge]**

**SPIKA:** Mheshimiwa Musukuma, umetaja mwenyewe neno diplomasia. Nina uhakika watu wanaowekeza huko ni wengi kuliko hao Wachina. Kwa hiyo, wewe endelea na mchango wako, lakini ondoa hayo majina ya China ili tusiletewe maswali hapa ndani, kwa sababu wapo wawekezaji zaidi ya Wachina huko. *(Makofi)*

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Spika, nakuomba radhi na nimefuta.

Mheshimiwa Spika, hawa wawekezaji wenye kiwango kidogo, namwomba Mheshimiwa Waziri pale ambapo sisi tumefanya kama alivyoeleza kwenye ripoti yake, hatuhitaji hao wawekezaji. Mwekezaji aje naye akafanye utafiti, aje akwambie amepata sehemu fulani. Siyo anaenda kuzama kwenye duara limeshafika anazama halafu anatoa leseni milioni 300, anafukuza wachimbaji wadogo, hii si sawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, namuunga mkono kabisa Mheshimiwa Waziri kwamba, ni vizuri wawekezaji waje wafanye *technical support* za kwao ambazo sasa hata wakiamua kuwekeza tunajua tuna mwekezaji mwenye nguvu kiasi gani, kulikoni kuwa na wawekezaji ambao kwa kweli baada ya muda mchache tutakuja kujikuta sisi ndio tumekuwa wakimbizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lingine, naomba Serikali hasa Wizara ya Mheshimiwa Waziri, nimekuwemo humu ndani nilianza kutembelea *refinery* ya Mwanza, ikiwa inajengwa, tukaenda *refinery* ya Geita, nipo siku nyingi. Nampongeza sana, amemtaja Mama Masasi, mama yangu, kwa kweli kama tukimpima *temperature* mapigo ya moyo sidhani kama yupo sawa, kwa sababu mipango yetu haieleweki. Leo sisi ndio tuliwahamasisha hawa watu watengeneze huu uwekezaji wa mabilioni, watu wameenda Benki wamekopa wametekeleza uwekezaji lazima

uingie kwenye Benki, halafu sasa hivi Serikali imekuja na mpango mwingine. Huyu mwekezaji hana uwezo wa kununua dhahabu, ina mapigo yake ya kununua, badala ya Serikali iungane na hizi *refinery* kama alivyosema Mheshimiwa Profesa ili tupate dola. Tunakuja tena na wazo *BOT* inataka kununua dhahabu, jamani hamhitaji kweli elimu yetu tuwasaidie labda mawazo mapya? Hawa watu wanakufa na presha na *refinery* ambazo hazifanyi kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa nini *BOT* tusiungane nao kwenye zile *refinery* halafu wakanunua hiyo dhahabu kwa kutumia zile *refinery,* inahitaji kuwa na *degree* kweli? Badala ya kumwezesha mtu ambaye wamemhamasisha wao Serikali, amewekeza matrilioni ya pesa, nyingine ni za Serikali. Sasa wanamwacha, kitakuwa kitete, kitapigwa mnada kile, kikipigwa mnada ile *scraper* tunapeleka kwenye nondo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri yeye ni kijana, ni Msomi Mwanasheria mzuri, hebu apitie upya wakati tunawahamasisha hawa wawekezaji tulizungumza vitu gani nao mpaka wakahamasika na wamekwama wapi? Tuanzie hapo kuwakwamua, kuliko kuwa na mawazo mapya kila bajeti, hii siyo sawa, unawakatisha tamaa watu wengine ambao walidhani sasa Tanzania tumepata *refinery* hizo mbili, mimi wenyewe mtu wa Geita nilitegemea *CSR,* watu wa Mwanza, Ilemela walitegemea *CSR*. Tumebaki kuangalia rangi tu, *refinery, refinery, what about this one?* wanatuchanganya bwana! Wanashindwa kuwa wakweli? *(Makofi/ Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, ni lazima wasimamie mipango yao, hatuwezi kila mwaka tukawa na mipango, unapanga hiki, kikikaa *level* unahamia kwingine, watueleze kama ni 10% zipo huko mbele, watu wasiwekeze Tanzania. Mawazo ya Mheshimiwa Waziri ni mazuri, namuunga mkono asimamie maamuzi, yeye ni kijana, aache *legacy,* aliwashauri Mheshimiwa Profesa Muhongo na mimi Daktari narudia mle mle kuwa na mipango mizuri, Waziri awekeze kwenye utafiti. Hii nchi tuna dhahabu kila kona, tunahitaji kusimamia maamuzi yetu, aweke ripoti hapo, mtu anataka kuja kuchimba tunamwambia dhahabu ipo Chunya, dhahabu ipo Bagamoyo bei gani? Tunauziana vitu

vimeshafanyiwa kazi na wataalamu. Hii nchi ina shida ya kununua helikopta? Tunapiga maneno kutoka bilioni 81, leo anakusanya trilioni moja pointi kitu, halafu anapewa bajeti ya bilioni 400, hiki kitu gani? *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, naomba niishie hapo, mimi ni Daktari imetosha kushauri. *(Makofi/Kicheko)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Musukuma, naona unachangia mambo mengi kwa wakati mmoja. Wewe mwenyewe ni darasa la saba, wewe mwenyewe ni Daktari, halafu leo nilikuwa natafakari kama hilo vazi ni la Kibunge au hapana?

Waheshimiwa Wabunge, ataingia Mheshimiwa Mwenyekiti kunipokea, kabla hajaingia; kulikuwa na hoja hapa ya kuzagaa kwa tembo kwenye makazi ya mashamba ya wananchi. *(Makofi/Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge, sasa baada ya kuwatafuta Viongozi wetu upande wa Serikali Waziri na Naibu Waziri wameenda kwenye jambo la muhimu kabisa kule Arusha, linalohusu pia Maliasili na Utalii. Kwa hiyo, tutalishughulikia jambo hili siku ya Alhamisi na tutafanya hivyo kwa jambo hili na lile lingine la mikopo ya kausha damu ambalo tulikuwa tumewaambia watu wa Serikali walifanyie kazi. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, jambo lingine, tulitangaza Semina ya Kilimo saa saba, sasa saa saba tutaanza na Semina ya Nishati, maswali ambayo Waheshimiwa Wabunge mliuliza kipindi kile cha maonesho. Saa saba, mpaka saa tisa, halafu saa tisa, itaanza Semina hiyo ya Wizara ya Kilimo. Kwa hiyo, zote mbili zinatafanyika leo Waheshimiwa Wabunge, mkitoka hapa moja kwa moja Msekwa ili kutunza wakati.

Baada ya kusema hayo, Mheshimiwa Mwenyekiti, anakuja kunipokea ili aendelee na ratiba iliyo mbele yetu. *(Makofi)*

*Hapa Mwenyekiti (Mhe. Najma Murtaza Giga) Alikalia Kiti*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Mchangiaji ambaye Mheshimiwa alikuwa ameshamtaja Mheshimiwa Profesa Shukrani Elisha Manya na Mheshimiwa Lucy John Sabu, atafuatia.

**MHE. PROF. SHUKRANI E. MANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa nafasi ya kuchangia hoja ya Waziri wa Madini. Nitangulie kusema kwamba, naunga mkono hoja kwamba, Wizara hii ipewe fedha iweze kutekeleza majukumu yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kuwapongeza Wizara pamoja na Taasisi zake *TEITI, STAMICO,* Tume ya Madini, *GST* pamoja na *TGC*, kwa sababu kwa pamoja wameweza kuchapa kazi. Katika kipindi chao wameweza kufikia lengo la kisera la tangu mwaka 1997, ambapo sekta ilikuwa inachangia asilimia 1.7, katika kipindi chao lile lengo la kisera la kufika 10%, limeweza kufikiwa na kwa hiyo tunawapongeza sana na waendelee kuchapa kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu leo utajikita juu ya hoja ya tathmini ya vihatarishi katika usimamizi wa Sekta ya Madini Nchini Tanzania. Kwa nini, nimechagua kuongelea hoja hii? Ni kwa sababu Sheria yetu ya Madini kama ilivyorekebishwa mwaka 2017, sasa imeweza kutenda kazi kwa miaka saba na ni kweli kwamba, kuna ambayo yanafanya kazi na kuna ambayo yawezekana hayakufanya kazi kama ilivyotarajiwa na kwa hiyo, tuna sababu zote za kuangallia vihatarishi sababu zake, namna ya kuepuka hasara na maboresho gani yafanyike ili kuendelea kupata faida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitangulie kusema kwamba, naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Dkt. Musukuma Kasheku, aliyoiongea juu ya *refinery* kwamba, ni jambo ambalo Serikali ilihimiza wawekezaji kufanya. Hatari yake ni kwamba, kama Serikali haitaweka mkono wake pale maana yake uwekezaji ule utakufa na hautakuwa na tija na haitakuwa ni tija kwa Serikali, lakini pia kwa uwekezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu nyingine ambayo napenda kuchangia ya kwanza, kabisa ni utoaji wa leseni katika

maeneo yanayopaswa kuhifadhiwa. Hatari yake ni kwamba, tunapotoa leseni katika maeneo ambayo yana umuhimu mkubwa wa kijiolojia, wakati fulani nilishajaribu kuyaongea hapa ni kwamba, urithi huo utapotea. Mfano, ambao nataka niuweke wazi hapa ni Mlima wa Mautia upo hapa Kongwa, mlima huu ndio Mlima ambao kwa mara ya kwanza duniani kwenye sayari yetu madini ya *yoderite* yaligunduliwa kwanza na yapo sehemu mbili peke yake duniani. Sasa mlima huu umetolewa leseni kunachimbwa kokoto, kunachibwa mawe, maana yake ni kwamba, baada ya muda mfupi mlima huu utapotea, tutakuwa tumepoteza urithi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pendekezo langu kwake Mheshimiwa Waziri, aende akaifute leseni inayochimba kokoto na mawe Mlima wa Mautia na *NEMC* waingie pale walifanye kuwa eneo Lindwa *(Protected Area)*. Hiyo ni pamoja na maeneo mengine yote ambayo yana umuhimu mkubwa wa kijiolojia na tayari leseni za uchimbaji kokoto zimekwishatolewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ni aya ya 159 ya Hotuba ya Mheshimiwa Waziri imezungumzia juu ya Mtanzania mwenye leseni ndogo ya uchimbaji kupewa msaada wa kitaalam au kiufundi au kiteknolojia na kwa jinsi hiyo, waweze kufanya ubia. Sasa ni kwamba, lengo lilikuwa ni jema na wachimbaji wadogo ni kweli, hata wao wenyewe huwa wanawatafuta wawekezaji kutoka nje ili waingie ubia na hatimaye waweze kuchimba kwa tija.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kihatarishi kilichopo hapa ni kwamba, msaada wa kitaalamu umekuwa kitanzi kwa wachimbaji wadogo na wengi wamefikia mahali wakapoteza maeneo yao, lakini kihatarishi kingine ni mingi ya migodi itokanayo na ubia huu wa wachimbaji wadogo na wataalam kutoka nje hatimaye inakuwa ni migodi ya kati ilhali inatambuliwa kama ni migodi midogo na hivyo, kupoteza mapato ya Serikali. Kwa hiyo, Tume ya Madini inalo jukumu la kufanya, ili hali hii isiweze kuendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ni Kanuni ya 21(1) ya Kanuni za Haki Madini ya Mwaka 2018. Kanuni hii ilifuta *Retention*

*License* na kuzirudisha Serikalini bila ya kulipa faida kwa wale wawekezaji. Ni kweli, lengo lilikuwa ni jema, lakini katika zile ni kweli kwamba, Kabanga *Nickel* imeweza kuendelezwa na hatimaye tumeingia nayo ubia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatari iliyopo ni kwamba, leseni hizi nyingi zilifikia mahali zikawa mwiba kwa Serikali. Lengo langu la kuweka hii hoja ni kwamba, Serikali inapaswa kuona vihatarishi hivi ili tufike mahali tuseme baada ya Sekta ya Madini iliyoanza kushamiri hapa Tanzania miaka ya 90, sasa tunao uzoefu wa miaka 30. Kwa hiyo, ifikie mahali tuseme Serikali yetu sio ya kupelekwa Mahakama za Kimataifa na kushtakiwa kwa ajili ya mikataba. Ifikie mahali tukome, kwa uzoefu tulionao tunapaswa kuwa ni *giants* katika madini *such that* hatushtakiwi na hatushindwi kesi hizo. Kwa hiyo, vihatarishi hivyo Serikali iwe inaviangalia mapema ili tufikie mahali tunapoita wawekezaji sio wanageuka kutushtaki na hatimaye kuwalipa mabilioni ya pesa nyingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja nyingine ni katika *CSR* na *local content*. Katika mapendekezo ya *CSR* na *local content* mwekezaji anapokuja anapaswa aingie ubia, lakini mwekezaji wa ndani anatakiwa awe na 20% ili kufanya kampuni ya ubia. Sasa kihatarishi kilichopo hapa ni kwamba, tunajua madini ni *capital intensive* na unahitaji mtaji mkubwa; je, wazawa wameandaliwa kuweka 20% ili waweze kuweka *JV company* itakayoweza kufanya *supplies? (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama si hivyo, matokeo yake ni kwamba, tunakuwa na kampuni ambayo katika makaratasi inakidhi, unaona Mtanzania ana 20%, *yes*, halafu wa nje ana 80%, lakini mifumo yetu imeenda mbali kuhakiki kwamba, kinachoonekana katika makaratasi yale ndiyo faida pia inayokwenda kwa yule mwekezaji wa ndani? Kama mifumo hiyo haipo maana yake ni kwamba, takwimu tunazozitoa kwamba manunuzi ya ndani yamepanda wakati faida kwa kinyumenyume inakwenda kwa mwekezaji, sio sahihi. Kwa hiyo Serikali iangalie, ijenge mifumo ambayo mwekezaji anapoingia na yule wa ndani, kwanza ameandaliwa kwa kupewa *capacity building,* lakini pia amefundishwa namna ya kuingia *JV* ili faida inayotokana na ubia

huu iweze kumwendea hasa yule ambaye amekusudiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu nyingine ninayopenda kuchangia ni uthabiti na mwendelezo wa ukuaji wa Taasisi za Wizara ya Madini. Kumetokea *movement,* yaani uhamisho wa wataalam ndani ya Wizara na hasa wale ambao wanaonekana wamekuwa na uzoefu mkubwa kidogo. Unashangaa tu kwa namna moja au nyingine anahamishwa hapa anakwenda pale. Kihatarishi ninachokiona hapa ni kwamba, taasisi hazikui, zitaendelea kuwa na wataalam ambao uzoefu wao ni mdogo wakati wale wenye uzoefu mkubwa wamehamishiwa sehemu nyingine. Kwa jinsi hiyo unakuta taasisi haikui, yaani kila siku inakuwa ni kujifunza, maana anapewa mtu ambaye ni mchanga wakati mwenye uzoefu amehamishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka jana nilichangia hoja ya kwamba, ndani ya Taasisi za Wizara ya Madini kuna uwiano mbaya wa maslahi, mishahara. Niliongea sana katika bajeti ya mwaka jana, sipendi kurudia hiyo hoja. Kama hili jambo linaendelea kwa sababu, najua halijafanyiwa kazi, maana yake ni kwamba, Mheshimiwa Waziri anaendelea kufanya kazi na *staff* ambao hawana ari. *They are not motivated,* kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri anapiga ngoma, anapeleka malengo, *they are not motivated and this is for sure*. Mheshimiwa Waziri aende akalifanyie kazi hili kwa sababu, wakati mwingine watakuwa wanarudisha nyuma malengo yake anayopaswa kuyafanyia kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja. Ahsante sana kwa kunipa nafasi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Profesa Shukrani Elisha Manya. Nilimtaja Mheshimiwa Lucy John Sabu, Mheshimiwa Jumanne Kishimba ajiandae.

**MHE. LUCY J. SABU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa fursa hii ili niweze kuchangia Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Madini. Kwanza kabisa ni pongezi kwa Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kuipa kipaumbele Wizara ya Madini

kuwa ni sekta yenye mchango katika uchumi wa nchi yetu na bajeti ya madini imekuwa ikiongezeka kutoka shilingi bilioni 88 mpaka shilingi bilioni 231. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, nachukua nafasi hii kuipongeza Wizara kwa kazi kubwa na nzuri wanayoifanya ikiongozwa na Waziri, Mheshimiwa Antony Peter Mavunde, pamoja na Watendaji wote wa Wizara. Pia nachukua nafasi hii kuipongeza Wizara na nampongeza Waziri kwa wasilisho zuri la Hotuba ya Bajeti ya Madini ambayo amezingatia na kuwapa kipaumbele wachimbaji wadogo. Kwenye kila ukurasa ukisoma amewagusa kwa namna moja ama nyingine wachimbaji wadogo. Kwa upande wa wachimbaji wadogo, eneo hili lina vijana na wanawake wengi. Nawapongeza tena katika mipango yao ya ununuzi wa mitambo ya kuchoronga kwa ajili ya wachimbaji wadogo. Pia, mpango wa kufanya utafiti wa kina kupitia *vision 230* utawasaidia wachimbaji wadogo kuelekeza nguvu zao katika maeneo yenye madini na kupunguza nguvu waliyokuwa wanaitumia kuchimba katika maeneo ambayo hayana madini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ununuzi wa *helicopter* ambayo itawekewa vifaa vya utafiti pamoja na ujenzi wa Maabara ya *GST* itasaidia kwenye utafiti wa sampuli za madini. Nawapongeza sana Wizara kwa maono haya makubwa na mazuri. Tunamwombea kwa Mwenyezi Mungu Mheshimiwa Waziri aendelee kujituma kwa ajili ya Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu leo utajikita zaidi kwenye eneo la wachimbaji wadogo. Nachukua nafasi hii kuipongeza Wizara kwa kuja na mpango wa Mradi au *Program* ya *MBT (Mining for Brighter Tomorrow)*. Naipongeza sana Wizara kwa sababu, mradi huu ni mahususi kwa ajili ya vijana na wanawake katika eneo ambalo utahusisha utoaji wa leseni, lakini pia utawasaidia wachimbaji wadogo kwa upande wa vifaa na mitambo. Kama tunavyofahamu na kwa mujibu wa sensa, vijana ni kundi ambalo linakadiriwa kuwa zaidi ya 74%. Nashukuru kwa maono haya ya Wizara ambayo yatasaidia vijana wengi kujiajiri katika eneo hili, sambamba na *support* ambayo Serikali itaitoa kwa ajili ya wachimbaji wadogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, naipongeza Wizara kwa kufuta leseni na maombi ya leseni 2,648. Pia, naipongeza Kamati kwa kusisitiza kwamba, jambo hili liwe endelevu ili kuwazuia watu ambao wamekuwa wakihodhi ama kushikilia maeneo makubwa bila kuyaendeleza. Hali hii imekuwa ikisababisha kuikosesha nchi mapato, lakini pia kuikosesha wawekezaji ambao ni sahihi. Namwomba Mheshimiwa Waziri watakapokaa na Tume yake kwa ajili ya kupanga maeneo haya, kipaumbele kiwe ni kwa wachimbaji wadogo ili kuwapatia maeneo ambayo yatakuwa na madini kwa lengo la kupunguza changamoto ya ajira kwa upande wa vijana na wanawake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafahamu kwamba, Serikali imekuwa ikitoa mikopo ya asilimia nne kupitia Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. Naiomba Wizara ya Madini pamoja na Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa waweze kuona ni namna gani wanaweza wakashirikiana ili kutoa mikopo kupitia hiyo asilimia nne kwa ajili ya vifaa ama mitambo ama *crusher* kwa ajili ya wachimbaji wadogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni katika ukurasa wa Hotuba ya Bajeti ya Madini ambapo Wizara imeelezea kwamba, imeendelea kuhakikisha wawekezaji wanazingatia kutenga ama kuweka *CSR*, kwa ajili ya maeneo yanayozunguka madini/migodi. Kama ambavyo imeoneshwa katika Hotuba ya Bajeti, nawapongeza Wizara kwa kuendelea kusimamia hilo, lakini naendelea kusisitiza kwamba, waendelee kulisimamia kwa umakini wa hali ya juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa natoa wito kwa Wizara, nawaomba kwa namna ambavyo fedha hizi zinatengwa, kwa ajili ya *CSR*, nawasihi waendelee kuhakikisha fedha ambazo zinatengwa kwa ajili ya kusaidia miradi ama shughuli mbalimbali za kijamii, basi fedha nyingine itengwe kwa ajili ya kusaidia vijana na wanawake katika maeneo mbalimbali kwa ajili ya kuwa-*support* katika mitambo ama vifaa ambavyo wataendelea kuvitumia katika eneo la uchimbaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo napenda kuikumbusha na kuishauri Serikali ni kwamba, ihakikishe inatafuta namna ya kurudisha ruzuku. Kwa sababu, tunafahamu kipindi cha nyuma, Wizara ilikuwa inatoa ruzuku kwa ajili ya wachimbaji wadogo na ilikuwa inawasaidia wachimbaji wadogo kwa ajili ya uanzishaji wa maeneo ya uchimbaji. Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Waziri, atakapokuwa anahitimisha hoja yake, atueleze wana mpango gani wa kurudisha ruzuku kwa ajili ya wachimbaji wadogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa fursa hii na nasema kwamba, naunga mkono hoja iliyoko Mezani na naiombea Wizara iendelee na kazi. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Lucy John Sabu. Nilimtaja Mheshimiwa Jumanne Kishimba, atafuatiwa na Mheshimiwa Sebastian Kapufi.

**MHE. JUMANNE K. KISHIMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipatia nafasi ya kuchangia kwenye Wizara hii ya Madini. Namshukuru Mheshimiwa Rais kwa kumteua Mheshimiwa Mavunde kuwa Waziri wa Madini. Kwa nini nasema hivyo? Ni kwa sababu Mheshimiwa Mavunde amekuwa Mjumbe wa Kamati ya Madini kabla hata hajawa Waziri. Kwa hiyo, analifahamu vizuri sana suala zima la madini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wachangiaji wengi sana wameongelea suala hili la wachimbaji wadogo. Wachimbaji wadogo wengi wanatazama wachimbaji wenyewe, ukweli usiopingika ni kwamba, Mji wangu wa Kahama ni eneo la pili kwa Tanzania kwenye soko la madini ambalo lina dhahabu nyingi. Wanufaika wa uchimbaji mdogo siyo wale wachimbaji wenyewe peke yao, ni wale wananchi wanaofanya huduma na shughuli nyingine pale kwenye ile migodi ya wachimbaji wadogo na ndiyo hasa tunaowapigania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye eneo langu moja tu la Mgodi la Mwime lina wachimbaji zaidi ya 200,000. Ukisema aje mwekezaji mmoja awaondoe watu 200,000, maana yake ni Mji mzima wa Kahama ume-*collapse* kabisa. Yaani ni kwamba,

tutakwenda kwenye matatizo makubwa na Waheshimiwa Wabunge wameongea vizuri humu kwamba, kwa nini yeye anataka lile eneo tu ambalo watu wapo? Kwa nini hataki kwenda kwenye eneo ambalo lipo wazi? Ugomvi wetu ndiyo upo hapo tu kwa sababu, kama ataendelea kupenda mahali pale wapo watu, haya tuulizane wote, siku akipenda na ng'ombe wetu, tutamruhusu achukue? Akitaka na maeneo ya mpunga alime mpunga, tutakwenda wapi? Kwa hiyo, suala hili sio dogo kama tunavyoliongea, sasa hivi lina migogoro mingi mno. Mheshimiwa Waziri anafahamu, amekuja kwangu Kahama karibu mara mbili, tumekaa tumelijadili sana, lakini kwa kuwa, kwenye taarifa yake limo, basi tumwombe alichukue kwa umakini na tahadhari kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi Shinyanga kumetokea ugomvi kati ya wawekezaji na wananchi na ingekuwa hatari zaidi kama polisi wasingewahi. Wale wawekezaji walikuwa wanapiga picha tu, lakini wananchi wamekuja kwa vurugu kubwa sana, kitu ambacho hatukutarajia. Kwa hiyo, namwomba sana Mheshimiwa Waziri, aliangalie jambo hili kwa mapana sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala hili hasa la wachimbaji wadogo wa dhahabu, kama alivyosema Mheshimiwa Musukuma, tukubaliane kuwa ni la watu wa darasa la saba, kwa hiyo, labda mawazo mengi yangetoka kwao kusudi tuumalize huu mgogoro kwa sababu, wao ndiyo waanzilishi wa hii kazi na wao wamekuja tu ku-*legalize tu*. Kwa hiyo, tumwombe Mheshimiwa Waziri kwenye Kamati zake au Tume zake, aweke na wale wachimbaji wabobezi ili kusudi tumalize hii migogoro. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna utoroshaji wa dhahabu. Ni nani anayeusababisha? Ni Serikali yenyewe. Mimi nimechimba mawe, nimekulipa mrabaha wako kwenye mawe. Dhahabu zipo za aina tatu, kuna moja ni *free gold* ambayo ni dhahabu unayoweza kuipata peke yake. Ipo dhahabu ya pili, unaisaga peke yake kwa *mercury* na ya tatu ni ya *illusion;* dhahabu ya *illusion* unaweza kuweka watu wa Serikali pale, hii nyingine mtu anafanyia kwake. Huyu mtu umechukua hela yake ya mawe, ukasema hata asipoonekana mimi sina kesi na wewe. Haya amepata dhahabu yake, wewe ulishamnyang'anya asilimia tisa,

sasa analeta kweli uchukue tena asilimia tisa? Mtu unamjua na risiti unayo. Kwa nini huyu asiruhusiwe aje auze bure? Hili suala la utoroshaji liishe, vinginevyo haitawezekana hata tukifanyaje, haitawezekana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mnasema Mmasasi hapa wamemkatalia, ataipataje sasa dhahabu, hebu tuelezane wote. Dhahabu yote iliyoko kule imekuwa *financed* na wale watu wadogowadogo. Ni kama vile wakulima wa mboga, si wanalima wanachukua hela kwa madalali? Ataipataje yeye dhahabu? Wamruhusu hii dhahabu ambayo wao wamechukua ushuru wa mawe aende akaiuze bila ushuru, lakini ukiona zile fomu za kuuza dhahabu zilizowekwa na Benki Kuu; wanataka ili uuze dhahabu uende na *ID*, uende na *TIN Number*. Kweli mtu wa dhahabu huwa ana *TIN Number*? Dhahabu unachimba kwa *TIN Number?* Haiwezekani, lakini je, mzungu akileta dola huwa wanamuuliza *TIN Number? (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndugu zangu wao ndiyo wamesoma, sasa wao ndiyo viongozi wetu, tufanyaje sasa? Huku wanalia hatuna dola, aliye na dola wanamwambia alete *TIN Number,* ana dhahabu, wanakataa dhahabu, afanyeje sasa? Kwa hiyo, tumwombe Mheshimiwa Waziri, sijui tutashauri namna gani, lakini akae na Waziri wake wa Fedha waone kweli sababu ya kutorosha dhahabu ni nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, dhahabu ni kitu kinakaa mfukoni. Leo ukifika nchi za jirani ukiwa na dhahabu unapewa *premium*. *Premium* maana yake kama dhahabu ina dola 2,000 unapewa 2,010, huku mimi naleta dhahabu niliyokulipa kwenye mawe unataka tena unikate asilimia tisa lakini, ukiwa nayo mfukoni wale wananipa na hela ya juu, sasa tufanyaje? Mheshimiwa Waziri, kweli atawakamata lakini itaishia wapi, ndiyo hoja yetu. Kwa hiyo, tumwombe tu Mheshimiwa Waziri alifikirie kwa mapana sana ili kusudi huu mgogoro umalizike na Serikali ipate dola. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeona lingine hapa ameongea Mheshimiwa Waziri kwamba atajitahidi, anataka kusema kwamba watu wanaotaka ku-*export* madini lazima waya-*add value* hapa. Mheshimiwa Waziri, hilo suala litawezekana kweli? Litawezekana

kweli? Tutarudi tena kwenye matatizo, afanye *analysis*. Kwa nini nasema hivi? Kwa sababu, leo hii duniani madini zaidi ya manne yamekwishatengenezwa madini feki na yanatumika. *Lithium* leo tena inatoka hapa Dodoma kwa Mheshimiwa Waziri, imekwama na imekuwa *scraper,* ndani ya mwezi mmoja siyo mali tena, kwa sababu Wachina wamegundua kwamba kwenye chumvi kuna *Lithium* na chumvi tani moja ni shilingi 200,000 au shilingi 200 kwa kilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ukibaki huku unang'ang'ana na sheria za ku-*add value* utaikuta hiyo dunia? *Nickel* yote inatengenezwa ya bandia na wewe unasema una-*reserve,* utakuwa una-*reserve* au unatakataka? Mheshimiwa Waziri aruhusu, aache kabisa maneno ya kwenye vitabu, aachane nayo, dunia haiwezi kusubiri tena vitabu. Aruhusu watu wauze madini ili tupate hela hayatokuwa madini tena. Hakutokuwa na madini tena, madini yote sasa hivi yanapelekwa kwenye maabara yanatengenezwa ya bandia na yanatumika, utafanya nini? Huwezi! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo chuma cha bandia kinatengenezwa kutoka kwenye karatasi ngumu za nailoni utafanyaje, utafanya nini na wewe unasubiri. Namwomba sana Mheshimiwa Waziri, ajaribu kufikiria kwa mapana sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya mchango huo, nakushukuru sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Jumanne Kishimba. Nilimtaja Mheshimiwa Sebastian Kapufi na muda uliobakia atamalizia Mheshimiwa Salome Makamba.

**MHE. SEBASTIAN S. KAPUFI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana na niseme tu kama walivyotangulia kusema wenzangu, mimi ni mdau katika sekta hii ya madini na napata manufaa kwa kupitia uchimbaji. Kwa hiyo, nitajitahidi kuongea nikiakisi hali halisi ilivyo uwandani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa lugha aliyokuja nayo ambayo anatuambia kwamba "Madini

ni Maisha, Madini ni Utajiri." Nakubaliana kabisa na hilo, lakini nataka twende mbali zaidi kwa maana ya intelejensia ya uchumi. Wazungumzaji wengine wamesema Tanzania kwa ujumla wake na mara ya mwisho hapa nikichangia nilielezea kwa maana tu ya dhahabu tunasomeka kama wanne Barani Afrika, ukiacha Ghana ambayo ni ya kwanza kwa maana ya Barani Afrika. *Point* yangu inakuja hapa amesema Mzee wangu pale, leo hii usipoitoa dhahabu chini ya ardhi ikaja juu na baada ya hapo ikauzwa, ni jiwe kama lilivyo jiwe lingine, hutoiona thamani yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kule kwetu Mpanda, leo hii nikiongea na wewe kwa maeneo ambayo ni ya wachimbaji, wachimbaji wetu hawa wadogo kuna wakati anatoa mawe yenye asili ya dhahabu. Akiona kama hili lina madini kidogo anaweza kwenda kujengea hata nyumba, anaweza hata akapiga piga ikawa kokoto. Kwa hiyo, tafsiri yangu ni nini? Ni jiwe kama jiwe lingine usipokwenda kuitafuta thamani yake. Kwa hiyo, tusipokuwa makini tutabaki kuwa washangaaji wakati tukijisifu tuna-*reserve* ya kutosha ya dhahabu. Nikilisema hilo namwomba sana Mheshimiwa Waziri, nilipozungumzia suala la intelejensia ya uchumi, kwa nini hatujiulizi kuna baadhi ya nchi zinazotuzunguka hawana dhahabu, lakini leo ni wauzaji wakubwa wa dhahabu wanafanya vipi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapozungumzia suala la intelejensia ya uchumi, twende mbali zaidi, tuepukane na hizo tozo na kodi nyingi. Amesema Mheshimiwa Kishimba hapa na huku nyuma kuna wimbo mmoja uliimba kwamba mkulima mmoja katika kulima lima tu kachimba chimba kakutana na almasi, mwingine katika kuchimba choo anakutana na dhahabu. Hivi huyu aliyekutana na dhahabu katika mazingira ya kawaida unasemaje, aifiche au aipeleke sokoni na akiipeleka sokoni kwa nini anakutana na urasimu? Hili ndilo linatokea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siku za hivi karibuni nilikuwa kwenye nchi moja ya jirani. Naambiwa Mheshimiwa dhahabu ya hapa ukivuka tu mpaka ukiingia kwenye nchi ile pale wanakukaribisha kwa mikono miwili uweze kuuza mali yako. Hiyo ndiyo namna ambapo nchi nyingine zilivyo, sijasema tufanye wizi na vitu vingine, lakini tufungue milango. Madini haya siyo Tanzania pekee

tuliyonayo, nchi nyingine zinayo. Sasa katika mazingira ambayo tunajisifu tuna huu utajiri mkubwa, lakini ukija kuangalia watu wake unauona umaskini uliosheheni, nyuso zetu zimejaa umaskini na wakati huo tunasema tuna mali ya kutosha, hapana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoke hapo, naomba sasa nielezee suala lingine ambalo tunalihitaji, suala la motisha. Tunapozungumzia wachimbaji wadogo ambako huko na mimi nipo, nitatoa mfano wa pale kwetu Mpanda, eneo ambalo kwa muda wote na Serikali ikasema maeneo kama Dirifu, maeneo kama Kapanga tunayatenga kwa ajili ya wachimbaji wadogo. Serikali ikaenda mbali zaidi kutoa hata vifaa vya utafiti ili watu hawa wachimbe kwa uhakika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasikitika maeneo yote hayo sasa hivi baadhi ya wawekezaji, mtu mmoja hapa amesema wawekezaji uchwara, wamekwenda, wamerubuni watu wetu, wameyanunua maeneo kiasi cha kwamba wachimbaji wadogo sasa hivi ninavyoongea hawana maeneo ya kuchimba. Madhara yake ni nini? Leo ukizungumzia Damuchafu, ukizungumzia P*anyaroad,* wana majina mengi; hivi wachimbaji pale kwangu unaambiwa takribani zaidi ya 35,000 ambao siyo rasmi, hawa wote waruhusu waingie mjini, hapo mjini patatawalika kweli! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu hawa wamefichwa katika maeneo hayo kwa ajira zisizokuwa rasmi kwa maana ya kujiwekeza wenyewe katika eneo la uchimbaji. Kwa hiyo, niombe sana na wataalam watusaidie, wataalamu wapo mbali na utaalam wao waende mbali zaidi, kama leo wataalam wapo na ndiyo wao wanao-*issue* leseni wasiishie tu kutafuta maduhuli ya Serikali ili kuhakikisha mafao ya Serikali yameongezeka, bali waangalie na masuala mengine ya jamii kwa mapana yake na hasa suala hilo ulilosema la ulinzi na usalama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoke hapo, nashukuru kwa maana ya uchimbaji wenye tija. Kila mmoja hapa ameongelea suala la *GST*. Nikubaliane na wewe, taarifa ya Mheshimiwa Waziri imesheheni masuala yote hayo kwamba bila kufanya uwekezaji kwa maana ya utafiti, wachimbaji hakuna

watakachofanya. Kwa hiyo hilo nikubaliane nalo, lakini naomba twende mbali zaidi, kwa mfano kule kwangu Katavi, tunapoongelea habari ya dhahabu, usafishaji wa dhahabu sioni taarifa ikituambia habari ya madini mengine yanayokwenda sambamba na hilo. Tuna fedha, tuna shaba, utakuta tumejikita tu kwenye kuongelea dhahabu, dhahabu, dhahabu vipi madini mengine hayo shaba, fedha na kadhalika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli, nashukuru Waziri amesema kwa maana utafiti wa kina tunauhitaji ambao ni zaidi ya 50% na maabara kubwa ya kisasa ambayo anakusudia ijengwe Dodoma. Akitimiza *Vision 2030* ili kuakisi hiyo kauli mbiu yake kwamba "Madini ni Maisha na Utajiri," nakubaliana naye, lakini ili tufike huko kwa maana madini ni maisha, madini ni utajiri, namwomba Mheshimiwa Waziri wangu, nimesema eneo kama lile la Mpanda, leo mwananchi akichimba dhahabu yake kinachomsumbua sasa hivi ni *how to process*. Inafika mahali mtu mwingine madini, mfano dhahabu, fedha, shaba inaonekana kama ni tatizo, yaani tatizo kuwa na jiwe moja kuua ndege watatu, *it's not a problem.* Suala hapo watusaidie ifike sehemu mwananchi huyo wa Mpanda asione madini yake kama ni tatizo kwa sababu tu ya kushindwa kuya-*process*. Ichukuliwe hiyo kwamba ni fursa na ni neema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoke hapo.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa muda wako umeisha, kengele ya pili imelia.

**MHE. SEBASTIAN S. KAPUFI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Sebastian Kapufi. Nilimtaja Mheshimiwa Salome Makamba.

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Niungane kabisa na wachangiaji wengine kuunga mkono hoja hii ya Wizara ya Madini. Pia, nimpongeze kaka yangu

Mavunde kwa kuaminiwa kukaa katika kiti hicho, anatosha na ameshafanya mapinduzi makubwa mpaka leo tumefika hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tarehe 31 Julai, 2017, Bunge hili lilifanya mapinduzi makubwa sana katika eneo la madini kwa kutunga sheria mbili, Sheria Na. 5 na Sheria Na. 6 ambazo zinahusisha utunzaji wa rasilimali hasa hizi za madini na rasilimali zote zilizopo Tanzania. Katika Sheria hizo moja kati ya jambo ambalo lilitiliwa mkazo ni kuhakikisha kwamba Watanzania wananufaika na rasilimali zao. Moja kati ya kifungu muhimu ambacho tulikijadili sana ndani ya Bunge hili kilikuwa kinasisitiza kwamba wawekezaji wote wakubwa katika maeneo ya migodi wahakikishe Tanzania inapata *share* au hisa kwa 16%. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kupata huko hisa kwa 16% maana yake ni kwamba Watanzania tungeweza kupata faida inayotokana na uzalishaji wa migodi hii mikubwa kwa 16%, sehemu ya faida ya migodi hiyo. Mpaka leo tunavyozungumza ni Mgodi mmoja tu wa Barrick ambao unatoa faida *(dividend)* ya 16% kwa Taifa la Tanzania. Tunayo migodi mingi kwa sasa hivi inakadiriwa tunakaribia kufikisha migodi 15 ambayo mingine ndiyo inaanza, mingine inafanya kazi. Huu Mgodi mmoja wa Barrick pekee yake ulitoa zaidi ya shilingi bilioni 100 kwa ule mwaka wa kwanza tu ambao tulitunga sheria. Walivyoenda kufanya mahesabu yao ya mwaka tulipata zaidi ya shilingi bilioni 100. Nini kinachoikwamisha Serikali kutufanya sisi tuweze kuongeza pato la Taifa? Ningetamani sana kujua wamefikia wapi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mgodi wa *Anglo Gold Ashanti (GGN)* wanapata faida nyingi sana, ndiyo mlipakodi mkubwa sana kwenye nchi hii katika migodi yote tuliyonayo, lakini, *as we are speaking,* bado wapo kwenye mazungumzo ambayo sheria iko wazi imeweka *deadlines*, imeweka ukomo wa mazungumzo. Muda umeshapita bado wapo kwenye mazungumzo hakuna *dividend* tunayoipata, hawa watu wanaendelea ku-*realise profit*, tumekwama wapi? Ningetamani nipate majibu ya Serikali kuhusiana na jambo hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri amezungumza hapa kuhusu wachimbaji wadogo lakini na Wabunge wenzangu wengi wamezungumza kuhusu wachimbaji wadogo. Tumekuwa tunapata ahadi nyingi sana, wanasema mara wanawawezesha mikopo, mara wanawapelekea vifaa. Mheshimiwa Waziri, hawa watu wanafanya kazi kwenye mazingira magumu. Hii mikopo wanaowapeleka kuchukua; kwanza, wanajiunga kikundi, wanaenda kuchukua mkopo, dhamana ni nyumba zao binafsi. Kile kikundi ni kikundi ambacho kinatakiwa kitambulike kisheria, mali zake ndizo zitumike kama dhamana na wakishindwa kurejesha mali hizo ndizo zikamatwe. Wanachukuliwa nyumba zao, familia zao zinateseka, ni nini mkakati wa Serikali hii ya Awamu ya Sita, kuhakikisha kwamba vikundi vya wachimbaji wadogo vinawezeshwa mikopo, vinawezeshwa vifaa, vinawezeshwa rasilimali na vinalindwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hivi kwa sababu hawa watu hawana mitaji, hawana vifaa, wameondolewa kwenye maeneo ambayo yana-*potential* wamepelekwa pembeni kwenye maeneo ambayo hayana mali, wanaona maisha ni magumu hawawezi kuchimba wanahitaji ma-*compressor,* na vitu vingine. Ndiyo maana hawa watu, unaona wanaenda kufikia hatua ya kuuza leseni zao kwa wachimbaji wa nje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa wameanza kuuza, kwa sababu mwisho wa siku binadamu anaishi kwenye *nature,* ukimbana huku anatokea huku. Wanaona bora waanze kuuza leseni, sasa hivi Wizara imekuwa kama askari, wameenda kuleta sheria hapa wanasema ili kuuza hiyo leseni kwa mchimbaji wa nje au wa kigeni inabidi uje hapa upitishe muhtasari, sijui Afisa Madini asaini. Mheshimiwa Waziri, hasaidii anaongeza ukiritimba na mianya ya rushwa ambayo itafanya sekta hii izidi kuwa ngumu kama sekta zingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri jambo moja, wachimbaji wapo, changamoto wanazozipata zinajulikana. Tukae chini, wachimbaji wadogo na Serikali kujua changamoto ni nini, zinaweza kutatuliwa vipi, huwezi kunizuia mimi kuuza leseni yangu. Hii nchi ni nchi huru, ukiniwekea ukiritimba nitapinga tu Mahakamani, kwa sababu, kuuza leseni ni haki ya mtu. Ni kama

ambavyo mtu anaamua kuuza nyumba yake, ni mali yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Waziri akisema anatunga sheria ya kumkataza, ni kweli sheria itakuwepo kwenye makaratasi, lakini utekelezaji wake utatengeneza mwanya wa kumpa fedha ya kutosha Afisa Madini na kuwapa fedha watu wa Tume. Huwezi kuzuia maji kwa kuziba kwa mkono, unayatengenezea mkondo ili mwisho wa siku uzuie mafuriko. Kwenye hili nashauri kabla Mheshimiwa Waziri kuja na hizo kanuni zake za namna ya kuweza kuuza hizi *PML,* alete kwetu sisi wachimbaji. Sisi wachimbaji ndiyo tunajua matatizo yetu, tuweze kumshauri namna ya kukabiliana na hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utatuzi wa migogoro, kaka yangu Mavunde ni Wakili mzuri sana, naamini ana uwezo mkubwa sana wa kutatua migogoro ya wachimbaji hasa wachimbaji wazawa na ameanza kulionyesha hilo kule kwetu Kahama. Kule Arusha nimeletewa barua hapa kuna mgogoro mkubwa sana kwa ndugu yetu huyu Ole Laizer na mwenzake anaitwa Franone, wana mgogoro mkubwa na humu kuna shutuma nzito sana, kuna shutuma za rushwa na shutuma za kugushi nyaraka. Huyu jamaa amechangia Serikali zaidi ya shilingi milioni 800 na tulimshangilia hapa ameokota mawe, amefanya nini, lakini *documents* zinakuwa *forged* kwenye Ofisi za Madini, naomba Mheshimiwa Waziri, atatue mgogoro huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, huyu ndugu yetu amefika mpaka kwa Waziri Mkuu, Wabunge kadhaa humu tumeletewa barua analalamika. Hili liko ndani ya uwezo wa Mheshimiwa Waziri, atatue huu mgogoro kama kuna Wawekezaji wawili na bahati nzuri wote ni wazawa na leo nimesikia wametangazwa hapa. Mgogoro utatuliwe, hawa wawekezaji wajengewe uwezo, tupate mabilionea na matrilionea kwenye nchi hii kwa sababu hakuna mtu anayependa umaskini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho, nataka niongelee kidogo kwa wananchi wanaoishi kwenye maeneo ya wawekezaji wa migodi. Hawa ndugu zangu kwenye migodi karibu Tanzania nzima wanaitwa *intruders* au wavamizi wa migodi, lakini nataka

tutafakari kidogo hapa. Migodi mingi mikubwa ina *fence* ya waya, ina ukuta, ina askari wale *Private Security* wa mgodi, ina mbwa, ina sungusungu, ina Askari wa Tanzania (Askari Polisi). Hivi huyu *intruder* mmoja anawezaje kwenda kuweka ngazi akavuka hizo *levels of security* mpaka akaingia ndani ya mgodi kwenda kuiba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hawa vijana wanaoitwa *intruder* wanaingia ndani, wanakwenda kuiba mle ndani kama wanavyoshutumiwa wakitoka nje wanapigwa risasi na askari wanauawa. Ile mali waliyoiba mle ndani inachukuliwa na hao *levels of security* niliotoka kuwaeleza hapa. Ndiyo maana leo ukienda Bulyanhulu matajiri wengi ni sehemu ya mfumo wa usalama wa hiyo migodi. Ukienda Tarime matajiri wengi waliojenga ma-*guest* na maghorofa siyo wachimbaji wadogo, ni watumishi wa hiyo migodi, ni askari wetu wanaofanya kazi kwenye hiyo migodi, ni wale ambao wanahusika na usalama wa hiyo migodi na watu wanapigwa risasi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mtu mmoja kule Tarime alikuwa anamwambia Mheshimiwa Matiko hapa amepigwa risasi nyuma. Kiusalama mtu akiwa anakimbia huwezi kumpiga risasi ya kichwani nyuma, utapiga kwenye miguu. Kwa hiyo, nataka niseme hivi sisi Watanzania kazi yetu ni kulinda Watanzania wenzetu, hawa watu wametolewa kwenye maeneo yao ya migodi ambayo walizoea kufanya kazi ya uchimbaji. Niseme tu mchimbaji huwezi kumpeleka kulima mpunga au mkulima wa mpunga huwezi kumpeleka kuvua samaki. Kama wamewatoa kwenye maeneo yao kupisha uwekezaji, wawatafutie maeneo ya uchimbaji waweze kuchimba, kuwekeza na kuishi maisha yao ya kiutamaduni walioyazoea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Salome, ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge huyo ndio mchangiaji wa mwisho kwa mchana huu au kwa asubuhi hii. Nina matangazo machache kabla kusitisha Shughuli za Bunge.

Kwanza, tuna tangazo la wageni ambao wameingia tena muda huu. Kuna wageni ambao wapo kwenye Jukwaa la Mheshimiwa Spika, ambao ni wageni wa Mheshimiwa Antony Mavunde ambaye ni Waziri wa Madini: Tuna Ndugu Haroon Kinega ambaye ni Mtendaji Mkuu wa Shirikisho la Wachimbaji Wadogo wa Madini Tanzania; Ndugu Simon Shayo, Makamu wa Rais, *Anglo Gold Africa*; Ndugu Baraka Ezekiel, Mkurugenzi Mkuu, *Busolwa Mining;* na Ndugu Heneriko Yohana Maganga, Mkurugenzi wa *Achimwene Business Group*. Karibuni. *(Makofi)*

Wageni wengine ni wageni wa Waheshimiwa Wabunge, tuna wageni 54 wa Mheshimiwa Rose Busiga, Wajumbe wa UWT kutoka Jimbo la Busanda, Mkoa wa Geita. Ahsanteni na karibuni sana. *(Makofi)*

Kuna wageni watatu wa Mheshimiwa Fatma Toufiq, ambao ni Watumishi wa Taasisi ya *Al-Khairiya Islamic Foundation* kutoka Jijini Dar es Salaam. Karibuni sana wageni wetu. *(Makofi)*

Tuna wageni wengine wa Mheshimiwa Antony Peter Mavunde, ambao ni Kampuni za Madini zenye Ubia na Serikali: Tuna *Twiga Minerals Corporation Limited*, tuna *Tembo Nickel Corporation Limited*, tuna *Nyati Minerals Sands Limited* na tuna *Faru Graphite Corporation*. Nafikiri wote walikuwepo hawa, lakini bora niwataje kwa sababu wasije wakaonekana hawajatajwa. Kuna *Mamba Mineral Corporation Limited*, kuna *Sotta Mining Corporation*, kuna *Duma TanzGraphite Limited* na kuna *Williamson Diamond*. *(Makofi)*

Pia tuna Kampuni za Uchimbaji: kuna *Buckreef Gold Company Limited*, tuna *Shanta Mining Company Limited*, tuna *Lindi Jumbo Limited*, tuna *Mantra Company Limited*, tuna *Jitegemee Holding Company Limited*, tuna *Dangote Company*. (Makofi)

Tuna Kampuni za utoaji huduma pia za madini ambazo ni *East African Suppliers*, tuna *Magari Company Limited*, *Tanzania Youth Mining* na *UNIVESCO Limited.* Karibu sana Kampuni zetu hizo. *(Makofi)*

Pia tuna *Chamber of Minerals* au *Miners* na tuna Chama cha Wanafunzi wa Madini Tanzania. Wengine ni Shirikisho la Vyama vya Wachimbaji Madini Tanzania. Karibuni sana wageni wetu. *(Makofi)*

Wageni wetu wote mliopo karibuni kwa ujumla wake. Kabla ya kusitisha shughuli za Bunge naomba niwataje wachangiaji ambao watachangia jioni ya leo. Tutaanza na Mheshimiwa Juliana Masaburi, Mheshimiwa Iddi Kassim Iddi, Mheshimiwa Hassan Zidadu, Mheshimiwa Masache Njelu na Mheshimiwa Godwin Emmanuel Kunambi.

Baada ya matangazo hayo, nasitisha Shughuli za Bunge hadi saa kumi na moja kamili jioni.

*(Saa 7.03 Mchana Bunge lilisitishwa hadi Saa 11.00 Jioni)*

*(Saa 11.00 Jioni Bunge Lilirudia)*

*Hapa Naibu Spika (Mhe. Mussa A. Zungu) Alikalia Kiti*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tukae.

Katibu.

**NDG. YONA KIRUMBI – KATIBU MEZANI:**

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Madini kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa namwita Mheshimiwa Juliana Masaburi, wajiandae Mheshimiwa Iddi Kassim Iddi na Mheshimiwa Hassan Zidadu.

**MHE. JULIANA D. MASABURI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuchangia bajeti ya Wizara ya Madini.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa kibali cha kusimama hapa leo hii, kipekee nampongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mama yetu Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kuipigania nchi yetu kwa kuleta maendeleo na kukuza diplomasia ya uchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu, nimpongeze kaka yangu Mheshimiwa Mavunde kusema ukweli toka mwaka jana mwezi Agosti ameteuliwa watu wengi ikiwemo mimi nilijiuliza kwamba ataweza huyu jamani, lakini umeni-*prove wrong,* ninazo sababu za kusema hivi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa toka Waziri ameteuliwa kwenye Wizara hii amekuja na ubunifu wa hali ya juu. Kiongozi yeyote mzuri anapimwa kwa kiongozi aliyemtangulia, wote tunafahamu Wizara hii kabla Mheshimiwa Antony Mavunde hajateuliwa aliyekuwa Mheshimiwa Waziri wa Wizara hii alikuwa ni kaka yetu Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu, Mheshimiwa Dotto Mashaka Biteko amefanya mapinduzi makubwa kwenye sekta hii ya madini, mapinduzi makubwa sana, lakini alivyoteuliwa kaka yangu Mheshimiwa Antony Mavunde na yeye kaendeleza ubunifu mkubwa na kaitendea haki Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikienda moja kwa moja kwenye kuchangia na kushauri, lakini sana sana leo nitampongeza sana. Kwanza nampongeza kwa ujasiri mkubwa alioufanya wa kufuta leseni zote za maeneo ambayo hayaendelezwi, amefanya kitendo cha kishujaa, amefanya kitendo cha kijasiri na naomba niendelee kumtia moyo asiishie hapo, maana kuna watu au kuna wachimbaji au kuna wafanyabiashara walikuwa wanachukua haya maeneo wanayakatia leseni halafu wanayaweka mfukoni hawayafanyii kitu chochote.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza wanasababisha nchi kukosa mapato ambayo yanatokana na sekta ya uchimbaji, lakini

ni wao wao walikuwa wanasababisha migogoro baina ya wakulima na wachimbaji na wafugaji pia. Kwa hiyo nakupongeza sana kaka yangu na namtia moyo, aendelee kwa nguvu zote kulisimamia hili. Kwanza ni kitu ambacho kitamwachia *legacy* kubwa sana, kila kiongozi ana maono yake, lakini kwa hili maono yake yataacha alama kubwa kwenye hii Wizara. Kufuta hizi leseni zitampa mwaya wa kuzikagua upya na kupanga haya maeneo vizuri zaidi, kwa hiyo nampongeza kwa hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili, naipongeza tena Wizara kwa kuamua kujenga maabara mpya ya *GST*. Waheshimiwa Wabunge wote tunafahamu wachimbaji walikuwa wanasafirisha sampuli za madini kupeleka nje ya nchi, lakini sasa hivi kwa kujengwa hii maabara itawawezesha kupima hizi sampuli za madini hapa hapa kwenye maabara yetu. Kwa hiyo, nampongeza sana kaka yangu Mheshimiwa Mavunde.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la tatu, nimpongeze kwa huu uamuzi wa Wizara kununua helikopta inayofungwa vifaa vya kupima madini kwenye ardhi, ile helikopta nilivyoona alivyoongea kwamba wanaifunga vifaa ambavyo vitakuwa vinapima chini sasa na inatoa ripoti sahihi eneo fulani lina madini, eneo fulani halina, hii itasaidia hata wachimbaji kutochimba chimba tu hovyo kusababisha uharibifu wa mazingira, hii itawapa tija sana Wizara kujua nini wanafanya, wapi wanatafuta na muda gani watafute hayo madini na wayapate. Kwa hiyo, haya ni mapinduzi makubwa sana ambayo wanayafanya ndani ya Wizara hii ya Madini na ni mapinduzi makubwa sana ambayo yanafanywa na Serikali ya Awamu ya Sita.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja na nampongeza na namtakia kila la kheri. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Iddi Kassim Iddi, wajiandae Mheshimiwa Zidadu na Mheshimiwa Njelu Kasaka.

**MHE. IDDI K. IDDI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipatia fursa hii ya kuchangia bajeti ya Waziri, kaka yangu Mheshimiwa Antony Mavunde.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa nichukue fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kuwa na afya njema na leo kushiriki kutoa mchango wangu kwenye hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri. Pia nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa ambayo anaendelea kuifanya pia kwa kutuletea mradi mmoja mkubwa sana kwenye Kata ya Segese ambapo mradi unahusisha *NEMC* na watu wa madini ambapo wataenda kujenga Tawi la Chuo Kikuu pale Segese, Kijiji cha Bumva ambapo itaenda kuwa chachu ya kusaidia wachimbaji wadogo wadogo kwenye eneo lile. Nimpongeze sana kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Msalala, tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais lakini tunampongeza sana Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue fursa hii kumpongeza pia Mheshimiwa Waziri wa Madini, kaka yangu Mheshimiwa Antony anafanya kazi kubwa sana na katika sekta hii upole wake, unyenyekevu wake, namna ya kusikiliza wananchi na kutatua kero zake ameonesha umahiri mkubwa sana kiasi cha kuonesha kwamba, sisi na wananchi wote kwa ujumla na wachimbaji wote nchini wanamuunga mkono.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo nataka nichangie mambo kadha wa kadha. Kabla sijasahau niseme kwamba naunga mkono hoja ya Kamati pamoja na bajeti hii kwa asilimia mia moja. Nataka kwanza kabisa nimwombe Mheshimiwa Waziri, naona jitihada kubwa ambazo anaendelea kuzifanya pamoja na wataalam wake kwa namna gani wakusanye mapato ambapo tunaona takribani trilioni moja anaenda kukusanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, niombe jambo moja ili bajeti hii ambayo leo tunaipitisha, tunafahamu kwamba wapo wasaidizi wake kwenye Mikoa kule ma-*RMO* na watendaji mbalimbali kwenye maeneo yale ndiyo wanaenda kutoa ushirikiano mkubwa katika kuhakikisha kwamba wanakusanya maduhuli ya kutosha kwenye maeneo haya. Sasa mishahara na maslahi ya watu hawa ambao wanaenda kukusanya matrilioni ya fedha, bado ni changamoto kwa watendaji huko mikoani.

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue mfano, *RMO* wa Kahama anafanya kazi kubwa sana toka amekuja anapambana huku na huku kutatua migogoro, anapambana kukusanya maduhuli, lakini sasa ukija kwenye maslahi hapo ndipo tatizo linaanzia, kwa hiyo niombe tutoe motisha na twende tukawaongezee mishahara watendaji hawa ambao tumewapa jukumu kubwa. Dawa kubwa ya kuhakikisha kwamba wanaendelea kuongeza kasi kwenye ukusanyaji wa maduhuli kwenye maeneo haya ni kuwaongezea mishahara watendaji hawa kwenye maeneo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili, nizungumzie suala zima la *CSR*. *CSR* kwanza kabisa niwapongeze wawekezaji wa Mgodi wa Bulyanhulu kwa kuonesha ushirikiano wao wa kuendelea kutoa fedha za miradi ya *CSR* ambayo itatekelezwa kwenye jamii hiyo na nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri kwa nia njema ambayo amekuja nayo ya kwenda kupitia upya kanuni za usimamizi wa fedha za *CSR*.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kabisa baada ya kuwa wametoa kanuni mpya sasa hivi tunaona miradi ya *CSR* inacheleweshwa na ukitafuta sababu ya kwa nini miradi hii ya *CSR* inacheleweshwa unakuta changamoto kubwa ipo kwetu Watanzania, tunakosa uzalendo, tunakosa namna ya kuona kwamba wananchi wanastahili miradi ile, fedha inayotolewa na wahisani, iweze kukamilika kwa wakati na miradi ile iweze kuwanufaisha wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, natoa mfano kuna fedha tulitenga bajeti ya mwaka huu wa fedha ya *CSR*, fedha ambayo tulikuwa tukijenga darasa moja kiasi cha shilingi milioni 26. Leo hii wananchi na viongozi wamegoma kusaini makubaliano hayo ambayo yupo Mkurugenzi na timu yake wameenda kuleta *proposal* ya kujenga darasa moja milioni 43, badala ya milioni 26 kama ilivyotolewa na watu wa TAMISEMI.

Mheshimiwa Naibu Spika, utaona ni namna gani kutokana na hawa watumishi ambao hawana uzalendo, fedha hizi leo zimekaa, ukiangalia wahisani wapo tayari kutoa hela muda wowote, lakini sisi wenyewe tumeendelea kuvutana,

tumeendelea kusigana na fedha zile haziwezi kwenda kutimiza miradi hii kwa wakati. Hii inaendelea kuwaumiza wananchi. Niombe sana Mheshimiwa Waziri akitoka hapa basi aende akaharakishe mchakato huo na ikiwezekana watushirikishe.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza wawashirikishe Madiwani wa kwenye maeneo hayo, lakini pia watushirikishe na Waheshimiwa Wabunge tuweze kushiriki kwenye maeneo hayo katika kuhakikisha kwamba tunasimamia fedha hizi ziweze kutekelezwa kwa wakati. Ni aibu kubwa mno wahisani wanatoa fedha halafu tunaopatiwa fedha hatutaki fedha hizo ziende kutumika. Leo hii wananchi wamegoma kusaini utekelezaji wa miradi mpaka lini itafanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia *North* Mara walikaa zaidi ya miaka miwili hawajaitumia fedha ile, kwa hiyo niombe sana Mheshimiwa Waziri kwenye suala zima la *CSR* aende haraka akalipitie upya atushirikishe Waheshimiwa Wabunge wa maeneo hayo, awashirikishe Madiwani wa kwenye maeneo hayo ili fedha hizi ziweze kwenda huko zifanye kazi kwa uhakika.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nichangie kwenye suala zima la *GST* na *STAMICO*. Mheshimiwa Waziri kama alivyosema Profesa Muhongo nakubaliana naye kabisa, kwamba utafiti ndiyo injini na ndiyo dira ya wachimbaji wadogo wadogo. Tunapozungumzia mafanikio ya wachimbaji wadogo wadogo hatuwezi kuacha kuainisha kati ya *GST* na watu wa *STAMICO. GST* kazi yao ni nini? *GST* kazi yao ni kubaini uwepo wa miamba kwenye leseni ambazo wachimbaji wadogo wadogo wanapatiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa nampongeza sana kwa mkakati ambao Waziri amekuja nao wa kuhakikisha kwamba eneo zima linaenda kupimwa na taarifa zote zitakusanywa ili wachimbaji wadogo wadogo waweze kupatiwa taarifa hizo. Sasa niendelee kumsisitiza Waziri kwamba, ili wachimbaji waende kunufaika ni muhimu sana taarifa hizi ziende zikafanyike haraka na wachimbaji wapatiwe taarifa hizi ili ziweze kuwasaidia kwenye uwekezaji, wachimbaji wengi wanafilisika kwa sababu ya kutokuwa na taarifa sahihi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimpongeze sana Waziri kwa hatua ambazo amechukua za kufuta leseni, ni hatua nzuri sana nampongeza na hapa niombe aendelee kutoa elimu kwa sababu kuna watu wengine mpaka sasa hawaelewi ni namna gani na ni leseni zipi amezifuta, inawezekana wakasema kwamba ni leseni zote, hapana, watoe elimu kwa wachimbaji tujue ni leseni za aina gani ambazo wamezifuta, siyo leseni zote ambazo zimefutwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo niseme kwamba suala zima la taarifa ni muhimu mno na nimwombe Mheshimiwa Waziri, kuna Migodi mikubwa kama *Barrick*, North Mara, maeneo mengi wameshayafanyia tafiti. Jimbo la Msalala kuna eneo la Segese, ukija mpaka eneo la Nyangarata na pale Bulyanhulu ni maeneo ambayo leseni hizi tayari wameziachia.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimwombe sana Mheshimiwa Waziri na wao wafanye kama sehemu ya *CSR,* wachague maeneo ambayo tayari wao wameshayafanyia tafiti ambayo wao hayawafai waende wakatuoneshe, watupe *data* za maeneo hayo, watengeneze vikundi na waweke mashimo kwenye maeneo yale ili wasaidie wachimbaji kwenda kuchimba kwenye maeneo yale iwe kama sehemu ya *CSR* kwenye maeneo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa hizi wanazo wamezikalia, wachimbaji wanaozunguka kwenye maeneo haya, kama alivyosema dada yangu Mheshimiwa Salome, hawa watu hawana shughuli nyingine ya kufanya tofauti na madini na nakubaliana naye. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, Mheshimiwa Iddi kengele ya pili hiyo.

**MHE. IDDI K. IDDI:** Mheshimiwa Naibu Spika, sijakuelewa hapo. *(Kicheko)*

**NAIBU SPIKA:** Kaa chini. Mheshimiwa Hassan Zidadu jiandae Mheshimiwa Kasaka. *(Kicheko)*

**MHE. HASSAN Z. KUNGU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja iliyopo mbele yetu kwa maana ya Wizara ya Madini. Kwanza kabisa niungane na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kumpongeza na kumshukuru Mheshimiwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa namna anavyomimina miradi kwenye majimbo yetu. Pili, nampongeza Mheshimiwa Waziri wa Madini pamoja na Mheshimiwa Naibu Waziri na Watendaji wote wa Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nijielekeze kwenye hoja nne; hoja ya kwanza ni hoja ya ofisi za madini. Ni jambo jema sana kwamba kila eneo lenye madini kuwe na ofisi za kuuzia madini, hili ni jambo zuri na ni jambo jema, lakini sasa kwa kule kwangu, Wilaya ya Tunduru tunayo masoko ya madini, tunayo masoko kwa sasa yapo mawili, Soko la *Generation* na Soko la *TUDECO*.

Mheshimiwa Naibu Spika, haya masoko yote tayari yana wanunuzi, wapo wanunuzi wa Ki-Sri Lanka, pia wapo wanunuzi wa Ki-Thailand. Sasa kuna soko jipya ambalo linajengwa, soko la tatu na kwa maana ya tasfiri ya Mkurugenzi lile soko likikamilika maana yake wale wote wa masoko mawili yale waondoke wanunuzi waende wakakae kwenye soko moja, jambo ambalo linazua mgogoro mkubwa sana kwenye wilaya yetu, kwa maana ya wale wanunuzi wa madini.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunao wanunuzi wengi sana Tunduru, sasa wao wanaomba ama wanataka kwenye yale masoko mawili ambayo wameanza kufanya kazi za ununuzi wa madini waendelee kubaki pale pale kwenye masoko yao na badala yake lile soko jipya linalojengwa sasa, kwa kuwa kuna wanunuzi wengi wanakuja wanahitaji kufanya shughuli za ununuzi wa madini Tunduru, basi waingie kwenye lile soko jipya.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Mheshimiwa Waziri alichukue hili kwa uzito wa aina yake, kwa sababu tayari limeshaanza kuleta sintofahamu katika mapato ya ndani ya Halmashauri, Tunduru tunategemea sana hawa wanunuzi. Kwa hiyo, twende tukawape *comfort,* wao wameridhia kukaa kwenye

yale masoko yao ya zamani, tusiwahamishe kwenda kuwapeleka kwenye soko jipya, wao wana wametoa sababu nyingi kwamba, masoko ya zamani yana vyumba vikubwa, lakini soko jipya vyumba vyake ni vidogo. Pia hata ukipiga hesabu kwa namna ya pesa wanazolipa kwa mwezi kwenye masoko haya ya zamani wanalipa pesa nyingi zaidi tofauti na lile soko jipya, watakapokwenda kulipa pale watakwenda kulipa pesa ndogo maana yake ni nini, maana yake ni kwamba tunakwenda kupunguza mapato ya halmashauri.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wangu katika hili nataka masoko yale yote matatu yatumike kwa pamoja Wa-Sri Lanka wawekwe kwenye soko lingine, Wa-Thailand wawe kwenye soko lingine na wengine waende kwenye soko lingine, hata ukitaka kuleta ushindani wa kiununuzi hawa wanunuzi wakiwa maeneo tofauti tofauti kunakuwa na ushindani mkubwa na wachimbaji wadogo wadogo watakwenda kunufaika kwa maana watakwenda kupata bei kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tofauti na wanunuzi wote ukiwaweka sehemu moja, wachimbaji tuna kawaida moja kwamba ukiingia ofisi moja halafu ukaonekana kwenye ofisi nyingine tafsiri yake bei utakayoipata kwenye ofisi ya kwanza, ofisi ya pili lazima ishushe bei kwa sababu tayari yule atakuwa ameshamwonesha mnunuzi mwingine. Ukienda kwenye ofisi ya yule mnunuzi ambapo hajui kama uliingia kwenye ofisi nyingine, maana yake atakuona wewe ni mchimbaji mpya na atakupa bei kubwa. Kwa hiyo, kugawanya ofisi zote tatu kama uwezekano huo upo, basi kwa Tunduru tunaomba Mheshimiwa Waziri atupe msaada huo, masoko yote matatu yafanye kazi badala ya kutumia soko moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja ya pili, ni suala la uchimbaji katika hifadhi. Kule kwetu eneo kubwa sana ni la hifadhi ya Selous. Ile hifadhi yote ina madini, lakini lakini ile hifadhi imekwenda mpaka karibu kwa jirani yangu Mheshimiwa Mhata na yeye kule anayo Hifadhi ya Lukwika – Lumesule, kwangu kuna Selous, lakini pia kuna Mtetesi kuna madini mengi sana na kulikuwa kuna kauli ya Mheshimiwa Rais ya kwamba watu

wafanye shughuli za uchimbaji wa madini yale bila kuathiri hifadhi zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri sasa najiuliza yale madini yapo kwenye hifadhi na wapo watu wanakwenda kuchimba kinyemela. Bahati mbaya sana wakikamatwa wanafungwa na wengine wanatozwa faini kubwa kweli kweli, wengine wamefungwa mpaka sasa na wengine wanapigwa risasi. Sasa yale madini kama yapo maana yake yangeweza kuchimbwa watu wangeuza tungeweza kuongeza pato la Taifa kupitia madini.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa haya madini yanakaa kwenye hifadhi mwisho wake ni nini, yanakaa kule ili iweje, kwa nini tusiyaondoe tukaongeza pato la Taifa. Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Waziri atapokuja ku-*wind up* hapa atueleze suala la madini ya kwenye hifadhi kutengeneza labda utaratibu maalum ambao watu wanaweza kupewa vibali maalum vya kwenda kuchimba bila kuathiri shughuli za uhifadhi, bila kuathiri wanyamapori. Twende tukachimbe kwa vibali maalum, tupate madini yale, tuuze, tupate pesa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ni suala la mikopo kwa wachimbaji wadogo. Hili jambo limekuwa likisemwa tu lakini ukifuatilia uhalisia watu wanaopata mikopo ile ya wachimbaji wadogo wadogo si wachimbaji wadogo wadogo, ni wachimbaji wakubwa na ni wachimbaji wa kati, lakini wale wachimbaji wadogo wadogo hawapati kabisa ile mikopo. Naomba hili nalo Waziri atakapokuja ku-*wind up* hapa aseme ni nini kifanyike ili wale walengwa waende wakanufaike na mikopo hii, kwa sababu ukiangalia mikopo yote iliyotoka inaitwa mikopo ya wachimbaji wadogo wadogo, lakini waliopata mikopo hii si wachimbaji wadogo wadogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunao wachimbaji wadogo wadogo wengi kule hatujawahi kuona hata kikundi kimoja cha wachimbaji wadogo wadogo ambao wamepata mikopo hii. Ukifuatilia vizuri wanaopata mikopo hii ni wale watu ambao tayari wana unafuu, tayari wana kila kitu, ndiyo wanaokwenda kupewa hii mikopo. Kwa hiyo, niombe sana kwenye hili lichunguzwe ama

lifuatiliwe kwa umakini, wachimbaji wale wadogo wadogo waende wakapate ile mikopo kama ilivyotarajiwa ama ilivyoelekezwa na hatimaye tuweze kuwasaidia wachimbaji hawa wadogo wadogo ili waweze kuinuka kiuchumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la nne na la mwisho kabisa, ni suala la uchenjuaji wa madini ya dhahabu. Mwaka jana niliwahi kuchangia hapa juu ya suala la uchenjuaji wa madini. Tumeambiwa, ama mwaka jana niliwahi kusema hapa kwamba kwa sasa kuna utaratibu ambao tunakwenda kuzuia zebaki ama *mercury* na badala yake tutumie sumu aina ya *cyanide*.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala hili linakwenda kuwadidimiza wachimbaji wadogo wadogo, hatuendi kuwasaidia wachimbaji wadogo wadogo. Maana yangu ni nini? Maana yangu ni kwamba, wachimbaji wadogo wadogo kila siku wanahemea kupitia *mercury* na wanakamatisha ama wanachenjua dhahabu kupitia *mercury*. Kila siku wale wanakwenda kuchenjua yale marudio ama *makanyelo,* ule mchanga wa dhahabu hauwezi kufika hata roba moja, hauwezi kufika hata kilo mia moja. Wakati mwingine mtu anachenjua kwa siku kilo 20, kilo 30 anapata *point* zake mbili tatu akienda kuuza anapata ugali wake wa kila siku. Kumkataza mtu huyu kutumia *mercury* na badala yake ukamwambia atumie *cyanide* ni kana kwamba umemwambia aache kabisa uchenjuaji wa madini ya dhahabu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nini nasema hivyo? Ili uweze kutumia *mercury*…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Zidadu kengele ya pili hiyo.

**MHE. HASSAN Z. KUNGU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kasaka, jiandae Mheshimiwa Kunambi.

**MHE. MASACHE N. KASAKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kupata nafasi ya kuchangia Wizara hii ya Madini, Wizara ambayo tunategemea muda mfupi ujao kuwa inaongoza kutuletea fedha za kigeni ndani ya hii nchi yetu, lakini pia kuongoza katika kuchangia kwenye pato la Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri pamoja na timu yake kwa kazi kubwa wanayoifanya, lakini pia kwa kuja na *slogan* nzuri (madini ni maisha, madini ni utajiri). Hakika *slogan* ni nzuri sana. Tunaomba *slogan* hii iende kwa vitendo ili wananchi wetu hawa waweze kuona sasa wanaweza kuupata utajiri. Wameanza vizuri, tumeona kupitia bajeti hii namna ambavyo wameanza kuelekeza nguvu kubwa sana kwenye utafiti.

Mheshimiwa Naibu Spika, bila kufanya utafiti hatutaweza kuwakwamua wachimbaji wadogo wa nchi hii. Bila kufanya utafiti hatutaweza kuhakikisha kwamba hii sekta na yenyewe inakua na inaongoza kwenye pato la Taifa. Nimpongeze Mheshimiwa Waziri kwenye hili na naomba haya ambayo wameeleza hapa yaende kwenye vitendo ili wananchi wetu waweze kunufaika na wao waone kwamba hii sekta inaweza kuwasaidia vizuri zaidi. Kwenye hili hapa tumeweza kuona kwenye taarifa ya Waziri aliposema, namna ambavyo wameweza kurusha ndege nyuki ambazo zimeweza kufanya utafiti kwenye maeneo kadhaa, lakini pia namna wanavyowekeza kwenye utafiti na wameweza kuomba fedha ya kununua ndege ili kuhakikisha utafiti unafanyika vizuri zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme tukiwekeza vizuri kwenye utafiti tutaweza kuwasaidia sana wachimbaji wadogo ambao ndio wapo wengi sana kwenye nchi hii, ndio wataweza kuinuka kiuchumi na tutaweza kupata fedha nyingi zaidi. Tumeona kwenye mpango hapa wameweza kueleza mpango wa *MBT*. Ni mpango mzuri sana kwa namna ambavyo mpango huu utekelezaji wake utaweza kuwasaidia wachimbaji wadogo. Mimi natokea Wilaya ya Chunya ambapo kule tuna wachimbaji wadogo wengi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kupitia mpango huu tuone namna nzuri na bora zaidi kwa maeneo ambayo yatakuwa yamefanyiwa utafiti, hawa wachimbaji wadogo wapewe taarifa zake lakini pia wapelekewe miundombinu. Tunapowekeza miundombinu na kuwapelekea hawa wachimbaji wadogo kwa maana kwamba kuwe kuna barabara nzuri kwenda kwenye maeneo hayo, kuwe kuna miundombinu ya umeme, kuwe kuna miundombinu ya maji na mengineyo. Tukiweza kufanikisha hayo hata huu Mradi wa *MBT* utaweza kutoa matokeo mazuri na chanya na kila mtu anaweza kusaidika.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili hapo kwenye huo Mradi wa *MBT* ni namna ya kuweza kuwapata hao wachimbaji wadogo wadogo. Hili lazima twende kwa uangalifu na umakini mkubwa sana ili kuwafikia walengwa wenyewe. Mtu ambaye hana mtaji, hana karasha, hana kitendea kazi, ndiyo ambao twende kuwakusanya pamoja, kuwe utaratibu mzuri zaidi. Tukiweza kuwafikia hawa wataweza kukua mmoja mmoja na baadaye na hawa wataweza kusimama na kwenda kwenye maeneo mengine na wataweza kufanya uzalishaji mzuri zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumepata taarifa wiki hii hapa na Mheshimiwa Waziri alitupa taarifa hapa ya namna ambavyo aliweza kufuta leseni za wachimbaji wakubwa na wa kati ambazo zimekaa muda mrefu hazijaendelezwa. Naomba sana hii elimu iweze kwenda vizuri sana kwa wachimbaji wetu nchi nzima. Wengi wamepata hofu na mashaka kwamba, je, wameanza kufuta huku na sisi wenye maombi ya leseni ndogo ndogo tutaenda kufutiwa maombi yetu? Kwa hiyo elimu hii ikiweza kwenda vizuri kwenye maeneo haya, imani yangu watu wataweza kujua nini ambacho Serikali ina nia na nini ambacho inataka tufanye.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili kwenye maeneo haya ambayo Mheshimiwa Waziri ameyafuta, tuone namna iliyokuwa nzuri na bora. Suala sio kuyafuta maeneo, tunayafuta tunayafanyia nini? Tumeyafuta maeneo yamerudi Serikalini. Niombe sasa kupitia Serikali kupitia Taasisi ya *GST,* twende tukayafanyie utafiti haya maeneo. Tukifanya utafiti wa kina tukajua miamba ikoje pale tutaweza kurudi kwenda kuyagawa

hayo maeneo. Tukiyagawa vizuri tuyatangaze kwa wananchi wetu ili wachimbaji wale waje wayaombe na kufanya uchimbaji wenye tija.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunapofanya utafiti, taarifa nyingi tunakaa nazo ofisini, lakini tukifanya utafiti na taarifa zile tukawapatia wale wachimbaji hasa wale wachimbaji wadogo, wataweza sasa kutumia zile tafiti kuweza kuzalisha vizuri. Pia, wataweza kuwa na tija na kuhakikisha kwamba wanachangia kwenye pato la Taifa pamoja na kuhakikisha kwamba ile *vision* ya 2030 inakamilika kama yalivyo maono ya Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kupitia hayo maeneo tunaweza tukaona namna iliyokuwa bora, ule Mradi wa MBT tukaanzia kwenye maeneo hayo ambayo Serikali imeyafuta na tukaanza nayo. Tukianza nayo hayo kwa sababu tayari yatakuwa yako chini ya Serikali na tumeshayafanyia utafiti, tutaweza kunufaika vizuri zaidi na wananchi wetu wataweza kunufaika.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na mambo kwenda hivi na Wizara kuhakikisha kwamba imeweka utaratibu mzuri, lakini bado maeneo mengi ambako tuna uzalishaji mkubwa, huduma nyingi za kimiundombinu hazijafika. Maeneo mengi uchimbaji unafanyika lakini miundombinu yake ni mibaya. Barabara zinazoenda huko ni mbaya, watu huko hawana umeme, watu hawana maji na ndiyo kuna uzalishaji mkubwa, tunategemea mapato makubwa sana kutoka huko.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimtolee mfano Mheshimiwa Waziri, maeneo kama ya Itumba anayafahamu, maeneo ya Mlimanjiwa, maeneo ya Shoga na mengineko uzalishaji mkubwa sana unafanyika huko lakini miundombinu ya barabara ni mibovu sana, miundombinu ya mawasiliano ni migumu, miundombinu ya maji hakuna na umeme haujawafikia wachimbaji wetu. Niombe; tunazalisha kikubwa, tunaleta pato kubwa sana kwenye Serikali yetu kwenye bajeti, basi hii fedha iweze kurudi. Kule ambako unamkamua ng’ombe maziwa ndiyo umpelekea pia nyasi za kutosha ili aweze kunenepa. Tupeleke miundombinu hiyo huko ili wale wachimbaji wetu waweze kuzalisha dhahabu za kutosha na madini mengine na sisi tutaweza kunufaika zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna jambo ambalo Wizara inafanya hasa inapopata wawekezaji wakubwa. Namna ambavyo inawatoa wawekezaji wadogo ambao wengine tumezoea kuwaita wagunduzi na kuwahamishia maeneo mengine ili kupisha uwekezaji mkubwa. Serikali nia yake ni njema lakini namna ambavyo tunawahamisha hawa wawekezaji wadogo wadogo au wachimbaji wadogo wadogo kwenda kuwapeleka katika maeneo mengine, wakati mwingine tunakuwa hatuwatendei haki, kwa sababu leo unawatoa wachimbaji wadogo ambao wamekuwepo pale kwa muda mrefu, unawapeleka kwenye maeneo mengine ambako bado miundombinu yake, si sawa. Unawapeleka huko hata barabara hakuna, umeme hakuna, maji hakuna. Tuone namna ambavyo tunapowatoa hawa tunapowapeleka huko tuweke miundombinu mizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nina wachimbaji wangu pale Makongolosi kwenye maeneo ya kule Gepu. Serikali imetwaa yale maeneo na kuweza kuyatangaza tuweze kupata wawekezaji wakubwa. Tunapowatoa wale wachimbaji wadogo kutoka maeneo ya Gepu kuwapeleka katika maeneo mengine ambayo Serikali imewapangia, tuhakikishe miundombinu ya maeneo hayo ni rafiki ili kuwasaidia waweze kuchimba vizuri; bila hivyo tutawahamisha na watakwenda kupata hasara na uchimbaji wao hautaweza kuwanufaisha vizuri zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Kunambi, wajiandae Mheshimiwa Tumaini na Mheshimiwa Kanyasu.

**MHE. GODWIN E. KUNAMBI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema. Nieleze tu kwamba katika Sekta hii ya Madini, tangu nimeingia Bungeni huu ni mchango wangu wa kwanza kwenye sekta hii muhimu kwa Taifa letu na hivyo basi, nitauita *episode one* maana michango yangu yote huwa inakwenda kwa *episodes.* Sasa kwa kuwa huu ni mchango kwa awamu ya kwanza nauita *episode one*.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunafahamu na nitakuwa mchoyo wa fadhila kama sijamshukuru Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan. Kwa kweli ameiinua sana sekta hii muhimu ya madini. Pia nimpongeze kaka yangu Mheshimiwa Mavunde, *young leader, energetic and vibrant*. Anafanya vizuri sana na Waingereza wanasema *all starts well, ends well, brother* atamaliza vizuri; atusikilize tuko tayari kumsaidia. Tunafahamu sekta yake ni nyeti sana na ni mzigo mkubwa sana kwake, lakini huko nyuma tulizoea kusema mzigo mkubwa mpe Mnyamwezi, lakini tunafahamu hata Mgogo anaweza. Ndiyo maana Mheshimiwa Rais akamwamini, akalie hicho kiti vizuri kiasi kwamba atekeleze majukumu yake ili aache *legacy*. Ni kijana mwenzetu tunafahamu atatuachia historia na sisi wengine tutajifunza huko mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba nijielekeze, lakini pia nisisahau kumpongeza Katibu Mkuu wake Mahimbali kama Katibu Mkuu wa Wizara. Ni mzalendo, anafanya kazi nzuri na wanashirikiana vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa niende kwenye mchango wangu. Nampongeza kwa sababu, wote ni mashahidi miezi miwili iliyopita tumesikia kazi aliyoifanya. Amefuta leseni zaidi ya 2,875 kwa muda mfupi tu. Awamu ya kwanza alifuta leseni 2,648 na awamu ya pili 227, ukijumlisha unapata takwimu ya leseni ya jumla ya 2,875, ni jambo la kumpongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja yangu hapa, sijamwona Mheshimiwa Mavunde ninayemjua mie katika hili. Mheshimiwa Mavunde ninayemjua mie nikiwa Mkurugenzi wa Jiji la Dodoma, Mbunge wangu sijamwona katika hili. Nataka nimwone, nafahamu uwezo wake na ujasiri wake. Amechukua hatua kwa kufuta leseni; kufuta leseni ni hatua moja, hawa watendaji wa Tume amechukua hatua gani? Nataka kumwona Mheshimiwa Mavunde kwenye eneo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama kuna leseni zinapitishwa hazina vigezo halafu Mtendaji Mkuu wa Tume yupo, wasaidizi wake wapo, nadhani bado kuna kazi ya kufanya na ndiyo maana nikasema tutamsaidia. Ningekuwa mimi tayari

ningepeleka mapendekezo kwa Mheshimiwa Rais, Mtendaji Mkuu wa Tume…

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Taarifa.

**TAARIFA**

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampa taarifa mzungumzaji kwamba leseni zinazofutwa na Waziri hazifutwi kwa sababu Watendaji wa Tume wamekosea, ila ni kwamba zinafutwa kwa sababu watu walipewa leseni kwa kufuata utaratibu, lakini hawazifanyii kazi. *(Makofi)*

**MHE. GODWIN E. KUNAMBI:** Mheshimiwa Naibu Spika, sipokei hiyo taarifa. Tunafahamu wanafanya *application* kwenye mfumo, mfumo haujiendeshi wenyewe kuna watu wanao u-*control.* Kwa hiyo mtu mpaka anaomba kama kuna shida ya mfumo tuambiwe maana kama mfumo unaweza ukapokea maombi ambayo ni *incomplete* na uka-*process* na mtu akawa *granted* nadhani kuna *challenge* ya mfumo. Kwa hiyo, ningependa kusikia Mheshimiwa Waziri anapohitimisha atuambie Watanzania; je, kuna changamoto ya mfumo au watendaji? Kama ni watendaji, ni muhimu sasa ukachukua hatua stahiki dhidi yao usiogope. Amezungumza habari ya kuwafutia na nimwambie kwa dhati, hiyo sekta ni nyeti sana na hatutaki aharibikiwe tunataka tumsaidie, kesho yake ni ndefu sana kuliko leo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine niende *STAMICO. STAMICO* ni Shirika la Serikali lililoanzishwa mwaka 1972. Hayati Baba wa Taifa alipoanzisha *STAMICO,* lengo lake maeneo yote ya kimkakati, madini yote ya kimkakati yawe chini ya *STAMICO.* Leo hii *and I stand to be corrected; STAMICO* kwenye *gold, active license* ni leseni moja tu ya *STAMIGOLD*. Sasa hizo zingine zimeenda wapi? Kama kuna idadi ya leseni zimefutwa na *STAMICO* na Tume ya Madini atuambie utakapokuwa anafanya majumuisho sababu zilizopelekea kufutwa hizo leseni.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nini tunafuta leseni? Hii Tume ya Madini ni Taasisi ya Serikali, *STAMICO* ni Taasisi ya Serikali, kwa nini umfutie mwenzako? Fedha zinazokusanywa na *STAMICO* zinakwenda Hazina, tumekwama wapi? Hili ni jambo ambalo ningependa kusikia kauli yake juu ya hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ni Buhemba, Kaka yangu Mheshimiwa Mavunde, a-*take action*. Buhemba ni leseni ya *STAMICO* lakini inaonekana iko *inactive,* inakwenda kwenye *default stage*. *Brother* airudishe *STAMICO,* hilo ni kaa la moto tunafahamu. Namwomba Waziri asimame imara, tutamsaidia, Buhemba airudishe *STAMICO*.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ni kuhusu machimbo ya Kigosi iliyokuwa Hifadhi ya Taifa, sasa iko *TFS*. Nafahamu kulikuwa na mchakato wa kutoa leseni umefikia hatua gani na *STAMICO* wana nafasi gani katika eneo hilo? Kaka asimame imara, amepewa *instrument* ya kwake si ya mtu mwingine, tutamsaidia. Tunafahamu maamuzi ni magumu, lakini afanye tu maamuzi, kesho Mungu atamtetea.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ambalo nataka nilizungumzie hapa bayana, tunafahamu wote tuna uhaba wa dhahabu *(reserve* ya *gold)*, sisi leo hii *BOT* angeweza kununua dhahabu *STAMICO*, lakini *BOT* anakwenda kununua dhahabu kwa wachuuzi wadogo wadogo ambazo ziko chini ya viwango. *STAMICO* ilikuwa na uwezo wa kuzalisha dhahabu na tuna-*refinery* nyingi sana hapa nchini, tungepata dhahabu hapa na *STAMICO* angemuuzia Benki Kuu na Benki Kuu wangeuza nje ya nchi tungepata fedha za kigeni. Hatuna sababu kama nchi yenye dhahabu ya kutosheleza tukawa tuna uhaba wa fedha za kigeni, kazi kwake kaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ni kuhusu *task force*. *Task force* ni chombo kinachoundwa kutatua changamoto ya muda mfupi. Hivi mpaka leo *task force* ipo inafanya nini? Kamati ya Ulinzi na Usalama huko iko chini ya *DC* haiwezi kufanya hizo kazi? Sasa ombi langu, Mheshimiwa Waziri anavyoenda kuhitimisha aniambie, je, kuna haja ya kuendelea kuwa na *task force?* Kama kuna haja, ni muhimu sasa *task force* ikawa ni

chombo kilichopo kwa mujibu wa sheria. Maana sasa hivi hiyo *task force* haipo kwa mujibu wa sheria, ni *instruction* tu ya Waziri. Sasa kama wanadhani *task force* ina umuhimu wa kuendelea kuwepo, ni muhimu sasa ikawa kwa mujibu wa sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, jambo ambalo pia ningependa niliweke hapa bayana kwenye sekta hii muhimu kwa Taifa letu ni suala la nafasi ya Kamishna wa Madini, Wizara ya Madini. Hapa tuna Tume ya Madini ambayo ndiyo inasimamia maeneo yote nchi nzima, Wizarani kuna mtu anaitwa Kamishna wa Madini, ana nafasi gani? Kazi yake ni nini? Tunaambiwa anamshauri Waziri, lakini pia Tume ya Madini bado inamshauri Mheshimiwa Waziri. Sasa naona umefika wakati Mheshimiwa Waziri, Wizara yake itazame upya nafasi ya Kamishna wa Madini Wizarani, ni muhimu ikaondolewa ili kusudi sisi Watanzania tuone ahueni ya fedha za Serikali.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, Mheshimiwa Kunambi, mengine mwandikie Mheshimiwa Waziri.

**MHE. GODWIN E. KUNAMBI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana na naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Magessa, wajiandae Mheshimiwa Kanyasu na Mheshimiwa Dkt. Mabula.

**MHE. TUMAINI B. MAGESSA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa nafasi hii ambayo umenipatia kuchangia Wizara ya Madini. Namshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa fursa aliyonipatia leo tena kusema maneno kadhaa ya madini kwenye Bajeti hii ya Madini. Nampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa kuendelea kuilea vyema hii Sekta ya Madini ambayo inaendelea kukua siku baada ya siku. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimpongeze sana ndugu yangu Waziri wa Madini, Mheshimiwa Mavunde kwa kazi kubwa anayoifanya na Naibu Waziri, ndugu yangu Mheshimiwa Kiruswa kwa kazi kubwa ya usimamizi wa sekta hii kufikia mahali imekuwa

sasa tunaanza kuzungumzia habari ya kuchangia pato la Taifa kwa 10%.

Mheshimiwa Naibu Spika, niwapongeze sana wataalam wakiongozwa na Katibu Mkuu, ndugu yangu Mahimbali. Pia, niwapongeze viongozi mbalimbali wa Taasisi ambazo ziko chini ya Wizara hii ikiwemo *GST* na *STAMICO* kwa kazi kubwa ambayo wameendelea kuifanya katika mazingira magumu. Kila mmoja anajua kwamba *GST* wanahitaji kupewa fedha za kutosha ili kufanya utafiti ndani ya nchi hii, lakini bado kila mwaka tumesema kile kinachotoka bado hakitoshi kufanya hiyo *survey* ambayo wanatakiwa kuifanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, yako mambo mazuri ambayo tunategemea kuyaona baada ya *GST* kuwezeshwa kwa kina ambayo sasa hivi hayaonekani. Vilevile yako mambo mazuri ambayo tunategemea kuyaona, kwamba wachimbaji wadogo wawe wamewezeshwa baada ya kuhakikisha kuwa *STAMICO* imewezeshwa kiasi cha kutosha ili kuweza kufanya uendelezaji mzuri na uwezeshaji wa wale wachimbaji wadogo kule chini.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile niwapongeze wachimbaji wadogo wote wa nchi hii ambao wameendelea kufanya kazi yao katika mazingira magumu, lakini wakiendelea kuikuza Sekta hii ya Madini. Niwapongeze ndugu zangu wachimbaji wa kati, wapo walioanza wakiwa wachimbaji wadogo na sasa wamekwenda kati. Hata hivyo, wanazo changamoto kubwa; nafikiri kuna mahali elimu ya kwenda kwenye mitaji mikubwa haipo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu uchimbaji ni *capital intensive business* ambayo inahitaji mtaji mkubwa kidogo na kuna mahali ambapo hatuwezi kuupata ndani ya nchi hii. Kwa hiyo, bado kuna changamoto ambayo naiona na Serikali inatakiwa iwasaidie hawa ili waweze kwenda juu kama tulivyokuwa tunatarajia.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nijikite tu kwenye ushauri. Mwaka 2020 tulifanikisha kumaliza mazungumzo ambayo yaliifanya nchi yetu sasa ianze kupata zile *free carried shares*; ambapo *Barrick, Northern Mara* na ndugu zangu wa Bulyanhulu

pale Kakora waliweza kutupatia 16%. Hata hivyo, kama alivyosema dada yangu pale asubuhi, bado hoja ya migodi mingine mikubwa ikiwemo *Angro-Gold* ambayo ni *GGM,* mazungumzo yamefanyika kwa muda mrefu sana. Tunategemea mazungumzo hayo yafikie mwisho ili tuweze kupata hizo *free carried shares* ili hizo 16% tuendelee kuzipata. Hii itatusaidia sana kuhakikisha tunapata *dividend,* lakini pia itatusaidia kupata *Board Members* watakaoingia kule ili kutusaidia tutakapokwenda kufanya *evaluation* ya *CSR* tuweze kuwa na usahihi. Sasa hivi tunakwenda *blindly* na kila tunachoambiwa ndicho sahihi. Kwa hiyo tukipata hiyo tutakuwa na uhakika.

Mheshimiwa Naibu Spika, natokea eneo la dhahabu, bei ya dhahabu sasa hivi imechangamka kidogo. Kwa hiyo tukiwa na hii 16% maana yake kipindi hiki tuna uhakika wa nchi kupata fedha za kutosha na hivyo kuwa na hakika kwamba tunaweza kuifanya kazi miradi yetu ambayo inaonekana kukwama kwa sababu ya fedha.  Pamoja na hilo ambalo nimelisema, niwaombe sana viongozi wa Wizara hii tusichukue muda mrefu sana kwenye mazungumzo. Ni kitu gani kinakwama? Iliwezekanaje kule *Barrick* na sasa kwenye migodi mingine inaonekana inachelewa?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu hii ni de*posit* ya dhahabu ni kitu ambacho ni *renewable* na hivyo tunapochelewa maana yake inaendelea kuchukuliwa tukiwa hatuna 16%; lakini sisi kwenye hesabu tuko *comfortable as if deposit* ile ni *renewable,* kwamba itarudi, haitarudi. Tujikite kwenda kuhakikisha kwamba mazungumzo haya yanakwisha mapema na tunaanza kupata hicho ambacho kinatarajiwa.

*(Hapa kengele ya kwanza ililia)*

**MHE. TUMAINI B. MAGESSA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nafikiri hii ni kengele ya kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie suala lingine kwa wachimbaji wadogo. Kama walivyosema wenzangu, kwamba tunategemea mtu akipata *PML* iwe *attached* na angalau ile ripoti kidogo inayoonesha eneo alilopewa lina kitu gani. Hata hivyo kwa bahati mbaya tunapewa *plain PML* ambayo inamfanya yule

anayekwenda kuchimba aanze kubahatisha. Hii imewafanya Watanzania wengine kutafuta dawa za kienyeji ili kuomba dhahabu zije pale, kumbe ile *deposit* ilitakiwa iwepo. Kwa hiyo, tunatakiwa tunapompatia mtu *PML* angalau kuwe na *attached information* ya kuonesha ni nini kiko pale.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri kwa kuja na mpango mkubwa wa kuhakikisha kwamba tunakwenda kufanya *survey (geophysical survey)* ambayo itakwenda kuifanya nchi hii iwe *mapped* ili kuonesha nini kiko kwenye ardhi yetu kwa ajili ya uchimbaji. Kwa hiyo tumwezeshe Mheshimiwa Waziri kwenye bajeti hii ili aweze kulifanya hilo. Asipofanya tukaendelea kuwa na wachimbaji wanaokwenda kimya kimya bila kujua tutakuwa tunatengeneza maskini wengi badala ya kutengeneza watu wengi ambao wamefanikiwa kwenye madini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa ni kuhusu *CSR; CSR* ni changamoto. Niende moja kwa moja kwenye ukweli na kuishauri Serikali. Ni lazima tubadilishe sheria na kanuni za *CSR*. Inawezekana ilitungwa na kutengenezwa kwa nia njema lakini ime-*fail*. Kwa hiyo, twende kwenye kanuni na sheria ili tuzibadilishe.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maneno hayo, naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kanyasu, jiandae Mheshimiwa Mabula.

**MHE. CONSTANTINE J. KANYASU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Naomba nitumie nafasi hii kwanza kumpongeza Mheshimiwa Rais na Serikali nzima kwa kazi nzuri ambayo inaendelea kwenye Serikali. Kipekee nimpongeze Mheshimiwa Waziri na timu yake nzima kwa kazi nzuri ambayo wanaifanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Nishati na Madini na kipekee naweza kusema kwamba naunga mkono hoja ingawa nitakuwa na maoni na mapendekezo machache baadaye.

Mheshimiwa Naibu Spika, kupitia mabadiliko ya sheria ya mwaka 2019 na hii *local content law* ambayo tumeitengeneza takribani shilingi trilioni 1.6, dola bilioni moja na *point* zinazunguka kwa Watanzania kutokana na ushiriki wao kwenye maeneo mbalimbali. Ukiangalia kwenye mauzo yetu ya dhahabu zaidi ya 40%, inatokana na mchango wa wachimbaji wadogo. Maana yake ni kwamba hii sekta imewagusa Watanzania, lakini bado imeendelea kukua na kuwafaidisha Watanzania. Kwa hiyo tunaipongeza sana Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili, kabla sijaenda mbali nataka niweke kumbukumbu sahihi. Wakati anachangia rafiki yangu Mbunge, Mkurugenzi wa zamani wa Dodoma, amejaribu kuonesha kwamba mtendaji wa tume, tume yenyewe sijui na watu gani wachukuliwe hatua kwa sababu ya namna walivyotoa leseni. Nadhani hajui jambo hili vizuri, yaani mimi hapa naweza kuingia kwenye mfumo nikapeleka *coordinate*, kumbe *coordinate* ninazozipeleka labda zina hekta 100,000. Kazi ya watu wa tume ni kuangalia eneo lile kama halina mgongano na mtu mwingine. Sasa, kwa sababu nakwenda kuomba kitu ninachokijua, basi watanipatia; halafu watanipatia na muda. Kila leseni ina miaka ya utafiti na miaka ya kulipia. Itakapofika mahali umepewa hiyo leseni kwa kuomba mwenyewe ukiamini unakwenda kuchimba halafu kumbe hukuwa umejiandaa, sasa kosa la waliokupa liko wapi? Nadhani halifahamu vizuri hili eneo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka niwatie moyo watendaji wa Serikali wala wasiwe na wasiwasi na kauli ya Mheshimiwa. Ikiwezekana apate muda aende kwa Musukuma ili amshauri vizuri kuhusiana na jambo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya pili, kulikuwa na mazungumzo yanayoendelea kati ya…

**MHE. TABASAMU H. MWAGAO:** Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Taarifa.

**TAARIFA**

**MHE TABASAM H. MWAGAO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kumpa taarifa msemaji, ni kwamba tunamwomba sana Mheshimiwa Waziri wa Madini aje atoe semina ya namna ya kuingia kwenye mfumo na namna leseni zinavyopatikana. Kwa sababu kauli zinazotamkwa hapa na Waheshimiwa Wabunge zinaonesha kabisa kwamba uelewa ni mdogo sana katika jambo hili. Hili jambo linakuja kupunguza kabisa ari ya watendaji wetu wa Serikali kwa kazi kubwa wanayoifanya katika Sekta ya Madini. Roho imeniuma sana, ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. CONSTANTINE J. KANYASU:** Mheshimiwa Naibu Spika, naipokea hiyo taarifa na kwa kweli itasaidia.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili ni kuhusiana na hii *negotiation team* inayoendelea ambayo kwetu sisi imeshikilia haki za wananchi. Tulikuwa tunakwenda vizuri na Mheshimiwa Waziri wa Madini. Maeneo ya machimbo ya Katumaini, Samina na maeneo mengine yanasubiri hii *negotiation team* ikamilishe mazungumzo ili aidha wayaachie au walipe fidia. Sasa inakwenda kwa *speed* ndogo sana. Kule Magema ambako wananchi wapo wamekataa kufanyiwa utafiti kwa sababu hawa watu hawajawahi kuwalipa fidia.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi leo sitaki kuzungumzia vigingi bali nataka kuzungumzia namna ambavyo utaratibu wa mazungumzo unavyokwenda *slow* na namna unavyoathiri maisha ya watu walioko pale na hivyo kuitaka Serikali ifike mwisho. Kama kampuni zote zimeridhia, zimekubali na zimetoa *share* kwa Serikali, wao wanagoma, kwa nini Mheshimiwa Waziri asiwanyang'anye maeneo hayo? Kwa sababu yako wazi na yana mgogoro na wananchi. Kule Katumaini, Mizingamo na Samina ambako ni 83, kote kule yalikuwa ni maeneo ya wananchi yaliyo na eneo la ukubwa wa *kilometer square* 192. Kwa kuwa hawana uwezo wa kulipa na kwa kuwa mwaka huu Mheshimiwa Waziri ana-*renew license*, sasa, ni kwa nini asiwanyang'anye maeneo hayo tukawapa wachimbaji wadogo ili wao waendelee kuchimba kule ambako wanapataka? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine hapo ni kwamba, ni muhimu sana kuangalia uchimbaji wao unavyokwenda. Wanarukaruka sana kiasi kwamba, kama alivyosema Mheshimiwa Magessa, baada ya miaka kumi *almost* kila kona watakuwa wame-*touch* na wamehama, halafu watakwambia wanapunguza uwekezaji na matokeo yake utajikuta sehemu kubwa ambayo labda kama wangechimba taratibu wangeweza kuzalisha kwa muda mrefu zaidi. Kwa hiyo mimi nilitaka nishauri, kama *negotiation team* ime-*fail* kwenye eneo hili, kama imeshindikana, maeneo haya yakatwe kwenye leseni halafu wapewe wachimbaji wadogo na sisi tunataka wachimbaji wadogo wapewe maeneo haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la tatu, imezungumziwa kuhusu wachimbaji wadogo kupewa *first right of refusal,* halafu ndipo huyo mwenye leseni apate haki ya kupata mwekezaji au kuuza. Sijaelewa, labda ataliweka vizuri. Kwa sababu huyu ni *intruder* amekuja kwenye leseni yangu *unless* nina-*contract* naye, amekuja nimempa mkataba, najua uwekezaji wake ni shilingi ngapi, kwa hiyo siku nikiuza nitam-*compensate* nini? Huyu ni *intruder* amekuja kwenye leseni yangu naimiliki miaka mitano, nimelipa dola 10,000, halafu unampa *first right of refusal* ya maamuzi ya mimi mmiliki wa leseni; *how comes?* Hii kitu haiwezi kutokea. Utatengeneza kesi nyingi sana. Maana yake ni kwamba hakuna maana ya kuwa na leseni kwa sababu mtu anavamia popote halafu akitaka kuuza unamwambia huwezi kunitoa kwa sababu mimi nilikuja hapa. Hicho kitu hakiwezi kutokea, *unless* niwe sikuelewa jambo hilo, lakini kama nimemwelewa vizuri nafikiri hapo Mheshimiwa Waziri arudi aangalie upya. Tutatengeneza migogoro mingi sana halafu kutakuwa hakuna sababu ya kumiliki leseni. Sasa nitakata leseni ya nini kwa sababu mtu akija anachimba halafu nikitaka kumwondoa ananiambia huwezi kuniondoa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la mwisho ni kuhusiana na *refinery*….

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa.

**MHE. CONSTANTINE J. KANYASU:** Mheshimiwa Naibu Spika, aisee Mheshimiwa naomba sana uniache nimalizie…

**NAIBU SPIKA:** Taarifa.

**MHE. CONSTANTINE J. KANYASU:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye *refinery* shida iko kwenye sheria yetu.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kanyasu, kuna Taarifa.

**MHE. CONSTANTINE J. KANYASU: …**shida iko kwenye sheria yetu…

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kanyasu, kuna taarifa.

**TAARIFA**

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Naomba nimpe Taarifa mjomba wangu, anachangia vizuri. Watu ambao naamini Mheshimiwa Waziri anataka wapewe *first priority* pale ambapo mwenye leseni anataka kumuuzia mwekezaji, ni wale ambao mwenye leseni aliwaruhusu wakachimba maduara, wakafunga matimba, wakaendelea na uzalishaji, mwenye leseni hazalishi, inapofikia mwenye leseni anataka kuuza lile eneo hawafanyii *consideration* wale watu ambao wameweka uwekezaji pale. Yeye anachojali ni fedha yake anayolipwa na mwekezaji na namna ya kufanya *transfer* ya ile *right* yake, ndio anaowazungumzia na si ma-*intruder*. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kanyasu. Kanyasu.

**MHE. CONSTANTINE J. KANYASU:** Mheshimiwa Naibu Spika, anachokizungumza dada yangu *it is just a reciprocal* ya nilichosema mimi. Nilichosema *unless* kuna *contract* ya wale *mine right holder* na wale wanaokuja kuchimba, *then* hiyo haki ipo, lakini siyo wawe *intruders* halafu nataka kuuza unaniambia ana *first right of refusal. That is not.*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili kwenye eneo hili ni kuhusiana na *refineries*. Tunafeli wapi? Sheria yetu kwenye *section* 59 ukiisoma vizuri ni kama inabembeleza hivi. Inasema; "*59. The mineral right holder shall be required to set aside certain amount of minerals at such percentage as the Minister may, after consultation with the mineral right holder and the Commission, determine for processing, smelting or refining within the United Republic of Tanzania.*"

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza namna haka ka-*section* kalivyo ni kadogo, lakini pia kama vile kanatoa hiari. Ndiyo maana sasa Tanzania tumejenga *almost refineries* sita na zote hazina mzigo ilhali tumetunga sheria inayosema kwamba watu watatenga *percentage* ya madini kuipeleka kwenye *refinery*. Ukiisoma vizuri ni kwamba inahitaji kurekebishwa ili iwe na meno. Yaani isitengeneze haka ka-*may,* umenielewa? Halafu isitengeneze *option* ya ku-*consult* na mimi. Sasa ni sheria gani hiyo ambayo kwanza una-*consult* na mimi halafu ndipo nakubali na kisha tunakwenda kwenye utekelezaji? Ya wapi? Haiwezekani, vinginevyo huu uwekezaji mkubwa ambao watu wameweka mabilioni ya shilingi hautakuwa na maana yoyote.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nini *BOT* hawawezi kupata mzigo; rafiki yangu anasema *BOT* wananunua dhahabu kwa wachimbaji wadogo wadogo huku chini, nadhani pia hajui. *BOT* wananunua *refined gold* kutoka kwenye *refineries* ambayo *purity* yake iko 99.99%. Sasa wanaitoa wapi kama hizi *gold refinery* zote hazina mzigo?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nataka nimwombe Mheshimiwa Waziri, tupitie upya eneo hili ili tulione vizuri na tutengeneze mazingira ya Benki Kuu kupata mzigo na kuuza *value added gold* ambayo tumeikusanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Dkt. Mabula, ajiandae Mheshimiwa Amar.

**MHE. DKT. ANGELINE S. L. MABULA**: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa fursa ili niungane na wenzangu kuipongeza sana Wizara kwa kazi nzuri wanayoifanya, Mheshimiwa Waziri Mavunde pamoja na timu yake. Kutokana na muda naomba pongezi zangu ziishie hapo na nianze kwa kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nitakuwa na maeneo kama manne ya kuzungumza. Kwanza, ni kuhusiana na suala la Taasisi ya Jiolojia na utafiti wa madini. Tungeomba sana Wizara iitazame hii kama ndiyo roho ya Wizara, kwa maana ya kwamba wanahitaji kuwezeshwa kwa kiasi kikubwa ili waweze kufanya kazi zao za utafiti utakaowawezesha kutambua maeneo yote ambayo yana rasilimali ya madini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunazo tafiti nyingi ambazo ziko tayari, kama ambavyo Mheshimiwa Profesa Muhongo alivyosema, ukiwemo utafiti wa Mheshimiwa Profesa Muhongo ambao upo. Niombe wataalam wetu wachukue muda mzuri wa kupitia tafiti zilizopo katika ofisi zao. Kwa sababu hata haya yanayotokea tulipata taarifa zisizo rasmi na niliwaambia baadhi ya watendaji kwamba, kulikuwa na taarifa ambayo ilikuwa inazungumzia masuala ya mlipuko ule uliotokea Hanang. Kuna utafiti ambao upo na unazungumza kwamba, huenda kwa baadaye ingeweza kutokea. Labda kama wangekuwa wamepitia pengine tungeweza kuwa na tahadhari na hivyo tusingeweza kuyapata haya, hata ukiangalia yale ya Mbeya na kule kwingine. Kwa hiyo, niombe sana wataalam wajikite kuangalia tafiti zilizopo ndani ya ofisi na waendelee kufanya tafiti mbalimbali ili waweze kufanya kazi zao vizuri, hivyo lazima tuangalie. Hata wafanyabiashara wanawekeza zaidi kwenye matangazo, hivyo basi sisi tuwekeze zaidi katika suala zima la utafiti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la pili naongelea habari ya ushiriki wa Wizara katika maonesho na makongamano mbalimbali yanayofanyika kitaifa. Nilikuwa naangalia kwenye taarifa ya Mheshimiwa Waziri na sikuona mahali ambapo pengine wamezungumzia matokeo yake au namna ambavyo Wizara

imeweza ku-*adopt* yale tuliyojifunza au waliyojifunza katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimesema tuliyojifunza kwa sababu nilipata bahati ya kushiriki mkutano mmoja. Hiyo pia inatusaidia kwa sababu unakuta teknolojia za wenzetu ziko juu sana, ziko mbali na hivyo kuna fursa za kujifunza na watu wetu kujengewa uwezo. Basi angalau atakapo-*wind up* tuone haya makongamano yote na kazi kubwa iliyofanyika kimataifa na kitaifa, tuone ni wapi pengine kama Wizara kuna kitu tume-*tap* ambacho kinaweza kutusaidia kusukuma Wizara yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine nitaongelea kuhusu utwaaji ardhi, hasa pale ambapo mtu anaingia ana leseni yake ya madini. Mara nyingi tumejikuta tunawaondoa wachimbaji wadogo wadogo kwenye yale maeneo kwa sababu tu hana leseni. Ningeomba sana, tunahitaji kutengeneza matajiri wadogo wadogo wengi wanaokaribia kwenda kwa wakubwa. Kwa hiyo ni vizuri katika zile ardhi wanazotwaa tuone namna ya kutunga sheria na kuwa nayo ili iwalazimishe walau mwenye ile ardhi apate hata asilimia ndogo ya kuweza kuendelea kufaidika na ile ardhi yake kwa sababu ana haki zote za kumiliki ardhi na huyu ana haki zote za madini.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukienda kwenye Sheria ya Ardhi Kifungu cha 181; watu wa sheria watanikosoa, *I am standing to be corrected,* kwamba, unapokuta kuna mgongano wa sheria hizi bado Sheria ya Ardhi inasimama na inampa nguvu yule mwenye ardhi yake kuendelea. Sasa tuone namna ya kuwajengea uwezo hawa ili waweze kutumia ardhi zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kuna suala la ulipaji fidia katika maeneo haya. Kwa mfano kuna maeneo kama ya Geita Mji, eneo lile tayari liko kwenye leseni ya mtu lakini wale watu nyumba zinaanguka. Niombe sana na tumekwishalisema kwenye Kamati, mimi na-*declare interest* kwamba ni mjumbe wa Kamati. Wale watu tunawatesa, kama mwekezaji hajawa tayari kuchukua lile eneo awaachie waendeleze maeneo yao. Akilihitaji aje alipe kwa thamani ya sasa kuliko kuwaweka tu huku watu wanaendelea kuteseka na ardhi ni ya kwao. Niombe sana tuangalie haya kama

Serikali kwa sababu tumejikuta tunayumba katika masuala ya kuwawezesha hawa vijana wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine, ni suala la majadiliano ambalo limezungumzwa, wenzangu wamelizungumza. Naomba niseme tu nalo lichukue muda mfupi, tunao wenzetu kama Mama Masasi na Geita Gold *Mine refined mining* pale kwake, wanahitaji kupata hizi dhahabu kwa maana ya kwenda kuchakata na *BOT* ingeweza kupata mzigo mkubwa kama hii ya Mwanza ingewezeshwa na ile ya Mama Masasi Geita wangewezeshwa tusingekuwa pia na changamoto sana ya fedha za kigeni kwa sababu wangepata mzigo mkubwa wa kuweka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, lazima pia haya majadiliano yaende kwa haraka maana yake inakuwa kama tunawabembeleza kwamba angalau sehemu yake aiache ichakatwe hapa, huko ni kubembeleza mtu wakati sisi tunahitaji kupata *material* ile kwa maana ya kuwezesha hizi *gold refinery* zetu ziweze kufanya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie suala la mazingira, suala la mazingira kuna mahali ambapo kwa kweli watu wetu wanapata shida, kwenye Taarifa ya Waziri imezungumzia katika mikoa 30 hiyo ya kimadini wamefikiwa wachimbaji wadogo 22,431, lakini hawa wote wamejikuta wamekwenda kinyume na taratibu, kwanza katika suala zima la kutorudishia yale maeneo, kufukia mashimo, kutumia vibaya vifaa vya kujikinga, lakini kuna suala la matumizi yasiyozingatia utumiaji sahihi na suala la uhifadhi usio salama kwa baruti na viripuzi. Sasa hii ni hatari, tuombe sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba hapa Wizara ijikite katika elimu zaidi, hawa wachimbaji wadogo wanafanya kazi ile lakini pengine si wote waliopata elimu ya namna bora ya kutumia vile vifaa vya kinga, namna bora ya kuhifadhi mazingira pale ambapo wanakuwa wameshafanya kazi zao, lakini pia namna bora ya wao wenyewe kujilinda dhidi ya kazi ile ambayo wanaifanya. Niombe sana Wizara ichukue muda mwingi katika kuwaelimisha ili waweze kufanya kazi yao vizuri na tusijikute

tunapata hasara kwa wachimbaji wetu kujikuta wameumia kutokana na matumizi mabaya ya vile vitendea kazi wanavyofanyia kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la *STAMICO,* kwanza niipongeze sana Serikali kwa kulifufua Shirika hili na kulipa uwezo wa kufanya kazi. Katika mambo ya msingi ambayo Wizara pia imefanya pamoja na wingi wa mazuri waliyofanya lakini kwa suala la *STAMICO* limekwenda vizuri sana. Ombi langu kwa sababu ile ni kampuni inayofanya kazi yake kibiashara na ushindani na makampuni mengine makubwa ya *mining,* ningeomba sana tuangalie upya kama ambavyo tumesema katika maeneo mengine ile Sheria ya Manunuzi, taratibu za manunuzi zinawakwamisha, wafanye katika utaratibu ambao utafanya kazi zao ziwe rahisi, habari ya kwenda kufuatilia yale kwa kweli tunawarudisha nyuma hawa wenzetu, wanashindwa kwenda na ile kasi ya ushindani ambayo wanatakiwa waifuate kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ningeomba sana hili kwa sababu ni suala ambalo limekaa katika utaratibu mzuri wanawagusa wachimbaji wadogowadogo kwa sehemu kubwa na wameleta vitendea kazi ambavyo vinakwenda kuwasaidia wale vijana katika suala la uchimbaji. Kwa hiyo ni vizuri pia wakaangaliwa katika taratibu zingine za kimanunuzi angalau wajitegemee kwa maana ya kwamba iwe ni Taasisi ambayo haina ule mlolongo iende sawasawa na Taasisi zingine ambazo zinafanya kazi kibiashara na zina ushindani wa kibiashara. Tukitaka kuishindanisha na makampuni mengine tutakuwa tumeirudisha nyuma sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie kuungana mkono na wasemaji wote waliozungumzia suala la *CSR*. Wakati tunaliangalia kwa kweli lilikuwa linatia huruma, wanapoongea wale ambao wanafaidika walitakiwa wanufaike na hilo unakuta pesa zinatengwa nyingi, lakini kinachofanyika pale hakiendi sambamba na matarajio ya wananchi. Kwa hiyo, nasisitiza, tuone namna nyingine ya kuangalia upya suala la *CSR* katika hawa wawekezaji pamoja na kwamba kwenye taarifa inaonekana bilioni 17 zimetumika kwenye masuala ya *CSR,* lakini *actually*

ukienda kuangalia kwenye maeneo utajiuliza kweli hizi bilioni 17 zimefikia hatua hii kweli, yaliyoko haya kweli ni ya kiasi kipi? Kwa hiyo, tuone tu namna bora ya kushirikisha kama ambavyo *CSR* zingine zinatumika, siyo kwamba hawa ni *exceptional* kwamba wao wawe na utaratibu tofauti na maeneo mengine, hapo tutakuwa tumesaidia maeneo yanayonufaika na *CSR* katika uwekezaji wa madini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba nirudie tena kumpongeza Waziri na timu yake yote lakini nimpongeze Mheshimiwa Rais kwa namna ambavyo ameiangalia sekta hii na kuweka pia Waziri kijana ambaye anakwenda *speed* kubwa pamoja na mahitaji ya Taifa. Baada ya muda mfupi, nadhani madini yatazidi kuongoza katika mapato ya Taifa hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Amar dakika tano, ajiandae Naibu Waziri wa Madini.

**MHE. HUSSEIN N. AMAR:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kuwa mchangiaji wa mwisho na kupata hizi dakika angalau tano. Nianze kabisa kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia kuwa na afya njema na kuweza kusimama hapa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu ni dakika tano naungana na wenzangu kuhusu suala la kuwawezesha wachimbaji wadogo. Leo wachimbaji wadogo wameweza kuchangia pato hili la 10% kwa kutumia sururu, nyundo na makoleo, lakini tukiwawezesha vifaa vya kisasa, naamini tutachangia zaidi ya 10%. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili, wachimbaji wetu wamekuwa wakitumia ramli (kubahatisha), tunashukuru kwamba Serikali imeleta vyombo vya kisasa *GST* kwa ajili ya kufanya tafiti mbalimbali kugundua idadi ama wingi wa madini yaliyopo chini na sisi Wananyang'hwale tunaomba vifaa hivyo vije Nyang'wale kwa ajili ya kufanya tafiti hizo kwa sababu Mwenyezi Mungu

ametupa neema kubwa, milima yetu yote ya Nyang'hwale sasa hivi ina dhahabu. Kwa bahati mbaya wachimbaji wetu wanahabatisha, lakini iwapo wataleta vile vifaa na wakapunguza gharama ya zile tafiti, naamini Nyang'hwale itakuwa ina mchango mkubwa sana kwenye upande wa sekta ya madini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimwombe Mheshimiwa Waziri aunde timu ambayo itakwenda kwenye Mgodi wa Bulyanhulu kwenda kufuatilia uchimbaji unaoendelea kule *underground,* sisi Wananyang'hwale tumekuwa tukipata taarifa kwamba uchimbaji huu unaelekea Nyang'hwale. Tumekuwa tukipata hiyo *CSR* zaidi ya miaka mitano chini ya bilioni moja, lakini leo hii tumeambiwa wameshaiingia kwetu zaidi ya kilomita nne. Sasa tunahitaji Waziri atume Tume yake ikahakiki kama ni kweli, basi tubadilishe utaratibu uliopo ambao Msalala wanapata 67%, sisi Nyang'hwale tunapata 33%.  Kama uchimbaji huo umeelekea Nyang'hwale, tukae tujadiliane ili mapato tugawane sawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kulisema hilo, naomba sasa sisi kama Bunge tulipitisha utaratibu na kuwaomba wawekezaji wetu ambao wana uwezo wa kujenga mitambo ya *refinery* wameweza kupatikana akiwemo Mama Masasi na wengine wamewekeza fedha zao nyingi, leo hii dhahabu haipatikani kwenye mitambo hiyo. Namwomba Mheshimiwa Waziri aangalie namna gani tuwasaidie wawekezaji wetu hawa, wamekwenda sasa kufilisika kwa sababu dhahabu hazionekani, lakini pia *BOT* inaanza kununua dhahabu.  Waziri atakapoweka utaratibu mzuri wa dhahabu hizo kusafishwa kwenye migodi hiyo ya kusafisha ama kupandisha thamani, naamini *BOT* watapata dhahabu nyingi na ni za uhakika, tuachane na huu mtindo ambao wanasema watanunua kwa wachimbaji wadogowadogo, watapigwa kama miaka iliyopita. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nashauri kabisa kwamba tuwawezeshe hawa akinamama kama Mama Masasi nimemwona yuko hapa na wawekezaji wengine ambao wana mitambo hiyo ya kupandisha thamani, tuwawekee utaratibu mzuri. Tuliwashauri na tulipitisha Bungeni kwamba tutawawezesha

na kweli wameweza kukopa mitaji kutoka katika maeneo mbalimbali leo hii tunawatelekeza watakwenda wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho, nimshukuru sana Naibu Waziri Mkuu, mabilionea aliokuwa akisema hawa hapa, wako akina Baraka na wengine wengi, tunamwomba sasa na Mheshimiwa Mavunde, hawa waongezeke tupate matrilionea kwenye upande wa wachimbaji, naamini hilo linawezekana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja na ahsante sana kwa kunipa nafasi. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante.

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. SAADA MANSOUR HUSSEIN:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuweka mkazo katika utafiti wa madini katika sehemu mbalimbali nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa kuleta ubunifu katika madini. Nampongeza sana sana Mheshimiwa Mavunde kwa hili, aidha napongeza mchango wa madini katika kuongeza mchango mkubwa katika pato na uchumi wa Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wangu naomba Wizara ifungue soko la madini kule Zanzibar kwa sababu tuna hoteli kubwa na utalii umeongezeka sana. Naiomba Wizara ishirikiane na Wizara ya Madini Zanzibar wafanye utafiti wa uwepo wa madini katika Mkoa wa Kaskazini Unguja ili kubaini madini yaliyopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishauri Serikali ione namna ya kuwasaidia wachimbaji wadogo Zanzibar na Bara na mfano mikopo na vifaa vya uchimbaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Rais na Wizara kwa kuongeza fedha kwa ajili ya kufanya utafiti wa madini nchi nzima.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. ORAN M. NJEZA:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuwashukuru na kuwapongeza Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Mawaziri na viongozi wote wa Wizara ya Madini, kwa uongozi wao na utendaji uliotukuka.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia kutumia fursa hii kukupongeza wewe binafsi, Spika na uongozi wote wa Bunge kwa uongozi wenu mahiri na wenye ubunifu wa hali ya juu katika kuongoza mhimili wa Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpongeza Waziri wa Madini kwa hotuba nzuri iliyojaa ubunifu mkubwa na imedhihirisha utayari wa Taifa letu katika kuboresha maisha ya wananchi na pia utayari wetu wa Ushindani wa Kimataifa *(National Competitiveness)*. Bajeti hii inaenda sambamba na Dhima ya Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/2022 – 2025/2026 ambayo ni "Kujenga Uchumi Shindani na Viwanda kwa Maendeleo ya Watu."

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na mafaninikio ya sekta ya madini, Serikali inashauriwa kuchukua hatua za kuimarisha zaidi sekta hii muhimu ili kukabiliana na athari za kiuchumi hususani upungufu wa fedha za kigeni na kuongeza kasi ya mchango wa madini kwenye pato la Taifa. Kutokana na athari ya kiuchumi uliokumba dunia nzima, hii inaweza kuwa fursa kwa Serikali kuvutia uwekezaji zaidi kwenye madini hasa dhahabu, madini ya chuma na madini ya *calcium carbonate, lime* na *phosphate*. Dhahabu ina historia ya bei kutoyumba kwenye soko la dunia kwa vile mabenki yanatumia dhahabu kwenye kuwekeza na kutokana

pia na kuyumba kwa thamani ya shilingi na hata dola ya Marekani, Serikali inaweza kutumia dhahabu kama mbadala wa kuwekeza amana zake. Kutokana na mabadiliko ya kiuchumi kidunia, Benki Kuu nyingi duniani zimeanza kuwekeza zaidi kwenye dhahabu na hii ni ishara nzuri kwa bei ya dhahabu kuendelea kuimarika kwenye soko la dunia.

Mheshimiwa Naibu Spika, vita vya Urusi na Ukraine vimesabisha upungufu mkubwa wa uzalishaji wa mbolea na hii ni fursa kwa Serikali kuwekeza kwenye viwanda vya mbolea kwa kutumia malighafi zinazopatikana hapa nchini kama vile *phosphates, calcium carbonate, limestone* na *natural gas.* Katika kipindi cha mtikisiko wa uchumi, bei ya madini ya chuma na hata makaa ya mawe haiyumbi na Serikali inaweza kupata mapato mengi katika kipindi hiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, napendekeza Serikali kuchukua hatua za makusudi na kuharakisha uwekezaji kwenye Mradi wa Chuma *(Liganga Iron Ore)* ikiwa ni pamoja na Makaa ya Mawe *(The Mchuchuma Coal Mining and Power Projects)*. Mradi wa Liganga na Mchuchuma ulitarajia uwekezaji wa dola za Marekani bilioni tatu na kuzalisha ajira zaidi ya 30,000 na hii inaweza kuwa fursa nzuri katika hiki kipindi cha mahitaji makubwa ya bidhaa za chuma na pia kupunguza nakisi ya urari wa biashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na Mradi wa Liganga na Mchuchuma, napendekeza Serikali kuchukua hatua kuharakisha uwekezaji kwenye Mradi wa Madini ya Niobium ikiwa ni pamoja na ujenzi wa Kiwanda cha *Ferroniobium (FeNb)* ambacho kitakuwa cha kwanza Afrika na cha nne duniani. Kutokana na mahitaji makubwa ya ujenzi wa reli, madaraja na reli ya *SGR,* kuna mahitaji makubwa ya vifaa vya chuma ambavyo ni imara, lakini vyepesi na vyenye ubora wa kimataifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kutumia sheria zetu za uwekezaji, Serikali itumie fursa za kipindi hiki ili kuvutia wawekezaji kwenye madini ya viwandani ili yaongezwe thamani hapa kwetu na pia kuvutia malighafi ya madini toka nchi zingine ili yachakatwe hapa kwetu. Tanzania imebahatika kuwepo kwa madini ya *Niobium* ambayo inapatikana Milima ya Pandahill

Wilaya ya Mbeya na mahitaji ya *Ferroniobium (FeNb end product)* yanaendelea kuwa makubwa duniani na hapa kwetu pia.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inahitaji kujiwekea mikakati ya haraka *(quick wins)* ili kuhakikisha inaimarisha uchumi ikiwemo kuboresha urari wa biashara kukabiliana na athari za changamoto za kiuchumi duniani. Kwa kutumia rasilimali zetu za madini, Serikali inaweza kutengeneza fursa nyingi na kupitia Mradi wa *Niobium* na Kiwanda cha *Ferroniobium*, ajira 2,000 zitakazozalishwa wakati wa ujenzi na pia kutakuwepo ajira za kudumu zaidi ya 600 na *indirect jobs* 7,000. Mradi utazalisha mapato kila mwaka shilingi bilioni 500 (dola za Marekani milioni 220) ambapo mapato kwa Serikali kila mwaka shilingi bilioni 50 (dola za Marekani milioni 22) uhai wa mgodi ni zaidi ya miaka 30. Hiki kitakuwa kiwanda cha kisasa cha kwanza Afrika *(Modern Manufacturing Plant and Smelter)*. Pamoja na kuingiza teknolojia hii adimu na ujuzi *(skills transfer)* pia itakuwa inachangia huduma za kijamii *(Corporate Social Investment in Community)* na chanzo cha fedha ya kigeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, napendekeza Serikali iboreshe mazingira ya uwekezaji katika madini ili kukabiliana na ushindani wa masoko ya nje yanayovutia utoroshaji wa madini na kupoteza fursa ya kukusanya fedha za kigeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**NAIBU SPIKA:** Baada ya wachangiaji sasa tutaingia upande wa Serikali, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Madini.

**NAIBU WAZIRI WA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, naomba nitumie fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa kibali cha kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu jioni hii ya leo ili niweze kujibu hoja chache za Wabunge waliochangia kwenye bajeti yetu. La pili niendelee kumshukuru Mheshimiwa Rais, Mama Dkt. Samia Suluhu Hassan, ni Rais wetu mpendwa wa Awamu ya Sita, kwa imani aliyoendelea kuwa nayo juu yangu na Waziri wangu kwa kutuamini kumsaidia kuilea sekta hii nyeti kwa maendeleo ya Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la tatu, nitumie pia fursa hii kukushukuru wewe na Spika mwenyewe kwa jinsi mnavyolisimamia Bunge letu na kwa jinsi mlivyosimamia hoja ya Bajeti ya Wizara yetu tangu tulipoanza leo asubuhi. Pia niwashukuru Wanakamati wote wa Kamati ya Nishati na Madini kwa mchango wao mzuri na maoni waliyotoa ambayo kwa ujumla wake wametoa ushauri ambao utatusaidia sisi kama watendaji wa Wizara hii kuendelea kuboresha mazingira ya uwekezaji katika Sekta ya Madini ili Taifa letu lizidi kuneemeka kwenye madini haya ambayo Mungu ametujalia kwa wingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie vilevile fursa hii kukiri kwamba watu wengi waliochangia katika hoja yetu wametoa ushauri na ni ushauri ambao hatuna sababu yoyote ya kwenda kinyume nao, tutaufanyia kazi. Maoni mengi ni ushauri na kama kuna hoja za ufafanuzi ni chache sana kwa sababu ukiangalia tangu tulipoanza uchangiaji leo alianza Mheshimiwa Profesa Muhongo utadhani alikuwa na sisi wakati tulivyokuja na hii ndoto ya *vision* 2030. Ametembea kwenye hiyo Dira kwamba tunahitaji kuikuza hii sekta ya *GST* ambayo sisi katika Wizara tunaiona kama ndio *navigator*.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati watu wanafanya mashindano ya magari, kuna mtu ambaye kazi yake ni kuonyesha ramani inapita wapi. *GST* ndio mchora ramani na *STAMICO* ndiye anayetembea juu ya ile ramani ili kuhakikisha kwamba mianya yote na mapito yote ambayo *GST* imepita na kubaini madini, *STAMICO* ipo pale kufanya utafiti wa kina ili tuweze kuwa na taarifa sahihi kwa ajili ya uwekezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kwa ujumla kwa hoja zile za Kamati kuna moja ambayo ilikuwa inazungumzia suala la kuhakikisha kwamba mawakala ndio waruhusiwe kuuza makaa mbadala yaani *core rubricates* na hii ni hoja ambayo kwa mujibu wa mpango wa mauzo ambao ulishawekwa na Shirika la *STAMICO* hao mawakala ndio wanaokwenda kufanya hiyo biashara. *STAMICO* haitafanya hiyo biashara, wao watazalisha, mawakala wameshatambuliwa, watachukua na watawapelekea walaji wa mwisho na kwa bei iliyopunguzwa kwa sababu wataweka bei elekezi kama jinsi ambavyo mafuta huwekewa bei

kuanzia bandarini mpaka kwenye vituo vya vijijini kule, haya makaa pia yatakuwa *regulated* katika masuala ya kugawa bei yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kulikuwa na suala limejitokeza la kuhakikisha kwamba gharama wanayotozwa wachimbaji wadogo wanaotumia hizi ligi ambazo Mama yetu Dkt. Samia Suluhu Hassan alituletea, zimekuja tano, ziko nyingine 10 ziko njiani na hizi tano ambazo zimeshagawiwa katika baadhi ya Mikoa ikiwepo Mara, ikiwepo Mkoa wa Mbeya na zimeanza kufanya kazi, ni kwamba hizi zinatolewa kwa gharama nafuu sana ukilinganisha na gharama ya sekta binafsi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye masoko ya binafsi meta moja inachimbwa kwa shilingi 227,587.50, hiyo ndio gharama ya ku-*drill* kufanya uchorongaji kwenye mita moja kwa kutumia mitambo ya sekta binafsi, lakini kwenye hii mitambo ambayo tumeletewa na Mama yetu, Mama Samia Suluhu Hassan kupitia Shirika letu la *STAMICO* mita moja wanafanyiwa uchorongaji kwa shilingi 108,212.52. Kwa hiyo, hii ni kusema kwamba mitambo hii ililetwa kwa ajili ya kuwapa nafuu wachimbaji wadogo ambao wamejipanga na wanaweza wakachangia hiyo sehemu ya gharama ndogo, waweze kufanyia utafiti katika maeneo yao ili waweze kufanya uchimbaji wenye tija.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile Kamati ilielekeza na kutushauri na kutoa hoja kwamba tuimarishe kanzi *data* ya miamba ili wachimbaji wa madini waweze kupewa maeneo yenye taarifa sahihi za kijiolojia. Hii ndio kazi ya *vision 2030*.

Mheshimiwa Naibu Spika, *vision 2030* imelenga katika kuiwezesha *GST* iweze kuwa na maabara ya kisasa, iweze kuwa na uwezo mkubwa wa kutafiti madini kwa kutumia teknolojia ya kisasa kama hiyo ya urushaji wa ndege, sasa hivi tumewekeza katika kuomba bajeti ya kununua helkopta na hayo yote yanatupelekea kuweza kupata uwezo wa kubaini madini tuliyonayo na kiwango kilichopo ili wachimbaji wote wa madini wa ndani na wa nje, wadogo na wakubwa waweze kuwa wanakwenda kuomba leseni za maeneo ambayo zina taarifa sahihi za kijiolojia na hivyo tutafika mahali sasa shida yetu

haitakuwa tena ni kwamba nitachimba wapi madini, shida yetu tu ni kwamba unataka madini gani na yako kiasi gani na kazi yako ni kutafuta mtaji au wadau watakaokusaidia kuweza kuchimba madini hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilisema kwamba, Serikali izidi kuboresha mazingira ya kutoa fidia stahiki, hili ni suala ambalo linahusisha Wizara nyingine, Wizara ya Ardhi ndio huwa wanafanya tathmini, wanaona thamani halisi ya ardhi ambayo inatakiwa kufidiwa na fidia hizo hutolewa kwa mujibu wa Sheria na Kanuni za Wizara ya Ardhi, lakini sisi kama Wizara ya Madini tunafurahi kwamba tunashirikiana nao vizuri kabisa kuhakikisha kwamba mtu yeyote anayetakiwa kufidia, anapata stahiki yake kulingana na uthamini unaofanywa na Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye hoja hizi hizi ambazo Wabunge wamechangia leo hapa, kulikuwa pia na hoja iliyoletwa na Mheshimiwa Masache, Mbunge wa Lupa akisema kwamba, kuna shida kubwa katika matumizi ya *cyanide,* hapana, nafikiri ni Mbunge wa Tunduma ameleta hilo, Mheshimiwa Zidadu *cyanide* kweli inawezekana ikawa teknolojia yake bado iko juu kwa uwezo wa wachimbaji wadogo kuitumia.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikuhakikishie tu kwamba sasa hivi dunia inazidi kuja na teknolojia za aina nyingi na rahisi na rafiki ya kuchenjua madini ya dhahabu. Hii biashara ya kuendelea kung'ang'ania zebaki ni biashara ambayo dunia imeshaweka ukomo kwamba itafika mahali haitakiwi kutumika kwa sababu ya madhara yake. Kwa hiyo, tutakachofanya sisi kama Wizara ni kuzidi kwenda kutoa elimu kwa jamii husika juu ya namna mbalimbali ambayo uchenjuaji wa madini hayo unaweza ukafanyika bila kuathiri mazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu naona kengele ya kwanza imelia, kuna hoja moja ambayo haikuletwa moja kwa moja hapa ndani, lakini nadhani ni hoja ambayo tumekutana nayo kila mahali na kwenye maswali, naomba niitolee ufafanuzi mfupi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wabunge wengi wamekuwa wakitaka kujua kwamba hii minada ya maonesho ya vito utaratibu wake wa kuyaanzisha ukoje na unakwendaje? Minada hii ya maonesho ya madini ya vito kwanza ilikuwa inategemea tufanye marekebisho kwenye Sheria ya Madini, Kanuni ya Masoko ya Madini, Kanuni ya Eneo Tengefu la Mererani na Kanuni za Uongezaji Thamani Madini ili kuwezesha kufanyika kwa utaratibu wa urejeshwaji wa hayo masoko.

Mheshimiwa Naibu Spika, mpaka hapa tulipo sasa hivi Wizara imeshafanya kazi kubwa ya kuainisha namna utaratibu huo utakavyofanyika na tunategemea kufikia mwezi Julai, 2024 angalau tutaanza kwa minada ya ndani ambayo tulipendekeza kwamba ianze kufanyika katika Miji mikubwa ya Arusha, Dar es Salaam, Zanzibar na wakati huohuo tukijiandaa kuanzisha masoko au minada ya madini ya vito ya kimataifa yaani ile *international game fair.*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa Wizara ya Madini kupitia Tume ya Madini na Soko la Bidhaa Tanzania yaani *TMX* ndio wamechukua dhamana ya kuanzisha mfumo kama ule wa mazao wa *TMX* wa kuendelea na uanzishwaji wa hiyo minada ya madini ya vito kwa kuanzia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu ya muda niliopewa kwamba utakuwa umeisha, nitumie tu nafasi hii kuendelea kusema kwamba mimi kama Naibu Waziri wa Madini, maelekezo ya Kamati miongozo ninayopata na maelekezo ya Waziri wangu Mheshimiwa Anthony Peter Mavunde, kijana, jasiri, msikivu nakuhakikishia kwamba hayo yote yaliyoibuliwa kupitia mjadala wa hoja ya bajeti yetu, sisi tutakwenda kuyafanyia kazi. Wizara hii ni uti wa mgongo wa njia za kupatia fedha za kigeni za kuendeshea Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, habari ya biashara dhahabu kupatikana dhahabu yenye ubora wa kuweza kuhifadhiwa na Benki Kuu ya Taifa ni habari ambayo najua Mheshimiwa Waziri atatolea ufafanuzi lakini Benki Kuu wakati Mheshimiwa Dkt. Doto Biteko akiwa yuko na sisi tayari alishaweka utaratibu wa benki ili kuwapa wachimbaji wadogo fedha ambayo wao wenyewe sasa

watachimba madini, watapeleka kwenye *refinery* na kwenye hizo…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MADINI:** …*refinery,* madini yatatoka sasa yakiwa yamefikia asilimia ya kuwekwa kwenye Benki Kuu ya Taifa kama fedha au *reserve* ya fedha za kigeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, nakushukuru kwa kunipa nafasi na naunga mkono hoja yetu. Tunaomba mtupitishie bajeti tukafanye kazi. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru sana kwa nafasi ya kuhitimisha hoja yangu. Naomba nianze maneno yangu kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema aliyetuwezesha siku ya leo kushiriki kwenye jambo hili la kujadili Bajeti ya Wizara ya Madini ambayo ni sekta yenye mchango mkubwa katika uchumi wa nchi yetu ya Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue fursa hii kumshukuru sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan, Makamu wa Rais, Waziri Mkuu na Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu kwa maelekezo yao, miongozo yao katika namna bora ya utekelezaji wa majukumu ya Wizara hii ya Madini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua fursa hii pia kuishukuru sana Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini kwa ushauri na maelekezo yao ambayo wamekuwa wakiyatoa mara kwa mara kwenye kuboresha utendaji wa Wizara yetu ya Madini. Pia kipekee kabisa nachukua fursa hii kuwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wote waliopata nafasi ya kuchangia na wale ambao wametoa mchango wao kwa maandishi kwa jinsi ambavyo wamechangia katika namna nzuri ya kuboresha na

kuimarisha Wizara ya Madini ili mwisho wa siku tuweze kufikia matokeo tarajiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jumla ya wachangiaji walikuwa ni 16 na wawili wamechangia kwa maandishi. Kwa sababu ya muda naomba nianze kujibu hoja za Waheshimiwa Wabunge. Kwanza, mniruhusu nimshukuru sana Mheshimiwa Rais, ndani ya kipindi chake kifupi katika uongozi wa Nchi yetu ya Tanzania, sekta yetu ya madini imepiga hatua kubwa sana kimaendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wa Sekta ya Madini kwenye pato la Taifa umeongezeka kufikia 9.1%. Malengo tuliyowekewa Wizara ya Madini na Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi ni kuhakikisha sekta hii inatoa mchango katika pato la Taifa kwa 10% ifikapo mwaka 2025. Ni dhahiri kwamba, sekta hii inaendelea kukua na hii ni kutokana na maelekezo na miongozo mizuri ya Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sekta hii imeendelea kuwa na mchango mkubwa katika upatikanaji wa fedha za kigeni. Katika mwaka wa fedha uliopita mauzo ya bidhaa nje ya nchi, kwenye Sekta hii ya Madini, yalikuwa ni dola bilioni 3.1 na kuifanya sekta hii kuwa ndiyo sekta iliyoongoza kwa kuleta fedha za kigeni nchini kwa zaidi ya 56% ya fedha zote za kigeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika uongozi wa Mheshimiwa Rais uanzishwaji wa masoko 42 na vituo vya ununuzi 100 umesababisha kuwepo na mzunguko wa fedha zaidi ya shilingi 1,700,000,000,000 katika masoko yote haya. Katika mzunguko huu, Serikali tumekusanya mrabaha wa shilingi 426,000,000,000 kutokana na kazi hii ambayo inafanywa na wachimbaji wadogo wanaotumia masoko na vituo vya ununuzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wa sekta ya madini katika ukusanyaji wa maduhuli ya Serikali katika mwaka wa fedha uliopita tumekusanya maduhuli ya shilingi 678,000,000,000. 40% ya maduhuli hayo yamechangiwa na wachimbaji wadogo waliokaa jukwaani kule juu. Hii ni kazi kubwa ambayo imeendelea kufanyika. Ndani ya miaka mitatu ya Mheshimiwa Rais katika

mapato ya kodi ya ndani, sekta ya madini katika mwaka wa fedha uliopita tumechangia shilingi trilioni 2.1 sawa na 15% ya mapato yote ya kodi ya ndani ambayo yametokana na sekta hii ya madini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nilitaka niwaoneshe namna ambavyo kumekuwa na mchango mkubwa sana wa uongozi wa Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan. Mchango wake umefanya sekta hii inaendelea kukua na kukua zaidi.

Mheshimiwa Spika, sasa nije kwenye hoja za Wabunge, wamezungumza hoja nyingi sana. Baadhi nitazijibu hapa na nyingine nitazijibu kwa maandishi kwa sababu ya wingi wake:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naanza na hoja ya kwanza ya utafiti. Hoja hii imezungumzwa vizuri sana na Mheshimiwa Profesa Muhongo na wachangiaji wengine wengi, karibu Wabunge wote waliosimama hapa wamesema kuhusu utafiti.

Mheshimiwa Spika, Nchi yetu ya Tanzania kwenye eneo la madini tumeligawa katika vitu vinaitwa *QDS* ni *Quarter Degree Sheets* ambazo ziko 322. Nchi yetu ina ukubwa wa eneo la kilomita za mraba 945,000 ambazo ni sawasawa na ekari 233,000,000. *QDS* moja katika hizi 322 ina urefu wa kilometa 54 na upana wa kilomita 54. Kwa hiyo, *QDS* moja inatengeneza eneo la kilomita za mraba 2,819, sawasawa na ekari 720,252. Sasa maeneo haya tunayo 322. Kupitia *GST* tumefanikiwa kufanya utafiti wa *low resolution* kwa 100%. *Geological mapping* kwa 97%, lakini hatujafanya utafiti wa kina kwa maana ya *High Resolution Air Borne Geophysical Survey.* Hii tumeifanya kwa 16% tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ndiyo maana tukaja na *Vision 2030. Vision 2030,* maana yake ni kwamba, Wizara ya Madini tumejiwekea malengo, ukifika mwaka 2030 tuwe tumeipima nchi yetu kwa utafiti wa kina kwa 50%. Kama katika 16% ambayo tumeipima manufaa ndiyo haya na kodi ndiyo hizi, hivi *what if* tukienda katika 50%? Nchi yetu itapaa zaidi kiuchumi. Hiyo ndiyo dhamira yetu kubwa ya kufanya kwenye sekta yetu hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nawaondoa hofu Waheshimiwa Wabunge kwamba, eneo la utafiti ndiyo kipaumbele chetu. *GST* katika muda wote wa kuishi kwao, miaka 99, wamepima kwa utafiti wa kina eneo la 16%. Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, chini ya uongozi wake katika miaka yake mitatu kuanzia mwezi Julai, tunakwenda kutekeleza mradi ambao utagusa *blocks* mbili kubwa zenye eneo la ukubwa wa kilomita za mraba 165,574 ambayo ni sawasawa na 18% ya nchi nzima. Kwa hiyo, ukijumlisha 16% ambayo zimeshapimwa tayari, ukiongeza 18% ambayo tunaanza mwezi Julai, jumla tutakuwa tumepima 34% ya Nchi yetu ya Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, leo ni mwaka 2024, lengo ni kufikia 50% mwaka 2030. Tuna miaka sita mingine, tunaifikia hii azma. Tunakwenda kuipima nchi yetu kufikia 50% ili watu wetu waweze kunufaika. Manufaa yako mengi sana tukiipima nchi yetu. Tukiipima nchi yetu hii kwa kurusha ndege au *drone* au *helicopter* ambayo itakwenda chini, ziko hatua zifuatazo: Kwanza, tutakuwa tumepata viashiria vya miamba ya madini, wataalamu wanaita *anomalies,* tutazijua hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hatua ya pili, tutakwenda kwenye uchorongaji, *drilling.* Hatua ya tatu, tutakwenda kwenye *geo-chemistry* na baadae tutafanya *resource estimation.* Hii itatuambia kwamba, chini ya ardhi kuna madini kiasi gani na hiyo ndiyo taarifa ambayo tunaihitaji. Kwa hiyo, katika bajeti hii tunakwenda kununua *helicopter, jet ranger,* ambayo tutaifunga vifaa vitakavyokuwa na uwezo wa ku-*scan* ardhi kwenda chini kilomita moja kujua madini yaliyopo hapo. Hii itatupa nafasi ya kuweza kuwapanga vizuri wachimbaji wetu wadogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, leo wachimbaji wadogo wanapoteza mitaji yao na nguvu zao kwa sababu, wanachimba kwa kubahatisha. Serikali ya Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, ipo tayari kuwaongoza wachimbaji wadogo katika njia sahihi na tutunze mitaji yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Profesa Muhongo amegusia hoja ya Madini Kinywe *(Graphite);* ni kweli ni jambo muhimu sana. Hivi sasa baada ya dunia kwenda katika nishati safi

kwenye Kampeni ya *Net Zero Emission* kwa Mwaka 2050 matumizi ya madini ambayo ni *lithium, cobalt, nickel, manganese, vanadium* na *graphite* yamekuwa makubwa sana duniani kwa sababu yanakwenda kusaidia utengenezaji wa betri za magari ya umeme.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, hoja ya Mheshimiwa Profesa Muhongo ni hoja sahihi. Madini Kinywe hivi sasa ndiyo hitaji la dunia. Hivi sasa mahitaji ya Madini Kinywe duniani kwa mwaka ni tani milioni sita, uwezo wa uzalishaji ni tani 1,200,000. Anayeongoza ni China, anachangia *64%* katika *total market share* ya *graphite,* kwa Afrika wa kwanza ni Madagascar ambaye anachangia 13%, wa pili ni Msumbiji kwa 10% na wa tatu ni Tanzania kwa asilimia 0.64. Namhakikishia Profesa Muhongo huyu tunayemzungumza anachangia asilimia 0.64, ni ndugu yangu God Mwanga, mwekezaji mzawa, aliyeko pale Handeni kwa Msisi, ndiye ametufikisha katika asilimia 0.64.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa tuna miradi ifuatayo ambayo inakuja; tuna Mradi wa *Kudu Graphite,* Mradi wa *Tanz-Graphite* kule Doma, Mradi wa *Volt* ambao wanakuja, Mradi wa Lindi Jumbo wanakuja na Mradi wa *EcoGraph* kule Mahenge. Hawa wote wakianza uzalishaji tunaiweka Tanzania kwenye ramani ya uzalishaji wa Madini Mkakati, hasa Madini Kinywe. Kwa hiyo, nimwondoe hofu Profesa kwamba, tuko sawasawa katika eneo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu *helium*. Ni kweli kabisa Mwenyezi Mungu ametujalia katika Bonde la Rukwa tumeona kampuni mbili za utafiti, *Noble Helium* na *Helium One,* wamekwenda kufanya uchorongaji na *cape gas* yetu kule Rukwa inatuambia kwamba, tunakwenda kuzalisha *helium* yenye ubora sana duniani kwa maana ya *concentration* ya *helium gas* katika *gas* yote inayozalishwa, nikianza na Kisima cha Mbelele *One* ni *2.4,* ni kubwa sana. Wenzetu hawa wengine wa *Helium One* wenyewe wanakwenda katika *4.7 concentration* ya *helium gas.* Hii inatupa nafasi ya kwenda kuwa kinara duniani katika eneo hili. Nataka niwahakikishie kwamba, tutayatunza na kuyalinda maeneo haya kwa manufaa ya nchi yetu ya Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja ya pili, ni *CSR*. Nisizungumze maneno mengi, tumepitia na tumeiangalia ni kweli, kuna changamoto. Nataka nilihakikishie Bunge lako, tunakwenda kuipitia upya kanuni ya *CSR,* ili ikidhi matarajio na mahitaji ya dunia ya leo kwa hiyo, nawaondoa hofu Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja ya tatu ni *technical support*. Hapa naomba wanisikilize vizuri. Kifungu cha 8(3) cha Sheria ya Madini, Sura 123, kinatoa nafasi ya kumruhusu mmiliki wa leseni ndogo *(Primary Mining Licence)* awe ana nafasi ya kumwingiza mbia katika leseni yake. Leseni hii ni *exclusive,* kwa ajili ya Watanzania, lakini kwa sababu ya ukosefu wa teknolojia na mitaji ilitungwa sheria kumruhusu Mtanzania akimpata *partner* ambaye anaweza akatoa *technical support* afanye naye kazi pamoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumetoa miongozo na kama Wabunge wengi walivyochangia inakoelekea ni kana kwamba, *spirit* ya utungwaji wa sheria hii, kwa maana ya ile *technical support,* inaanza kupotea. Ikipotea maana yake ni tunawapoteza wachimbaji wadogo. Mimi niko hapa nimesimama, siko tayari jambo hili la wachimbaji wadogo kupotea, litokee katika mikono yangu, siko tayari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tumefanya yafuatayo, cha kwanza, mmiliki yeyote wa leseni, nikikupa leseni pale madini inakuwa na masharti yake. Nikikupa leseni, wewe ndiyo mchimbaji na ndiyo mwenye haki na madini. Ukimwingiza mchimbaji mdogo akichimba pale kwako ni kama umempangisha. Asilimia kubwa ya wenye leseni hizi hawachimbi wenyewe, wanaingiza wachimbaji wadogo ambao wanatumia nguvu zao. Masharti haya ambayo tunayaweka ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mtu yeyote anayetaka kupata *technical support* kwenye leseni yake, cha kwanza ahakikishe haingizi wachimbaji wadogo kwa sababu, kwa mujibu wa sheria mwenye jukumu la kulinda leseni ni mwenye leseni. Hilo ndiyo jukumu lake kwanza. Kama mtu anataka *technical support* asiingize mchimbaji mdogo katika eneo lake.

Mheshimiwa Naibu Spika, endapo atamwingiza mambo yafuatayo yatatokea:-

Mheshimiwa Naibu Spika, cha kwanza, kama mchimbaji mdogo kaingia kwenye leseni yako na wewe unataka kufanya *technical support,* kwanza lazima msajili mikataba kati ya wewe na yeye ili tume ifahamu kwamba, kuna makubaliano yaliyopo kati ya mwenye leseni na wenye maduara kwa sababu moja kubwa, mimi nikitoa leseni, nampa mmiliki haki madini; kwa hiyo, kwa mujibu wa sheria mwenye duara mimi simtambui. Sasa huyu mwenye leseni akipata mwekezaji au *technical support* au kuuza leseni yake, jambo la kwanza analolifanya ni kumwondoa mchimbaji mdogo ambaye ameweka maduara yake pale.

Mheshimiwa Naibu Spika, hatuwezi tukaiacha nguvu hii ya Watanzania ikapotea hivi hivi. Mtu kaweka nguvu yake, maduara yako pale, ndio maana tukasema sharti ni kwamba, kama unataka kupata *technical support* basi, usiingize mchimbaji mdogo, lakini wewe umemwingiza. Kwa hiyo, katika muktadha huo, basi haki ya kwanza kama unataka kuuza leseni yako apewe yule mchimbaji mdogo aliyekuwepo katika eneo lako kwa sababu, ameshaweka nguvu yake na wewe ndiye ulimruhusu awepo katika eneo lako na kwa hali ya kawaida siyo mvamizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu, kama mtu ni mvamizi na amekuwepo pale, wewe ndiye mwenye jukumu la kumtoa, leseni ni ya kwako. Ukija Tume ya Madini nakupa leseni wewe, ukiruhusu watu wengine waingie maana yake, *impliedly,* umekubaliana na uchimbaji wao. Sasa huwezi kukubaliana na uchimbaji wao, halafu usikubaliane na nguvu ambayo wameiweka pale.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali haiwezi ikawaacha hawa watu wanapoteza nguvu zao na mitaji yao. Kwa hiyo, hili ni eneo la kwanza ambalo tumesema kwamba, ikitokea mazingira hayo kama unakwenda kwenye *technical support,* basi haki ya kwanza ya msingi uwape wale ambao umewakaribisha kwenye leseni yako, wakishindwa hao endelea na mwekezaji unayemhitaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili tukasema, katika ufutaji wa leseni, kuna leseni ambazo zinarudi chini ya Waziri na utaratibu ni kugawa kwenye vikundi. Kikundi nikikipatia leseni ya madini halafu viongozi wachache kwenye hicho kikundi wakaenda kumtafuta mwekezaji pasipo kuwashirikisha watu wengine leseni ile ikahama, shida ni migogoro inarudi katika Wizara ya Madini. Tukasema hivi, kuanzia sasa, leseni yoyote ambayo tutaitoa kwa vikundi, viongozi hawatakuwa na uwezo wa kuingia makubaliano ya *technical support* au kuifanyia *transfer* mpaka Katibu Mtendaji wa Tume atakapojiridhisha kwamba, leseni hii ikitolewa ina manufaa kwa pande zote, vinginevyo hawa ambao wako katika maeneo hayo hawawezi kunufaika hata kidogo na itakuwa ni changamoto kubwa sana. Kwa hiyo, hiyo hasa ndiyo ilikuwa maana ya eneo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, lengo letu kubwa ni kuweka utaratibu mzuri. Bahati nzuri hatutakurupuka, tutakaa na wadau, tutatunga kanuni za *technical support* kwa kushirikisha wadau. Wote watakuwa *engaged,* kwa maana ya wachimbaji wadogo na tutajadili sote kwa pamoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ufutaji wa leseni. Leseni ni kama vile hati ya umiliki wa ardhi, mtu akipewa ina masharti yake, unapewa masharti ya kuendeleza eneo. Nikikupa leseni usipofuata masharti ya leseni, leseni hiyo nitaifuta. Leseni ambazo nimeanza kuzifuta hapa ni leseni kubwa za utafiti ambazo watu wanapewa kufanya utafiti, lakini hawafanyi. Watu hawa wanamiliki maeneo makubwa, watu wetu wanakosa maeneo ya kufanyia kazi. Wachimbaji wadogo wakiingia katika maeneo hayo ambayo mwenye leseni anatakiwa kuyalinda na kuanza kuchimba, anakimbilia kwa Mkuu wa Wilaya kuomba askari na kwenda kuwatoa na hivyo kuichonganisha Serikali na watu wake. Kwa hiyo tumesema mtu yeyote ambaye hakidhi masharti ya leseni, kwa mujibu wa kifungu cha 63(2) cha Sheria ya Madini ambacho kinanipa nafasi ya kumpa *default notice* na kumtaka arekebishe makosa yake, asiporekebisha, tunafuta leseni. Hapa naomba ieleweke.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimesikiliza hoja ya Mheshimiwa Kunambi, sijaelewa ni katika mazingira gani Mtendaji wa Tume

anapaswa aondoke kwa sababu, aliyepewa leseni hajatimiza masharti ya leseni? Ni katika mazingira gani? Kwa sababu, mimi nakupa leseni ufanye utafiti, hufanyi. Nafuta, halafu namtoa Samamba! Haiwezekani. Mheshimiwa Kunambi, Mkoa wote wa Lindi una leseni za utafiti 102, Lindi yote imening'inia, watu hawazifanyii kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nitaendelea kufuta, nafuta na nitafuta sana leseni mpaka tukae sawasawa. Katika maombi na leseni tulizozifuta mwezi Machi, tarehe 22, watu 34 wameingiza maombi ya kushikilia maeneo ya ekari 4,315,000, sawasawa na Mikoa ya Dar es Salaam 12, halafu wachimbaji wadogo wanalia hawana maeneo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, watu 54 wameshikilia maeneo yenye ukubwa wa ekari 13,000,000 sawa na mikoa ya Kilimanjaro minne yaani hawa nawaacha jamani? Najua Waheshimiwa Wabunge huwa wanaona mimi mpole sana kwa sababu tu ya sura yangu ya kipaimara, lakini nataka kuwaambia katika hili la maslahi ya umma nitakuwa mkali sana mpaka tukae sawasawa. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu *MBT* na *Vision 2030;* hoja ya *MBT*, Wizara ya Madini imekuja na hoja ya *Mining for a Brighter Tomorrow* ambayo lengo lake ni kuwasaidia akinamama na vijana ili waweze kukuza sekta hii ya madini. *Illustration* ya *MBT* ni ndogo sana. Ukienda Mkuranga kuna mama pale anazalisha kifusi cha mchanga na kokoto, lakini hana uwezo wa kupeleka Dar es Salaam kuuza kwa mlaji wa mwisho. Anakuja mwenye usafiri ananunua kifusi kwa shilingi 20,000 anakwenda kuuza Dar es Salaam kwa shilingi 320,000. Yule mama amekosa tu namna ya kutoa kifusi Mkuranga kukipeleka Dar es Salaam kwa mlaji wa mwisho. *MBT* inakwenda kujibu maswali hayo magumu kwa akinamama na vijana wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunakwenda kusaidia upatikanaji wa maeneo, vifaa, mitambo na magari. Katika mitambo 10 ambayo Mheshimiwa Rais ametununulia ya uchorongaji, miwili tunai-*dedicate* kwa ajili ya vijana na wanawake, hiyo ni *specific* kwa ajili yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna hoja ya Mheshimiwa Kapufi alizungumza kwamba, *concentration* kubwa sana imekuwa kwenye dhahabu tunayasahau na haya madini mengine, ipo wapi teknolojia ya uchenjuaji? Nakubaliana na Mheshimiwa Kapufi, *geological set up* ya kule kwake ni ngumu sana kwenye uchenjuaji. Hali hii inapelekea tuwe na teknolojia kubwa ya kuweza kutusaidia, Serikali imefanya nini katika hilo? Serikali imefanya yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye eneo la *Buzwagi Special Economic Zone* ambalo tumetenga ekari 1,333, mle ndani mwezi uliopita nimetoa leseni kwa Kampuni ya *Tembo Nickel Refining Company Limited* ambao wanakwenda kuwekeza Kiwanda cha Usafishaji wa Madini cha dola 500,000,000 yaani *multi-metal processing facility* ambayo itatumia teknolojia ya *hydrometallurgy* ambayo tuna-*skip* eneo la uyeyushaji *(smelting)*. Itakuwa teknolojia ya kisasa ya kubaini baadhi ya madini ambayo huwezi kuyaona kwa macho ya kawaida katika teknolojia ambayo tunayo hivi sasa. Kwa hiyo, hiyo ni hatua ya kwanza ambayo tumeifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hatua ya pili, nimekutana na wadau wiki iliyopita *Dodoma Hotel* hapa Dodoma. Nimewa-*captivate* kuja kuwekeza hapa nchini Tanzania na sasa hivi tayari tunazo kampuni tatu za kuja kufunga mitambo ya uchenjuaji madini metali ili kuondokana na changamoto ambayo anakutana nayo Mheshimiwa Mbunge. Kwa hiyo, nimwondoe hofu, mipango ya Serikali iko sawasawa na tutalifanya hilo jambo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge wamezungumza kuhusu *free trade interest*, ni kweli. Kifungu cha 10 cha Sheria ya Madini kimeweka sharti la lazima la *state participation*, nchi kuweza kunufaika. Waheshimiwa Wabunge ni kweli kama Wabunge walivyosema tunaendelea na majadiliano yamechukua muda mrefu, lakini nataka kutoa *commitment* kwa Wabunge, tulikuwa tuna *SPGNT* hivi sasa tuna *GNT* ambayo iko chini ya Mamlaka ya Waziri, iko kwangu. Nimeshawapa maelekezo na kikao cha kwanza kinaanza tarehe 6 Mei, cha mazungumzo na nimewaambia tuyaharakishe mazungumzo haya

ili nchi ianze kunufaika. Waheshimiwa Wabunge katika hili naomba wanipokee, tumeshalichukua na timu tayari imeshaundwa, nishaunda timu, kazi inaendelea. Ndani ya muda mfupi tutaanza kuyaona matokeo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niwape habari njema katika eneo hili. Katika Mradi wa Nyanzaga, Sengerema kwa Mheshimiwa Tabasam, ambapo upo chini ya *Sotta Mining Company Limited*; Serikali tukiwa na ubia wa 16% vilevile Kampuni ya *OreCorp* wakiwa na ubia wa 84%. Baada ya kupatikana kwa mwekezaji mwingine ambaye ni Kampuni ya Perseus kutoka Australia, moja ya sharti tulilompa alipokuja kununua hisa za *OreCorp* tulimwambia *free carried interest* yetu isiwe 16% iwe 20%. Mwekezaji ameridhia na nchi itaanza kupokea 20% katika eneo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ambalo limesemewa sana hapa ni sehemu ya *refinery*, Mheshimiwa Kanyasu kasema. Kwanza kabisa nataka nitumie fursa hii kuwapongeza sana wawekezaji wazawa hasa mama yangu Mama Sara Masasi wa *GGR* na *STAMICO* na tulioingia nao ubia. Tunaendelea na mazungumzo katika Kamati ambayo nimeiunda. Kama Mheshimiwa Kanyasu alivyosema, Sheria yetu katika Kifungu cha 59, kinatoa mamlaka kwa Waziri kushauriana na wamiliki wa haki madini juu ya kiwango kitakachotengwa kwa ajili ya masuala ya *smelting* na *refinery*, tumepitia kila kifungu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuweza kusaidia upatikanaji wa dhahabu kwenda kwenye *refinery* hizi, tumeona tunahitaji kukaa ndani ya Serikali na hasa katika kukiboresha kifungu kile ili kikidhi matakwa ya matarajio yaliyowekwa; kwa maana *spirit* ya kile kifungu ilikuwa ni kuhakikisha sehemu ya dhahabu au ya madini mengine yoyote yanabaki hapa nchini kwa ajili ya kufanyiwa *refinery* au kufanyiwa namna yoyote ya kuongeza thamani. Sasa tumeona kuna baadhi ya maeneo kuna mapungufu, tumeangalia ile sehemu ambayo inatoa mwanya wa tafsiri tofauti tofauti.

Mheshimiwa Naibu Spika, kilichofanyika, tumeitana kwa haraka sana chini ya usimamizi wa Mheshimiwa Waziri wa Sera,

Bunge na Uratibu na tutaifanya kazi hiyo kwa haraka sana ili tuweze ku-*accommodate* jambo hilo, tuli-*address* na mwisho wa siku tuwasaidie hawa wawekezaji wazawa. Tunaunga mkono sana akina mama Masasi na wengine kwa kazi hii ya *refinery*. Serikali itahakikisha kwamba tunasimamia kwa dhati jambo hili litokee na mwisho wa siku mitaji yao isiuliwe. Kwa hiyo, nataka kuwaondoa hofu Waheshimwa Wabunge katika eneo hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye *local content* Mheshimiwa Profesa Manya kasema vizuri, kwamba tumewaandaa Watanzania? Nilikutana na watoa huduma wote Mwanza tarehe 27 Desemba na nikawaambia waanzishe kwanza chama cha watoa huduma katika maeneo ya migodi kwa maana ya *local content*. Pia, nikamwita Raphael Maganga, mtu wa *TPSF* kwamba, lazima tuiandae sekta binafsi yenye nguvu ya kupokea haya mabadiliko makubwa ambayo tunayafanya. Ninavyozungumza na Mbunge leo hapa Bungeni, ni kwamba, tayari chama hicho kimeundwa na wahusika wenyewe wako hapa kinaitwa *TAMISA*, tutaanza sasa utaratibu ambao niliutolea maelekezo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, cha kwanza, nimeelekeza Tume ya Madini kuhakikisha wananiletea *procurement plan* ya migodi yote nchini ili zile bidhaa ambazo wanaziagiza sana kwa wingi tuone namna zianze kuzalishwa hapa nchini kulinda ajira za Watanzania. Kwa hiyo, katika hoja hiyo ya Profesa, tunaendelea kuwajengea uwezo na tupo tunafanya pamoja na *TPSF*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ilizungumzwa pia hoja kuhusu Mererani masuala ya mitobozano Waheshimiwa Wabunge walisema hapa. Nimeanza kuchukua hatua, jana nimewaita ofisini, Onesmo Mbise wa *Franone* na Saniniu Laizer, (bilionea Laizer), tumekaa nao, tumejadili hatua ya kwanza ya utatuzi wa migogoro. Dhamira yetu Wizarani ni kuona kwamba *mining activities* zinafanyika, kwa hiyo, lengo letu siyo kuwarudisha watu nyuma. Tumeanza hatua ya kwanza, jana tumekaa kikao, tutaendelea na hatua ya pili ya kutatua mgogoro huo ili mwisho wa siku Mererani irudi katika hali yake ya kawaida. Kwa hiyo namwondoa hofu Mbunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna hoja hapa imesemwa kuhusiana na Buhemba kwamba kwa nini *STAMICO* wame…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri omba fedha.

**WAZIRI WA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ili Wizara iweze kutekeleza majukumu yake na malengo yaliyopangwa ikiwemo ukusanyaji wa maduhuli ya shilingi 1,164,850,027, naomba Bunge lako Tukufu liliridhie na kupitisha makadirio ya shilingi 231,983,614,000 kwa ajili ya matumizi ya Wizara na taasisi zake kwa mwaka wa fedha 2024/2025 kwa mchanganuo ufuatao: shilingi 140,661,200,000 sawa na 60% ya bajeti yote ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo; na shilingi 91,322,414,000 sawa na 39% ya bajeti yote ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Kati ya fedha hizo shilingi 24,872,875,000 ni kwa ajili ya mishahara ya watumishi na shilingi 66,000,449,539 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo ya Wizara na taasisi zilizo chini yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**NAIBU SPIKA:** Hoja imeungwa mkono.

Katibu.

**NDG. MICHAEL CHIKOKOTO, *ndc* – KATIBU MEZANI:**

**KAMATI YA MATUMIZI**

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tukae.

Katibu.

**NDG. MICHAEL CHIKOKOTO, *ndc* – KATIBU MEZANI:**

**KITABU CHA PILI - MATUMIZI YA KAWAIDA**

**Fungu 100 – Wizara ya Madini**

Kifungu 1001 – *Administration and Human Resources Management*………..……………..Sh. 6,505,985,167
Kifungu 1002 – *Finance and Accounts Unit*……....Sh. 1,655,015,861

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa kwa mamlaka ya Kiti tunaingia kwenye *guillotine*. *(Makofi)*

**NDG. MICHAEL CHIKOKOTO, *ndc* – KATIBU MEZANI:**

**Fungu 100 – Wizara ya Madini**

Kifungu 1001 – *Administration and Human Resources Management*……..……..……….…..Sh. 6,505,985,167
Kifungu 1002 – *Finance and Accounts Unit*…..…...Sh. 1,655,015,861
Kifungu 1003 – *Policy and Planning Division*……......Sh. 2,292,932,391
Kifungu 1004 – *Internal Audit Unit*…..……..…………...Sh. 737,324,594
Kifungu 1005 – *Legal Services Unit*………...……….Sh. 2,153,912,585
Kifungu 1006 – *Government Communication Unit*...Sh.1,240,735,086
Kifungu 1007 – *Procurement Management Unit*……..Sh.927,864,390
Kifungu 1009 – *Management Information Systems Unit*……………………………..………Sh. 771,276,000
Kifungu 2001 – *Minerals Division*………..….…........Sh. 74,287,367,926
Kifungu 1008 – *Monitoring and Evaluation Unit*…........Sh. 750,000,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**KITABU CHA NNE - MIPANGO YA MAENDELEO**

**Fungu 100 – Wizara ya Madini**

Kifungu 2001 – *Minerals Division*……..…………….…Sh. 140,661,200,000

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**NDG. MICHAEL CHIKOKOTO, *ndc* – KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa taarifa kwamba Kamati ya Matumizi imemaliza shughuli yake.

**MWENYEKITI:** Bunge linarejea.

*(Bunge lilirejea)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tukae. Mtoa hoja. *(Makofi)*

**T A A R I F A**

**WAZIRI WA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 123(3)(a) na (b), ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023, naomba kutoa taarifa kwamba, Bunge lako likikaa kama Kamati ya Matumizi limekamilisha kazi yake. Naomba taarifa ya Kamati ya Matumizi ikubaliwe na Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

**NAIBU SPIKA:** Hoja imeungwa mkono, sasa nitawahoji kuhusu hoja ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Madini kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025. Wote wameafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Madini kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 Yalipitishwa na Bunge)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri hongera sana wewe na Naibu wako na timu yako; Katibu Mkuu, Makamishna wa Tume. Tumpongeze Mheshimiwa Dkt. Doto, Naibu Waziri Mkuu kwa kukulea vizuri, amekuachia Wizara ya Madini pamoja na madini yake. Kwa namna ulivyojieleza umeonesha sasa umekomaa kwenye Wizara hiyo. Tatizo lako moja tu, uko uko. *(Makofi/Kicheko)*

Nasitisha Shughuli za Bunge mpaka siku ya Alhamisi, saa 3.00 asubuhi.

*(Saa 12.54 Jioni Bunge liliahirishwa hadi Siku ya Alhamisi, Tarehe 2 Mei, 2024, Saa Tatu Asubuhi)*